

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Nane – Tarehe 18 Aprili, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Tunaendelea na Mkutano wetu wa Saba, Kikao cha leo ni Kikao cha Nane.

Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:** Hati za kuwasilisha Mezani.

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI  
YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI  
YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA  
SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Rais, TAMISEMI juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**MHE. CECILIA D. PARESSO - K.n.y. MSEMAJI MKUU WA  
KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA  
UTAWALA BORA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**SPIKA:** Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

## **MASWALI NA MAJIBU**

Na. 60

### **Kuboresha Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*HCMIS*)**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** Aliuliza:-

Je, ni lini Mfumo wa Taarifa za Watumishi *LAWSON* utaboreshw na kuondoa dosari zilizopo sasa hivi kama vile watumishi wa Umma kuondolewa kwenye makato ya mikopo wakati hawajakamilisha malipo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Jimbo la Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (*Human Capital Management Information System*) au kwa *version* nyengine ya *LAWSON Version 9* unaotumika sasa kwa ajili ya kukusanya taarifa za kiutumishi na malipo ya mishahara ulianza kutumika mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mfumo huu una changamoto ambazo zinasababisha watumiaji wasio waadilifu kuutumia vibaya kinyume na utaratibu ikiwemo kusitisha makato ya mkopo kabla mkopo wote haujamalizika kulipwa. Hii ilibainika kutohana na kaguzi za mara kwa mara zinazofanywa na Serikali ambapo hadi sasa watumishi wa aina hiyo wapatao 65 kutoka katika mamlaka za ajira 32 wamechukuliwa hatua mbalimbali baada ya kugundulika kuwa wametumia vibaya dhamana walizokabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, kutohana na changamoto hii, Serikali inaendelea na hatua za kuhamia kwenye toleo jipya

la mfumo huu (*LAWSON Version 11*) ambao unatarajia kuwekwa mifumo zaidi ya udhibiti ili kuhakikisha kwamba maafisa wenye dhamana ya usimamizi wake hawafanyi mabadiliko yoyote bila kugundulika.

Mheshimiwa Spika, usanifu wa mfumo huu ili kuweza kuhamia katika toleo jipya la *LAWSON Version 11* unaendelea ambapo wataalam wetu wa Wakala wa Serikali Mtandao (*EGA*) ndio wamepewa jukumu la kusimamia usanifu na usimikaji wake. Baada ya maboresho haya miundombinu madhubuti ya kuzuia matumizi mabaya ya mfumo itaimarishwa.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawilli ya nyongeza. Ni wazi kwamba Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba mfumo huu una upungufu na una changamoto nydingi ambazo nimeelezea mojawapo. Sasa nataka *commitment*ya Serikali kwamba hiyo *Version 11* itaanza kutumika lini? Swali langu la kwanza.

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; changamoto nydingine ya mfumo huu ni kwamba, unasimama peke yake (*stand alone system*) na wakati ukiangalia kwenye taasisi zetu, kwa mfano Mamlaka ya Serikali za Mitaa, kuna mifumo mingi, tulitegemea kwamba mifumo hii ingekuwa inaongea; kuna *EPICA*, kuna *LGMD*, sasa je, Mheshimiwa Waziri atanihakikishia kwamba mfumo huu mpya *Lawson Version 11* utakuwa unaongea na mifumo mingine? (*Makofii*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza nimpongeze sana kwa namna ambavyo amekuwa akisimamia suala zima la *management* ya rasilimali watu katika utumishi wa umma na yeye mwenyewe pia alikuwa katika utumishi wa umma na tunafahamu mchango wake na tunauthamini.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la kwanza, kwamba sasa Toleo hili la 11 (*Lawson Version 11*) litaanza lini; nimhakikishie tu kwamba, katika Mwaka huu wa Fedha tumeshatenga Shilingi milioni 486 katika Idara yetu ya Usimamizi wa Rasilimali Watu pamoja na Idara yetu ya TEHAMA na nimhakikishie tu kwamba katika Mwaka huu wa Fedha suala hili litakamilika. Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, tumewakabidhi suala hili Wakala wa Serikali Mtandao ili waweze kusanifu na usimamia usimikaji wake.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili, kwamba ni lini sasa mfumo huu wa usimamizi wa rasilimali watu au taarifa za kiutumishi na mishahara utaweza kuzungumza na mifumo mingine kama mifumo ya kifedha kama *EPICA* na mingine; nimwambie tu kwamba tunaiona hoja yake na hata *e-government* wamekuwa wakifuautilia suala hili kwa makini sana, si tu katika suala zima la kuongea, hata katika kuhakikisha pia gharama za mifumo yenye na udurufu wa kuwa na mifumo mingi wakati kunawenza kukawa na mifumo michache ambayo inaweza ikazungumza.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu kwamba pamoja na faida nyingine tutakazozipata tutakapoingia katika *Lawson Version 11* ni pamoja na kuunganisha mifumo mingine kama *EPICA* lakini pia kuhakikisha Mifumo kama ya *NECTA*, *NIDA*, *RITA* pamoja na mingine nayo pia ni lazima izungumze na Mfumo wetu wa *Lawson*.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwalimu Bilago, kuna shida gani ya Walimu tena huko! Swali la nyongeza!

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Wakati Serikali inafuatilia wafanyakazi hewa na ikagundua kwamba kulikuwa na wafanyakazi hewa wapatao 20,000, ni jambo sahihi na ni kweli kwamba Serikali hiyo iliwaondoa kwenye Mfumo wa *Lawson* wale walipatikana kuwa hewa. Sasa nataka kujiuliza, na Waziri anisaidie, baada ya kugundua wafanyakazi 20,000 Serikali imekaa kimya habari ya ajira, naomba Serikali itoe kauli juu

ya ajira ya wafanyakazi wakiwemo Walimu na Sekta nyingine za Idara ya Afya pamoja na Kilimo na kadhalika, naomba kauli ya Serikali.

**SPIKA:** Swali hilo nalikataa kwa sababu leo ni siku ya Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ili asianze kutoa yaliyo ndani ya hotuba yake lakini namuagiza Mheshimiwa Waziri katika kujibu hoja za Wabunge baadaye aichukue hoja hii iwe mojawapo ambayo ataifafanua, maana yake ni swali muhimu sana Mheshimiwa Mwalimu Bilago, sio kwamba nimelitupa, hapana, nimekuwekea akiba ili lije lijibiwe vizuri zaidi.

Tunaendelea na Ofisi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, swali la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini.

Na. 61

### **Hali ya Maziwa Madogo Nchini**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** Aliuliza:-

Maziwa Madogo nchini kama vile Ziwa dogo la asili la Tlawi katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu yanaelekea kukauka kutokana na kuongezeka kwa magugu maji, kadhalika Ziwa Babati na Ziwa Manyara pia yana dalili ya kukauka na Mamlaka za Serikali za Mitaa hazina uwezo wa kuyaokoa:-

- (a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuyaokoa maziwa hayo muhimu katika ustawi wa nchi yetu na kizazi kijacho?
- (b) Je, kwa nini kusiwe na mpango kabambe wa Kitaifa kuyaokoa maziwa hayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA Alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaona umuhimu mkubwa wa kuokoa Ziwa dogo la Tlawi liliopo Halmashauri ya Mbulu na maziwa mengine kote nchini yanayokabiliwa na tishio la kukauka na magugu maji kutokana na kuongezeka kwa shughuli za binadamu hususan kilimo na ufgaji usio endelevu, uvuvi haramu na athari ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu huo, mwaka 2008 Serikali iliandaa Mkakati wa Taifa wa Hatua za Haraka za Kuhifadhi Mazingira ya Bahari Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa. Mkakati huu unaelekeza Wizara na sekta na halmashauri zote nchini kuchukua hatua za haraka kuzuia shughuli zote za binadamu kufanyika kandokando ya maziwa, mito na mabwawa ili kuzuia uharibifu wa mazingira unaoweza kusababisha kukauka kwa maziwa hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kunusuru Ziwa dogo la Tlawi, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu imechukua hatua zifuatazo:-

1. Mradi wa *DADP's* Wilaya ya Mbulu umetenga Shilingi milioni 100 katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 kwa ajili ya kuondoa magugu maji katika Ziwa Tlawi.
2. Katika Bajeti ya Mwaka 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu imepanga kutenga kiasi cha Shilingi 15,742,000 ili kutekeleza shughuli za kunusuru Ziwa Tlawi pamoja na kuainisha mipaka ya ziwa hilo, uvamizi wa watu katika shughuli za kilimo, kuhimiza kilimo endelevu pamoja na miinuko inayozunguka ziwa hilo, kutoa elimu kwa wananchi ya kuhifadhi

mazingira na vyanzo vya maji, kuimarisha Kamati za Mazingira na ulinzi shirikishi kwa ziwa katika ngazi za kata, vijiji na mitaa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada zinazofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, Serikali itafanya tathmini ya kina kubaini chanzo cha ukubwa wa tatizo na kuchukua hatua stahiki za ziada kuhimili athari katika Maziwa ya Tlawi, Babati na Manyara ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyataja kuwa yako kwenye tishio la kukauka.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali madogo ya nyongeza. Hivi sasa Serikali inatumia gharama kubwa sana katika kuanzisha mabwawa mapya kupitia maji ya mvua; lakini rasilimali hizi za asili nyingi zimeelekea kutoweka, kwa hiyo, nilidhani Serikali pia itakuwa na mkakati.

Mheshimiwa Spika, hivyo nina maswali madogo mawili, la kwanza, fedha zilizotajwa katika Bajeti ya Mwaka 2016/2017 hazikuweza kupatikana hadi sasa na hivi sasa tunaingia Bajeti ya Mwaka 2017/2018, lakini hali inayotishia ziwa hili inaonesha hivi punde litakauka; je, Serikali itatoa lini fedha milioni mia moja kupitia Mradi wa *DADP's* ambayo imekusudiwa kwa nia njema katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kama ambavyo Mheshimiwa Naibu Waziri amewajibu Watanzania pamoja na mimi na wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini, Serikali haionti umuhimu sasa wa kutuma timu ya wataalam kupitia maziwa yote ya asili katika nchi yetu ili iweze kutoa ushauri wa kitaalam na kuchukua hatua za kunusuru maziwa hayo kwa haraka na wataalam hao watakwenda lini? (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa lile swalii la kwanza sijui kama Waheshimiwa wa Wizara ya Kilimo wapo, lakini kama hawapo basi Mheshimiwa Naibu Waziri endelea tu, maana yake la kwanza linahusu *DADPs*.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Mbunge atakubaliana nami kwamba baada tu ya kupata swali lake hili nilifanya ziara katika Mkoa wa Manyara na kati ya maziwa ambayo nilikwenda kuyaona ni Ziwa Babati, tukiwa na Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini Mheshimiwa Pauline Gekul pamoja na Mheshimiwa Jitu Soni, na bahati mbaya siku ile Mheshimiwa alipata ajali, pole sana, lakini Mwenyezi Mungu alitusaidia.

Mheshimiwa Spika, basi niseme kifupi kwamba, bajeti haijawkisha, Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali la kwanza kwamba fedha hazijapatikana, milioni 100 lakini leo tuko Aprili na bajeti yetu inakwisha Juni. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba sisi tunafanya kila linalowezekana kama Serikali kuhakikisha fedha hizo zimefika ili zifanye kazi iliyokusudiwa; na zile nyingine zilizopangwa kwa ajili ya kazi nyingine inayofuata.

Mheshimiwa Spika, la pili, timu ya wataalam itakwenda lini; hili namhakikishia kwa sababu hili sasa nimeahidi kwa niaba ya Serikali, kwamba tutafanya tathmini katika maziwa yetu. Tunaelewa changamoto ambayo sasa vyanzo vya maji vimerekibiliwa, mito mingi inakauka, maziwa yetu mengi yanakauka, mabwawa yetu mengi yanakauka. Kwa hiyo, sisi kama wenye dhamana hii ya kusimamia mazingira, kwa dhati kabisa tumeamua na katika bajeti ya mwaka huu wa fedha inayokuja mtaona jinsi ambavyo tutaanza kushughulikia vyanzo vya maji, kurudisha uhai wa vyanzo vya maji ili viweze kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuahidi kwamba niliyowaahidi kwenye maziwa ambayo nimeyataja kwanza wataalam watakwendwa tena waliobobea kutoka kwenye sekta zote ambao wako *competent* na wataweza kutushauri kama Serikali ili tuweze kuja na mpango sasa madhubuti wa kuhakikisha kwamba maziwa yetu yanaendelea kubaki.

Na. 62

### **Kero za Muungano Zilizopatiwa Ufumbuzi wa Kudumu**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM (K.n.y. MHE. MARYAM SALUM MSABAHA) Aliuliza:-**

Tangu mwaka 2005 kumekuwa na changamoto nyingi katika kero za Muungano:-

Je, mpaka mwaka 2016 ni kero ngapi zimeshapatiwa ufumbuzi wa kudumu?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA Alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 hoja 15 ziliwasilishwa kutafutiwa ufumbuzi. Kati ya hoja 15 zilizowasilishwa ni hoja 11 zimeshapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, Serikali zote mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinaendelea kushughulikia kero za Muungano kadiri zinavyojitokeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud Abdallah, swali la nyongeza

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika nakushukuru, nina maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza; kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameliambia Bunge na kuwaambia

Watanzania kwamba kuna kero 11 ambazo zimeshapatiwa ufumbuzi, naomba Mheshimiwa Waziri ututajie kero zote 11 ambazo tayari zimeshapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, la pili; Mheshimiwa Waziri, Benki Kuu ni chombo cha Muungano na kilianzishwa mwaka 1966 baada ya kuvunjika kwa Bodi ya Sarafu ya Afrika Mashariki yaani *East African Currency Board*. Tangu kipindi hicho gawio la upande wa pili yaani ya Zanzibar imeonekana kwamba gawiwo (*shares*) hilo la upande wa pili hazitolewi kama ambavyo tulivyoweka *shares* zetu.

Mheshimiwa Spika, ni tatizo gani la msingi lililopelekea *shares* zetu za upande wa Zanzibar, kulingana na fedha ambazo tuliziweka, kwamba fedha hizi hazitolewi kama tulivyopangiwa au inavyotakikana kupatiwa sisi kutoka Zanzibar? Kama ni hivyo, sababu hizo ni kwa nini basi isionekane kwamba kuna haja ya haraka kuweza kupatiwa ufumbuzi na fedha hizo kutolewa upande wa Zanzibar, naomba majibu ya haraka.

**SPIKA:** Swali la pili nalikataa kwa sababu halina ufafanuzi, *shares* zipi, kiasi gani kimetolewa, kiasi gani hakijatolewa ambacho ndiyo unakiulizia swali, kwa hiyo swali liko *general* mno, Mheshimiwa Naibu Waziri kwa swali la kwanza majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali ambalo limeulizwa na Mheshimiwa Mbunge la kwanza kama ulivyonielekeza ambapo ameomba kujua hizo kero 11 ni zipi ambazo zimeshapatiwa ufumbuzi naomba kuzisema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kero za Muungano zilizopatiwa ufumbuzi ni:-

(1) Utekelezaji wa sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora.

(2) utekelezaji wa *Merchant Shipping Act* katika Jamhuri ya Muungano na uwezo wa Zanzibar kujunga yaani *International Maritime Organization (IMO)*.

(3) Uvubi kwenye ukanda wa uchumi wa bahari kuu.

(4) Ushiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki

(5) Uwezo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kukopa ndani na nje ya nchi.

(6) Wafanyabiashara wa Zanzibar kulalamika kutozwa kodi mara mbili.

(7) Mfuko wa maendeleo ya Jimbo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(8) Ongezeko la gharama za umeme kutoka *TANESCO* kwenda *ZECO*.

(9) Ushiriki wa Zanzibar na Taasisi za Kimataifa

(10) Ajira ya Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano.

(11) Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia. Ahsante.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Katiba na Sheria, swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini.

Na. 63

**Kukarabati Mahakama za Mwanzo za Mahenye,  
Igominyi-Njombe**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** Aliuliza:-

Jimbo la Njombe lina Mahakama ya Mwanzo moja tu iliyopo Njombe Mjini.

Je, Serikali ipo tayari kukarabati Mahakama za Mwanzo za Mahenye na Igominyi ili wananchi waweze kupata huduma hiyo jirani?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Sheria na Katiba, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto kubwa zinazoikabili Mahakama ni uhaba na uchakavu wa miundombinu. Sehemu nyingi nchini hazina majengo ya Mahakama na baadhi ya majengo yaliyopo ni chakavu na ni ya muda mrefu. Aidha, ni kweli kwamba Mahakama za Mwanzo za Igominyi na Mahenye ni chakavu sana kiasi cha kushindwa kuendelea kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, mpango uliopo ni kujenga majengo mapya na siyo kukarabati yaliyopo, hasa ikizingatiwa kuwa majengo haya yapo kwenye hifadhi ya barabara. Ni kweli Mahakama hizi zinahitajika sana na ni moja ya miradi ya kipaumbele katika ujenzi wa Mahakama za mwanzo katika Wilaya ya Njombe. Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017 kipaumbele ni ujenzi wa Mahakama ya Mkoa na kwa mwaka 2017/2018 imepangwa kujengwa

Mahakama ya Mwanzo Mahenye-Uwemba; na Mahakama ya Mwanzo Igominyi imepangwa kujengwa katika mwaka 2019/2020 kulingana na upatikanaji wa fedha.

Pamoja na hayo, Mahakama imeshapata nafasi katika Ofisi ya Kijiji cha Uwemba kwa ajili ya kuendesha shughuli za Mahakama ya Mwanzo Mahenye ili huduma iendelee kutolewa wakati mipango ya ujenzi inaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwalongo ameridhika, swalii la nyongeza Mheshimiwa Mwalongo. (*Kicheko*)

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi. Nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Pamoja na Mahakama hiyo lakini iliko tatizo kubwa sana la Mabaraza ya Kata. Mabaraza ya Kata yamekuwa ni mwiba mchungu sana kwa wananchi katika maeneo mbalimbali na hasa hasa katika Jimbo la Njombe. Kinachosababisha, moja; ni kukosa weledi. Je, Serikali sasa ipo tayari kuajiri mtaalam mmoja mmoja katika Mabaraza ya Kata ili asaidiane na wale wananchi wanaokuwa wajumbe wa Mabaraza haya ili kupunguza matatizo yanayojitokeza kwa kukosa utaalam?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; je, Serikali ipo tayari kutoa mafunzo kwa wajumbe wa Mabaraza haya ya Kata ili kusudi wanapofanya kazi zao za kusuluuhisha migogoro mbalimbali kwa wananchi wawe na uelewa? Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kuhusiana na kuongeza idadi ya watumishi katika mabaraza ya kata. Nimhakikishie tu kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI imekuwa ikifanya kazi nzuri katika kuyasimamia mabaraza haya na lengo kubwa ni kuhakikisha kwamba Mabaraza haya ya Kata pamoja na Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya pamoja na mahakama zetu zote zinasogeza huduma karibu zaidi na wananchi kwa kuwa na miundombinu,

vitendea kazi, lakini pia kuwa na watumishi wa kutosha kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba tunalipokea, tutalifanyia kazi na Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, katika swalı lake la pili, kwamba, endapo Serikali tupo tayari kutoa mafunzo kwa watendaji hawa katika Mabaraza ya Kata; nimhakikishie ndiyo na Ofisi ya Rais TAMISEMI imekuwa ikifanya hivyo kila mara ili kuhakikisha kwamba wanaenda na wakati, wanafahamu sheria na masuala mengine wanayosimamia.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Nakushukuru sana kwa majibu mafupi, nilikuona Mheshimiwa Rashid Shangazi, swalı la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo lillipo Njombe linafanana kabisa na tatizo lillipo katika Kata ya Mtae Jimbo la Mlalo Wilayani Lushoto. Je, ni lini Serikali itayakarabati majengo yale machakavu ya Mahakama ile ya mwanzo Mtae?

**SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi, Mheshimiwa Waziri kweli atafahamu Mtae huko? Mheshimiwa Waziri wa Nchi, majibu tafadhali

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwanza kabisa nimhakikishie tu kwamba, azma ya Serikali kupitia Mahakama ni kuhakikisha kwamba tunasogeza huduma za mahakama karibu zaidi na wananchi. Ukiangalia tu katika mwaka huu wa fedha ambao tunaumaliza Serikali ilitenga zaidi ya Shilingi bilioni 46.5 na hata katika mwaka huu wa fedha ambayo bajeti yake tunaanza nayo zaidi ya Shilingi bilioni 18.1 pia zimetengwa kwa ajili ya kujenga mahakama mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalionaa suala hili, tutakwenda kuliangalia;

lakini katika mahakama ambazo ziko katika utaratibu kwa mwaka huu tunaomalizana nao ni ujenzi wa Mahakama Kuu, Tanga ambako na yeye pia anatoka, tunakamilisha ukarabati huo. Vile vile tunakamilisha ukarabati katika Mahakama Kuu, Dar es Salaam lakini pia tunaanza ujenzi katika Mahakama Kuu, Mara pamoja na Kigoma na vile vile tunakamilisha ujenzi wa Mahakama za Wilaya Bagamoyo, Kigamboni na M kuranga.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mahakama za Mwanzo tunakamilisha ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Kawe pamoja na Kinyerezi, vile vile katika mwaka huu wa fedha, zaidi ya Mahakama za Mwanzo 10 zitaweza kujengwa na kukarabatiwa.

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Moshi Suleiman Kakoso, Mbunge wa Mpanda vijijiini, Mheshimiwa Kakoso tafadhali

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba swali namba 64 lipate majibu, lakini kabla ya kujibwa naomba marekebisho madogo ya swali kama lilivyooneshwa hapo, naomba isomeke, Serikali iliahidi kujenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mpanda hadi Uvinza, si kama ilivyo hapo.

Na. 64

### **Barabara ya Mpanda-Uvinza**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** Aliuliza:-

Serikali iliahidi kujenga Barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mpanda hadi Uvinza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi huo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA  
MAWASILIANO** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijiini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya kutoka Mpanda hadi Uvinza yenyewe urefu wa kilometra 194. Katika kutimiza azma hiyo, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara ya Mpanda – Uvinza – Kanyani yenyewe urefu wa kilometra 256. Aidha, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania imesaini mkataba wa ujenzi kwa kiwango cha lami mwezi Julai, 2016 kwa sehemu ya Mpanda hadi Usimbili (Vikonge) yenyewe urefu wa kilometra 35 na Mkandarasi, Kampuni ya *China Railway Seventh Group* kutoka *China* ameanza kazi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na jitihada za kutafuta fedha za kuendelea na ujenzi wa sehemu iliyobaki ya kutoka Usimbili hadi Uvinza yenyewe urefu wa kilometra 159.

**SPIKA:** Hii shughuli leo hii! Mheshimiwa Kakoso swalii la nyongeza. (*Kicheko*)

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza niishukuru Serikali kwa jitihada ambazo zimefanywa, barabara ile imeanza kujengwa, lakini Serikali iliahidi barabara hiyo inapojengwa ingejengwa sambamba na kilometra 60 za kutoka Uvinza kuja eneo la Mishamo ili ziweze kuendana na kasi ya Mheshimiwa Rais na vile vile llani ya Chama cha mapinduzi. Je, ni lini eneo hilo la kipande cha kilometra 60 kutoka Uvinza kuja Mishamo kitaanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; kwa kuwa ujenzi wa barabara ulishaanza, tayari Serikali imetathmini wale ambaao wamefuatwa na barabara. Ni lini wale ambaao walioathirika kwa kufuatwa na barabara wataanza kulipwa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Edwin Amandus Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tuliahidi kwamba tungejenga kuanzia Uvinza na vile vile kuanzia huku ambako tumeanzia na nimuhidi tu kwamba, madam tumeanza kupata hizi fedha kwa ajili ya upande mmoja, tumeona tuanze hii wakati tunaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ule upande wa pili. Nimhakikishie mara tu tutakapozipata fedha tutatekeleza ahadi tulioitoa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watu ambaao wameifuata barabara; nimhakikishie tu Mheshimiwa Selemani Kakoso na wananchi husika kwamba watu wote walioifuata barabara hawatalipwa fidia na wale wote ambaao barabara imewafuata watalipwa fidia; na taratibu za kuwatambua zilishafanyika na nimhakikishie kwamba hilo totalitekeleza.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, swalii la nyongeza.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika ahsante kwa kunipa nafasi. Tatizo la ujenzi wa barabara liliopo Mpanda hadi Uvinza halina tofauti na tatizo la ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami liliopo Mbinga hadi Nyasa. Barabara ile iliahidiwa na Serikali kwamba itajengwa, napenda kujua ni lini sasa ujenzi ule utaanza? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Chikambo, kama ambavyo nilimweleza alipofika ofisini mbele ya Waziri wangu akifuatilia utekelezaji wa barabara hii akiongozana na Mheshimiwa Stella Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kwamba barabara hii inaanza kujengwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu kwamba tumechelewa katika taratibu za *Procurement* kwa sababu nafahamu fedha zinazotarajiwa kujengea barabara hii zinatoka *African Development Bank* na kwamba wao wana utaratibu wao wa *Procurement*, ni lazima tuufuate. Tumechelewa lakini tutahakikisha mara tutakapokamilisha taratibu za *Procurement* barabara hiyo itaanza kujengwa.

**SPIKA:** Waheshimiwa bado tupo Wizara hii hii, swali linaulizwa na Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufu, Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Silafi.

Na. 65

**Kujenga Barabara Zinazounganisha Mkoa wa Rukwa Kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. ALLY K. MOHAMED (K.n.y. MHE. SILAFU J. MAUFI)**  
Aliuliza:-

Rukwa ni mionganini mwa Mikoa inayozalisha mazao ya chakula hasa mahindi na mpunga kwa wingi na hivyo kusaidia upatikanaji wa chakula kwa Taifa. Maeneo mengi ya kilimo katika mkoa huo ikiwemo Bonde la Rukwa yanakabiliwa na changamoto ya barabara mbovu na hivyo wakulima kushindwa kusafirisha mazao yao kwa wakati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara za Kibaoni (Katavi) – Muze (Rukwa) – Kilyamatundu –

Kamsamba (Songwe) hadi Mlowo, Sumbawanga – Muze, Kalambazite – Chambe (Ilemba) na Miangalua – Kilyamatundu (Kipeta) kwa kiwango cha lami ili wakulima wasafirisha mazao yao kwa urahisi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge Viti Maalum wa Mkoa wa Katavi, kama ifuatayyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kibaoni – Kasansa – Kilyamatundu – Kamsamba hadi Mlowo ni mlongoni mwa barabara zinazounganisha Mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe. Barabara hii ni muhimu katika uchumi wa nchi kwa kuwa inapita katika Bonde la Ziwa Rukwa ambalo ni maarufu sana kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Aidha, barabara za Ntendo hadi Muze, Kalambazite hadi Ilemba na Miangalua hadi Chombe hadi Kipeta ni muhimu katika usafirishaji wa mazao ya kilimo katika Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano kwa kutambua umuhimu wa barabara hizi imeanza kuchukua hatua za dhati za kuhakikisha kuwa barabara hizi zinapitika katika majira yote ya mwaka. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017, Serikali ilitenga jumla ya Sh. 3,989,030,000 kwa ajili ya ukarabati na matengenezo ya aina mbalimbali ya barabara hizo pamoja na madaraja yake.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imedhamiria kuanza ujenzi wa Daraja la Momba ambalo linaunganisha barabara ya Sitalike – Kibaoni – Muze – Ilemba hadi Kilyamatundu na Kamsamba hadi Mlowo ambayo ni kiungo muhimu kwa Mikoa ya Katavi, Rukwa na Songwe. Daraja hili limetengewa

jumlah ya Sh. 2,935,000,000 katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 na limeombewa Sh. 3,000,000,000 katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Mikoa ya Rukwa, Katavi na Songwe kuwa Serikali inatambua umuhimu wa barabara hizi kiuchumi na kijamii na inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hizo ili hatimaye zijengwe kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Dah! Hii barabara ndefu kweli yaani Waheshimiwa tutalaumiana bure kwa kweli, hata ninyi wenyewe angalieni tu msitu wa watu, itakuwa ngumu kufanya maamuzi hapa. Mwenye swali lake, Mheshimiwa Ally Keissy. (*Kicheko*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, nakushuku sana. Kwanza naishukuru Serikali kusema kweli kutenga pesa za daraja kiungo muhimu sana kuhusu barabara. Hii barabara ni muhimu inaunganisha mikoa mitatu; Katavi, Rukwa na Songwe, ni muhimu kwa ajili ya wakulima wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka jibu sahihi, ni lini Serikali itakuwa tayari kujenga barabara ya lami katika mwambao wa Ziwa la Rukwa ili wananchi wafaidike? Atoe tarehe maalum, ni lini na mwaka gani? Maana hili daraja litajengwa, barabara inaweza ikaendelea hivyo hivyo kuwa tope wananchi wakateseka. Mwambao kule wanalima sana mazao muhimu sana. Kwa kuwa hii nchi ina njaa kila sehemu, tutakuwa tunakomboa sana wananchi wengine kutockana na mwambao wa Ziwa Rukwa kuwa na ardhi nzuri sana...

**SPIKA:** Mheshimiwa Keissy, hiyo barabara ya mwambao ni ya kutoka wapi kwenda wapi?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, hii barabara inaanzia Mkoa wa Katavi, Kibaoni inakwenda mpaka Songwe kupitia Mwambao wa Ziwa Rukwa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mhandisi Ngonyani.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Ally Keissy ameuliza kwa sauti nzuri. Nikupongeze sana kwa hilo kwa sababu imenitia moyo.

**SPIKA:** Leo ameamka vizuri leo. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Ally Keissy kwamba kama ambavyo nimejibu katika jibu la swali la msingi barabara hizi zote tunazifutia fedha. Nimhakikishie kwamba *procurement* ya kupata mjenzi wa daraja la Kamsamba ambalo ndilo tunaanza nalo ni katika muda wa wiki mbili, tatu zijazo tutakuwa tumeshakamilisha. Ile hela ambayo ilitengwa mwaka huu itatumika na hatimaye mwaka unaofuata kwa hela hizi ambazo tumezitenga ambazo nilieleza toka mwanzo nazo tutakuwa tumekamilisha hii kazi itakuwa imekwisha.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, sasa tunaenda kwenye barabara hizo. (*Makof*)

**SPIKA:** Swali moja la nyongeza. Muuliza swali la msingi CCM, sasa Upinzani, kutoka huko Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, natambua jitihada ambazo zimefanyika kwenye hii barabara ikiwemo ujenzi wa daraja la Mombasa.

Mheshimiwa Spika, nataka tu niulize swali dogo, barabara hii imekuwa katika ahadi, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete mwaka 2009 alipokwenda kwenye Halmashauri ya Mombasa aliweka ahadi ya kujenga hii barabara. Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Pinda alipokwenda kule vilevile alitoa ahadi ya kuhakikisha hii barabara inakamilika kwa sababu hili bonde linaunganisha Mikoa mitatu na ni muhimu kwa mazao yetu.

Mheshimiwa Spika, Rais wa Awamu ya Tano Mheshimiwa John Pombe Magufuli alisema katika Serikali yake hataki kusikia mambo ya michakato, ahadi, tunatafuta fedha, alisema mwenyewe. Watu wa Mikoa wa Songwe, Rukwa pamoja na Katavi tumekuwa tukilia kila mwaka ni kwa nini sasa mwaka huu msiweke *commitment* katika barabara zote mkatenga tu fedha kuelekeza katika Mkoa huu wa Rukwa, hususan hili barabara kutoka Mlowo mpaka Kamsamba na Kilyamatundu kwa kiwango cha lami ili tuache kuwasumbua tena katika kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde, barabara zote ziachwe hata ya Mbande – Kongwa nayo isijengwe kweli? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, nikuhakikishie barabara ya Mbande – Kongwa tunaijenga. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Silinde kwamba daraja la Kamsamba nadhani maswali yake yote ya nyuma yalikuwa yanaelekea hapo. Umeona kwamba sasa hii siyo ahadi tena tunatekeleza, siyo michakato, tunatekeleza. Kabla hujatekeleza taratibu za usanifu, upembuzi lazima zifanyike vinginevyo huwezi ukatekeleza. Kwa hiyo, hatua ya kwanza ya kufanya usanifu wa kina na upembuzi yakinifu tunaianza kwa kutafuta fedha na mara tutakapopata fedha, kazi hii tutaanza. Suala siyo michakato hapa tutatekeleza kama tulivyoahidi. (*Makof*)

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, swali linaulizwa na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia Mbunge wa Kinondoni.

Na. 66

**Vijana Waliojajiri Katika Sanaa Mbalimbali**

**MHE. MAULID S. MTULIA** Aliuliza:-

Taifa lina tatizo kubwa la ukosefu wa ajira rasmi kwa vijana. Vijana wa Jimbo la Kinondoni wameamua kujajiri katika sanaa mbalimbali kama vile maigizo, maonesho ya mitindo na michezo mbalimbali:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongeza vijana hawa vifaa, mitaji na menejimenti ili kuongeza tija katika kazi zao;
- (b) Je, Serikali imefikia wapi katika suala la hatimiliki ili Wasanii, Wanamichezo na Wanamitindo wetu waweze kupata haki zao.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANA NA MICHEZO** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

- (a) Mheshimiwa Spika, nianze wa kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutambua mchango wa sanaa mbalimbali kama sehemu ya chanzo cha ajira kwa vijana wetu kama Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge ambaye amelionesha hilo katika Jimbo lake la Kinondoni. Wizara yangu kwa sasa iko katika mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa, ambapo dhima kubwa ya

mfuko huo ni kusaidia kuinua kipato, kuongeza tija, kukuza uwezo na weledi kuptitia utaratibu wa upatikanaji fedha utakaowekwa na hivyo kuwawezesha wasanii kuzalisha kazi bora za sanaa zenye kukidhi viwango vya masoko ya ndani na ya nje.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki ambacho Mfuko wa Maendeleo ya Sanaa unaandaliwa, Serikali inashauri Halmashauri zote ziwasaidie vijana wanaojishughulisha na sanaa kwa kuwapa mikopo yenye masharti na riba nafuu kwa ajili ya mitaji kutoka kwenye asilimia 10 ya mapato ya kila Halmashauri kwa kuwa sanaa pia ni sehemu ya ujasiriamali na ni chanzo kikubwa cha ajira kwa vijana wetu kwa sasa. Aidha, sekta binafsi, mashirika, Serikali za Mitaa na taasisi mbalimbali zinaombwa kushirikiana nasi katika kuinua, kukuza na kuboresha vipaji kwa wasanii ili waweze kujikwamua kiuchumi.

- (b) Kuhusu Hakimiliki, Wizara yangu kuptitia Bodi ya Filamu, *COSOTA* na *BASATA* zimeendelea kuwaelimisha wasanii wa fani mbalimbali kuzisajili kazi zao ili ziweze kutambuliwa, kupata udhibiti na ulinzi kutokana na wizi wa kazi za sanaa. Aidha, Serikali imeendelea kushughulikia migogoro na biashara haramu ya kudurufu kazi za sanaa ili wasanii waweze kuongeza kipato chao.

Mheshimiwa Spika, haki na maslahi ya wasanii yanalindwa kwa Sheria Na. 7 ya mwaka 1999 ya Hakimiliki na Hakishiriki, Sheria Na. 4 ya Filamu na Michezo ya Kuigiza ya 1976 na Sheria Na. 23 ya Baraza la Sanaa la Taifa ya 1984. Serikali inaendelea na urasimishaji wa tasnia ya filamu na muziki ambapo kazi za wasanii hawa zinawekwa stempu za *TRA* ambazo huwzesha kubaini nakala halisi. Serikali na taasisi zake itaendeleza zoezi la urasimishaji kwa fani nyingine.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtulia, swali la nyongeza.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hivi sasa imekuwa soko holela la kazi za wasanii ambazo zinaingizwa kiujanja ujanja bila kufuata taratibu wala Serikali yetu kupata kodi kwa mujibu wa sheria, pia wasanii wengi wana malalamiko makubwa kwamba kazi zao zinazotumiwa na makampuni ya simu hawalipwi ipasavyo. Vilevile, wasanii wana manung'uniko mengi kwamba kazi zao za sanaa wanapokwenda kuziwa wanadhulumiwa na wanapewa kwa bei chee. Je, ni lini sasa Serikali itaamua kuleta mabadiliko ya sheria hizi ambazo Naibu Waziri amezitaja, Sheria Na. 7 ya Mwaka 1999, Sheria Na. 4 ya Mwaka 1976 na Sheria Na. 23 ya Mwaka 1984. Sheria hizi zote zinaonekana zina miaka mingi haziendi sawa na mabadiliko ya kasi yanayokwenda katika sanaa yetu Tanzania. (*Makofii*)

Swali la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kuambatana nami kwenda kukaa na wasanii ili tuwasikilize matatizo yao na tuweze kushirikiana nao ili kuwapatia ufumbuzi na kuhakikisha kazi zao zinaleta tija kama illiyokuwa kwa wasanii wa nchi nyingine?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri, Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Anastazia Wambura.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema ni kweli kwamba sheria zetu hizi zinazohusiana na usimamizi wa masuala ya sanaa na wasanii kwa ujumla zimepitwa na wakati, kwa sasa tunachokifanya ni kuandaa sera kwanza kwa sababu tulikuwa hatuna Sera ya Sanaa, tulikuwa na Sheria ya Filamu lakini hatukuwa na Sera. Kwa hiyo, kwa sasa tunaandaa Sera ya Filamu na vilevile tunaandaa Sera ya Maendeleo ya Sanaa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilisha sera hizi ambapo Sera ya Filamu tunatarajia kufikia mwishoni mwa mwezi wa Sita tuwe tumekamilisha kuandaa rasimu yake na baada ya kukamilisha sasa tutahuisha hizi sheria ili kusudi ziweze kuendana na wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalii lake la pili; kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru na niseme kwamba tuna kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kuanzisha Idara ya Sanaa katika Wizara yetu. Nia hasa ni kuhakikisha kwamba tunaongeza kasi ya maendeleo ya tasnia ya sanaa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kuambatana naye kwenda katika Jimbo lake, nimekubaliana na hili. Hata hivyo napenda kumjulisha kwamba Wizara yetu imeanzisha utaratibu kupitia utaratibu wa wadau tuzungumze. Kila Jumanne tunaongea na wadau wa sekta zetu nne; Sekta ya Habari, Sekta ya Sanaa, Sekta ya Utamaduni pamoja na Sekta ya Michezo. Kwa hiyo, huwa tunaongea na wadau ili kupata changamoto na kupanga ni jinsi gani tuweze kutatua changamoto hizi.

Mheshimiwa Spika, hivyo nichukue nafasi hii kuwaalika wasanii wote pale ambapo tutakuwa tukizungumzia masuala yao siku ya Jumanne fulani kwa mwezi basi waweze kuhudhuria pale Dar es Salaam na hapa Dodoma. Maalum kwa Jimbo lake la Kinondoni, Wizara yangu iko tayari na binafsi niko tayari kuambatana naye ili tuweze kusikiliza matatizo ya wasanii.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa, kwa sababu ya muda nawaona, lakini tukubaliane kwamba tuendelee muda ni mdogo sana, lakini namuunga mkono Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tukazanie mambo ya sanaa maana inaelekea mpira wa miguu unatupa shida kidogo. Watu wamepoteana uwanjani bao nne! Wakapoteana mjini

wanarudi mafungu mafungu. Namuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu vipi? Anasema hata sielewi kinachoendelea. (*Kicheko/Makof*)

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani.

Na. 67

### **Ugonjwa wa Mnyauko kwa Zao la Nazi**

**MHE. JUMAA H. AWESO** Aliuliza:-

Zao la nazi ni kitega uchumi na chanzo cha mapato kwa wananchi wa Halmashauri ya Pangani lakini zao hili linashambuliwa sana na ugonjwa wa mnyauko ambao umeliathiri zao hilo kwa kiwango kikubwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kufanya tafiti kuhusu ugonjwa huo ili kupata dawa inayofaa ili kuwawezesha wakulima waweze kuendeleza kilimo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge wa Pangani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa kunyong'onyea wa minazi (*Lethal Dieback Disease*) umekuwa ukifanyiwa utafiti kwa zaidi ya miaka 25 na Kituo cha Utafiti Mikocheni. Katika kipindi hicho aina mbalimbali za minazi ya kigeni mifupi na asili mirefu ilichunguzwa ili kuweza kupata minazi yenye ukinzani dhidi ya ugonjwa huo. Aina zote zilionekana kushambuliwa na ugonjwa kwa viwango tofauti. Minazi mirefu kutoka Mkoa wa Tanga na Lindi na aina mbili za minazi mifupi ilionekana kustahimili zaidi kuliko aina zingine ikiwemo aina ya *East African Tall (EAT)*.

Mheshimiwa Spika, aina hizo za minazi inayovumilia ugonjwa huo imepandwa katika shamba la mbegu huko Chambezi na Bagamoyo na mbegu zihauzwa kwa bei nafuu ya shilingi 2,000 kwa wakulima wanaohitaji. Pia Kituo cha Utafiti Mikocheni kinaendelea na uchunguzi wa kubaini wadudu wanaoeneza ugonjwa huu. Aidha, kituo kinaendeleza ushirikiano na taasisi nyingine za Kitaifa na Kimataifa zinazotafiti ugonjwa huu katika kutafuta suluhisho la kudumu la tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, tiba ya ugonjwa huu haijapatikana hadi sasa, hivyo, wataalam wanaelekeza kuzuia ugonjwa huu kwa njia mbalimbali ikiwemo kupanda mbegu zitokanazo na minazi iliyonekana kuwa na ustahimilivu wa ugonjwa; kukata na kuteketeza makuti ya minazi ilioathirika mara dalili za ugonjwa zinapoonekana; kutopanda miche ya minazi iliyooteshwa katika sehemu zeny ugonjwa; kutoruhusu kusafirisha miche ya minazi kutoka sehemu zeny ugonjwa kwenda sehemu zisizo na ugonjwa; kuangalia matumizi mbadala ya minazi mipevu inayokufa kama kutengeneza samani na bidhaa nyingine zeny thamani; na wakulima kuchanganya mazao kwenye mashamba yao ya minazi ili kupata mazao mengine kutoka katika mashamba hayo endapo minazi yao itakufa kwa wingi kutokana na ugonjwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauri Halmashauri ya Wilaya ya Pangani na Wilaya nyingine zilizoathiriwa na ugonjwa huu kuwa na mipango ya kuendeleza zao hili kuititia mipango yao ya maendeleo kwa kuvisaidia vikundi vyta wakulima katika Wilaya zao ziweze kupata mbegu zinazostahimili ugonjwa huu na pia kuanzisha vitalu vyta miche bora ya minazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aweso, Mbunge wa Pangani swali la nyongeza.

**MHE. JUMAA H. AWESO:** Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia suala la minazi ndiyo uchumi na ndiyo maisha ya wananchi wa Pangani. Ukitosha majibu ya

Mheshimiwa Waziri inaonesha ni kipindi cha miaka 25 mpaka sasa wamefanya tafiti lakini hawajajua mdudu ambaye anaeneza ugonjwa huo na wala hakuna tiba kama UKIMWI.

Kwa kuwa, mnazi ndiyo uchumi, je, Serikali haioni haja sasa ya kuangalia nchi ambazo zinalima zao hili la mnazi kwa wingi ili kupata ushauri kujua namna gani tunaweza kuokoa zao hili la mnazi. (*Makofi*)

Swali la pili; naomba sasa nipate *commitment* ya Waziri kwa kuwa tunaona jitihada zinazofanyika mpaka sasa hakuna majibu sahihi yaliyoweza kupatikana. Je, ili kuweza kuwaokoa wananchi wa Pangani kuondokana na umaskini kwa nini wasitupe zao mbadala ili kuhakikisha kwamba badala la mnazi tuwe na zao ambalo linakimu maisha ya wananchi wa Pangani?

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Kilimo, Mifugo na Uvubi, Mheshimiwa William Ole Nasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba imechukua muda mrefu sasa mdudu anayeambukiza ugonjwa huo kuweza kufahamika, lakini zaidi tiba kuweza kupatikana. Wizara na Serikali inaendelea kushirikiana na Taasisi za Kitaifa na Kimataifa ili kuangalia namna ya kutafuta tiba ya ugonjwa huu.

Mheshimiwa Spika, tunashirikiana na Taasisi za nchi zinazoongoza kwa kuzalisha minazi kama nchi za Indonesia, Ufilipino, India na Brazil ili kuangalia namna gani ya kuhakikisha kwamba ugonjwa huu tunautokomeza kama nilivyosema. Kwa sasa tunaangalia namna ya kudhibiti ili usiweze kuleta madhara makubwa zaidi wakati tunaendelea kutafuta tiba.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu Serikali kutafuta zao mbadala; nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge

kwamba Serikali na Wizara inafahamu jitihada ambayo yeye pamoja na Mheshimiwa *DC* Zainab Abdallah wa Pangani wanafanya katika kuleta zao la korosho Pangani. Nilipotembelea Pangani miezi michache iliyopita niliona jitihada kubwa zinazofanywa na Mheshimiwa Mbunge pamoja na *DC* na Halmashauri ili kujaribu kuwashawishi na kuwashimiza wananchi wapande mikorosho kama zao mbadala wakati Serikali inaendelea kutafuta tiba ya ugonjwa wa minazi.

Mheshimiwa Spika, vilevile Serikali inaendelea kuangalia namna gani tunaweza tukahimiza matumizi ya mazao mbalimbali yanayozalishwa na mnazi. Kwa sababu mnazi ndio zao la pekee duniani ambalo hakuna chochote ambacho hakitumiki, kuanzia mizizi mpaka matunda yote inatumika. Kwa hiyo, tunajaribu kuhimiza kwa mfano uchakataji wa mbata ili kuweza kutengeneza mafuta ya kupikia na kujipaka.

Waheshimiwa Wabunge mnafahamu kwamba mafuta ya nazi hayana lehemu katika maana ya *cholesterol* wala hayana mzio katika maana ya *allergy*. Kwa hiyo, tunaangalia uwezekano wa kuendelea kutumia *products* za mnazi kama njia mojawapo ya kuwasaidia wakulima wa minazi.

**SPIKA:** Bado tubakie Tanga, Mheshimiwa Yosepher Ferdinand Komba.

**MHE. YOSEPHER F. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika majibu ya msingi ya Waziri amesema ugonjwa unaotokana na minazi haujapatiwa ufumbuzi. Katika Mkoa wa Tanga, tuna Chuo cha *MAT/Mlingano*, Chuo cha Utafiti. Je, Serikali ina mpango gani wa kukifufua kile chuo ili wakulima wa mazao mengine kama korosho, mkonge, michungwa waweeze kupata uhakika wa mazao yao?

**SPIKA:** Mazao mbadala, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri William Olenasha.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Mheshimiwa Spika, tunafahamu umuhimu wa Chuo na Kituo cha Utafiti cha Mlingano. Mimi mwenyewe katika ziara yangu ya Mkoa wa Tanga nilipata fursa ya kutembelea pale, kuangalia changamoto zilizopo na tayari Wizara iko kwenye mkakati wa kutatua changamoto mbalimbali ambazo tuligundua katika kituo hicho ili iweze kuwasaidia wakulima wa Mkoa wa Tanga na maeneo mengine ya Tanzania katika kuboresha kilimo.

**SPIKA:** Tumalizie maswali mawili yaliyobaki kwa haraka Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Maji na Umwagiliaji Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki.

Na. 68

**Ujenzi wa Bwawa la Yongoma - Same**

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA Aliuliza:-**

Wilaya ya Same ni mionganini mwa Wilaya zinazokumbwa na baa la njaa mara kwa mara na Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi kupeleka chakula cha msaada; na kwa kuwa Wilaya ya Same ina mito mikubwa na maeneo yanayofaa kwa umwagiliaji:-

- (a) Je, Serikali inasema nini juu ya maombi ya muda mrefu yaliyowasilishwa Wizarani ya kujenga Bwawa la Yongoma ili maji yatumike kwa ajili ya umwagiliaji kwenye mashamba yaliyoko katika Kata za Maore, Ndungu, Kihurio na Bendera;
- (b) Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kujenga bwawa hilo ili kuokoa maisha ya wananchi na fedha nyingi za Serikali zinazotumika kununua chakula cha msaada mara kwa mara?

## **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Same Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kutokana na mabadiliko ya tabianchi, nchi yetu imekuwa inakumbwa na upungufu wa chakula katika maeneo machache. Ili kuondokana na hali hiyo, hivi sasa Wizara yangu inafanya mapitio ya mpango kabambe wa Taifa wa Umwagiliaji wa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, bwawa la Yongoma ni bwawa ambalo litakuwa na ukubwa wa kati na litahudumia Kata za Maore na Ndungu. Serikali inashauri bwawa hilo lipewe kipaumbele na Halmashauri husika kama hatua muhimu ya kukabiliana na suala zima la mabadiliko ya tabianchi. Aidha, bwawa la Kalimawe ambalo linahudumia Kata za Kihurio, Bendera, Kalimawe na Ndungu, Wizara inashauri lifanyiwe ukarabati na Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inahusika na ujenzi wa mabwawa makubwa ya kimkakati ambayo yanaweza kutumika kwa shughuli mbalimbali zikiwemo matumizi ya maji ya kawaida ya majumbani, umwagiliaji na uzalishaji umeme. Kwa sasa, Wizara inatekeleza miradi ya mabwawa ya Farkwa (Dodoma), Lugoda (Iringa) na Kidunda (Morogoro Vijiji). Aidha, Wizara imekuwa ikitoa maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kuweka kwenye mipango yake utaratibu wa kujenga mabwawa ya ukubwa wa kati na madogo. Wizara ipo tayari kutoa msaada wa kitaalam utakapohitajika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Mbunge wa Same Mashariki, swali la nyongeza.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kweli nimesikitishwa sana na majibu wa Waziri ambaye naamini ni msomi na najua ni mtaalam wa mambo

ya maji. Nimesikitika sana, kwanza mradi huu ambao uligharamiwa na Serikali ya Japan ulipelekwa Wizarani tangu 2012. Mwaka jana mwezi Novemba nikamwona Waziri nikamweleza, akaniomba nilete ile *proposal* na maombi nikampelekea.

Mheshimiwa Spika, licha ya kwamba hata hakunipa majibu, nashangaa leo akitesha bwawa hili ni dogo ambalo gharama zake 2012 ilikuwa milioni 800 na linahudumia wananchi ambao ni zaidi ya 40,000. Hata hivyo, kibaya zaidi amejichanganya tena na huo mradi wa Kalema *dam* ambao mwenyewe mwaka jana tukiongea juu ya bwawa hili. Nilimweleza wazi kwamba hawa *UN-CDF* wamekuwa tayari kulihudumia bwawa hili, nilichokuwa nimekosa kwenye Halmashauri ilikuwa utaalam.

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa Umoja wa Mataifa, wamekuwa tayari na Serikali ya Norway imeonesha kwamba iko tayari kusaidia mradi huu, leo anajichanganya hapa na kusema anarudisha Halmashauri. Mradi huu wa Kalimawe ni *square kilomita 24*; Je, hilo ni bwawa la kat? Hapo nilikuwa nazungumzia masikitiko yangu. Swali langu ni kwamba kama Waziri aliona hili lingerudishwa kwenye Halmashauri, kwa nini hakunijibu hivyo, tangu mwaka jana Novemba?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Wizara hii kutokana na ripoti ya Mkaguzi wa Ufanisi katika Ujenzi wa Miradi ya Maji Mijini, imeonesha uzembe mkubwa sana na upotevu mwingi wa hela za miradi, kiasi kwamba naamini ndio maana wanashindwa hata kujenga miundombinu ya kumwagilia maji ili wananchi wetu, wakulima waweze kuvuna....

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Spika, nauliza je, kama Wizara inaona haiwezi kufanya mambo ya umwagilaji badala yake walijua kuchakachua tu miradi ya maji, kwa nini wasiachie kazi hiyo au watumishi wake wakafukuzwa? (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji mwenyewe Mhandisi Lwenge, maswali hayo mawili mazito sana.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba jinsi tunavyojibu maswali haya inategemea na namna ulivyouliza. Wewe umeuliza kwamba hili bwawa umeleta maombi kwa muda mrefu, sasa na sisi tunatengeneza majibu kulingana na swali ulilouliza. Kwa hiyo, hatujafanya uzembe wa aina yoyote katika kujibu.

Mheshimiwa Spika, pia naomba nimpe taarifa pia kwamba miradi hii ya mabwawa ya umwagiliaji ilikuwa ina wafadhili mbalimbali ikiwepo *JICA* ndiyo walioweza kufadhili. Hatukuwa tumeiweka katika mipango ya bajeti ya Serikali ambayo sisi tunasimamia moja kwa moja. Sasa maombi yake tumesema kwamba sasa tunafanya mapitio, siyo kwa bwawa lake tu yako mengi nchi nzima, ili tuweze kuona ni namna gani tutayashughulikia.

Mheshimiwa Spika, pia swali la nyongeza la pili, kwamba kuna mradi ambao una uzembe, ambao haridhiki na utekelezaji wake. Naomba atuletee ili tuweze kuona nini kifanyike na kama kuna watu waliofanya uzembe basi tuwachukulie hatua. (*Makofi*)

**SPIKA:** Naona Mheshimiwa Anne Kilango Malecela naye amesimama, aah... samahani kumbe sijamwona vizuri. Sasa tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, swali la Mheshimiwa Deo Ngalawa Mbunge wa Ludewa. (*Kicheko*)

Na. 69

#### **Kulirejeshea Fedha Shirika La Posta Tanzania**

**MHE. DEO F. NGALAWA** Aliuliza:-

Shirika la Posta Tanzania lilitumia fedha zake kuwalipa Wastaafu wa lilitokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kulirejeshea Shirika hilo fedha hizo ili kulinusuru?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Deo Francis Ngalawa, Mbunge wa Ludewa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Shirika la Posta Tanzania lilitumia fedha zake kuwalipa wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki na kuwasilisha madai Serikalini ili lipate kurejeshewa fedha zake. Hadi sasa Shirika limelipa shilingi bilioni 5.9 na Serikali imesharejesha shilingi bilioni 2.7 kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, Novemba, 2016 Serikali ilirejesha Shilingi milioni 700; Desemba, 2016 Shilingi 1,000,000,000; na Januari, 2017, Serikali ilirejesha Shilingi 1,000,000,000. Aidha, Serikali itaendelea kurejesha kiasi kilichobaki cha Shilingi 3,200,000,000 kwa kadri fedha zitakavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Msajili wa Hazina inaendelea na jukumu la kuwalipa pensheni ya kila mwezi wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika Mashariki wapatao 292.

**SPIKA:** Swalii la nyongeza Mheshimiwa Ngalawa.

**MHE. DEO F. NGALAWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Jumuiya ya Afrika Mashariki ilivunjika mwaka 1977, mpaka leo hii ni miaka 40. Shirika hili limekuwa likisucasua sana lakini moja kati ya vigezo inavyolifanya lisuesue ni kwamba hela yake ambayo ilitakiwa iingie kwenye operesheni ndiyo hiyo ambayo inatumika kuwalipa wale wastaafu wa Afrika Mashariki. Je, Serikali ina mpango gani sasa hivi kuanza kuwalipa wale wastaafu yenyewe moja kwa moja bila kutumia fedha za shirika?

Pili, fedha hizi ambazo tayari Shirika la Posta linaidai Serikali ni lini zitakamilishwa kulipwa kwa sababu imefikia kipindi Shirika linasuasua, ikafikia kipindi hata ule mwaka 2016 Shirika hili lilifungiwa akaunti zake kwa sababu *TRA* ilikuwa inalidai sh. 600,000,000. Je, kulikuwa na *fairness* gani ya kufungia zile hela wakati shirika hilo linaidai Serikali shilingi bilioni tano?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza Serikali ina mpango gani wa kulipa yenyewe, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Serikali sasa hivi iko kwenye jitihada za kuhakikisha kuwa malipo haya yanalipwa na Serikali yenyewe na kwa kuwa tayari watumishi wote wa Shirika la Posta wanaendelea kuchangia kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, wastaifu hawa wataendelea kulipwa na Mifuko hii badala ya kulipwa tena na Shirika la Posta.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni lini fedha hizi zitalipwa. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, tutaendelea kulipa kwa kadri fedha zinapopatikana na ni jukumu la Serikali kulipa fedha hizi tunafahamu, tumejipangia mpango itakapofika Juni 30, shilingi bilioni 3.2 zote zitakuwa zimeshalipwa.

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha. Matangazo halafu nitapokea miongozo kama ipo.

Waheshimiwa Wabunge, mtaona kwa kweli wengi hamkupata maswali ya nyongeza kwa sababu ya suala la muda, muda wetu ni mdogo sana na tuko wengi kwa kweli.

Kwa hiyo tuvumiliane kidogo na tutakuwa tukibadilishana hapa mezani kusudi macho yetu yaweze kuona watu tofauti tofauti kadri inavyowezekana.

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu wageni walioko kwenye Jukwaa la Spika ninao wageni maalum kabisa ambaao ni kutoka Ofisi ya Mheshimiwa Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma wakiongozwa na Katibu Mkuu, Utumishi, Ndugu Lauren Ndumbaro, karibu sana. Amefuatana na Katibu Mkuu Ikulu, Ndugu Alphayo Kidata ,hongera sana kwa kuteuliwa. (*Makofii*)

Wengine ni Ndugu Valentino Mlowola, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU na Jaji Harold Nsekela, Kamishna Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, karibuni sana. (*Makofii*)

Pia, tunao Viongozi kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu EngineerMusa lyombe. Yupo Naibu Katibu Mkuu Elimu, Ndugu Benard Makali. Pia yupo Naibu Katibu Mkuu upande wa Afya, Dkt. Zainab Chaula, huyu alikuwa Mganga Mkuu wa Hospitali yetu ya Mkoa hapa Dodoma, hongera kwa kuteuliwa Dkt. Zainab. Pia wameambatana na Wakurugenzi mbalimbali na Wakuu wa Idara zilizo chini ya Ofisi hizo zote mbili. Karibuni sana. (*Makofii*)

Pia niwatambue wageni 13 kutoka *The White Ribbon Alliance for Safe Motherhood in Tanzania* wakiongozwa na Ndugu Dainess Tuni ambaye ni Muuguzi, karibuni sana. (*Makofii*)

Wageni wengine wote ambaao mmekuja hapa Bungeni leo naomba niseme karibuni sana hapa mjengoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada, anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kuhudhuria ibada katika *Chapel* iliyopo jengo la Pius Msekwa ghorofa ya pili leo Jumanne tarehe 18 Aprili, mara baada ya kusitisha

shughuli za Bunge saa Saba mchana. Aidha, Wanamaombi wa Mkoa wa Dodoma watahudhuria ibada hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na shughuli zingine zilizoko mezani

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Katibu hebu niorodheshee majina ya Waheshimiwa Wabunge wanaoomba Mwongozo halafu unipe.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kumtambua pia Naibu Katibu Mkuu Utumishi, Ndugu Suzan Mlawi pale ulipo ahsante sana niwie radhi hawakuwa wameniletea jina lako mapema, karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, pia mtakumbuka kuna Mheshimiwa mwenzetu ambaye aligongwa na bodaboda hapo nje ya geti na akawa ameumia sana, sasa nashukuru kuwatangazieni kwamba amejunga na sisi Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, naomba usimame hapo ulipo. Ahsante sana na karibu tena Bungeni tunakutakia kila la kheri uendelee kupata afya njema zaidi. (*Makofi*)

Sasa tuendelee na miongozo kama nitakavyowataja. Ataanza Mheshimiwa Doto Biteko.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 69 na nitaismwa. Kwanza naomba kutoa hoja ya kuahirisha shughuli za Bunge ili tujadili jambo ambalo nataka kuliombea mwongozo.

Kanuni ya 69 inasema: "(1) Mbunge anayependa mjadala unaoendelea juu ya hoja yoyote uhairishwe hadi wakati wa baadaye, anaweza kutoa hoja "kwamba mjadala sasa uahirishwe" na atataja mjadala huo uahirishwe hadi wakati gani na pia atalazimika kutoa sababu, kwa nini anataka mjadala huo uahirishwe.

Mheshimiwa Spika, siku ya Alhamisi ya terehe 13 Aprili, huko katika Kijiji cha Makengeni Askari wetu nane waliuawa na watu wanaodhaniwa kuwa ni majambazi. Askari hawa walikufa wakiwa wanatekeleza majukumu ya kutulinda raia pamoja na mali zetu. Tukio hili siyo tukio la kwanza katika eneo la Kibiti. Tukio hili vilevile liliwahi kutokea tarehe 21 Februari, 2017 ambapo watu watatu waliuawa akiwemo Mkuu wa Upenelezi wa Wilaya ya Kibiti ambaye anaitwa Peter Kubezya. Askari huyu bahati njema namfahamu vizuri. Alikuwa OCS wa Wilaya ya Bukombe na baadaye akapandishwa akaenda huko Kibiti akauawa na hao watu wanaodhaniwa kuwa ni majambazi.

Mheshimiwa Spika, kama Askari hawako salama kwa kiwango hiki, rai wa kawaida hali yao ikoje? Kwa hiyo, jambo hili limetokea Kibiti lakini linaweza kutokea Kongwa, linaweza kutokea Bukombe, linaweza kutokea mahali pengine popote kama Taifa hatujachukua hatua madhubuti. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba sasa tuahirishe shughuli za Bunge, tujadili jambo hili ili:-

- (1) Bunge kama chombo cha uwakilishi wa wananchi, kije na kauli ya kuitaka Serikali kutoa kauli ya kueleza kwa nini mambo haya yanaendelea kujitokeza na Serikali wakati wote inaendelea kutoa kauli na matukio haya yanaendelea kutokea.
- (2) Sababu ya pili, naomba Bunge hili tujadili ili tuwaondoe wananchi hofu kwa sababu ukweli ni kuwa, wananchi wa Tanzania kwa sasa kwa matukio haya yanayoendelea kutokea wana hofu kubwa juu ya usalama wao na maisha yao na mali zao kutokana na matendo haya.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja tuahirishe shughuli za Bunge, tuweze kujadili jambo hili.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Ahsante sana, nimewaona mnaounga mkono hoja, nitalitolea mwongozo baadaye. Mheshimiwa Chumi!

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru pia kwa kunipa nafasi. Jambo nililokuwa nimeomba kupata nafasi ni hili ambalo Mheshimiwa Doto Biteko ameshalieleza kwa ufasaha na kwa kina. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo kwa Kanuni ya 68(7), isomwe pamoja na Kanuni ya 46(1), inayohusu Waziri anayeulizwa swali atakuwa na wajibu wa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu kama liliyyoulizwa.

Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano alipokuwa anajibu swali la Mheshimiwa Silafu Jumbe Maufi, Mbunge wa Viti Maalum Swali Na. 65, hajalijibu swali hili kwa ukamilifu, bahati nzuri sana alipokuwa anajaribu kuuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Silinde, bado Naibu Waziri hakulijibu swali hili kiukamilifu.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu, suala hili limekuwa likijirudia rudia mara kwa mara kwa Naibu Waziri huyu kutojibu maswali kwa ukamilifu sijui tatizo ni nini. Ameulizwa swali la barabara, amegusia daraja tu, wakati mwingine akiuliza Mbunge swali anasema hata Mbunge mwingine aliniletea.

Mheshimiwa Spika, naomba labda hili suala liweze kutolewa ufanuzi ni kwa nini Waziri anakuwa hajibu swali kikamilifu anapokuwa anaulizwa, hii siyo mara ya kwanza suala hili limekuwa likijirudia mara kwa mara. Ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Lalamiko hilo si lingeletwa na muuliza swal? Mwenye swal lake karidhika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Siko mbali na Mwongozo uliombwa na Mheshimiwa Mbunge wa kwanza na wa pili, Mheshimiwa Cosato Chumi, juu ya kuahirisha shughuli za Bunge kujadili jambo hili la dharura. Suala hili kwa leo tunaomba busara yako itumike na utaratibu zaidi ili suala hili tuweze kupata nafasi ya kuweza kulijadili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninayezungumza pamoja na kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, lakini nimekuomba binafsi kwako kwamba, leo busara itumike zaidi leo, tupatiwe nafasi, tuangalie hali halisi ya usalama wa raia na mali zao.

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Maudhui ya Mwongozo niliotaka kukuomba ameueleza vizuri sana Mheshimiwa Doto Biteko, nadhani tusubiri mwongozo wako. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante Sana. Mheshimiwa Molel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naungana na wenzangu kuhusiana na mwongozo ambao tayari umekwishaombwa. Ningependa tu kukazia na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 14. Kwa hiyo, naungana na wenzangu waliotangulia. Ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsante sana. Miongozo mingine yote tumekwishajibu moja kwa moja, umebakia mmoja wa Mheshimiwa Doto Biteko.

Waheshimiwa Wabunge, nami kwanza niungane na Waheshimiwa wote ambao mmeonesha kuguswa sana na suala la kuuawa Askari wetu kiwango cha kufikia nane kwa wakati mmoja! Kwa kweli, ni jambo ambalo linasikitisha sana. Kwa niaba ya Bunge zima hili ningependa kutoa salamu za pole na rambirambi kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini na kipekee kwa Waziri wa Mambo ya Ndani kwa jambo hili kubwa ambalo limetushtua wote katika nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge, nitoe tangazo kwanza ambalo nimeletewa sasa hivi na Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu, anaomba Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje Ulinzi na Usalama, mukutane saa saba na nusu mchana leo, mtaambiana mahali pa kukutana.

Katika Kikao hicho Kamati hili inakusudia kukutana na Waheshimiwa Mawaziri husika ili kupata taarifa rasmi ya matukio haya ambayo tumekuwa tukiyaongelea hapa na namna ambavyo Serikali imejipanga ili kuyakabili matukio mengine yanayoweza kujitokeza na kuhatarisha hali ya usalama wa Polisi na hali ya usalama wa raia na mali zao. Kwa hiyo, tayari Kamati yetu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama iko *on*. Kama mnavyojua hapa Bungeni *at least* tunaweza kujadili jambo baada ya Kamati yetu kulifahamu kwa undani wake, nashukuru kwamba tayari Kamati sasa imeshaanza kuchukua hatua za kulifuatilia kwa karibu.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii nimruhusu Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa vile yupo, angalau aweze ku-share na sisi kidogo jambo hili ambalo limetokea kwa Askari wake, jambo ambalo ni la kusikitisha sana.

Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Mchemba, karibu sana.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru kwa salamu za pole ulizozitoa kwa niaba ya Bunge lako Tukufu. Niseme tu kwa Waheshimiwa

Wabunge kwamba, jambo lililotoka ni jambo bayo kwa namna yoyote ile na kwa *understanding* ya aina yoyote ile na ni jambo ambalo halikubaliki. Kwa hiyo, niwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa umoja wenu kwa jambo hilo, hasa ikizingatiwa kwamba ninyi ni wawakilishi wa wananchi. Specifically niwashukuru pia Waheshimiwa Wabunge wa kutokea maeneo yale, Mheshimiwa Ally S. Ungando, Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa pamoja na Ndugu yangu Mheshimiwa Abdallah Ulega, Mbunge wa Mkuranga.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu, maelekezo ya namna ya kufanya kazi jambo hili yalishatolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye Kauli yake wakati anamaliza hotuba yake. Jambo hili ni mwendelezo wa mambo yale ambayo yalishatoka na Mheshimiwa Waziri Mkuu akawa ameshatuelekeza. Kwa sababu ya utekelezaji kwamba jambo hili limetoka na utekelezaji wake namna ya kukabiliana ni mkakati, nisingependa kwenda kwenye undani wa kitu gani tunakipanga na umetoka kuweka vizuri kwamba tunaweza tukapata fursa ya kuelezea kwenye Kamati ikawa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, jambo moja tu ambalo ningeomba Waheshimiwa Wabunge mridhie na Kiti chako kiridhie ni kwamba, tangu Kiongozi wetu ametoa maelekezo hayo Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumeweka utaratibu wa namna ya kuwahakikisha wananchi wetu wanaoishi maeneo hayo usalama wa kwao pamoja na mali zao. Wengine walikuwa wanahoji kwamba, wananchi wanakuwaje salama kama Askari wenyewe wameweza kushambuliwa?

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie tu kwamba Askari wetu wamekutana na ajali hiyo wakiwa kazini na kazi waliyokuwa wanaifanya ni ya kuhakikisha kwamba raia pamoja na mali zao wako salama. Mazingira mengine ya kuepuka kuwa-expose sana, kuwaweka sana Askari wetu

katika mazingira ya *risk* kama hayo ni sehemu ya mikakati ya kuhakikisha kwamba tunakomesha uhalifu huo unaowahuhusu raia wetu pamoja na Askari wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kuguswa kwenu, tuwaombe mridhie kwamba, Serikali kama ilivyotolewa kwenye Kauli ya Waziri Mkuu, inalichukulia jambo hili kwa uzito mkubwa na kwa utofauti mkubwa, kuweza kuhakikisha inarejesha hali ya kawaida katika maeneo ambayo uhalifu umekuwa ukijitokeza na kujirudia rudia. Ni uhalifu pamoja na masuala mengine yote ambayo yanaweza yakaweka hofu kwa wananchi wetu hasa yanapotokea kwa kujirudiarudia na kusababisha washindwe kufanya kazi zao wakiwa katika mazingira ya utulivu na uhakika wa kutokuwa na hofu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali inawahakikishia wananchi wa maeneo yale pamoja na wengine wote kwamba, matukio ya uhalifu ya aina hii yaliyotokea ndiyo yametupa chachu zaidi ya kuhakikisha tunapambana na uhalifu ili kuweza kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa katika mazingira salama. Jambo moja tu tunaloomba kwa wananchi, tunawaomba waendelee kutoa ushirikiano kwa vyombo vyetu vya dola kuhakikisha kwamba, jambo la usalama linapewa kipaumbele na linakuwa ni jambo letu sote, Askari pamoja na raia wa kawaida. Wasiogope kutoa taarifa, tumetengeneza mazingira na tutawahakikishia hilo la kuwalinda watoa taarifa ili tuweze kuhakikisha kwamba, hatutoi fursa kwa wahalifu na uhalifu wenyewe kutawala katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niishie hapa, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na niendelee kutoa pole kwa familia za Askari waliopatwa na shida hizo. Walikuwa kazini na Watanzania wote wapenda haki wako pamoja na Askari wetu wanapokuwa mstari wa mbele katika kupigania usalama wa raia pamoja na mali zao hapa nchini kwetu. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kwa kutuhakikishia shughuli inayoendelea. Niwahakikishie na kuwaomba tena Mheshimiwa Doto Biteko na Wabunge wote kwamba, tutulie kwa sasa. Nimezungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu asubuhi, amenihakikishia kabisa kwamba, vyombo vyote vya ulinzi na usalama wa nchi yetu hivi sasa viko kazini, siyo katika maeneo hayo tu, *alert* ni kwa nchi nzima.

Kwa hiyo, tuwape nafasi na Kamati yetu ifanye kazi hii badala ya sisi wote kuifanya kwa sasa. Kama Kamati itaona umuhimu wa jambo hilo bado tupo, tutapeana taarifa, tunaweza bado tukarudi na tukalizungumza ikibidi, hapa mbele. Nawashukuruni kwa kunikubalia. Katibu.

#### **NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

#### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali  
kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Ofisi ya Rais,  
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais,  
Mnejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Mawaziri wa Nchi kadri mlivyojipanga, anayeanza kutoa hotuba, Mheshimiwa George Simbachawene Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, karibu sana kwa hotuba yako. (*Makof*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha tena kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa heshima kubwa nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza nchi yetu vema na utekelezaji makini wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2015. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nawapongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Mbunge, kwa uongozi wao mahiri na kunipatia miongozo na maelekezo mbalimbali ambayo yamesaidia kuboresha utendaji wa kazi katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe na Naibu Spika, kwa uongozi imara na madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia afya njema na hekima katika kuongoza mhimili huu muhimu kwa mandeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, inayoongozwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijiini, kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuongoza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Kamati imepokea na kuchambua kwa kina na hatimaye kupitisha makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 na maoni na ushauri uliotolewa umesaidia Ofisi ya Rais, TAMISEMI kuboresha na kukamilisha bajeti yake kwa muda muafaka na kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa naomba nitoe pole zangu nyingi kwako Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na kiongozi mahiri, aliyewahi kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu, Hayati Samuel John Sitta. Kipekee naomba mnitumie fursa hii kumpa pole nyingi sana Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, kwa kuondokewa na mpendwa wake. Tunakuombea Mungu aendelee kukufariji. Aidha, Bunge lako Tukufu liliondokewa tena Waheshimiwa Wabunge wawili kwa kufariki dunia na aliyefariki ni Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, aliyekuwa Mbunge wa Dimani - Zanzibar na Mheshimiwa Dkt. Elly M. Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum CHADEMA. Taifa limepoteza viongozi muhimu waliokuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie fursa hii kukupa pole wewe Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wote, ndugu wa marehemu, jamaa na wapendwa wote wa karibu kwa kundokewa na wapendwa wao. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa tatu hadi wa ukurasa wa sita wa hotuba yangu, nimetoa hoja ya kuomba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka 2016/2017, pamoja na kuliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha mpango wa bajeti, Ofisi ya Rais ,TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na Halmashauri, pamoja na majukumu ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, hivyo naomba niendelee na ukurasa wa saba.

Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri iliidhinishiwa shilingi triliioni 6.02 kwa ajili ya mishahara, matumizi mengineyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi triliioni 3.78 ni mishahara, shilingi bilioni 646.14 ni matumizi mengineyo na shilingi triliioni 1.6 ni kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo. Hadi Februari mwaka 2017, fedha zilizopokelewa ni shilingi triliioni 3.56 sawa na asilimia 59.1 ya bajeti yote.

Mheshimiwa Spika, maduhuli na mapato ya ndani, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliidhinishiwa kukusanya shilingi milioni 13.5. Hadi Machi, 2017 makusanyo yalikuwa shilingi milioni 14.6 sawa na asilimia 109 ya lengo. Ongezeko hili la maduhuli limetokana na mauzo ya vifaa chakavu na nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, maduhuli ya Mikoa. Kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Mikoa iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya shilingi milioni 330.1 hadi Machi, 2017. Kiasi cha shilingi milioni 868.4 zilikusanywa, sawa na asilimia 263 ya lengo. Ongezeko la makusanyo ya maduhuli limetokana na

kuimarishwa kwa usimamizi na matumizi ya mfumo wa ki-electronic wa ukusanyaji wa mapato, hususan katika hospitali za Rufaa za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani ya Halmashauri; katika mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya shilingi bilioni 665.4 kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato. Hadi Machi 2017 shilingi bilioni 351.7 zimekusanywa sawa na asilimia 52.8 ya lengo. Pamoja na makusanyo hayo kuwa chini kidogo ya lengo, kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la shilingi bilioni 62.6 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 289.1 zilizokusanywa hadi Machi, 2016. Ufafanuzi juu ya ongezeko hili unapatikana katika aya ya 12 ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na makusanyo ya ndani ya Halmashauri, itakumbukwa kuwa mgawanyo wa mapato ya ndani ya Halmashauri ilikuwa ni kwamba asilimia 60 ipelekwe kwenye miradi ya maendeleo na asilimia 40 kwa ajili ya uendeshaji wa Halmashauri. Mgawanyo huu haukuwa rafiki hasa kwa Halmashauri zenye makusanyo madogo na hata kupelekea kushindwa kumudu shughuli za uendeshaji wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo Serikali imeamua kufanya mgawanyo kwa Halmashauri zile zenye makusanyo madogo kutumia asilimia 60 kwa shughuli za uendeshaji wa Halmashauri na asilimia 40 kwa miradi ya maendeleo. Wizara yangu itaandaa orodha ya zile Halmashauri zenye sifa ya kuchangia asilimia 60 kwenye maendeleo na zile zenye sifa za kuchangia asilimia 40 kwenye maendeleo. Orodha hii itaandaliwa kwa kuzingatia hali za kiuchumi, fursa zilizopo na hali ya jumla ya uwezo wa Halmashauri husika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, usimamizi na udhibiti wa matumizi ya fedha kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha 2016/2017, nillifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Halmashauri zote zitaanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato kuanzia

tarehe Mosi Julai, 2016 na kuondokana na matumizi ya stakabadhi za kuandika kwa mkono ili kudhibiti upotevu wa mapato. Hadi Machi, 2017, Halmashauri 177 katil 185, sawa na asilimia 96.2 zinatumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato unaojulikana kama *Local Government Revenue Collection Information System*. Halmashauri nane ambazo ni mpya zitakamilisha ufungaji huo kabla ya tarehe 30 Juni, 2017.

Mheshimiwa Spika, katika usimamizi wa ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na sekta ya afya, mfumo tunaoutumia unajulikana kama *Government of Tanzania Hospital Management System (GoT - HOMIS)* umefungwa katika hospitali 19 za Rufaa za Mikoa na hospitali 43 za Wilaya na Vituo vya Afya 38 na zahanati moja. Mpango wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI ni kuhakikisha kwamba mfumo huu unafungwa katika vituo vyote 5,511 vya kutolea huduma ya afya.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa kumi hadi wa 10 hadi ukursa 14 wa hotuba yangu nimezungumzia shughuli mbalimbali ambazo zimeendelea kufanywa na Ofisi ya Rais TAMISEMI na ukurasa wa 15 hadi wa 18 nimeelezea kwa kina mfumo unaotumika katika ngazi za Halmashauri pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na matumizi ya mifumo hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mifumo hii ipo mifumo mingine ya usimamizi, ukusanyaji na udhibiti ambayo na yenewe inasaidiana na mifumo hii ya ukusanyaji wa mapato. Mifumo hiyo ni *EPICOR 9.05* ambayo inatarajiwa kuboreshwa na mfumo mwingine ni ule wa *Interbank Settlement System (TIS)*ha mifumo mingine kama ya *BEMIS*, *PlanRep* ambayo na yenewe kama nilivyosema katika hizo kurasa kwenye hotuba yangu nimeeleza kwa kina namna ambavyo inatumika na kusaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, dhana ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi (*D by D*) imeimarishwa katika ngazi zote za

Serikali za Mitaa. Wananchi wanashiriki katika kupanga na kufanya maamuzi kuhusu fursa na changamoto zinazowakabili kwenye maeneo yao. Vikao na mikutano ya kisheria vinafanyika ili kutoa fursa ya kufanya maamuzi shirkishi katika kutatua kero za wananchi na kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani katika Halmashauri kwa kutupatia vitendea kazi ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Halmashauri zote zimetakiwa kuwa na mfumo wa udhibiti wa ndani kuhusu matumizi ya fedha na mikataba ya ununuzi.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie usimamizi wa elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ofisi ya Rais TAMISEMI inahusika katika usimamizi wa uendeshaji wa elimu ya awali, msingi, sekondari kwa maana ya kidato cha kwanza hadi kidato cha nne, elimu maalum, elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi. Usimamizi wa elimu ya awali, msingi na sekondari maelezo yake yapo katika ukurasa wa 19 hadi 24 wa hotuba yangu na nimeelezea kwa kina juu ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Aidha, elimu ya awali, msingi nimeelezea katika ukurasa wa 25 hadi 32 ambao tumeelezea pia kwa kina juu ya elimu ya sekondari na elimu maalum.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mafanikio makubwa kuititia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi awamu ya kwanza na ya pili ambao kwa sasa utekelezaji wake upo katika awamu ya tatu. Kuititia mpango huo tumefanikiwa kuwa na vyumba vyaya madarasa ya elimu ya awali katika shule za msingi 14,946 katil ya shule za msingi 16,088 zilizopo sawa na asilimia 93.33.

Mheshimiwa Spika, uandikishwaji wa wanafunzi wa elimu ya awali umeongezeka kutoka 971,716 mwaka 2016 hadi kufikia wanafunzi 1,345,636 mwaka 2017 sawa na

ongezeko la asilimia 38.5. Aidha, jumla ya wanafunzi 4,370 wenye mahitaji maalum wameandikishwa kwenye madarasa ya awali.

Uandikishwaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kwa mwaka 2017 umefikia wanafunzi 1,842,513 ikilinganishwa na wanafunzi 1,896,584 kwa mwaka 2016. Aidha, wanafunzi 6,097 wa darasa la kwanza wenye mahitaji maalum wameandikishwa hadi Machi 2017 ikilinganishwa na wanafunzi 11,356 walioandikishwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017 jumla ya wanafunzi 3,188,149 wameandikishwa kwa darasa la awali na darasa la kwanza; uandikishwaji huu ni sawa na ongezeko la wanafunzi 319,849 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi wa darasa la kwanza kwa mwaka 2016. Hii inatokana na mafanikio chanya ya elimu msingi bila malipo na ndiyo maana tunaposikia wenzetu wakibeza wengine juu ya elimu msingi bila malipo kwamba haina tija, hii ndio tija yenye we kwamba wamejitokeza wananchi wengi na ni kwa sababu ya kuziondoa zile gharama ambazo wazazi walipaswa kuzilipa kabla wanapowaandikisha watoto wao. Hii imipelekea watoto wengi kupatikana na kuleta kwenye shule na ndio maana idadi imekuwa kubwa, kubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kutoa ufanuzi wa utofauti kati ya elimu msingi bure na elimu msingi bila malipo. Serikali inatoa elimu msingi bila malipo na sio elimu msingi bure. Waraka wa Elimu Namba Sita umetoa ufanuzi wa kina juu ya majukumu na wajibu wa kila mda. Imejengeka dhana kwa baadhi ya watu kwenye jamii kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inatoa elimu bure. Napenda kutumia nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi Zisizo za Kiserikali, wadau wengine wa elimu, wazazi na walezi kuendelea kutoa ushirikiano na kuwajibika ili kuhakikisha kwamba baadhi ya changamoto za shule zetu zinashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, si kweli kwamba Serikali kwa kugharamia fedha za uendeshaji wa shule, chakula kwa wanafunzi wa bweni na gharama za mitihani basi wadau, wazazi wabweteke na kujiondoa kabisa katika kuhudumia watoto wao na kushiriki katika kushughulikia changamoto za kujenga madarasa na changamoto za kuwashudumia watoto wao chakula wanapokuwa majumbani mwao, lakini changamoto nyingine za sare na kushiriki katika shughuli zozote zinazoweza kuboresha maeneo ya shule zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wadau mbalimbali ambao wameweza kutoa michango yao katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika shule zetu za awali na msingi.

Mheshimiwa Spika, wapo wadau mbalimbali wa ndani na wa nje ambao wameshiriki katika kusaidiana na Serikali katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Pia wako wadau wengine wa taasisi nyingine kwa kupitia programu mbalimbali na natambua mchango wa *Equip T* waliowezesha utoaji wa mafunzo kwa kuwajengea uwezo Walimu 24,162 na Walimu Wakuu 5,343, Maafisa Mipango katika Halmashauri 51 na kuanzisha vituo vya utayari (*Readiness Centers*) vipatavyo 3,000 kwa watoto wapatao 160,000 walio nje ya shule.

Mheshimiwa Spika, aya ya 37, wadau hao ni Benki ya dunia, Ubalozi wa Sweeden kupitia shirika lao la Maendeleo la Sweden (*SIDA*) na Uingereza kupitia Shirika lao la Maendeleo la Uingereza (*DFAD*) na kupitia programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (*Education Program For Results*). Wamewezesha Serikali kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa kutoa elimu nchini. Kupitia progamu hii Serikali imeweza kulipa madeni ya walimu yasiyo ya mishahara shilingi bilioni 10.5, pia ununuzi wa vifaa maalum vyenye thamani ya shilingi bilioni 4.2, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule za msingi 19 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.7.

Mheshimiwa Spika, katika kupitia mchango wa uimarishaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu

(LANES) Serikali imesambaza jumla ya vitabu 7,435,520 vya kiada vya darasa la kwanza na la pili katika shule za msingi. Usambazaji huu umefanya uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kuwa kimoja kwa wanafunzi watatu kutoka kitabu kimoja kwa wanafunzi saba mwaka 2010. Aidha, fedha shilingi bilioni 5.1 zimepelekwa katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ufuatilaji. Maelezo ya kina juu ya mafanikio haya yanapatikana katika aya ya 36 hadi 41 na ukurasa wa 22 hadi 24 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia kumechangia kuongeza ufaulu kwa mtihani wa Taifa wa darasa la nne kutoka asilimia 88.87 mwaka 2015 hadi asilimia 93.36 mwaka 2016. Aidha, ufaulu katika mtihani wa Taifa wa kumaliza shule ya msingi umeongezeka kutoka asilimia 68.4 mwaka 2015 hadi asilimia 70.36 mwaka 2016. Wanafunzi wote waliofaulu mtihani huo wamechaguliwa kuijunga na kidato cha kwanza mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, elimu ya sekondari; hadi kufikia Machi, 2017, jumla ya wanafunzi 483,072 kati ya wanafunzi 555,291 walichaguliwa kuijunga na kidato cha kwanza sawa na asilimia 86.9 waliokuwa wameripoti shulenii. Aidha, wanafunzi 1,117 wenye ulemavu wamejungu na kidato cha kwanza katika shule zinazoandikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum, sawa na ongezeko la asilimia 41 ikilinganishwa na wanafunzi 648 wenye ulemavu waliojunga katika kidato cha kwanza mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ya utekelezaji wa mpango ya elimu ya sekondari ulihusu uboreshaji wa miundombinu katika shule ya sekondari 540. Kazi zilizofanyika ni ukarabati wa vyumba vya madarasa. Pia kupitia programu ya *Education Program For Results (EP4R)* Ofisi ya Rais, TAMISEMI imefanikiwa kusambaza nakala za vitabu 1,412,832 vya masomo ya historia, jiografia na kiingereza kwa kidato cha kwanza hadi cha nne na vitabu 159,737 ikiwemo 83,189 vya masomo ya sayansi na vitabu 76,548 vya masomo ya sanaa kwa kidato cha tano na cha sita. Kama nilivyosema

kwa sababu ya muda, maelezo yote yanapatikana katika kurasa nilizozinukuu kabla sijaanza kusoma eneo hili.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Disemba, 2016, baada ya utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais la kuhakikisha kila mwanafunzi anakaa kwenye dawati, mikoa yote imejitosheleza kwa madawati na kuwa na ziada. Aidha, kutokana na uandikishaji na usajili wa wanafunzi wa darasa la awali, la kwanza na kidato cha kwanza mwaka 2017 hadi Machi tumekuwa na upungufu wa madawati 302,787 kwa shule za msingi na madawati 204,526 kwa shule za sekondari. Uandikishwaji huu haujawahi kutokea ni mkubwa sana na ni mafanikio makubwa na ndio maana na changamoto zinaibuka tena. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2016 wanafunzi 410,519 walifanya mtihani wa Taifa wa kidato cha pilii ambapo kati yao wanafunzi 372,228 sawa na asilimia 90.67 walifaulu mtihani huo. Kwa upande wa mtihani wa Taifa wa kidato cha nne jumla ya wanafunzi 277,313 walifaulu kati ya wanafunzi 349,324 waliofanya mtihani huo sawa na asilimia 75.99. Aidha, katika mtihani wa Taifa wa kidato cha sita uliofanyika jumla ya wanafunzi 63,528 walifaulu kati ya wanafunzi 65,277 waliofanya mtihani huo sawa na asilimia 98.7.

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Walimu wote wa shule za msingi na sekondari wa nchi hii, wamefanya kazi kubwa na kwa sababu wamefanya vizuri na ndiyo maana hatusikii wakilaumiwa na hivyo basi, tusikie wakiwa wanapongezwa. Kwa niaba ya Serikali naomba niwapongeze sana, tupo nao bega kwa bega na tutahakikisha changamoto zao zinazowakabili tunazipunguza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie elimu maalum; Ofisi ya Rais, TAMISEMI inahusika pia na usimamizi wa uendeshaji wa elimu maalum ambapo shule maalum za msingi zipo 31 na vitengo 156 vya elimu maalum katika shule za sekondari 66. Shule za elimu maalum zinazohudumiwa na

Walimu 1,673 ambao ni wataalam wa elimu maalum katika shule za msingi na sekondari; inategemeana na aina ya ulemavu wa wanafunzi. Serikali imenunua vifaa vyatufundishia na kujifunzia kwa shule maalum vyenye thamani ya shilingi bilioni 4.2 kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ili kuboresha utoaji wa elimu maalum katika kundi hilo.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ni juu ya motisha kwa Walimu ambayo inatolewa lakini kwa sababu ya muda naomba niwapeleke hadi aya ya 54 hadi 55 ukurasa wa 31 na 33 wa hotuba yangu nimeelezea namna tulivyoshughulikia shule zetu zilizoathiriwa na tetemeko la ardhi Kagera.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Sekta ya Afya ya Msingi; katika ukurasa wa 33 hadi 40 aya ya 57 hadi 68 imeelezea shughuli zilizotekelizwa katika Sekta ya Afya zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba nitoe maelezo kwa ufupi katika baadhi ya maeneo muhimu.

Mheshimiwa Spika, uratibu na usimamizi wa huduma ya afya ya msingi unafanywa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Halmashauri zenye Hospitali za Wilaya ni 139 kati ya Halmashauri 184 zilizo sawa asilimia 75.5. Kati ya hospitali hizo 44 zinamilikiwa na sekta binafsi kuititia mashirika ya dini na watu binafsi, vituo vyatufundishia viliyopo ni 771 kati ya vituo 4,420 sawa na asilimia 17.4 kati ya vituo hivyo 535 vinamilikiwa na Serikali. Zahanati zilizopo ni 6,229 kati ya 12,545 zinazohitajika sawa na asilimia 49.7. Serikali kwa kushirikisha nguvu za wananchi inaendelea na ujenzi wa vituo vyatufundishia 244 na zahanati 1,538.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Afya kama nilivyosema, kwa kirefu inapatikana katika kurasa nilizozinukuu na eneo lingine ninalotaka kuligusia ni huduma kwa wazee. Sera inaelekeza wazee watambuliwe kuanzia umri wa miaka 60 na kuendelea ili wapatiwe huduma za afya bila malipo. Hadi mwezi Machi, 2017, jumla ya wazee 346,889 wametambuliwa ambapo kati yao wazee 74,590 wamepata vitambulisho vyatufundishia matibabu bila malipo. Aidha, hospitali za Mikoa, hospitali

za Halmashauri na vituo vyote nchini vya kutolea huduma ya afya vimeelekezwa kuandaa vyumba maalum kwa ajili ya huduma ya wazee. Lengo la Serikali ni kuwapatia wazee wote vitambulisho vya matibabu bila malipo. Hili ni jukumu la Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa kufanya hivyo na sisi Waheshimiwa Wabunge na Madiwani lazima tulisimamie jambo hili.

Mheshimiwa Spika, watu wenyе ulemavu; Serikali inaendelea kuimarisha huduma za watu wenyе ulemavu kwa kuanzisha Kamati Maalum za Watu Wenye Ulemavu katika Mikoa 26 na Halmashauri 184. Nia yetu ya kutimiza matakwa ya Sheria Na. 9 ya Watu Wenye Ulemavu ya Mwaka 2010 na kuwafikia walemvu hadi katika ngazi za msingi kwenye kata, vijiji na mitaa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa Mfuko wa Pamoja wa Afya (*Health Basket Fund*); hadi mwezi Machi, mwaka 2017, jumla ya shilingi bilioni 79.7 kati ya shilingi bilioni 106.26 ziliidhinishwa na zimepelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Asilimia 33.3 ya fedha hizi hutumika kwa ajili ya ununuzi wa madawa na vifaa tiba pamoja na kutoa mafunzo kuhusu usimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, kuanzia Julai 2017, utaratibu umeandaliiwa ili fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja zipelekwe moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ya msingi kwa lengo la kurahisisha ununuaji na upatikanaji wa madawa.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie, kuanzia mwaka huu wa fedha, fedha za *Basket Fund* zitakwenda kwenye hospitali zetu za Mikoa, hospitali za Wilaya, vituo vya afya na zahanati na tumeweka utaratibu wa kuzisimamia huko ili kusitokee lawama ya kusema hakuna dawa kwa sababu watu wameshikilia fedha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nizungumzie Mradi wa Uimarishaji wa Afya ya Msingi kwa kuzingatia matokeo. Kupitia mradi huu utoaji wa fedha kwa ajili ya huduma ya afya utazingatia matokeo (*Result Based Financing*). Fedha zilizotengwa katika

Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni shilingi milioni 535.8, hadi sasa zimetolewa shilingi milioni 443.3 ambazo zimewezesha usimamizi shirkishi. Mikoa ilipokea fedha na kuimarisha vituo vilivyopata alama sifuri katika ngazi za kuvipatia vituo hadhi ya daraja ya nyota (*star rating*). Timu ya wataalam inaendelea kufanya tathmini ya vituo vya afya vitakavyokarabatiwa kupitia mpango huu ambapo kiasi cha shilingi bilioni 71 zitatumika.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie uwezeshaji wa wananchi kiuchumi. Halmashauri zote 184 zimetenga shilingi bilioni 56.8 kutokana na mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake. Hadi kufikia Machi, 2017, fedha zilizopelekwa kwenye mifuko ni shilingi bilioni 15.6 sawa na asilimia 27.5 ya malengo. Fedha hizi zinatumika kwa ajili ya mkopo kwa vikundi vya ujasiriamali vya vijana na wanawake illi kukuza kipato na ajira.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie kwa kifupi usimamizi na uendelezaji wa vijiji na miji. Ukurasa wa 41 hadi 42, aya ya 70 hadi 72 katika hotuba yangu nimeelezea shughuli za usimamizi na uendelezaji wa vijiji na miji.

Mheshimiwa Spika, pia nataka nizungumzie kuhusu Mfumo wa Uboreshwaji wa Uperekaji wa Fedha za Ruzuku katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfumo wa *LGDG* ulioboreshwa pamoja na Mpango wa Upangaji Mipango Shirikishi wa Fursa na Vikwazo, upo katika ukurasa wa 43 na 45 wa Aya ya 73 hadi 74 ambapo tumeelezea fedha zilizopangwa kwa mwaka uliopita na sasa *LGDG* imeanza kutoa fedha kwa kiwango, kwa mfano, Halmashauri zimepelekewa jumla ya shilingi bilioni 58.2 kati ya shilingi bilioni 156 na jumla ya Maafisa 977 wakiwemo Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Maafisa Mipango, Maafisa Maendeleo ya Jamii na Maafisa Utumishi nao wamejengewa uwezo juu ya mpango huu mpya wa kupeleka fedha za ruzuku.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie sekta ya barabara; ukurasa wa 45 hadi 52, Aya ya 75 hadi 87,

nimeelezea juu ya uboreshaji na uendeshaji wa miundombinu ya barabara pamoja na uendelezaji wa miji ya kimkakati. Nitatoa maelezo machache kwa eneo hili kwa sababu ya muda. Mwezi Machi, 2017, shilingi bilioni 142.15 zimepelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kati ya shilingi bilioni 249.7 zilizotengwa. Fedha hizi zimetumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenyе urefu wa kilometa 11,111.57 kwa lengo la kilometa 34,024 zilizopangwa. Maelezo zaidi yanapatikana katika kurasa nilizozinukuu.

Mheshimiwa Spika, katika sekta hiyo ya barabara, tunayo programu ya uboreshaji wa barabara kuititia fedha za Jumuiya ya Ulaya (*European Union*) ambapo urefu wa barabara zenyе kilometa 88.666 kwa kiwango cha lami kwa gharama ya shilingi bilioni 36 kwa Halmashauri katika Mikoa ya Iringa na Ruvuma inaendelea kutekelezwa. Hadi sasa jumla ya kilometa 10.2 zimewekewa tabaka la lami na katika Halmashauri za Wilaya ya Iringa kilometa 9.5 na Mufindi kilometa 0.7 kwa gharama ya shilingi bilioni 10.23.

Mheshimiwa Spika, pia kwenye sekta hiyo tuna mradi unaoitwa *Road Transport Policy Support Program, phase two* ambao na wenyewe unaendelea kutekelezwa katika kujenga kilometa 121.6 kwa gharama ya shilingi bilioni 10.8 kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, pia ipo programu nyingine ya Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID*) kuititia Programu ya *Feed the Future* Awamu ya Pili, tunatekeleza mradi wa ukarabati wa kilometa 304 kati ya kilometa 1,000 za barabara zilizopo kwenye mpango katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Kiteto, Mvomero na Kilombero. Lengo la mradi ni kuboresha usafiri kwenye njia za barabara katika maeneo yanayozalisha mazao ya chakula kwa wingi.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili la miundombinu kuna mradi wa uendelezaji wa miji ya kimkakati ambao unatekelezwa katika Miji yetu Mikuu yote nchini ikiwemo na Mtwara Mjini na Dodoma Manispaa.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie sasa programu ya kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Miji 18, nayo ni katika sekta hiyo hiyo ya miundombinu. Katika Miji midogo 18 iliyopo katika mikoa mbalimbali tumepanga kujenga jumla ya kilometra 220 za barabara ambazo zimesanifiwa kwa kiwango cha lami ambapo kilometra 31.28 zimejengwa na kilometra 51.17 zinaendelea kujengwa. Aidha, ujenzi wa stendi ya mabasi, vituo vyatia maegesha na machinjio ya kisasa vipo katika hatua mbalimbali katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hilo la miundombinu kuna Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (*DMDP*); katika kutekeleza mradi wa *DMDP*, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeweza kuingia mkataba wa Wataalam Washauri wa mradi kufanya tafiti za kina, usanifu wa barabara za mitaa na uhuishaji wa maeneo ya makazi yasiyopimwa katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, usanifu wa mifereji ya maji ya mvua kilometra 32.8 na udhibiti wa taka ngumu umefanyika katika Halmashauri za Manispaa za Dar es Salaam. Ujenzi wa miundombinu ya barabara zenyenye jumla ya kilometra 15 katika maeneo ambayo hayafikiki tumeanza kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, programu nyingine, hizo tumeelezea kwenye ukurasa wa 53 hadi 57 wa hotuba yangu, lakini pia aya ya 88 na 85 nimetoa maelezo ya kina juu ya programu mbalimbali zinazotekelizwa. Programu nyingine ni kama Programu za Maboresho ya Fedha za Umma, maelezo kwa kirefu yako kwenye Hotuba yangu lakini Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo ambapo sasa kupitia utekelezaji wa programu hii idadi ya Maafisa Ugani imeongezeka kutoka wataalam 3,326 hadi 13,532 katika kipindi kinachoishia Desemba, 2016. Ukarabati wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji umeongezeka eneo linalomwagiliwa kutoka hekta 264,388 hadi hekta 463,615. Maelezo zaidi yapo katika ukurasa niliyonukuu.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Mifugo; nchi yetu inakadiriwa kuwa na jumla ya kaya 1,745,776

zinazojishughulisha na shughuli za ufugaji pekee na kaya 4,901,837 zinazojishughulisha na shughuli za kilimo na mifugo. Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya ufugaji na maelezo zaidi nimeeleza katika aya nilizozinukuu.

Mheshimiwa Spika, programu ya maji na usafi wa mazingira; hadi Mwezi Machi, 2017, shilingi bilioni 62.5 zimepelekwa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji kupitia Programu Ndogo ya Maji Vijiji na Usafi wa Mazingira. Miradi ya maji iliyotekeliza na kukamilika ni 1,301 kati ya 1,810 iliyokuwa imepangwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa programu ya Serikali kwa kutumia shilingi milioni 180 kwa ajili ya kutekeleza kampeni ya Taifa ya Usafi wa Mazingira na Maji na imehusisha kutoa elimu na ukarabati wa vyoo katika shule 139. Maelezo zaidi ya programu hii ya maji na *details* zake zimeelezwa katika kurasa nillizozinukuu.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie sasa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI; sehemu ya tatu ya hotuba yangu, ukurasa wa 58 hadi 62, Aya ya 96 hadi 103 nimetoa kwa kina taarifa ya fedha pamoja na shughuli mbalimbali zinazotekeliza na taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais TAMISEMI yaani Shirika la Elimu Kibaha, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Tume ya Walimu, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa (*LAPF*) na Shirika la Masoko ya Kariakoo.

Mheshimiwa Spika, nzungumzie kidogo Tume ya Utumishi wa Walimu; ili kuiwezesha Tume ya Utumishi wa Walimu kutekeleza majukumu yake, Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Tume ilitengewa shilingi bilioni 10.04 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, hadi Machi 2017 Tume imepokea shilingi bilioni 3.9 sawa na asilimia 39.7 ya bajeti. Kazi zilizofanywa ni kuendesha vikao vya kisheria ambapo mashauri ya nidhamu 242 yamehitimishwa kwenye ngazi ya Wilaya.

Mashauri 303 yamefanyiwa uchunguzi, Walimu 1,885 wamesajiliwa na Walimu 2,565 wamethibitishwa kazini,

Walimu 1,597 waliojiendeleza wamebadilishwa vyeo, Walimu 2,800 wamepewa vibali nya kustaafu kazi na Walimu wa mikataba 102 wameandaliwa mafao yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine iliyofanyika ni uchambuzi na upangaji wa majalada ya wazi na siri na Walimu 301,480 pamoja na kuandaa mpango mkakati wa taasisi. Maelezo ya taasisi zilizoko chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa kirefu yatapatikana katika kurasa ambazo nimezinukuu.

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie Mpango wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Maandalizi ya Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, yamezingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo Endelevu ya Maendeleo 2016-2030, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaolenga kujenga uchumi wa viwanda na mwongozo wa Kitaifa kuhusu Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/2018, Ofisi ya Rais, TAMISEMI itaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali katika ngazi ya Wizara, Taasisi, Mikoa na Halmashauri kama ilivyoainishwa ndani ya hotuba yangu katika ukurasa wa 63 hadi 67.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha ujao wa 2017/2018, malengo mapya yatakayotekelezwa katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI na taasisi zilizoko chini yake ni kama ifuatavyo:-

Kuimrisha utoaji wa huduma ya afya lishe ambapo Halmashauri zote nchini zimetenga shilingi bilioni 11.4 ambayo ni sawa na shilingi 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano, hii ni kwa ajili ya huduma ya chanjo na lishe. Vilevile wadau wa maendeleo na mashirika yasiyo ya Kiserikali yametenga kiasi cha shilingi bilioni 26.48 kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Kitaifa wa Afya za Lishe.

Mheshimiwa Spika, mpango mwingine mpya ni uanzishwaji wa Wakala wa Barabara za Vijiji; kuanzia mwezi Julai mwaka 2017, Ofisi ya Rais, TAMISEMI inatarajia kuanzisha Wakala wa Barabara Vijiji ambao utakuwa na jukumu la kufanya tathmini ya mtandao wa barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa na kusimamia matengenezo ya barabara hizo kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, wadau mbalimbali walishirikishwa na kutoa maoni ambayo yamesaidia kuboresha muundo wa chombo hicho ambacho katika kuboresha usimamizi wa barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa, fedha za utekelezaji wa majukumu na wakala zitatokana na bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mpango mwingine ni mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi (*Decentralized Climate Finance Project*). Kwa kutambua athari ya mabadiliko ya tabia nchi, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uingereza (*UKAID*) kupitia Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo (*International Institute for Environment and Development*) na Shirika Lisilo la Kiserikali la *Haki Kazi Catalyst* itatekeleza mradi wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, lengo la mradi ni kuibua na kutekeleza miradi ambayo itasaidia kupunguza au kuondoa athari za mabadiliko ya tabianchi katika Halmashauri. Katika Mwaka wa Fedha 2017/2018, mradi huu utaanza kutekelezwa kwa Halmashauri 12 zilizoathirika kwa kiwango kikubwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi kwa gharama za shilingi bilioni mbili.

Mheshimiwa Spika, shukrani; naomba kumalizia Hotuba yangu kwa kuwashukuru wadau wa maendeleo ambao wameendelea kushirikiana nasi katika kutekeleza programu za miradi mbalimbali katika Sekta za Afya, Elimu, Maji, Barabara, Fedha, Kilimo, Maboresho ya Mfumo wa Serikali za Mitaa. Wadau hao ni Benki ya Dunia, Benki ya

Maendeleo ya Afrika, Shirika la Maendeleo la Uingereza, Jumuiya ya Nchi za Ulaya, Shirika la Maendeleo ya Japani (*JICA*), Shirika la Maendeleo ya Canada (*CIDA*), *UNFPA*, *UN HABITAT*, Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (*BTC*), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (*GIZ*), Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID*), Shirika la Maendeleo la Sweden (*SIDA*), *UNICEF*, *UNDP* pamoja na nchi zote zinazochangia kuititia Mfuko wa Pamoja wa Kusaidia Bajeti ya Serikali. Ofisi yangu itaendelea kushirikiana na wadau wote wa maendeleo wa ndani na nje ili kutimiza azma ya kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatambua kazi kubwa inayofanya na viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge wa Kisarawe kwa kazi nzuri anayoifanya na kutoa mchango wake kwa Taifa hili. Kusema kweli napata msaada mkubwa na nafanya kazi kwa raha sana kwa kushirikiana na Mheshimiwa Jafo. Pia nimshukuru Mhandisi Mussa lyombe, Katibu Mkuu; nimshukuru Ndugu Benard Makali, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Masuala ya Elimu; na Dkt. Zainab Chaula, Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Masuala ya Afya. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, aidha, niwashukuru Wakuu wa Idara wote na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Niwashukuru sana Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wote na Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji nchini kwa ushirikiano mzuri wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yetu ya Wizara ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Kibakwe kwa kuendelea kuwa wavumilivu mara zote ninapokuwa mbali nao katika kutekeleza majukumu haya ya Kitaifa, naahidi kuendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote. Aidha, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunipa moyo katika kutekeleza majukumu haya mazito ya kuwatumikia wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa kazi zilizopangwa kufanyika mwaka wa fedha 2017/2018. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinaomba idhini ya kukusanya sh. 773,187,789,615/= . Makusanyo haya yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu na nyaraka, zabuni, faini mbalimbali, marejesho na masurufu ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, makusanyo kwa upande wa Mamlaka ya Serikali za mitaa yanatokana na kodi za ushuru mbalimbali unaotozwa na mamlaka hizo kulingana na Sheria ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa Sura Namba 290. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika jedwali namba 15 katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Bunge lako Tukufu, likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ya jumla ya sh. 6,578,627,470,495/= tu kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa 26 na Halmashauri 185. Mchanganuo wake ni kama unavyoonyeshwa katika jedwali namba 16.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina, makadirio ya matumizi ya fedha ya mafungu 28 chini ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, randama na majedwali ni sehemu ya hotuba yangu. Hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ni [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz)

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Nakushuuru sana Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa hotuba yako nzuri sana ambayo umeitoa kuhusu Wizara hiyo kubwa, pana na nyeti. Tunasema ahsante sana kwa hotuba hiyo.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA GEORGE BONIFACE SIMBACHAWENE (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**I. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha tena kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu. Kwa heshima kubwa nampongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza nchi yetu vyema na utekelezaji makini wa llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015. Vilevile, nawapongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (MB) kwa uongozi wao mahiri na kwa kunipatia miongozo na maelekezo mbalimbali ambayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi katika Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

**2. Mheshimiwa Spika,** napenda kukupongeza wewe mwenyewe na Naibu Spika kwa uongozi imara na madhubuti katika uendeshaji wa shughuli za Bunge. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kuwajalia afya njema na hekima katika kuongoza Mhimili huu muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

**3. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, naomba kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa

inayoongozwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijiini kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa kutosha katika kuiongoza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI). Kamati imepokea, kuchambua kwa kina na hatimaye kuitisha makadirio ya Bajeti ya OR - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2017/18. Maoni na ushauri uliotolewa umesaidia OR - TAMISEMI kuboresha na kukamilisha bajeti yake kwa muda muafaka na kwa ufanisi.

**4. Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa, naomba nitoe pole zangu nydingi kwako wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na kiongozi mahiri aliyewahi kuwa Spika wa Bunge hili Tukufu, Hayati Samuel John Sitta. Kipekee naomba nitumie fursa hii kumpa pole nydingi sana Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta (Mb.) kwa kuondokewa na mpendwa wake, tunamwomba Mlangu aendeleee kukufariji. Aidha, Bunge lako Tukufu liliondokewa tena na Waheshimiwa Wabunge wawili kwa kufariki Dunia. Waliofariki ni Mheshimiwa Hafidhi Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Diani, Zanzibar na Mheshimiwa Dkt Elly M. Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum - Chadema. Taifa limepoteza viongozi muhimu waliokuwa na mchango mkubwa kwa maendeleo ya nchi yetu. Napenda kutumia fursa hii pia kukupa pole wewe Mheshimiwa Spika, waheshimiwa Wabunge wote, ndugu wa marehemu, jamaa na wapendwa wao wote wa karibu kwa kuondokewa na wapendwa hawa. Mwenyezi Mungu azilaze Roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**5. Mheshimiwa Spika**, kutokana na taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Mwenyeekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya OR - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2016/17. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Mpango na Bajeti ya OR - TAMISEMI Fungu 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 02 pamoja na mafungu 26 ya Mikoa kwa mwaka wa fedha 2017/18.

## **Majukumu ya OR-TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**6. Mheshimiwa Spika, OR - TAMISEMI inatekeleza majukumu yafuatayo:-**

- i) Kusimamia utekelezaji wa Sera ya Ugatuaji Madaraka (D byD), Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maendeleo Mijini na Vijiji;
- ii) Kuziwezesha Tawala za Mikoa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;
- iii) Kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria;
- iv) Kuratibu shughuli za utoaji wa huduma mijini kama vile usafiri na usafirishaji, upatikanaji wa maji safi na usafi wa mazingira;
- v) Kusimamia shughuli za Tume ya Utumishi wa Walimu;
- vi) Kusimamia shughuli za Elimu ya Msingi na Sekondari;
- vii) Kujenga uwezo wa watumishi wa OR – TAMISEMI ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi; na
- viii) Kusimamia utendaji wa Mashirika, Taasisi, Programu na Miradi iliyopo chini ya OR - TAMISEMI.

**7. Mheshimiwa Spika, majukumu yanayotekelawa na Mikoa ni kama ifuatavyo:-**

- i) Kuhakikisha kunakuwepo amani, usalama na utulivu katika Mikoa na Wilaya;
- ii) Kusimamia na kuratibu shughuli zote za maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iii) Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitekeleze majukumu yake kwa ufanisi;
- iv) Kufuatilia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali zinazotekelawa na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo yake;
- v) Kuratibu usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vi) Kusimamia uendeshaji wa Afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; na

- vii) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi utawala.

**8. Mheshimiwa Spika,** majukumu yanayotekelawa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:-

- i) Kudumisha amani, usalama na utulivu katika maeneo ya Serikali za Mitaa;
- ii) Kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa wananchi wake;
- iii) Kutekeleza shughuli za maendeleo yanayolenga katika kuboresha huduma za kijamii na kiuchumi katika maeneo ya Serikali za Mitaa;
- iv) Kupanga mipango ya maendeleo endelevu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia Sera za Kitaifa zinazolenga kuwepo kwa mipango ya maendeleo Vijiini na Mijini;
- v) Kuchukua hatua madhubuti za kulinda na kuendeleza hifadhi ya mazingira katika Serikali za Mitaa;
- vi) Kuendeleza Sera ya Serikali ya Upelekaji wa Madaraka kwa Umma yanayohusu maeneo ya siasa, fedha, utawala na mahusiano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa;
- vii) Kuhamasisha ushiriki wa wananchi kwa lengo la kuimarissha demokrasia katika maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
- viii) Kukusanya na kusimamia mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kutumia mapato hayo kuwaletea wananchi maendeleo katika sekta za uchumi na kijamii.

**II. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17**

**9. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2016/17, OR - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri iliidhinishiwa **shilingi 6,023,559,414,000.00** kwa

ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **shilingi 3,775,875,780,000.00** ni Mishahara, **shilingi 646,143,942,000.00** ni Matumizi Mengineyo na **shilingi 1,601,540,142,000.00** ni kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo. Hadi Februari, 2017 fedha zilizopokelewa ni **shilingi 3,559,466,814,596.24** sawa na **asilimia 59.1** ya bajeti yote.

#### **Maduhuli na Mapato ya ndani ya OR – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**10. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, OR-TAMISEMI iliidhinishiwa kukusanya **shilingi milioni 13.5**. Hadi Machi, 2017, makusanyo yalikuwa **shilingi milioni 14.6** sawa na **asilimia 109** ya lengo. Ongezeko hilo la maduhuli limetokana na mauzo ya vifaa chakavu na nyaraka za zabuni.

#### **Maduhuli ya Mikoa**

**11. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Mikoa iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **shilingi milioni 330.1**. Hadi Machi, 2017, kiasi cha **shilingi milioni 868.4** zilikusanywa sawa na **asilimia 263** ya lengo. Ongezeko la makusanyo ya maduhuli limetokana na kuimarishwa kwa usimamizi na matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato hususan katika Hospitali za Rufaa za Mikoa.

#### **Mapato ya Ndani ya Halmashauri**

**12. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya **shilingi bilioni 665.4** kutoptana na vyanzo vya ndani vya mapato. Hadi Machi, 2017 **shilingi bilioni 351.7** zimekusanywa sawa na **asilimia 52.8** ya lengo. Pamoja na makusanyo hayo kuwa chini kidogo ya lengo, kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la **shilingi bilioni 62.6** ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi bilioni 289.1** zilizokusanywa hadi Machi, 2016. Ongezeko la makusanyo limetokana na kuimarishwa kwa usimamizi, elimu

na uhamasishaji kwa walipa kodi pamoja na kuongezeka kwa matumizi ya mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo, Halmashauri zote zimeagizwa kuendelea kukusanya mapato ili zifikie malengo yaliyowekwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2017 (**ufafanuzi umeoneshwa kwenye jedwali Na. 1**).

**13. Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu ya mwaka wa fedha 2016/17, nililifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba Halmashauri zote zitaanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato kuanzia tarehe 1 Julai, 2016 na kuondokana na matumizi ya stakabadhi za kuandika kwa mkono ili kudhibiti upotevu wa mapato. Hadi Machi, 2017 Halmashauri **177** kati ya **185** sawa na asilimia **96.2** zinatumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato. Halmashauri **8** ambazo ni mpya zitakamilisha ufungaji wa mfumo kabla ya tarehe 30 Juni, 2017. Halmashauri hizo ni Halmashauri za Wilaya za Mpimbwe, Itigi, Madaba, Kibiti, Bumbuli na Songwe na Halmashauri za Miji za Nanyamba na Mbulu. Vilevile, mfumo wa kielektroniki wa Usimamizi wa Huduma za Afya unaojulikana kama *Government of Tanzania Hospital Management Information System* (GoT-HOMIS) umefungwa katika Hospitali **19** za Rufaa za Mikoa, Hospitali **43** za Wilaya, Vituo vya Afya **38** na Zahanati **1**. Mpango wa OR-TAMISEMI ni kuhakikisha mfumo huo unafungwa katika vituo vyote **5,511** vya kutolea huduma za afya. Mifumo yote hii inalenga kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi na kuimarisha makusanyo ya mapato.

### **Mabadiliko ya Muundo wa OR-TAMISEMI**

**14. Mheshimiwa Spika**, OR-TAMISEMI imekamilisha mapitio ya miundo ya OR – TAMISEMI makao makuu, Mikoa na Halmashauri ambayo iko katika hatua za mwisho za kupitishwa na Mamlaka husika. Mabadiliko ya miundo hiyo yanakusudia kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu. Mabadiliko ya muundo wa OR-TAMISEMI yanalenga kuleta uwajibikaji zaidi wa Mikoa yote, Wilaya zote, Halmashauri zote, Tarafa zote, Kata zote, Vijiji vyote, Mitaa yote na Vitongoji vyote nchi nzima.

## **Usuluhishi wa Migogoro**

**15. Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na migogoro ya mipaka ya kiutawala inayohusisha Kijiji na Kijiji, Wilaya na Wilaya, Mkoa na Mkoa, migogoro kati ya wafugaji na wakulima na watumiaji wengine wa ardhi. Serikali imeunda timu ya wataalamu ambayo inashirikisha Wizara tano ambazo ni Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, OR-TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maji na Umwagiliaji ili kuchambua, kupitia na hatimaye kushauri namna bora ya kumaliza migogoro hiyo. Tayari timu ya wataalam imeleta taarifa yake ambayo hivi sasa inafanyiwa kazi katika ngazi ya Makatibu Wakuu.

**16. Mheshimiwa Spika**, migogoro ya wakulima na wafugaji inatokana na kugombania rasilimali hasa ardhi kwa ajili ya matumizi ya kilimo, ufugaji na maji. Wakati Serikali inaendelea kufanya kazi mikakati mbalimbali ya kutatua migogoro kwa nchi nzima, naomba kutumia nafasi hii kuwaomba wananchi kuzingatia Sheria na Taratibu zilizopo katika utumiaji wa ardhi ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima. Aidha, niwaombe sana viongozi wote katika ngazi zote wasimamie suala hili kwa haki.

## **Ushughulikiaji wa Malalamiko**

**17. Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia kero za watumishi na wananchi, OR – TAMISEMI imeanzisha na kuimarisha Dawati la Malalamiko ambapo kupitia dawati hilo kila Taasisi ina Afisa maalum anayeshughulikia na kuratibu utunzaji wa rejestya ya malalamiko. Utaratibu huu umeimarisha uwajibikaji katika Taasisi zote zilizo chini ya OR –TAMISEMI na kuongeza imani ya wananchi kwa Serikali iliyopo madarakani. Hadi Machi, 2017 OR - TAMISEMI imepokea jumla ya malalamiko **143** kutoka kwa watumishi na wananchi na kuyapatia ufumbuzi kwa wakati.

**18. Mheshimiwa Spika**, dhana ya Upolekaji wa Madaraka kwa Wananchi (D by D) imeimarishwa katika ngazi zote za Serikali za Mitaa. Wananchi wanashiriki katika

kupanga na kufanya maamuzi kuhusu fursa na changamoto zinazowakabili kwenye maeneo yao. Vikao na Mikutano ya kisheria vinafanyika ili kutoa fursa ya kufanya maamuzi shirkishi katika kutatua kero za wananchi na kuboresha utoaji wa huduma.

### **Watumishi wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**19. Mheshimiwa Spika**, tumeendelea kusimamia nidhamu ya watumishi katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao. Watumishi wasio waadilifu na wazembe wameendelea kuchukuliwa hatua kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya watumishi **102** walichukuliwa hatua mbalimbali zikiwemo kufukuzwa kazi, kupewa onyo, kuvuliwa madaraka, kushushwa mshahara, kufikishwa mahakamani na kutakiwa kurejesha fedha zilizopotea. Natoa wito kwa Watumishi wote katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yao kwa weledi na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

### **Udhibiti wa Watumishi Hewa**

**20. Mheshimiwa Spika**, jumla ya watumishi **13,369** ambao ni watoro, wastaafu na waliofariki wameondolewa katika orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali ambapo watumishi **541** walikuwa katika Sekretarieti za Mikoa na watumishi **12,828** katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Watumishi hewa waliobainika wameisababishia Serikali hasara ya **shilingi bilioni 25.4**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi bilioni 2.7** sawa na asilimia **11** zimerejeshwa Serikalini. Ufuatiliaji unaendelea ili kuhakikisha fedha zilizobaki zinarejeshwa pamoja na kuwachukulia hatua waliohusika na upotevu huo.

### **Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**21. Mheshimiwa Spika**, suala la udhibiti wa matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

linasimamiwa na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290, Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, Sheria ya Ukaguzi wa umma ya mwaka 2008, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004, Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake. Sheria hizi zimeainisha ngazi mbalimbali za usimamizi na udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha za Halmashauri. Miogoni mwa Viongozi wanaohusika na usimamizi ni pamoja na Waheshimiwa Wabunge, Baraza la Madiwani, Kamati za Kudumu za Halmashauri, Wizara ya Fedha na Mipango, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Kamati za Bunge za Bajeti, Utawala na Serikali za Mitaa na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Kila ngazi ya uongozi ikitekeleza Wajibu wake ipasavyo, tutaongeza ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha za Umma. OR – TAMISEMI itaongeza ushirikiano na wadau hao ili kuhakikisha inakuwepo mifumo madhubuti ya udhibiti wa mapato na matumizi ya fedha za umma na ongezeko la uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## **Matumizi ya TEHAMA**

**22. Mheshimiwa Spika**, OR – TAMISEMI imefanikiwa kufunga mifumo saba (7) ya TEHAMA ambayo inafanya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mifumo hiyo ni;- Mfumo Funganishi wa Usimamizi na Udhhibiti wa Matumizi ya Fedha (IFMS – EPICOR 9.05), mfumo wa malipo unaojulikana kama “Tanzania Interbank Settlement System - TISS”), Mfumo wa Uandaaji wa Mipango na Bajeti (PlanRep), Mfumo wa Takwimu za Elimumsingi (BEMIS), Mfumo wa Taarifa za shule (SIS), mfumo wa ukusanyaji mapato (LGRCIS) na mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi wa Vituo vya kutolea huduma za afya (GoT-HOMIS).

**23. Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa Uendeshaji na Usimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya umesaидia katika upatikanaji wa taarifa sahihi na kwa wakati kutoka ngazi za kituo, usimamizi wa dawa na vifaa tiba, usimamizi

wa rasilimali watu na mapato yatokanayo na uchangiaji wa huduma za afya.

**24. Mheshimiwa Spika**, Mfumo Funganishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha za Mamlaka za Serikali za Mitaa (*IFMS*) – *Epicor 9.05* umefungwa katika Halmashauri **169** kati ya **185** zilizopo sawa na asilimia **91.3**. Matumizi ya mfumo huo yamesaidia kuongeza uwazi na uwajibikaji katika usimamizi wa fedha za umma, kuboresha utendaji katika kutekeleza bajeti zilizopangwa ili kuondokana na hoja za matumizi nje ya bajeti, kudhibiti uhamishaji wa fedha kutoka mradi mmoja kwenda mwingine kinyume na utaratibu, kurahisisha utendaji kazi katika shughuli za malipo, usuluhisho wa kibenki na kupata taarifa sahihi na kwa wakati.

**25. Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa “Tanzania Interbank Settlement System” (TISS) ambao umeshafungwa katika Halmashauri za Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya, Dodoma, Tanga na Morogoro unasimamiwa na OR - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango. Mikoa iliyobaki itafungiwa mfumo huo katika mwaka wa fedha 2017/18. Mfumo huu unasaidia kuimarisha usimamizi na udhibiti wa malipo kutoka kwenye akaunti ya Halmashauri kwenda kwenye akaunti ya mlipwaji (mteja) na malipo yanafanyika moja kwa moja kutoka kwenye akaunti zilizopo Benki Kuu (BoT). Aidha, kupitia mfumo huo, Serikali ina uwezo wa kutumia fedha zake wakati wowote kupitia akaunti zilizoko Benki Kuu. Mfumo huu unakusudia kuondoa utaratibu wa malipo kwa njia ya hundi ambao siyo salama katika udhibiti wa fedha za umma.

**26. Mheshimiwa Spika**, faida za mifumo ya kielektroniki ni kuongeza ufanisi katika utendaji kazi, kupunguza gharama, kuongeza uwajibikaji, upatikanaji wa taarifa sahihi na kufanya maamuzi kwa wakati. Uwekaji wa mifumo ya kielektroniki upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa na uwekezaji wa miundombinu lengo likiwa ni kuweka mifumo hiyo katika Mikoa na Halmashauri na vituo vyote vya kutolea huduma. Vilevile, matumizi ya mifumo ya TEHAMA imesaidia kupunguza

mianya ya ufujaji na uvujaji wa mapato kwa kuwezesha malipo kufanyika moja kwa moja Benki. Kadhalika, Halmashauri zimeweza kuwa na takwimu sahihi za walipa kodi, kutoa Hati za Madai (Demand Note) kwa kodi na tozo mbalimbali katika ngazi za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**27. Mheshimiwa Spika**, OR - TAMISEMI imekamilisha ufungaji wa Tovuti katika Mikoa 26 na Halmashauri 185 ili kuwawezesha wadau mbalimbali kupata taarifa na kufahamu majukumu yanayotekelawa na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mafunzo yametolewa kwa Maafisa habari na TEHAMA wa Mikoa na Halmashauri zote kuhusu matumizi ya Tovuti hizo ili kuhakikisha zinatumika kwa ufanisi katika kuwahabarisha Watanzania masuala mbalimbali yanayotekelawa na Serikali pamoja na kuimarisha Utawala Bora na kuongeza uwajibikaji.

**28. Mheshimiwa Spika**, Serikali itaendelea kuimarisha Kitengo cha Ulaguzi wa Ndani katika Halmashauri kwa kukipatia vitendea kazi ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Halmashauri zote zimetakiwa kuwa na mfumo wa udhibiti wa ndani kuhusu matumizi ya fedha na mikataba ya ununuzi.

#### **Usimamizi wa Elimu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**29. Mheshimiwa Spika**, OR - TAMISEMI inahusika na usimamizi na uendeshaji wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari (kidato cha I – VI), Elimu Maalumu, Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi.

#### **Elimu ya Awali na Msingi**

**30. Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na mafanikio makubwa kuititia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi Awamu ya Kwanza na ya Pili ambao kwa sasa utekelezaji wake uko katika Awamu ya Tatu. Kuititia mpango huo, tumefanikiwa kuwa na vyumba vyaya madarasa ya Elimu ya Awali katika Shule za msingi **14,946** kati ya Shule **16,088** zilizopo sawa na asilimia **93.33**.

**31.** **Mheshimiwa Spika**, uandikishaji wa wanafunzi wa Elimu ya Awali umeongezeka kutoka **971,716** (Wavulana **480,053** na Wasichana **491,663**) mwaka 2016 hadi kufikia wanafunzi **1,345,636** (wavulana **664,539** na wasichana **681,097**) mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia **38.5** (**ufafanuzi umeoneshwa kwenye jedwali Na. 2**). Aidha, jumla ya wanafunzi **4,337** wenyewe mahitaji maalum wameandikishwa kwenye madarasa ya Awali.

**32.** **Mheshimiwa Spika**, uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza kwa mwaka 2017 umefikia wanafunzi **1,842,513** (wavulana **931,674** na wasichana **910,839**) ikilinganishwa na wanafunzi **1,896,584** mwaka 2016 (**ufafanuzi umeoneshwa kwenye jedwali Na. 3**). Aidha, Wanafunzi **6,097** wa Darasa la Kwanza wenyewe mahitaji maalum wameandikishwa hadi Machi 2017 ikilinganishwa na Wanafunzi **11,356** walioandikishwa mwaka 2016.

**33.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017, jumla ya Wanafunzi **3,188,149** wameandikishwa kwa Darasa la Awali na Darasa la Kwanza. Uandikishwaji huu ni sawa na ongezeko la Wanafunzi **319,849** ikilinganishwa na idadi ya Wanafunzi hao kwa mwaka 2016. Mafanikio haya bado ni matokeo chanya ya utekelezaji wa Mpango wa Serikali wa utoaji wa Elimumsingi bila malipo ambao umetoa fursa kwa watoto wengi kupata elimu. Nawaomba wazazi na walezi wote wahakikishe Wanafunzi wote waliofikia umri wa kujinga na madarasa ya Awali na Darasa la Kwanza wanaandikishwa kuanza Shule kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizopo.

**34.** **Mheshimiwa Spika**, kuna tofauti kati ya Elimumsingi BURE na Elimumsingi bila malipo. Serikali inatoa Elimumsingi bila malipo siyo Elimumsingi BURE. Wananchi wanakuwa wazito kujitolea hata nguvu zao katika kuchangia shughuli mbalimbali zinazohusu elimu kwa kizingizio kuwa Serikali ya Awamu ya Tano inatoa Elimumsingi BURE! Napenda kutumia nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Asasi zisizo za Kiserikali,

Wadau wengine wa Elimu, Wazazi na Walezi kuendelea kutoa ushirikiano ili kuhakikisha uwepo wa miundombinu muhimu ya shule kwa ajili ya wanafunzi wa Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari.

**35. Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwapongeza EQUIP-T waliowezesha utoaji wa mafunzo ya kuwajengnea uwezo Walimu **24,162** kuhusu stadi za uongozi, mfumo wa kukusanya takwimu na kuwapatia "tablets" Walimu Wakuu **5,343**. Wadau hao wametoa pia mafunzo ya kuandaa Bajeti kwa Maafisa Elimu na Maafisa Mipango katika Halmashauri **51** na kuanzisha vituo vya utayari "Readness Centers" vipatavyo **3,000** kwa watoto wapatao **160,000** walio nje ya Shule.

**36. Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia Mpango wa Uimarishaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu "LANES", imepeleka fedha **shilingi bilioni 5.1** katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kote kwa ajili ya ufuatiliaji. Aidha, **shilingi bilioni 18** zitapelekwa katika Shule za Msingi za Serikali nchini kabla ya Julai, 2017 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**37. Mheshimiwa Spika**, Serikali inatekeleza Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (**Education Programme For Results-EP4R**) kwa lengo la kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa kutoa elimu nchini. Programu hii inatekelezwa kwa uhisani wa Benki ya Dunia, Ubalozi wa Sweden (Swedish for International Development Agency-SIDA) na Ubalozi wa Uingereza (*Department for International Development-DfID*). Programu hii mpya inatekelezwa kwa muda wa miaka minne kuanzia 2014/15 hadi 2017/18 kwenye sekta za Elimu ya Msingi na Sekondari.

**38. Mheshimiwa Spika**, kupitia Programu hiyo, Serikali imeweza kulipa madai ya walimu yasiyo ya Mishahara **shilingi bilioni 10.05**, ununuzi wa vifaa vya Elimu Maalum vyenye thamani ya **shilingi bilioni 4.2**, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Shule za Msingi **19** kwa gharama ya **shilingi bilioni 1.75**.

**39. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2017, Serikali kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali, imekamilisha ujenzi wa nyumba za walimu **45,348** kwa Shule za Msingi, hivyo kuwa na upungufu wa nyumba **182,899**. Kwa upande wa Shule za Sekondari, jumla ya nyumba **14,346** zimejengwa, hivyo kuwa na upungufu wa nyumba **69,794**. Vyumba vya madarasa vilivyopo kwa Shule za Msingi ni **120,766** katи ya vyumba **266,872** vinavyohitajika. Aidha, kuna vyumba vya madarasa **39,620** katи ya **52,188** vinavyohitajika kwa Shule za Sekondari. Vile vile, matundu ya vyoo yaliyopo kwa Shule za Msingi ni **167,496** katи ya mahitaji ya matundu ya vyoo **517,606** yanayohitajika na matundu **62,664** katи ya **90,425** yanayohitajika kwa Shule za Sekondari. Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wa maendeleo ili kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia (**ufafanuzi umeoneshwa kwenye jedwali Na.4 & 5**)

**40. Mheshimiwa Spika**, kuboreshwa kwa mazingira ya kufundishia na kujifunzia kumechangia kuongeza ufaulu wa Mtihani wa Taifa wa Darasa la Nne kutoka asilimia **88.87** mwaka 2015 hadi asilimia **93.36** mwaka 2016. Aidha, ufaulu katika Mtihani wa Taifa wa Kumaliza Shule ya Msingi umeongezeka kutoka asilimia **68.4** mwaka 2015 hadi asilimia **70.36** mwaka 2016. Wanafunzi wote waliofaulu Mtihani huo wamechaguliwa kujunga na Kidato cha Kwanza mwaka, 2017.

**41. Mheshimiwa Spika**, Serikali imesambaza Vitabu **7,403,552** vya kiada vya Darasa la Kwanza na la Pili kwa Shule za Msingi ambavyo vimechapwa chini ya Mpango wa Uimarishaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu **"LANES"**. Usambazaji wa vitabu hivyo umesaidia kuboresha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kutoka **1:7** mwaka 2010 hadi **1:3** mwaka 2017. Lengo ni kufikia uwiano wa **1:1** ifikapo Mwaka 2020. OR-TAMISEM inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kufikia azima hiyo ambayo inakusudia kuboresha kiwango cha elimu itakayoleta ushindani na mchango mkubwa katika maendeleo ya viwanda.

## Elimu ya Sekondari

42. **Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya Wanafunzi **483,072** wakiwemo Wasichana **244,707** na Wavulana **238,365** sawa na asilimia **86.9** walikuwa wameripoti shulenii kati ya **555,291** waliochaguliwa kuijunga na kidato cha kwanza (**ufafanuzi umeoneshwa katika jedwali Na. 6**). Aidha, wanafunzi **1,117** wenye ulemavu wamejiunga na kidato cha kwanza katika shule zinazoandikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum sawa na ongezeko la asilimia **41** ikilinganishwa na wanafunzi **648** wenye ulemavu waliojiunga Kidato cha Kwanza Mwaka, 2016.

43. **Mheshimiwa Spika**, Awamu ya Pili ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari ilihuisha uboreshaji wa miundombini katika Shule za Sekondari **540**. Kazi zillizofanyika ni ukarabati wa vyumba vya madarasa **310**, ujenzi wa madarasa mapya **775**, ujenzi wa nyumba mpya za Walimu **183** (Six Multi Unit House) na matundu ya vyoo **6,490**. Jumla ya **shilingi bilioni 65.98** zilitolewa na kutumika kugharamia ujenzi huo na **shilingi bilioni 1.85** zilitolewa kwa ajili ya usimamizi, ufuatiliaji na taratibu za ununuzi. Mradi huo umefikia ukomo wa muda wake tarehe 31 Desemba, 2016 ambapo ujenzi wa miundombini katika shule hizo umekamilika kwa asilimia **100**.

44. **Mheshimiwa Spika**, ili kuboresha upatikanaji wa takwimu za Elimu kwa usahihi na kwa wakati, OR - TAMISEMI imefanikiwa kutoa mafunzo kwa Maafisa Elimu Vifaa na Takwimu **370** kutoka Halmashauri **184** na Maafisa Elimu Taaluma Mikoa 26 kuhusu matumizi ya mfumo wa uingizaji na utoaji wa takwimu kwa njia ya kielektroniki kwa Mwaka wa fedha 2016/17. Lengo ni kuhakikisha kunakuwepo na takwimu sahihi za elimu nchini zitakazowezesha kuandaan mipango na bajeti ya kila mwaka.

45. **Mheshimiwa Spika**, kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo (**Education Programme For Results-EP4R**), OR - TAMISEMI imefanikiwa kusambaza nakala za

vitabu **1,412,832** vya masomo ya Historia, Jiografia na Kiingereza kwa Kidato cha Kwanza hadi cha Nne na vitabu **159,737** vikiwemo **83,189** vya masomo ya sayansi na vitabu **76,548** vya masomo ya sanaa kwa Kidato cha Tano na Sita. Vitabu hivyo vimesambazwa kwenye shule za sekondari katika Halmashauri 184.

**46. Mheshimiwa Spika**, Shule za Sekondari nchini zinahitaji maabara **10,840**. Maabara zilizopo ni **5,562** sawa na asilimia **51.3** na upungufu ni maabara **5,278** ambazo zinaendelea kujengwa (**ufafanuzi umeoneshwa kwenye jedwali Na. 6**). Serikali kupitia mradi wa Mpango wa Uimarishaji wa Stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu "LANES" imefanikiwa kununua vifaa vya maabara vyenye thamani ya **shilingi bilioni 16.0** ambavyo vinasambazwa katika shule **1,696** zilizokamilisha ujenzi sawa na **asilimia 47** ya shule za sekondari **3,602**. Lengo ni kuhakikisha tunakamilisha ujenzi wa maabara zote ili masomo yote ya sayansi yafundishwe kwa vitendo.

**47. Mheshimiwa Spika**, Shule za Kidato cha Tano zimeongezeka kutoka Shule **279** mwaka 2016 hadi Shule **333** mwaka 2017 sawa na ongezeko la asilimia **16**. Uchaguzi wa wanafunzi wa Kidato cha Tano unatarajiwa kufanyika Mei, 2017 ambapo jumla ya Wanafunzi **53,942** (Wasichana **23,201** na Wavulana **30,741**) wanatarajiwa kuijunga na Kidato cha Tano. Aidha, Wanafunzi **759** (Wasichana **220** na Wavulana **539**) wanatarajiwa kuijunga na Vyuo vya ufundi.

**48. Mheshimiwa Spika**, Makatibu Tawala wa Mikoa wameagizwa kuhakikisha kila Tarafa inakuwa na walau Shule moja ya Kidato cha **5** na **6**. Serikali kupitia Mpango wa Elimu wa Lipa kwa Matokeo imetumia jumla ya **shilingi bilioni 21.18** kwa ajili ya upanuzi wa miundombinu kwenye Shule **85** za Sekondari za Kidato cha Tano na Sita kwa ushirikiano na SIDA, Benki ya Dunia na DfID. Aidha, **Shilingi bilioni 2.85** zimetolewa kwa ajili ya ukarabati wa Shule kongwe zilizokuwa na uchakavu mkubwa wa miundombinu. Fedha hizo zimetumika kujenga vyumba vya madarasa **798**, matundu ya vyoo **1,759**, mabweni **24**, mabwalo sita **(6)**,

majengo ya utawala sita **(6)**, maabara tatu **(3)** nyumba za walimu saba **(7)**, maktaba moja **(1)**, uzio katika Shule tatu **(3)**, mfumo wa maji katika Shule nne **(4)** na mfumo wa umeme katika Shule moja **(1)**. Vilevile jumla ya shilingi milioni **208** zimetumwa kwenye akaunti za Halmashauri husika kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji.

**49. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2016/17, jumla ya shilingi **bilioni 36.8** zimepelekwa kwenye akaunti za Shule za Sekondari Kongwe **23** kwa ajili ya ukarabati na shilingi **bilioni 3.5** zimepelekwa katika Shule saba **(7)** za Sekondari za Ufundi kwa ajili ya ukarabati wa karakana. Aidha, OR-TAMISEMI kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) inaendelea na ukarabati wa Shule **11** kongwe ambao unahusisha mabweni na nyumba za walimu **40**.

**50. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Desemba, 2016 baada ya utekelezaji wa agizo la Mhe. Rais la kuhakikisha kila Wanafunzi anakaa kwenye dawati, Mikoa yote ilijitosheleza kwa madawati na kuwa na ziada. Aidha, kutokana na uandikishaji na usajili wa wanafunzi wa Darasa la Awali, Darasa la Kwanza na Kidato cha Kwanza mwaka 2017, hadi Machi tumekuwa na upungufu wa madawati **302,787** kwa Shule za Msingi na madawati **204,526** kwa Shule za Sekondari nchini. (**ufafanuzi umeoneshwa kwenye jedwali Na. 7 & 8**).

**51. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2016, Wanafunzi **410,519** (Wasichana **210,345** na Wavulana **200,174**) walifanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Pili, ambapo kati yao, Wanafunzi **372,228** (Wasichana **189,161** na Wavulana **183,067**) sawa na asilimia **90.67** walifafulu mtihani huo. Kwa upande wa Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne, jumla ya Wanafunzi **277,313** (Wavulana **141,424** na Wasichana **135,889**) walifafulu kati ya wanafunzi **349,524** walifanya mtihani huo sawa na asilimia **75.99**. Aidha, katika Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita uliofanyika, jumla ya Wanafunzi **63,528** (wavulana **39,466** na wasichana **24,062**) walifafulu kati ya Wanafunzi **65,277** (Wasichana **24,467** na Wavulana **40,809**) walifanya Mtihani huo sawa na asilimia **98.87**.

## **Elimu Maalum**

52. **Mheshimiwa Spika**, OR -TAMISEMI inahusika pia na usimamizi na uendeshaji wa Elimu Maalum ambapo Shule maalum za Msingi ziko **31**, na Vitengo **556** vya Elimu Maalum, katika Shule za Sekondari **66**. Aidha, Shule ya Sekondari ya Njombe ni maalum kwa ajili ya Walemaru wa Masikio kwa nchi nzima. Shule za Elimu maalum zinahudumiwa na Walimu **1,673** ambaao ni wataalam wa Elimu maalum katika Shule za Msingi na Sekondari kutegemeana na aina ya ulemavu wa wanafunzi. Serikali imenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa shule maalum vyenye thamani ya **shilingi bilioni 4.2** kwa mwaka wa fedha 2016/17 ili kuboresha utoaji wa elimu kwa kundi hili maalum.

## **Motisha kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata**

53. **Mheshimiwa Spika**, kuanzia Julai, 2016 Serikali ilianza kutoa posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Waratibu Elimu Kata. Posho hiyo inatolewa kama motisha kwa viongozi hao ili kuimarisha uongozi na usimamizi wa elimu katika shule na Kata. Hadi Machi, 2017 Serikali imetoa **shilingi bilioni 40.76** kwa ajili ya kulipa posho hizo. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 7.20** zimetumika kwa Wakuu wa Shule za Sekondari, **shilingi bilioni 25.77** kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi na **shilingi bilioni 7.79** zimelipwa kwa Waratibu Elimu Kata.

## **Kushughulikia Athari za Tetemeko la Ardhi Kagera**

54. **Mheshimiwa Spika**, Mkoa wa Kagera ulikumbwa na tetemeko la ardhi tarehe 10 Septemba, 2016 ambapo Shule ya Sekondari ya Ihungo iliyoko Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba na Shule ya Sekondari ya Nyakato iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba ziliharibika kabisa. Miundombinu iliyoharibiwa katika Shule ya Sekondari ya Ihungo ni madarasa **16**, mabweni **7**, nyumba za walimu **20**, ukumbi **1**, bwalo **1**, jiko **1**, chumba cha Kompyuta kimoja, maktaba **1**, jengo la kilimo, jengo la utawala, nyumba ya

padre **1**, vyoo matundu **32**, maabara **3** na vyumba nya mabafu **40**. Kwa upande wa Shule ya sekondari Nyakato uharibifu ulihuisha mabweni **14**, madarasa **18**, jengo moja la utawala, maabara **2**, nyumba **10** za watumishi na maktaba moja.

**55. Mheshimiwa Spika**, Shule ya Sekondari ya Ihungo ilikuwa na wanafunzi **748** wa kidato cha tano na sita na shule ya Nyakato ilikuwa na wanafunzi **567** wa kidato cha tano na sita. Wanafunzi **372** wa kidato cha sita wa shule ya Sekondari ya Ihungo na Wanafunzi **227** wa shule ya sekondari Nyakato walihamishiwa kwa muda katika Shule ya Sekondari ya Omumwani iliyokuwa inamilikiwa na Jumuia ya Umoja wa Wazazi CCM na hivi sasa inamilikiwa na Serikali. Wanafunzi **376** wa kidato cha tano katika shule ya sekondari Ihungo walliobaki walihamishiwa kwa muda katika Chuo cha Ualimu Bukoba Lutheran (BLTC). Aidha, wanafunzi **340** wa Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari Nyakato walihamishiwa katika shule nyingine nne (4) ndani ya Mkoa wa Kagera.

**56. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea na ujenzi wa Shule ya Sekondari Ihungo na Nyakato ambazo zinajengwa upya kabisa. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati wadau wote wa elimu waliota michango yao ili kurejesha miundombinu ya shule iliyoharibiwa na tetemeko.

#### **Uboreshaji wa Huduma za Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe**

**57. Mheshimiwa Spika**, uratibu, usimamizi na utoaji huduma za afya, Ustawi wa Jamii na Lishe katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni moja kati ya majukumu muhimu ya OR-TAMISEMI. Hospitali zenyehadhi ya Wilaya ni **119** kati ya Wilaya **139**. Kati ya Hospitali hizo, **69** zinamilikiwa na Serikali sawa na asilimia **49.6** na Hospitali **50** zinamilikiwa na Sekta Binafsi kuititia Mashirika ya Dini na watu binafsi. Vituo nya afya vilivyopo ni **507** kati ya vituo **4,420** vinavyohitajika.

Zahanati zilizopo ni **4,470** kati ya **12,545** zinazohitajika. Serikali kwa kushirikisha nguvu za Wananchi inaendelea na ujenzi wa vituo vya afya **244** na zahanati **1,538**.

**58. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Halmashauri za Wilaya za Kishapu na Rufiji na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga zilipanuliwa na kukamilika, vituo vya afya 17 na zahanati 70 zilikamilishwa. Kukamilika kwa miundombinu hiyo kumesaidia Wananchi **595,000** kupata huduma bora karibu na maeneo yao na kuwapunguzia adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo. Aidha, ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa mipya ya Njombe, Katavi, Geita na Simiyu unaendelea ambapo Serikali imepeleka **shilingi bilioni 4.6** katika Mikoa hiyo. Kati ya fedha hizo, **shilingi milioni 994** zilitumika kulipa fidia ya ardhii iliyo tengwa na **shilingi bilioni 3.5** zitemumika kwa ajili ya ujenzi.

**59. Mheshimiwa Spika**, OR-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Wadau wa Maendeleo imefanya tathmini ya ukarabati wa Vituo vya Afya 100 kwa lengo kuboresha huduma za dharura za upasuaji wa akina mama wanaojifungua kabla ya Juni, 2017. Kazi hiyo inatarajiwaa kugharimu **shilingi bilioni 66.6** mpaka kukamilika. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 33.3** zitatumika katika ukarabati wa miundombinu na kiasi cha **shilingi bilioni 33.3** kitatumika katika ununuvi wa vifaa tiba.

**60. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha huduma za dharura na Rufaa ngazi za Vituo vya afya kwa Mama na Mtoto, Serikali imetoea magari ya kusafirisha wagonjwa (ambulances) **50** kwa vituo vya afya hamsini (**50**) vilivyopo katika Mikoa ya Kigoma, Mara, Geita, Simiyu, Mwanza, Kagera, Shinyanga, na Tabora. Mikoa hiyo ilipewa kipaumbele kutokana na kiwango kikubwa cha vifo vya Mama na Mtoto ikilinganishwa na Mikoa mingine. Lengo la Serikali ni kupunguza vifo vya mama na mtoto kutoka **556** vya sasa hadi **292** kwa vizazi hai **100,000** ifikapo mwaka 2021 ili kufikia viwango vya kimataifa.

## **Huduma za Lishe**

**61.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuboresha hali ya lishe nchini, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali imeandaa Mpango wa Taifa wa Afua za Lishe wa miaka mitano kuanzia 2016/17 hadi 2020/21 (National Multisectoral Nutrition Action Plan) ambao umesheheni majukumu ya kila sekta na Wadau mbalimbali katika kukabiliana na tatizo la utapiamlo nchini. Aidha, zoezi la utoaji matone ya vitamin A na dawa za Minyoo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano lilifanyika mwezi Desemba, 2016 ambapo jumla ya watoto **7,862,837** walihusika na zoezi hilo. Katika kupambana na tatizo la utapiamlo, OR-TAMISEMI inaendelea kuimarisha Kamati za Lishe katika Mikoa na Halmashauri.

## **Usafi wa Mazingira na Afya**

**62.** **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwezi Julai, 2016 hadi Februari, 2017, jumla ya maeneo **20,056** yalikaguliwa na kati ya hayo, **1,837** yalifungwa kutokana na kuendesha shughuli zao katika mazingira machafu ambayo yanahatarisha jamii kupata magonjwa ya kuambukiza. Aidha, maeneo **5,892** yalipewa notisi za kufanya marekebisho na maeneo **712** wamiliki wake walifikishwa mahakamani kutokana na uvunjifu wa Sheria kwa kushindwa kutekeleza maelekezo kuhusu usafi. Hatua nyingine zilizochukuliwa ni pamoja na ujenzi wa madampo ya kisasa, ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kudhibiti taka ngumu na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua.

## **Huduma za Ustawi wa Jamii**

**63.** **Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha utoaji huduma za Ustawi wa Jamii tumetengeneza na kuzindua mwongozo wa utekelezaji wa Sera za Huduma kwa Watoto walio katika Mazingira Hatarishi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufadhili wa Wadau wetu wa Maendeleo. Kupitia mwongozo huo, Halmashauri zitaweza kupanga na kutekeleza vipaumbele vyta huduma za Ustawi wa Jamii. Jumla ya nakala **17,000** zilizalishwa na kati ya hizo **12,025**

zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na 208 kwenye Sekretarieti za Mikoa. Aidha, kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo, tunakamilisha Mfumo wa Takwimu za Ustawi wa Jamii ambao utaiwezesha OR-TAMISEMI kupata takwimu sahihi ili kuweza kupanga mipango yenyе uhalisia.

### **Huduma kwa Wazee**

**64. Mheshimiwa Spika**, Sera inaelekeza Wazee watambuliwe kuanzia umri wa miaka sitini na kuendelea ili kuwapatia huduma za afya bila malipo. Hadi mwezi Machi, 2017 jumla ya wazee **346,889** wametambuliwa ambapo kati yao Wazee **74,590** wamepata vitambulisho vya matibabu bila malipo. Aidha, Hospitali za Mikoa, Hospitali za Wilaya na Vituo vya afya vyote nchini vimetenga chumba maalum kwa ajili ya huduma za wazee. Lengo la Serikali ni kuwapatia wazee wote vitambulisho vya matibabu bila malipo.

### **Watu wenye ulemavu**

**65. Mheshimiwa Spika**, Serikali inaendelea kuimarisha huduma za watu wenye ulemavu kwa kuanzisha Kamati za Watu wenye Ulemavu katika Mikoa 26 na Halmashauri 184. Nia yetu ni kutimiza matakwa ya Sheria Na. 9 ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010 ya kuwafikia walemvu hadi katika ngazi za msingi kwenye Kata, Vijiji na Mitaa.

### **Mfuko wa Pamoja wa Afya (Health Basket Fund)**

**66. Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi, 2017 jumla ya **shilingi bilioni 79.70** kati ya **shilingi bilioni 106.26** zilizoidhinishwa zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. **Asilimia 33.3** ya fedha hizo zimetumika kwa ajili ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba pamoja na kutoa mafunzo kuhusu usimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya. Aidha, kuanzia Julai 2017, utaratibu umeandalisha ili fedha za Mfuko wa Afya wa Pamoja zipelekwe moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma za Afya ya Msingi kwa lengo la kurahisisha ununuzi na upatikanaji wa dawa. Hata

hivyo, Halmashauri zitaendelea na jukumu la kusimamia matumizi ya fedha hizo ili kuhakikisha dawa na vifaa tiba vinanunuliwa ili kuboresha huduma kwa wagonjwa (ufafanuzi umeoneshwa kwenye jedwali Na. 9).

### **Programu ya Kupambana na UKIMWI (Global Fund)**

**67.** **Mheshimiwa Spika**, mradi huu unashughulikia udhibiti wa magonjwa matatu ya UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria. Fedha zilizotengwa katika mwaka wa fedha 2016/17 ni shilingi **bilioni 1.68** kwa ajili ya uratibu katika OR - TAMISEMI. Hadi Machi, 2017 **shilingi milioni 909.8** zimepokelewa sawa na asilimia **54** ya fedha zilizoidhinishwa na kutumika kwa shughuli za uratibu na ufuatiliaji. Kwa upande wa shughuli za kudhibiti UKIMWI, hadi kufikia Machi 2017, jumla ya **shilingi bilioni 1.096** zimetolewa kwenye Mikoa **11** na Halmashauri **71**. Kwa upande wa Kifua Kikuu, hadi kufikia Machi 2017, **shilingi bilioni 1.727** zimepelekwa kwenye Mikoa **21** na Halmashauri **114**. Fedha hizo ni kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa watoa huduma na ufuatiliaji wa shughuli zilizopangwa.

### **Mradi wa Uimarishaji wa Afya ya Msingi kwa kuzingatia Matokeo**

**68.** **Mheshimiwa Spika**, kupitia mradi huu, utoaji wa huduma za afya unazingatia matokeo (result based financing) kwenye Mikoa ya Mwanza, Pwani, Simiyu, Tabora, Shinyanga, Kagera, Kigoma na Geita. Fedha zilizotengwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 ni **shilingi milioni 535.8**, ambapo hadi sasa zimetolewa **shilingi milioni 443.3**. Mradi huu umewezesha kufanya usimamizi shirikishi katika Mikoa ya Singida, Tanga, Kigoma na Dodoma ambayo imepokea fedha za kuimarisha vituo vilivyopata alama sufuri katika zoezi la kuvipatia vituo hadhi ya daraja kwa nyota (*Star rating*). Serikali imepanga kutumia shilingi **bilioni 71** kwa ajili ya kuboresha vituo vya kutolea huduma vilivyopata alama sufuri katika mwaka wa fedha 2016/17. Timu ya Wataalam inaendelea na tathmini ya vituo vya afya

vitakavyokarabatiwa kupitia mpango huo. Lengo ni kuhakikisha huduma za afya kwa wagonjwa zinaimarishwa hususan huduma za mama na mtoto.

### **Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

**69. Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zote **184** zimetenga shilingi **bilioni 56.8** kutokana na mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake. Masharti ya kupitisha bajeti ya kila Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2016/17, yalikuwa ni kwa kila Halmashauri kuonesha fedha zilizotengwa kwa ajili ya mfuko wa Vijana na Wanawake kwa kuzingatia mapato ya ndani ya Halmashauri husika. Hadi kufikia Machi, 2017, fedha zilizopelekwa kwenye mifuko ni **shilingi bilioni 15.6** sawa na asilimia **27.5** ya malengo. Fedha hizi zinatumika kwa ajili ya mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali vya Vijana na Wanawake ili kukuza kipato na ajira (**ufafanuzi umeoneshwa kwenye jedwali Na. 10**).

### **Usimamizi na Uendelezaji Vijiji na Miji**

**70. Mheshimiwa Spika**, ustawi wa jamii yetu utategemea sana jinsi tutakavyosimamia na kuimarisha uendelezaji wa Miji na Vijiji. Katika upimaji wa mipaka ya kiutawala tumefanikiwa kupima Vijiji **10,667** katи ya Vijiji **12,545** sawa na asilimia **85**. OR-TAMISEMI imezielekeza Sekretarieti za Mikoa kuzisimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa kukamilisha upimaji wa mipaka katika Vijiji **1,878** vilivyobaki. Vilevile, Vijiji **1,640** katи ya Vijiji **12,545** vimeandaliwa mpango wa matumizi bora ya ardhi. Tunaendelea kusimamia kazi hii kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**71. Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zimeanza kutumia mfumo wa taarifa za kijiografia katika uendelezaji wa Vijiji na Miji. Mfumo huo unawezesha uwepo wa uwazi katika uombaji, upimaji, upangaji wa ardhi ikiwemo utoaji wa Hati Miliki za ardhi kwenye Vijiji na Miji pamoja na utunzaji wa kumbukumbu za masuala ya ardhi, nyumba na anwani

za makazi. Mfumo huu unapunguza gharama za uandaaji wa mipango ya uendelezaji Miji na Vijiji na kutatua migogoro ya mipaka.

**72. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka za Seikali za Mitaa **177** kati ya **185** zipo katika hatua mbalimbali za kukamilisha uandaaji wa Mipango ya Jumla (General Planning Schemes) ya Uendelezaji wa Miji kwa lengo la kudhibiti ujenzi holela. Mfumo huu unasaidia kupunguza gharama za uandaaji wa mipango ya uendelezaji wa Vijiji na Miji, kudhibiti uendelezaji holela wa Vijiji na Miji. OR-TAMISEMI inaendelea kuratibu utekelezaji wa mipango ya jumla kwa ajili ya Miji Midogo **800** inayoibukia ili iendelezwe kwa mpangilio unaofaa. Tathmini inaonesha Miji hiyo ina fursa nyingi za kimazingira, kiuchumi na kijamii zitakazochangia kukuza uchumi wa wananchi wa kipato cha chini.

#### **Mfumo Ulioboreshwa wa Kupeleka Ruzuku katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGDG)**

**73. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali kupitia mfumo wa Upelekaji wa Ruzuku ya Maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGDG) imefanikiwa kupeleka jumla ya **shilingi bilioni 58.02** kati ya shillingi **bilioni 156.0** kwenye Halmashauri **185** ambapo asilimia **80** ya fedha hizo ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Sekta za kilimo, barabara, elimu, afya na maji. Asilimia **20** ya fedha za LGDG ni kwa ajili ya ufuatiliaji, tathmini, kujenga uwezo na upimaji wa Halmashauri kwa kuzingatia vigezo vya utoaji wa fedha hizo. Jumla ya Maafisa **977** wakiwemo Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Maafisa Mipango, Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Utumishi na Waweka Hazina walipatiwa mafunzo kuhusu mfumo wa LGDG ulioboreshwa ili kuimarisha usimamizi hadi ngazi za msingi za Serikali za Mitaa. Mfumo huu umeboreshwa ili kuimarisha dhana ya ubia kati ya Serikali na Wananchi kwa maana ya Wananchi kushiriki katika Miradi ya Maendeleo na Serikali kukamilisha pale walipofikia. Aidha, mfumo umeboreshwa ili uwezeshe kubainisha juhudzi za Wananchi, kuzitambua na kutumia fedha hizi kuunga mkono juhudzi hizo za Wananchi.

## Mfumo wa Fursa na Vikwazo Kwa Maendeleo (O&OD) Awamu ya Pili

74. **Mheshimiwa Spika**, Mfumo wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O & OD) ulioboreshwu unatekelezwa katika Halmashauri **10** ambazo ni Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, Kilombero, Morogoro, Kisarawe, Bagamoyo, Chalinze, Kondoa, Hai, Siha na Same. Mfumo huu unasisitiza ushirikiano kati ya jamii na Serikali katika kupanga matumizi ya rasilimali zilizopo kwa kuzingatia mahitaji ya jamii husika. Kupitia mfumo huu, wananchi wanashiriki kuibua fursa na kutambua vikwazo vinavyowazunguka katika maeneo yao. Maandalizi ya mfumo ulioboreshwu yamegharimu **shilingi bilioni 1.06** ambazo zimetumika kuandaa miongozo ya ufuatiliaji na uendeshaji wa kutambua, kuchambua na kutoa usaidizi wa jitihada za jamii pamoja na kufanya mafunzo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa **185**. Lengo la Serikali ni kusambaza mfumo huo katika Halmashauri zote nchini.

### Matengenezo na Ukarabati wa Barabara

75. **Mheshimiwa Spika**, hadi mwezi Machi, 2017 shilingi **bilioni 142.15** zimepelekwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kati ya **shilingi bilioni 249.7** zilizotengwa. Fedha hizo zimetumika kwa ajili ya matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita **11,111.57** kati ya lengo la kilomita **34,024** zilizopangwa. OR- TAMISEMI kwa kushirikiana na *The Africa Community Access Programme* (AfCAP), Mfuko wa Barabara na Wadau wengine wa barabara imejenga uwezo wa kufanya utafiti kuhusu ubora wa kazi za barabara kwa lengo la kubaini teknolojia inayofaa ili kupunguza ghamra za matengenezo na kuboresha mbinu za utengenezaji wa barabara zinazomilikiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Kazi hii inafanyika kupitia maabara ya utafiti wa barabara iliyopo OR - TAMISEMI Dodoma.

76. **Mheshimiwa Spika**, tumeendelea kujenga uwezo wa kitafiti kwa kuwapatia wataalam wetu mafunzo ya kuangalia ubora wa kazi za barabara kwa kushirikiana

na Taasisi za TANROADS – (Central Material Laboratory) na "Council for Scientific and Industrial Research (CSIR)" ya Afrika ya Kusini. Ili kuboresha kazi hiyo ya utafiti, tumefanikiwa kununua vifaa vya maabara vyenye thamani ya **shilingi milioni 162.5**. Vifaa hivi vya maabara, vinatumika kuongeza ufanisi na uwezo wa kuangalia ubora wa kazi za barabara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, barabara zenyе urefu wa kilomita **33** zimekarabatiwa kwa kiwango cha lami na madaraja **6** yamejengwa kupitia fedha za miradi ya maendeleo za Mfuko wa Barabara.

**77. Mheshimiwa Spika**, tunaendelea na kazi ya usanifu wa barabara zitakazopunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam ambayo itahusisha ujenzi wa daraja litakalouniganisha maeneo ya Kinondoni na Muhimbili. Miradi mingine itakayotekelozwa ni ujenzi wa daraja la Ruvu Juu na barabara za kupunguza msongamano katika Jiji la Mbeya.

#### **Programu ya Kuboresha Barabara Maeneo ya Vijijini (Removal of Bottleneck)**

**78. Mheshimiwa Spika**, lengo la programu hii ni kuhakikisha kuwa barabara katika maeneo ya Vijijini zinapitika wakati wote kwa kuboresha maeneo korofii ambayo ni kikwazo cha kupitika hususan nyakati za masika. Utekelezaji unahusisha kuinua tuta maeneo ya mabondeni, kujenga madaraja na makalvati kwenye maeneo ya mito inayokatiza barabara na kujenga barabara za zege kwenye maeneo yenye miinuko mikali.

**79. Mheshimiwa Spika**, programu hii inatekelezwa katika Halmashauri **11** ambazo ni Manispaa ya Dodoma na Halmashauri za Wilaya za Bahi, Kyela, Rungwe, Busokelo, Iramba, Rufiji, Babati, Wanging'ombe, Chunya na Hai. Halmashauri zilizokamilisha utekelezaji wa mradi ni Manispaa ya Dodoma na Halmashauri za Wilaya za Babati, Wanging'ombe na Hai. Utekelezaji wa programu unafanyika kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uingereza (DfID) ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 24.4** ziliidhinishwa kwa

mwaka wa fedha 2016/17. Hadi Machi, 2017 fedha zote zimepokelewa na kutumika katika ujenzi wa madaraja matano (5), makalvati makubwa 23, kunyanya matuta na kujenga barabara zenye urefu wa **kilomita 38.95** kwa kiwango cha changarawe. Aidha, mafunzo yametolewa kwa Wahandisi wa Sekretarieti za Mikoa yote **26**, Wahandisi na Mafundi Sanifu wa Mamlaka za Serikali za Mitaa **185**. Vilevile, mafunzo kuhusu matumizi ya mfumo wa usimamizi wa barabara za Halmashauri (DROMAS) kwa ajili ya kuandaa ramani za barabara, mipango na kutoa taarifa yamefanyika.

**Mradi wa Uboreshaji wa Barabara katika Mikoa ya Iringa na Ruvuma kupitia fedha kutoka Jumuia ya Ulaya**

**80. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Jumuia ya Ulaya (European Union) inatekeleza mradi wa ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita **88.661** kwa kiwango cha lami kwa gharama ya **shilingi bilioni 36.75**. Mradi huu unatekelezwa kwenye Halmashauri za Wilaya za Iringa (34.967km), Mufindi (14.971km), Songea (13.769km) na Mbanga (24.954km). Hadi sasa jumla ya kilometra **10.20** zimewekewa tabaka la kwanza la lami katika Halmashauri za Wilaya za Iringa (km 9.50) na Mufindi (km 0.70) kwa gharama ya **shilingi bilioni 10.23**. Aidha, mafunzo ya kuwajengea uwezo yametolewa kwa wataalam wa barabara wa OR - Rais – TAMISEMI, na Halmashauri za Mikoa ya Iringa, Morogoro, Ruvuma.

**81. Mheshimiwa Spika**, kupitia Programu ya "Road Transport Policy Support Programme – Phase II (RTPSP – II)", Serikali kwa kushirikiana na Jumuia ya Ulaya ("EU") inafanya ukarabati wa barabara zenye urefu wa kilomita **121.6** kwa gharama ya **shilingi bilioni 10.80** kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa mbalimbali. Kati ya barabara hizo, kilomita **11.8** za barabara zitaboreshwa kwa kiwango cha lami kwa kutumia fedha kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara.

**82. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) kupitia Programu ya "Feed the Future" awamu ya pili na ya tatu, inatekeleza

mradi wa ukarabati wa km **304.1** kati ya km **1,000** za barabara zilizopo kwenye mpango katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Kiteto, Mvomero na Kilombero. Lengo la mradi ni kuboresha usafiri kwa njia ya barabara katika maeneo yanayozalisha mazao ya chakula kwa wingi. Awamu ya kwanza ya mradi huo ilikamilika mwaka 2016 ambapo jumla ya kilometra **179.89** zilikarabatiwa kwa kiwango cha changarawe katika Halmashauri zote nne zilizo chini ya mradi huu kwa gharama ya **shilingi bilioni 8.75**.

### **Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati Tanzania**

**83.** **Mheshimiwa Spika**, Mradi wa Kuboresha Miji ya Kimkakati Tanzania (Tanzania Strategic Cities Project-TSCP) unatekelezwa na Serikali kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia (IDA Credit) kuititia mpango maalum wa utoaji fedha uitwao *Specific Investment Loan (SIL)* na ruzuku kutoka DANIDA. Mradi unatekelezwa katika Miji saba (7) ambayo ni Halmashauri za Majiji ya Arusha, Mbeya, Mwanza na Tanga na Halmashauri za Manispaa za Dodoma, Kigoma-Ujiji, Illemela na Mtwara-Mikindani na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu Dodoma - CDA.

**84.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha wa 2014/15, Serikali iliingia makubaliano ya kupata mkopo wa nyongeza wenye jumla ya **shilingi bilioni 81.58** kutoka Benki ya Dunia ambapo tayari jumla ya **shilingi bilioni 26.36** kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita **12.74** zinazoendelea kujengwa kwa kiwango cha lami katika miji saba na CDA. Fedha hizo pia zinatumika kukamilisha ujenzi wa madambo 6. Aidha, **shilingi bilioni 4** zimepokelewa kutoka DANIDA kwa ajili ya kugharamia uimarishaji wa Taasisi na kufunga mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri 7 pamoja na uwekaji wa taa za barabarani.

**5.** **Mheshimiwa Spika**, kuititia mradi huu, Serikali imenunua na kusambaza vifaa vya kukusanya, kusafirishia na kudhibiti taka ngumu katika miji yote ya mradi (Tanga, Mwanza, Arusha, Mbeya, Mtwara-Mikindani, Kigoma-Ujiji na

Dodoma). Vifaa vilivyonunuliwa na kusambazwa katika miji hiyo ni malori **40** na mitambo **28** kwa gharama ya **shilingi bilioni 66.09**.

### **Programu ya Kuzijengea Uwezo Mamlaka za Miji 18**

**86.** **Mheshimiwa Spika**, kupitia programu hii, jumla ya kilomita **220** za barabara zimesanifiwa kwa kiwango cha lami ambapo kilomita **31.28** zimeshajengwa na kilomita **51.17** zinaendelea kujengwa. Aidha, jumla ya stendi **11** za mabasi zimesanifiwa, stendi moja ya mabasi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea imejengwa na kukamilika na stendi tatu (3) katika Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda na Halmashauri za Mji za Korogwe na Njombe zinaendelea kujengwa. Vilevile, vituo vitano (**5**) vya maegesho ya magari ya mizigo vimesanifiwa na ujenzi wa kituo kimoja cha maegesho ya malori katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga unaendelea. Machinjo **7** ya kisasa yamesanifiwa na ujenzi wa chinjio moja (1) unaendelea. Kazi nyininge zilizofanyika ni usanifu wa masoko **9**, ukarabati wa madampo, ununuzi wa vifaa vya menejimenti ya taka ngumu katika Miji (7) na uandaaji wa Mipango Kabambe ya uendelezaji wa Miji 8. Utekelezaji wa mradi huu unakusudia kuboresha miundombinu ya barabara pamoja na usimamizi wa taka ngumu na usafirishaji ili kuifanya kuwa Miji ya kisasa na kuongeza wigo wa mapato.

### **Mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar Es Salaam-DMDP**

**87.** **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza mradi wa DMDP Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeweza kuingia mikataba na Wataalamu Washauri wa mradi, kufanya tafiti za kina, usanifu wa barabara za Mitaa na uhuishaji wa maeneo ya makazi yasiyopimwa katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, usanifu wa mifereji ya maji ya mvua kilometra **32.8** na udhibiti wa taka ngumu umefanyika katika Halmashauri za Manispaa za Dar es Salaam. Utekelezaji wa mradi unaendelea ambapo kazi za *package* ya kwanza katika Manispaa ya Ilala, Temeke na Kinondoni zimeanza kutekelezwa kwa kuanza na ujenzi wa miundombinu ya

barabara yenyé jumla ya kilomita **15** katika maeneo ambayo hayakuhitaji kulipa fidia.

#### **Programu ya Maboresho ya Fedha za Umma (PFMRP IV)**

**88.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Programu ya Maboresho ya Fedha za Umma Awamu ya Nne iliidhinishiwa **shilingi bilioni 3.6**. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya **shilingi bilioni 2.24** zilitolewa na kutumika. Programu hii imechangia katika kuimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato, matumizi ya mfumo wa Epicor, usimamizi wa mifumo ya ununuzi katika Sekta ya Umma, kuimarisha huduma za ukaguzi wa ndani na kuimarika kwa maandalizi na uwasilishaji wa taarifa za fedha kwa kutumia viwango vya Kimataifa vya uhasibu katika Sekta ya Umma (International Public Sector Accounting Standards – IPSAS).

#### **Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP)**

**89.** **Mheshimiwa Spika**, kuititia utekelezaji wa programu hii idadi ya Maafisa Ugani imeongezeka kutoka watalaan **3,326** hadi **13,532** kwa kipindi kilichoishia Desemba, 2016. Ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji umeongeza eneo linalomwagiliwa kutoka hekta **264,388** hadi **463,615** ambapo tija katika uzalishaji wa mazao ya kilimo imeongezeka kwa wastani wa asilimia **3.3** kwa mwaka.

**90.** **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zitaendelea kutekeleza na kukamilisha miradi mbalimbali katika sekta ya kilimo kwa kutumia bakaa ya mwaka wa fedha wa 2015/16. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Washirika wa Maendeleo inakamilisha maandalizi ya Awamu ya Pili ya utekelezaji wa programu ambayo inatarajiwaa kuanza mwaka wa fedha wa 2017/18.

#### **Sekta ya Mifugo**

**91.** **Mheshimiwa Spika**, nchi yetu inakadiriwa kuwa na jumla ya Kaya **1,745,776** zinazojishughulisha na

ufugaji pekee na Kaya **4,901,837** zinazojishughulisha na kilimo na mifugo. Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya ufugaji yatakayowafanya wafugaji waache kuhamahama kwa kutenga maeneo maalum ya malisho, majosho, mabwawa/malambo ya kunyweshea mifugo pamoja na kuchimbiwa visima. Hadi mwezi Machi, 2017 majosho yaliyojengwa na kukarabatiwa ni **5,017**, mabwawa/malambo yaliyojimbwa ni **3,661** na visima vya maji vilivyojimbwa ni **985** katika maeneo ya wafugaji. Lengo la Serikali ni kuimarisha sekta hii ili iwe na mchango mkubwa katika maendeleo ya viwanda.

### **Programu ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RWSSP)**

**92. Mheshimiwa Spika**, Hadi mwezi Machi 2017, **shilingi bilioni 62.5** zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji kupitia Programu ndogo ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira (RWSSP). Lengo kuu la programu hii ni kuboresha huduma ya maji na usafi wa mazingira kwa kuongeza kiwango na ubora wa upatikanaji wa huduma hiyo. Miradi ya maji iliyotekeliza na kukamilika ni **1,301** kati ya **1,810** iliyokuwa imepangwa katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji nchini. Serikali imetumia **shilingi milioni 180** kwa ajili ya kutekeleza kampeni ya kitaifa ya usafi wa mazingira ambayo imehusisha kutoa elimu, kukarabati vyoo katika shule **139**.

**93. Mheshimiwa Spika**, vyombo vya watumiaji maji (COWSO) **1,799** vimeundwa kati ya **5,226** kwa ajili ya usimamizi na uendeshaji wa vituo vya maji ili kuhakikisha miradi hiyo inakuwa endelevu. Aidha, jumla ya vituo vya huduma za maji **1,918** vimejengwa kati ya **6,892** ambavyo vimepangwa kujengwa hadi kufikia Juni, 2017 ambapo wananchi **1,295,000** wananaufaika na huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya vijijini. Vilevile, Kaya **1,662,550** zimehamasishwa na kujenga vyoo bora na vituo **1,029,404** vya kunawia mikono katika ngazi ya familia.

**94. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la

Uingereza (DfID) imeanzisha mpango wa lipa kwa matokeo (**Payment by Results**) ambapo jumla ya Halmashauri 74 zimeingia kwa awamu ya kwanza kwa kuzingatia vigezo mbalimbali. Mpango huu unakusudia kutoa motisha kwa Halmashauri zinazofanya vizuri katika usimamizi wa miradi ya maji. Motisha imelenga katika kuongeza vituo vya kuchotea maji katika maeneo yote ya miji na Vijiji. Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba **asilimia 85** ya wananchi waliopo vijijini na **asilimia 95** ya wananchi waliopo mijini wanapata maji na salama ifikapo mwaka 2020.

### **Utekelezaji wa Sera ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)**

**95. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Sera na Sheria ya ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ya mwaka 2014 na Kanuni zake za mwaka 2015, OR – TAMISEMI imeweka utaratibu wa mafunzo kwa kuiwezesha Halmashauri kuibua miradi inayoweza kuwawutia Wawekezaji, kutenga ardhi kwa ajili ya wawekezaji na kuandaa mikataba yenye maslahi kwa Halmashauri na wananchi kwa ujumla. Utekelezaji wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi utazipunguzia Halmashauri nakisi ya bajeti, kupata teknolojia mpya na kuongeza mapato.

### **III. TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI**

#### **Tume ya Utumishi wa Walimu**

**96. Mheshimiwa Spika**, ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake, katika mwaka wa fedha 2016/17, Tume ilitengewa **shilingi bilioni 10.04** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi Machi, 2017 Tume imepokea **shilingi bilioni 3.9** sawa na **asilimia 39.7** ya bajeti. Kazi zilizofanyika ni kuendesha vikao vya kisheria ambapo mashauri ya nidhamu **242** yamehitimishwa kwenye ngazi ya Wilaya, mashauri **303** yamefanyiwa uchunguzi, walimu **1,885** wamesajiliwa, walimu **2,567** wamethibitishwa kazini, walimu **1,597** waliojiendeze wamebadilishwa vyeo, walimu **2,800** wamepewa vibali vya kustaafu kazi, walimu wa mikataba **102** wameandaliwa

mafao yao na mirathi **74** imeshughulikiwa. Vilevile, majalada ya wazi na siri ya walimu **301,480** yamechambuliwa na kupangwa, ziara na mikutano ya walimu kwenye Wilaya **16** imefanyika, Mpango Mkakati wa Taasisi umeandaliwa na Mkutano wa kazi wa wajumbe wa Tume umefanyika.

### **Shirika la Elimu Kibaha**

**97. Mheshimiwa Spika**, hadi Machi, 2017, Shirika la Elimu Kibaha kupitia Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi Mkoani Pwani limefanikiwa kutoa huduma kwa wagonjwa **185,354** wakiwemo wagonjwa wa nje **135,500** na wagonjwa wa ndani **49,854** katи ya lengo la kuhudumia wagonjwa **200,000**. Majeruhi wa ajali za barabarani **930** (wanawake **185** na wanaume **745**) na majeruhi wasio wa ajali za barabarani wapatao **513** (wanaume **355** na wanawake **158**) wamehudumiwa. Aidha, hospitali imetoa msaada wa kitaalam kwa kuwajengea uwezo madaktari na wauguzi wa Hospitali **7** zilizoko Mkoa wa Pwani na kuweshesha Kituo cha Afya Mkoani kuanza kutoa huduma za upasuaji kwa mama wajawazito. Shirika limefanikiwa kufunga mtambo wa kuzalisha "Oxygen" wenyе uwezo wa kuhudumia wagonjwa zaidi ya **50** kwa wakati mmoja. Mtambo huo unasaidia kutoa huduma kwa wagonjwa wanaohitaji Oxygen na kupunguza gharama zilizokuwa zinatumika awali kupata huduma hiyo.

### **Chuo cha Serikali za Mitaa**

**98. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Serikali za Mitaa kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kufanya utafiti na ushauri (consultancy). Hadi Machi, 2017 Chuo kimefanikiwa kukusanya **shilingi milioni 936.2** kutoka kwenye vyanzo vya mapato ya ndani sawa na asilimia **20.9** ya makisio ambayo yalikuwa **shilingi bilioni 4.5**.

**99. Mheshimiwa Spika**, kazi zilizotekelawa ni udahili wa wanafunzi wapatao **3,443** ambapo wanafunzi wapya walikuwa **2,582**, kuendesha mitihani, kugharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wanachuo **3,129**

kuwawezesha watumishi **15** wa Chuo kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu, kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na kufanya matengenezo ya miundombinu ya Chuo.

### **Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**100. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17, Bodi iliweka lengo la kukusanya mtaji wa **shilingi bilioni 3.1** kutoka kwenye Halmashauri zinazodaiwa michango na marejesho ya mikopo ya **shilingi milioni 935.8**. Hadi mwezi Machi, 2017, michango iliyowasilishwa ni shilingi **milioni 515.5** sawa na **asilimia 55** ya makadirio. Aidha, Michango yote ya Akiba na nyongeza ya mtaji iliyowasilishwa na Halmashauri imefikia jumla ya **shilingi bilioni 6.9** sawa na **asilimia 52.7** ya kiasi kilichopaswa kuchangwa cha jumla ya shilingi **bilioni 13.1**.

**101. Mheshimiwa Spika**, Bodi katika kutekeleza majukumu ya msingi imefanikiwa kutoa mikopo ya **shilingi milioni 120** kwenye Halmashauri ya Wilaya za Bukombe kwa ajili ya ujenzi wa soko la mazao ya kilimo na mifugo Ushirombo na **shilingi milioni 150** kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya mabasi. OR - TAMISEMI inaendelea na mpango wa kuboresha muundo wa Bodi hii ili kutekeleza majukumu yake ya kutoa mikopo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufanisi.

### **Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa-LAPF**

**102. Mheshimiwa Spika**, malengo ya Mfuko wa Pensheni wa LAPF katika mwaka wa fedha 2016/17 yalikuwa ni kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 623.10**. Hadi kufikia Machi 2017, Mfuko umekusanya **shilingi bilioni 329.54** sawa na **asilimia 50.6** ya lengo la kipindi cha miezi tisa. Fedha hizo zimetokana na michango, malimbikizo ya michango, michango ya wananchama wa hiari, ghamrama za kubadili mfumo, mapato ya uwekezaji, mapato ya dhamana zilizoiva na mapato mengineyo. Aidha, Mfuko umekusanya mapato yatokanayo na uwekezaji **shilingi bilioni 70.03** na kulipa mafao kiasi cha **shilingi bilioni 100.86**.

## **Shirika la Masoko Kariakoo**

**103.** **Mheshimiwa Spika**, Shirika la Masoko Kariakoo lilianzishwa kwa Sheria ya Mashirika ya Umma Sura 132 ya mwaka 1974 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 1985 na mwaka 2002. Lengo la Shirika ni kusimamia na kuendesha masoko ya kisasa katika Jiji la Dar es Salaam. Katika mwaka wa fedha 2016/17, Shirika liliadiria kukusanya mapato ya **shilingi bilioni 2.7** ambayo yanatokana na vyanzo vya mapato ya ndani yaani ushuru wa mazao, kodi ya pango na ada ya kutumia soko. Hadi Machi 2017, Shirika limekusanya **shilingi bilioni 1.22** sawa na asilimia **45**. Fedha hizo zimetumika kulipa mishahara ya watumishi wa Shirika, uendeshaji wa biashara, ukarabati wa mindombinu ya soko, ununuzi wa vifaa vya kudumu na kulipa gawio HAZINA, ukarabati wa mfumo wa maji safi katika jengo la Soko Kuu na soko dogo na ukarabati wa nyumba ya soko iliyopo Mbezi.

## **IV. MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

**104.** **Mheshimiwa Spika**, maandalizi ya Mpango na Bajeti ya OR - TAMISEMI yamezingatia llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Malengo Endelevu ya Maendeleo 2016-2030, Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaolenga kujenga uchumi wa viwanda na Mwongozo wa Kitaifa kuhusu Mpango na Bajeti kwa mwaka 2017/18.

**105.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, OR - TAMISEMI, itaendelea kutekeleza shughuli mbalimbali, kama ifuatavyo:-

- i) Kujenga uwezo wa watumishi wa OR -TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kutoa mafunzo mbalimbali;
- ii) Kuendelea kuratibu masuala mtambuka kama vile UKIMWI/VVU, Utunzaji wa Mazingira, Utawala Bora na Kupambana na vitendo vya Rushwa;

- iii) Kuzipanga Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Madaraja kwa lengo la kufahamu uwezo wa Mamlaka hizo katika kutoa huduma na kugawa rasilimali kulingana na mahitaji;
- iv) Kuendelea kusimamia ugatuaji wa madaraka, nyenzo na rasilimali kutoka Serikali Kuu kwenda Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuzijengea uwezo wa kutoa huduma;
- v) Kuimarisha matumizi ya Serikali Mtandao (e-government na TEHAMA) ngazi ya OR - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vi) Ufuatiliaji na uperembaji wa shughuli mbalimbali kwenye Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vii) Kuwezesha na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Taasisi zilizopo chini ya OR-TAMISEMI ambazo ni Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Serikali za Mitaa (LAPF), Shirika la Elimu Kibaha, Chuo cha Serikali za Mitaa, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar es salaam (DART), Tume ya Utumishi wa Walimu na Shirika la Masoko Kariakoo;
- viii) Kusimamia fedha za Mfuko wa Barabara na wadau wengine kwa ajili ya matengenezo ya barabara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ix) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Sera, programu za maboresho na miradi iliyo chini ya OR – TAMISEMI;
- x) Kuendelea na mchakato wa kuandaa Sera ya Maendeleo Mijini na kufanya mapitio ya Sera ya Maendeleo Vijijini; na
- xi) Kutoa maelekezo mahususi kuhusiana na ukuaji na usimamizi wa maendeleo ya miji nchini.

### **Tawala za Mikoa**

**106. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Tawala za Mikoa zitatekeleza majukumu yafuatayo:-

- i) Kudumisha amani, utulivu na usalama katika maeneo yao ya utawala;

- ii) Kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitoe huduma bora kwa wananchi;
- iii) Kuandaa Mipango Mikakati ya Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Kuzingatia Mpango wa Pili wa Maendeleo na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015;
- iv) Kuanzisha na kurasimisha utengaji wa maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda, kilimo, ufugaji, makazi, hifadhi za wanyamapori, misitu na vyanzo vya maji;
- v) Kutekeleza mwongozo wa Serikali Mtandao (e-Gov) katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma;
- vi) Kuimarisha ukuzaji wa mazao ya kilimo na biashara na kuhakikisha usalama wa chakula;
- vii) Kuimarisha usimamizi wa huduma za ugani zinazoendana na mahitaji ya soko na kuhakikisha zinaendana na Sera ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika kilimo na maendeleo ya viwanda;
- viii) Kuendelea na ujenzi, ukarabati na uwekaji wa vifaa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa, Ofisi na Makazi ya Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya;
- ix) Kuimarisha Timu za Afya za Mikoa na Serikali za Mitaa ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma za afya zilizoboreshwa katika Halmashauri, Mikoa na Hospitali za Rufaa;
- x) Kuendesha mikutano ya Kisheria ya Kamati ya Ushauri ya Wilaya (DCC) na Mkoa (RCC) ili kuimarisha utawala bora na uwajibikaji katika ngazi zote; na
- xi) Kuanzisha na kusimamia madawati ya kuratibu malalamiko kuhusu huduma zinazotolewa kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

## **Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**107. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini zitatekeleza majukumu yafuatayo:-

- i) Kuendesha Mikutano ya Kisheria ngazi ya Halmashauri, Kata, Vijiji na Mitaa ili kuimarisha masuala ya utawala bora na uwajibikaji;
- ii) Kuandaa mipango kabambe ya Maendeleo ya Miji na kujumuisha katika mipango mikakati kama njia ya kushughulikia maeneo yasiyopangwa mijini;
- iii) Kuboresha usafi wa mazingira kwa kuhakikisha usimamizi wa taka-maeneo ya kukusanya, kusomba na madampo ya taka, miundombinu ya taa za barabarani, vyoo, jumuiya na mfumo wa maji taka;
- iv) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya shughuli za maendeleo na utawala;
- v) Kujenga, kukarabati miundombinu ya kijamii na kiuchumi hususan katika sekta za elimu, maji, afya, kilimo, mifugo, uvuvi na barabara kwa kuzingatia ubora wa kitaifa;
- vi) Kuimarisha ubora wa afya na huduma za lishe na kuongeza upatikanaji wa huduma za lishe katika ngazi ya jamii na vituo vya kutolea huduma; na Kuthaminisha mali zote zinazohusiana na ardhi na kuhuisha kwenye daftari la kumbukumbu kwa ajili ya makusanyo ya kodi kwa Halmashauri zote za mijini na vijijini.

## **V. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS - TAMISEMI KWA MWAKA 2017/18**

### **Tume ya Utumishi wa Walimu**

**108. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18 Tume imetengewa **shilingi bilioni 12.42** kwa ajili ya

utekelezaji wa majukumu ya Tume katika Ofisi ya Makao Makuu na Wilaya **139**. Kazi zilizopangwa kutekelezwa ni:-

- i. Kutolea uamuzi rufaa 43, mashauri ya nidhamu **1,512** yaliyopo na rufaa mpya 200 zinazotarajiwa katika ngazi ya Makao Makuu. Aidha, mashauri ya nidhamu 3,096 yaliyopo wilayani , mapya 1,000 na rufaa 100 zinazotarajiwa;
- ii. Kuwezesha Makao Makuu na Wilaya **139** kufanya vikao vya kisheria ili kushughulikia masuala ya kuthibitisha kazini walimu waliojiendeleza na mashauri ya nidhamu rufaa za walimu;
- iii. Kufunga na kuanza kutumia Mfumo wa Utunzaji wa taarifa za watumishi kwa njia ya kielektroniki;
- iv. Kuwajengea uwezo watumishi na Wadau wengine wa Tume ili kutekeleza majukumu yao ipasavyo;
- v. Kuhakikisha uwiano katika usambazaji wa walimu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na Shule;
- vi. Kuratibu na kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Tume kwenye ngazi ya Makao Makuu na Wilaya 139; na
- vii. Kuwajengea uwezo watumishi wa Tume na wadau wengine wa Tume ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

### **Shirika la Elimu Kibaha**

**109. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18 Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- i) Kuendelea kutoa huduma za afya za kinga na tiba katika hospitali Teule ya Rufaa ya Mkoa wa Pwani ya Tumbi;
- ii) Kuendelea kutoa elimu ya afya ya mazingira, uuguzi na utabibu kwa wanafunzi **229** katika Chuo cha Sayansi na Tiba Shirikishi Kibaha;
- iii) Kuendelea kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi **1,725** wa Sekondari na **994** wa shule ya Msingi;
- iv) Kuendelea kutoa huduma za maktaba;

- v) Kuendelea kutoa huduma za maendeleo ya jamii ili kuwawezesha wananchi kuondokana na umaskini kwa kutoa mafunzo ya ufundu, ujasiriamali, kilimo na mifugo kupitia Chuo cha Maendeleo ya wananchi Kibaha;
- vi) Kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa watumishi **820** ikiwa ni pamoja na kulipa mishahara na stahiki zao kwa wakati na kuwapatia vitendea kazi;
- vii) Kuongeza uzalishaji wa maji tiba kwa ajili ya matumizi ya hospitali na kuuzia hospitali nyingine;
- viii) Kuboresha miundombinu ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi na Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi ili viweze kutoa huduma bora zaidi kwa jamii kulingana na uhitaji uliopo;
- ix) Kuendeleza ujenzi na upanuzi wa Hospitali Teule ya Rufaa ya mkoa wa Pwani ya Tumbi;
- x) Kujenga maabara ya Fizikia na Maarifa ya nyumbani (Home Economics) katika shule ya Sekondari ya wasichana Kibaha; na
- xi) Kutumia ardhi ya Shirika (emptyland) kwa ajili ya uwekezaji ili kuongeza mapato ya Shirika.

### **Chuo cha Serikali za Mitaa**

**110. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Chuo cha Serikali za Mitaa kimepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- i) Kuendelea na utoaji wa mafunzo ya muda mrefu kwa kudahili wanafunzi wapya **2,500**;
- ii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi yenyе kuzingatia uhitaji;
- iii) Kufanya tafiti mbalimbali na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala yanayohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iv) Kutekeleza majukumu ya kuwa Chuo Kiongozi cha Mafunzo (Lead Training Institution) katika

kusimamia ubora wa mafunzo yanayotolewa katika ngazi mbali mbali za Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGAs);

- v) Kusimamia na kuendeleza utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa Chuo;
- vi) Ukarabati wa miundombinu ya Chuo na utunzaji wa mazingira yake;
- vii) Kuimairisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Chuo;
- viii) Kupima na kufutilia upatikanaji wa hati ya umiliki wa ardhi ya eneo la Chuo yenye ukubwa wa ekari **592**;
- ix) Kununua eneo la upanuzi wa Chuo Dodoma mjini;
- x) Kununua magari matatu kwa ajili ya huduma za usafiri; na
- xi) Kujenga vyumba viwili vya mihadhara (lecture rooms).

### **Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa**

**111. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka fedha 2017/18, Bodi itaendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa mikopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kufanya ufuutiliaji wa uwasilishaji wa marejesho ya mikopo na michango kutoka kwenye Halmashauri zinazodaiwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodi. Sambamba na hilo, Bodi itapanua wigo wa kupata vyanzo vingine vya mapato kuititia mikopo yenye masharti nafuu, kuwekeza kwenye Dhamana za Serikali (Treasury Bills) na kununua Hisa.

**112. Mheshimiwa Spika**, Bodi itaendelea kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili waweze kufahamu majukumu ya Bodi na huduma zinazotolewa ili waweze kunufaika nazo. Hatua za muda mrefu zitakazochukuliwa

ni kufanya marekebisho ya muundo wa Bodi ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Mapitio ya muundo yamefanyika kuititia wataalam washauri na kutoa mapendekezo ambayo yatafanyiwa maamuzi na Bodi ili kuwa na Bodi iliyoboreshwa (Modified Local Government Loans Board) itakayotekeleza majukumu yake kuendana na mazingira ya sasa ya kiuchumi.

### **Mfuko wa Pensheni wa Serikali za Mitaa**

**113. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Mfuko umepanga kufanya shughuli zifuatazo:-

- (i) Kuanzisha Ofisi ndogo za uratibu katika Mikoa ya Tabora na Kagera;
- (ii) Kuandikisha wanachama wapya **17,500**;
- (iii) Kuendelea na utelekelezaji wa kutoa mikopo ya Maisha Popote, Elimu na Nyumba kwa wanachama wake;
- (iv) Kuiflikia zaidi sekta binafsi hasa kwenye mijini mikubwa kama vile; Dar Es Salaam, Arusha, Mwanza, Mtwara, Geita, Kahama, na Mbeya;
- (v) Kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Mabasi Msamu Morogoro na kuanzisha miradi mipy ya viwanda Morogoro, Same na ujenzi wa jengo la Ofisi Arusha;
- (vi) Kufanya uwekezaji katika Sekta ya Viwanda kwa kushirikiana na wadau wengine;
- (vii) Kuutangaza Mfuko na kutoa elimu kwa umma; na
- (viii) Kufuatilia ulipaji wa mikopo ya Serikali na gharama za kubadilisha.

## **Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART)**

**114. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka-Dar es Salaam umepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

- i) Kuendelea na Awamu ya Pili ya ujenzi wa miundombinu ya DART na usanifu wa awamu zinazofuata. Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) itagharamia ujenzi wa miundombinu ya barabara ya Kilwa hadi Mbagala kilomita **19.3** kwa gharama zinazokadiriwa kuwa **shilingi bilioni 326.54**;
- ii) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya DART Awamu ya Tatu itakayohusisha barabara ya Nyerere hadi Gongolamboto yenyeye urefu wa kilometra **23.3** kwa uhisani wa Benki ya Dunia;
- iii) Kufanya uwekezaji katika maeneo muhimu ya mradi ili kuongeza mapato. Wakala unatarajia kuacha kutegemea ruzuku ya Serikali Kuu kuanzia mwaka wa fedha 2018/19;
- iv) Kukamilisha taratibu za uhamishaji wa mfumo wa ukusanyaji wa nauli ITS/AFCs Serikalini baada ya kukamilisha uhakiki pamoja na kujenga uwezo wa watumishi wa Wakala;
- v) Kufanya mapitio ya michoro awamu ya pili kwa ajili ya ujenzi wa mfumo wa mawasiliano wa DART;
- vi) Kuimarissha ulinzi na usalama katika vituo vikuu vitano, vituo vidogo ishirini na saba, madaraja matatu ya watembea kwa miguu pamoja na karakana ya Jangwani;
- vii) Kufanya matengenezo ya miundombinu ya mfumo wa DART iliyokamilika kujengwa;
- viii) Kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao (e-GA) kukamilisha taarifa ya mfumo wa ukusanyaji wa nauli wa ITS/AFCs;

- ix) Kumsimamia Mto huduma (UDART) ili atekeleze mkataba kulingana na masharti yaliyomo;
- x) Kukamilisha taratibu za kumpata mto huduma kwa ajili ya ukusanyaji wa nauli, usimamizi wa mapato na mshauri mwelekezi katika Awamu ya Pili;
- xi) Kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Mawasiliano wa Wakala;
- xii) Kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa miundombinu Awamu ya Pili;
- xiii) Kuwajengea uwezo watumishi wa Wakala na kuhakikisha wanalipwa stahiki zao kwa mujibu wa Sheria;
- xiv) Kuimarisha usimamizi wa mto huduma ya Mpito UDART ili huduma zinazotolewa ziwe na viwango vinavyokubalika.

#### **MALENGO MAHSUSI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

**115. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, malengo mahsusи yatakayotekelezwa na OR-TAMISEMI na Taasisi zilizopo chini yake ni kama ifuatavyo:-

#### **Kuimarisha Utoaji wa Huduma za Afya na Lishe**

**116. Mheshimiwa Spika**, katika kupambana na tatizo la utapiamlo, kwa mara ya kwanza Mikoa na Halmashauri zote nchini zimetenga **shilingi bilioni 11.40** ambayo ni sawa na **shilingi 1,000** kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka 5 kwa ajili ya huduma ya chanjo na lishe. Vilevile Wadau wa Maendeleo na Mashirika yasiyo ya kiserikali wametenga kiasi cha **shilingi bilioni 26.48** kwa ajili ya utekelezaji mpango wa Kitaifa wa Afya za Lishe.

## **Wakala wa Barabara Vijijini**

**117.** **Mheshimiwa Spika**, kuanzia mwezi Julai, 2017 OR-TAMISEMI inatarajia kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini ambao utakuwa na jukumu la kufanya tathmini ya mtandao wa barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa na kusimamia matengenezo ya barabara hizo kila mwaka. Wadau mbalimbali wameshirikishwa na kutoa maoni ambayo yamesaidia kuboresha muundo wa chombo hicho muhimu katika kuboresha usimamizi wa barabara za Mamlaka za Serikali za Mitaa. Fedha za utekelezaji wa majukumu ya Wakala zitatokana na bajeti ya Mfuko wa Barabara na fedha kutoka kwa Wadau wa Maendeleo.

## **Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (Decentralised Climate Finance Project)**

**118.** **Mheshimiwa Spika**, kwa kutambua athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Uingereza (UKAID) kupitia Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo *International Institute for Environment and Development - IIED* na Shirika lisilo la Kiserikali la Hakikazi Catalyst, (HKC) itatekeleza mradi wa kukabiliana athari za mabadiliko ya tabianchi. Lengo la mradi ni kuibua na kutekeleza miradi ambayo itasaidia kupunguza au kuondoa athari za mabadiliko ya tabianchi kwenye Mikoa na Halmashauri.

**119.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/18, mradi huu utaanza kutekelezwa katika Halmashauri 12 kwa gherama ya **shilingi bilioni 2.0**. Halmashauri za Mikoa hiyo ndizo ziliyoathirika kwa kiwango kikubwa kutoptera na mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu umepangwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka minne kuanzia 2017/18 –2020/21.

## **Shukrani**

**120.** **Mheshimiwa Spika**, naomba kumalizia hotuba yangu kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa

Wabunge wote na kipekee kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya OR - TAMISEMI yamepatikana kutokana na ushirikiano mzuri na Wadau wa Maendeleo ambaao waliendelea kushirikiana nasi katika utekelezaji wa Programu na Miradi mbalimbali katika Sekta za afya, elimu, maji, barabara, fedha, kilimo na maboresho ya mfumo wa Serikali za Mitaa. Wadau hao ni Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID), Jumuiya ya Nchi za Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Japan (JICA), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA), UNFPA, UN-Habitat, Shrika la Maendeleo ya Ubelgiji (BTC), Shirika la Maendeleo la Ujeruman (GIZ), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA), UNICEF, UNDP, pamoja na nchi zote zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Kusaidia Bajeti ya Serikali. Ofisi yangu Itaendelea kushirikiana na Wadau wote wa maendeleo wa ndani na nje ili kutimiza azma ya kutoa huduma bora kwa wananchi kupitia miradi inayotekeliza kwa kuzingatia vipaumbele vya wananchi wenyewe.

**121. Mheshimiwa Spika**, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitatambua kazi kubwa iliyofanywa na viongozi wenzangu katika Wizara nikianzia na Mheshimiwa Selemani S. Jafo (Mb), Naibu Waziri OR - TAMISEMI, Mhandisi Musa I. Iyombe, Katibu Mkuu, Bernard M. Makali, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Elimu na Dkt. Zainabu A.S. Chaula, Naibu Katibu Mkuu anayesimamia Afya, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninawashukuru viongozi wa Taasisi zilizo chini ya OR - TAMISEMI pamoja na Wakuu wa Idara, Vitengo na watumishi wote kwa ujumla kwa kufanya kazi kwa juhudhi na maarifa ili kufanikisha majukumu tuliyopewa katika OR - TAMISEMI.

**122. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Kibakwe kwa kuendelea kuwa wavumilivu mara zote nilipokuwa mbali nao kwa

majukumu ya Kitaifa. Naahidi kuendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote. Aidha, naishukuru familia yangu kwa kuendelea kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu haya mazito ya kuwatumia wananchi.

## **VI. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUFANYIKA MWAKA WA FEDHA 2017/18**

### **Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani**

**123. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2017/18, OR - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaomba idhini ya kukusanya **shilingi 713,187,789,615.00**. Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, marejesho ya masurufu na mishahara. Makusanyo kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa yatatokana na kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Mamlaka hizo kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika jedwali hapa chini:-

### **Maduhuli na Makusanyo ya Ndani kwa Mwaka wa Fedha**

<b>Na.</b>	<b>OFISI/TAASISI</b>	<b>MAKADIRIO</b>
1.	OR – TAMISEMI	14,000,000.00
2.	Taasisi	22,752,063,908.00
3.	Mikoa	3,115,064,707.00
4.	Mamlaka za Serikali za Mitaa	687,306,661,000.00
<b>JUMLA</b>		<b>713,187,789,615.00</b>

**124. Mheshimiwa Spika**, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/18, jumla ya **shilingi Trilioni Sita, Bilioni Mia Tano Sabini na Nane, Milioni Mia Sita Ishirini na Saba, Laki Nne Sabini, Mia Nne Tisini na Tano (shilingi 6,578,627,470,495.00)** kwa ajili ya OR-TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa 26 na Halmashauri 185. Mchanganuo ni kama unavyooneshwa kwenye hapa chini.

**Muhtasari wa Fedha Zinazoombwa kwa Mwaka  
wa Fedha 2017/2018**

<b>AINA YA MATUMIZI</b>	<b>FEDHA ZINAZOOMBWA (SHILINGI)</b>
OR-TAMISEMI	
Mishahara	
Makao Makuu	8,491,975,200.00
Taasisi	15,318,027,000.00
Matumizi Mengineyo	
Makao Makuu	6,384,731,652.00
Taasisi	1,827,564,148.00
<b>Jumla ya Matumizi ya Kawaida</b>	<b>32,022,298,000.00</b>
<b>Tume ya Utumishi wa Walimu</b>	
Mishahara	7,800,146,000.00
Matumizi Mengineyo	4,622,145,495.00
<b>Jumla ya Matumizi ya Kawaida</b>	<b>12,422,291,495.00</b>
<b>MIKO A NA HALMASHAURI</b>	
MIKO A:	
Mishahara	168,579,832,000.00
Matumizi Mengineyo	41,297,783,000.00
<b>Jumla ya Matumizi ya Kawaida</b>	<b>209,877,615,000.00</b>
<b>HALMASHAURI:</b>	
Mishahara	4,075,783,400,000.00
Matumizi Mengineyo	190,392,615,000.00
Halmashauri (asilimia 40 Mapato ya Ndani)	274,922,665,000.00
<b>Jumla Matumizi ya Kawaida</b>	<b>4,541,098,680,000.00</b>
<b>MIRADI YA MAENDELEO</b>	
OR-TAMISEMI	417,256,688,000.00
Mikoa	75,259,322,000.00
Halmashauri (Ruzuku ya Serikali)	878,306,580,000.00
Halmashauri (asilimia 60 Mapato ya Ndani)	412,383,996,000.00
<b>Jumla Miradi ya Maendeleo</b>	<b>1,783,206,586,000.00</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>6,578,627,470,495.00</b>

**125.** **Mheshimiwa Spika**, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya matumizi ya fedha ya mafungu 28 chini ya OR-TAMISEMI. Randama na majedwali ni sehemu ya hotuba yangu.

**126.** **Mheshimiwa Spika**, hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya OR-TAMISEMI ambayo ni [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz)

**127.** **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nimwite Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Angella Kairuki ili aje asome hotuba ya Wizara yake. Mheshimiwa Waziri wa Nchi karibu tafadhalii. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais - Ikulu, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi, Ushauri wa Mafuta na Gesi, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sekretarieti ya Ajira, Tume ya Utumishi wa Umma, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupidisha Mpango wa utekelezaji na makadirio ya fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini katika nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

namuahidi kuendelea kutekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nashukuru uongozi wa Shirikisho la Vyama vya wafanyakazi (*TUCTA*), UWT Mkao wa Dar es salaam, Wajumbe wa Baraza Kuu (UWT) Taifa na Wafanyakazi wote nchini Tanzania kwa ujumla kwa kuendelea kunipa ushirikiano ninapoendelea kuwawakilisha.

Mheshimiwa Spika, vilevile nawashukuru kwa kipekee familia yangu kwa dhati ya moyo wangu kwa ushirikiano wanaonipa wakiongozwa na mume wangu na watoto wangu na kuwa wavumilivu ninapotekeleza majukumu yangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Mwenyekiti Jasson Rweikiza na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Mcemba kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kuitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha wa 2016/2017 na mapendekezo ya mpango wa utekelezaji na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018. Maoni na ushauri wa Kamati hii umetuwezesha na utaendelea kutuwezesha kutekeleza majukumu ya ofisi yangu kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli, kwa uongozi wake mahiri unaohimiza uadilifu, uwajibikaji na utendaji wenye matokeo katika Utumishi wa Umma. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake wa kijasiri wa kuhamishia Serikali Dodoma, uamuzi ambaa ulikuwa ni mgumu sana kufanyika kwa zaidi ya miaka 40. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pili, nimpongeze Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo anavyomsaidia Mheshimiwa Rais wetu katika kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti aliyonayo ya kuleta maendeleo kwa Zanzibar. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza pia Mheshimiwa Balozi Seif Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna anavyoendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa moyo wake wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda kipekee pia nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo ameendelea kuwa nguzo muhimu ya utekelezaji, usimamiaji na uratibu wa shughuli za kila siku za Serikali na shughuli za Serikali Bungeni. Aidha, nampongeza kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma kwa awamu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa namna ambavyo mnaliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara, umahiri na hekima ya hali ya juu. Nawapongeza pia Wenyevitî wa Bunge kwa umahiri na kazi nzuri wanayoifanya katika kuliongoza Bunge lako Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri wote wa Awamu ya Tano kwa mafanikio wanayoendelea kuyapata katika utekelezaji wa llani ya uchaguzi ya CCM pamoja na dira ya maendeleo ya mwaka 2025. Kwa namna ya pekee, nimpongeze na kumshukuru Mheshimiwa Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Naibu wake Mheshimiwa Selemani Jafo na Mawaziri wote kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii pia kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioeteuliwa na Mheshimiwa Rais ambao ni Mheshimiwa Anne Kilango

Malecela na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Profesa Kabudi kuwa Mbunge na Waziri wa Katiba na Sheria. (*Makof*)

Aidha, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa msiba wa marehemu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Dkt. Elly Macha, Mbunge wa Viti Maalum. Tunaomba Mola aziweke roho za marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Balozi John Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi Ndugu Alphayo Kidata Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Ikulu; Dkt. Lauren Ndumbaro Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Utumishi, Ndugu Susan Mlawi Naibu Katibu Mkuu - Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora; Wenyeviti, Makamishna, Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi yetu kufikia malengo yake. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nizishukuru sana nchi wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo kipekee nachukua fursa hii kushukuru na kuwataja wachache ambao ni:-

China, Japan, Uingereza, India, Korea ya Kusini, Ujerumani, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uhlanzi, Finland, Uswisi, Indonesia, Brazil, Italia, Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Ireland pamoja na Israel.

Mheshimiwa Spika, vilevile, nashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), Benki ya Dunia, *OFID-OPEC Fund*, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan, *DFID*, *KOICA*, *GIZ*, *DFATD*, *USAID*, *SIDA*, *UNDP*, Jumuiya ya Madola, *DANIDA*, *NORAD* pamoha na Taasisi ya *Bill and Melinda Gates Foundation*. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ari na ufanisi mkubwa, uzalendo wao, ari yao na imani yao kwa uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Magufuli na haya ndiyo yamewezesha Serikali yetu kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kulithibitishia kwa mara nyingine tena Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu kupunguza urasimu ili kuongeza kasi ya utekelezaji, kubana matumizi na kurejesha nidhamu ya Serikali na Utumishi wa Umma kwa kuongeza uwazi na kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ili wawajibike kwa wananchi ambao ndio wateja na waajiri wakuu wa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, vilevile, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika vita dhidi ya rushwa, ubadhirifu, ujisadi, uzembe, uvivu, ukiukwaji wa maadili na utumishi hewa kwa kuwajibisha wanaodhihirika kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua anazoendelea kuchukua Mheshimiwa Rais zinatakiwa kuungwa mkono na wananchi wote. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Serikali inayowahudumia wananchi wa kawaida itatimia kwa Watumishi wote wa Umma kufanya kazi kwa bidii, juhudii, maarifa na uadilifu mkubwa. Tunaendelea kusisitiza utoaji wa huduma bora kwa haraka na kwa staha ili kuwaondolea wananchi wetu usumbufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hotuba yangu itazungumzia mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na mpango wa utekelezaji na maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka wa 2016/2017 ulizingatia Dira ya Taifa ya

Maendeleo ya mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano pamoja na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015. Aidha, kwa shughuli zilizotekelawa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Rais - Ikulu pamoja na Taasisi zake inayojumuisha Ikulu na Baraza la Mawaziri katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 - Fungu 20 liliidhinishiwa shilingi bilioni 14.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 shilingi bilioni 11.063 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri - Fungu 30 linalojumuisha Ikulu na Taasisi zingine kama TAKUKURU, MKURABITA, TASAF, Taasisi ya Uongozi pamoja na PTF liliidhinishiwa shilingi bilioni 793.1 na Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 362.7 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 430.4 ni za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2017 shilingi bilioni 547.5 zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 260.6 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 286.9 ni za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ikulu; kwa kipindi cha Julai 2016 hadi Machi 2017, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali na kwa muhtasari ni kama ifuatavyo:-

- (i) Imeendelea kutoa huduma kwa Mheshimiwa Rais na familia yake ikiwa ni pamoja na ushauri kwa Mheshimiwa Rais katika maeneo mbalimbali ili kumsaidia kuweza kufanya maamuzi.
- (ii) Pia mikutano 31 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika na ambapo nyaraka 49 zilichambuliwa.
- (iii) Mkutano wa tathmini wa mwaka kati ya Wakurugenzi wa Sera na Mipango pamoja na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri

ulifanyika katika kipindi cha tarehe 13 -17 Februari, mwaka huu hapa Dodoma.

- (iv) Aidha, hotuba 18 za Mheshimiwa Rais zilichapishwa na kutangazwa katika vyombo mbalimbali nya habari nchini pamoja na vipindi maalum nya televisheni 24 nya makala ya Rais vilitengenezwa na kurushwa hewani kwenye vyombo mbalimbali nya habari;
- (v) Aidha, ushahidi wa Serikali Mahakamani ultolewa kwa kesi za madai nane zinazohusu Watumishi wa Umma na wananchi wengine dhidi ya uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano au dhidi ya uamuzi wa Katibu Mkuu Kiongozi.
- (vi) Pia shughuli za TAKUKURU, TASAF, MKURABITA, Utawala Bora, Sekretarieti ya Maadili na Taasisi ya Uongozi, *PTF* pamoja na maboresho mbalimbali na rufaa za Watumishi wa Umma nazo pia ziliratibiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa TAKUKURU waliendelea kuelimisha umma kuhusu athari zarushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo nya sheria na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya rushwa. Kwa kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, TAKUKURU wameendelea kuchunguza majalada 376 ambayo yamewasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani ambapo kati ya majalada hayo, majalada 157 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, aidha, shilingi bilioni 12.316 ziliokolewa kutohana na operesheni mbalimbali zilizofanywa na TAKUKURU na fedha kurejeshwa Serikalini. Kampeni ya LONGA NASI iliyobuniwa kuwahamasisha wananchi kutoivumilia rushwa na namna ya kuifkia TAKUKURU kutoa taarifa za vitendo nya rushwa imeendelea katika Mikoa yote. Vilevile, Kituo cha huduma kwa Mteja kimesaidia kutoa elimu

na msaada wa haraka kwa wananchi hususan wanaoombwa rushwa au kucheleweshwa kupata huduma. Aidha, TAKUKURU inapatikana kwa simu namba 113 na hadi sasa malalamiko 199,337 yameweza kupatikana kuitia nambari hiyo.

Mheshimiwa Spika, MKURABITA imeendelea kuchukua hatua ili kuwawezesha wananchi wanaomiliki rasilimali na biashara nje ya mfumo rasmi kuwa na uwezo wa kurasimisha mali na hatimaye kushiriki katika uchumi wa soko unaoendeshwa kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TASAF* au Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wameendelea kutoa kipaumbele katika maeneo ya ukuzaji uchumi, kuongeza fursa na kupunguza umaskini wa kipato, kuinua ubora wa malsha na ustawi wa jamii na katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, mwaka huu tangu mpango wa kunusuru uanze kuweza kuzifikia kaya 1,110,377 zenye jumla ya watu milioni 5.8 ambaao wameandikishwa. Mpango huu unatekelezwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara pamoja na Wilaya zote za Zanzibar. Aidha, jumla ya shilingi bilioni 202.2 zilihawilishwa kama ruzuku kwa kaya maskini.

Mheshimiwa Spika, pia mpango wa kutoa ajira za muda umetekelezwa katika miradi 3,553 ambapo kaya za walengwa 298,970 ziliweza kupata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar. Vile vile zoezi la uhakiki wa kaya maskini ambalo ni endelevu lilifanyika na kubaini kuwepo kwa kaya 68,914 nchini kote ambazo zilikosa sifa na zote zimeondolewa katika Mpango. Mgawanyo wa kaya hizo zilizoondolewa ni kama unavyoonekana katika ukurasa wa 22 wa hotuba yangu ambayo imegawiwa.

Mheshimiwa Spika, pia mfumo wa teknolojia, habari na mawasiliano wa utambuzi, uandikishaji, malipo na malalamiko ya walengwa umekamilika na unatumika katika

Ofisi za *TASAF* zilizoko Mamlaka za Serikali za Mitaa 142 kwa upande wa Bara pamoja na Unguja na Pemba na zimeunganishwa na Makao Makuu ya *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uongozi imeendelea kuwa kituo cha utaalam wa hali ya juu cha kuendeleza viongozi barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, mwaka huu, kozi 18 za muda mfupi zimetolewa kwa Viongozi wa Umma 631 ili kuimarisha utendaji wao. Aidha, maandalizi ya programu ya "Stashahada ya Uzamili katika Uongozi" yamekamilika na program hii itatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto Finland.

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya mafunzo itaanza Mwezi huu Aprili, 2017 na programu hii itahusisha Viongozi 32 Waandamizi wa Jeshi la Polisi. Aidha, maandalizi ya programu ya mafunzo kuhusu majadiliano ya mikataba ya Kimataifa ya biashara yatakayotolewa Kikanda nayo pia yamekamilika.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*) nao pia umeendelea kutoa mikopo, mafunzo pamoja na ushauri wa kibashara kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Kwa maelezo ya kina kuhusiana na shughuli zilizotekelawa na Ikulu, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, TAKUKURU, MKURABITA, *TASAF*, Taasisi ya Uongozi na *PTF* yapo katika ukurasa wa 10 hadi 36 wa hotuba ambayo mmegawiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wakala zake. Katika mwaka huu wa fedha tunaoumaliza wa 2016/2017, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wakala zilizo chini yake iliidhinishiwa shilingi bilioni 30.3 kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 22.7 ni za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7.550 ni kwa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu

Shilingi bilioni 18.704 zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizi shilingi bilioni 18 ni matumizi ya kawaida na sh. 690,000,000 ni kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Utumishi pamoja na Wakala zake imeendelea kuhakikisha kwamba utumishi wa umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Pia kuhakikisha kwamba, watumishi wa umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi pale wanapotoa huduma mbalimbali kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, miongozo na taratibu zilizowekwa. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Ofisi ya Rais, Utumishi na Wakala zake iliweza kufanya kazi zifuatazo:-

(1) Iliweza kufanya marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, kwa lengo la kuoanisha na kuwanishaa mishahara mionganoni na baina ya Watumishi wa Taasisi za Umma;

(2) Pia iliweza vibali vya ajira mpya kwa nafasi 9,721 kwa Waajiri ikijumuisha nafasi 3,174 kwa Jeshi la Polisi, nafasi 1,000 kwa Jeshi la Magereza, nafasi 852 kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, nafasi 297 kwa Jeshi la Uhamiaji pamoja na nafasi 50 kwa ajili ya ajira za Wataalam wa Afya katika Hospitali ya Mloganzila. Aidha, kibali cha ajira kwa nafasi 4,129 za Walimu wa masomo ya sayansi na hisabati pamoja na nafasi 219 kwa ajili ya mafundi sanifu wa maabara za shule vilitolewa, ambapo tayari Walimu wa sayansi na hisabati wameshapangiwa vituo vya ajira.

(3) Aidha, uhakiki wa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 18,823 yenye thamani ya shilingi bilioni 32.8 umefanyika na yameingizwa kwenye mfumo wa taarifa za kiutumishi na mishahara kwa ajili ya malipo. Aidha, madai ya malimbikizo ya mshahara ya watumishi 12,973 yenye jumla ya shilingi bilioni 21.6 bado yanaendelea kuhakikiwa.

(4) Watumishi 19,708 wameondolewa katika orodha ya malipo ya mishahara ya watumishi wa umma

(*payroll*) kutokana na sababu mbalimbali ili kudhibiti watumishi hewa pamoja na mishahara batili.

(5) Aidha, mafunzo ya maadili ya utendaji katika utumishi wa umma yametolewa kwa watumishi 9,763 kutoka katika taasisi 20 za umma.

(6) Pia, viapo vya ahadi ya uadilifu kwa Watumishi wa Umma 165,481 vimeratibiwa.

(7) Ofisi imeendelea kusimamia na kuratibu mafunzo ya Watumishi wa Umma katika ngazi mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi; ambapo watumishi wa umma 654 walihudhuria mafunzo mbalimbali nje ya nchi kupitia ufadhili wa Serikali ya India, Japan, China, Jamhuri ya Korea Kusini, Australia, Uhlanzi pamoja na Misri.

(8) Usanifu wa programu ya maboresho katika utumishi wa umma pia umeanza kufanyika kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Uingereza (*DFID*) na Benki ya Dunia.

(9) Pia miundo na mgawanyo wa majukumu ya ofisi/Wizara 20 pamoja na taasisi za umma tatu imefanyiwa mapitio ili kuendana na mahitaji ya sasa kwa nia ya kupunguza ukubwa wa Serikali, kuongeza ufanisi na kuimarisha utoaji wa huduma na uwajibikaji na hatimaye mwishoni miundo hii itahuishwa.

(10) Jumla ya malalamiko 1,346 kati ya 1,384 sawa na asilimia 97 yanayohusu ukiukwaji wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma yameshughulikiwa.

(11) Uratibu wa utekelezaji Serikali Mtandao chini ya programu (*RCIP*) umeendelea kufanyika. Miradi inayotekelzwa ni Mfumo wa Taarifa za Usajili wa Vizazi na Vifo, Mfumo wa Taarifa za Biashara, Mfumo wa Taarifa za Kitabibu, Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali, Mfumo wa Kielektroniki wa Nyaraka pamoja na Mfumo wa Taarifa za Ununuzi kwa Njia ya Kielektroniki au *e-Procurement*.

Mheshimiwa Spika, upande wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (*TPSC*). Kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala, kutoa shauri za kitaalam, kufanya utafiti na machapisho mbalimbali ya kitaalam katika utumishi wa umma. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 wameweza kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza wameweza kutoa mafunzo ya kuijandaa kufanya mitihani ya utumishi wa umma kwa watumishi watumishi 476. Wameweza pia kutoa mafunzo mbalimbali kwa Watumishi wa Umma, ambapo watumishi 594 walinufaika na mafunzo ya awali na watumishi 968 walipata mafunzo ya muda mfupi na wengine 13,990 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (*TaGLA*). Katika mwaka huu wa fedha hadi Machi, 2017, Wakala umeendelea kuwajengea uwezo watumishi wa umma kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo maalum ya muda mfupi kwa kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Wakala ya Serikali Mtandao (*eGA*) imeendelea kuratibu, kusimamia na kukuza matumizi ya TEHAMA Serikalini ili kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa usalama, urahisi na kwa gharama nafuu. Katika mwaka huu wa fedha hadi kufikia Machi wameweza kutekeleza shughuli zifuatazo:-

Moja ni Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa vituo vikuu vyta kuhifadhi taarifa na mifumo ya Serikali au *data center* imekamilika na vituo hivi kuanza kutumika. Vilevile jumla ya taasisi 63 za Serikali zimeweza kuunganishwa na mfumo wa mawasiliano kwa njia ya barua pepe na kufanya taasisi zilizounganishwa hadi sasa kutumia mfumo huo kufikia taasisi 201. Aidha, Kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali, mifumo mbalimbali ya TEHAMA imetengenezwa kama ilivyoelezwa katika ukurasa wa 52 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, pia mfumo wa kutoa huduma kwa njia ya simu za mkononi umeboreshwa kwa kutengeneza miundombinu ya kutoa huduma ya ujumbe mfupi kupidia namba maalum \*152\*00# ambapo mpaka sasa jumla ya taasisi 28 za Serikali zinatumia huduma hii ya *mobile platform*.

Mheshimiwa Spika, pia mfumo wa kielektroniki wa masijala au *e-Office* umetengenezwa ili kurahisisha ubadilishanaji wa nyaraka na utoaji wa maamuzi Serikalini. Mfumo huu unatumia hadi sasa na Taasisi sita za Serikali kama majaribio na kuwezesha kazi kufanyika katи ya Dar es Salaam na Dodoma kama Ofisi moja. Majaribio yatakapokamilika yataenda katika taasisi zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya TEHAMA imetolewa kwa kuandaa na kurusha vipindi vya runinga kupidia televisheni ya Taifa na tovuti ya wakala. Aidha, jumla ya vipindi 52 vimeandaliliwa na hadi sasa vipindi vitatu vimekwisharushwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa mwaka 2016/2017 walilitengewa shilingi bilioni 6.441 na katи ya fedha hizo shilingi bilioni 5.441 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni moja kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2017, shilingi bilioni 3.2 za matumizi ya kawaida zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kwa upande wa miradi ya maendeleo, shilingi milioni 123.4 nazo pia zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Viongozi wa Umma 15,881 walitumiwa fomu za tamko la rasilimali na madeni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2016. Hadi kufikia Machi, mwaka huu jumla ya Viongozi 15,346 sawa na aslimia 97.3 wameweza kurejesha fomu hizo. Haya ni mafanikio makubwa ukilinganisha na kipindi cha miaka ya nyuma. Aidha, kwa viongozi walioshindwa kurejesha matamko yao kwa wakati wamefuatiliwa.

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/2017, viongozi 116 walihakikiwa mali zao na taarifa zao. Kwa Viongozi walioonekana kuwa na tofauti au kasoro katika matamko yao wanafanyiwa ufuatiliaji wa karibu. Pia viongozi 15,524 waliweza kusaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu na kwa ambaao hawajasaini wanaendelea kupatiwa elimu ya umuhimu wa kusaini hati hiyo. Taarifa kamili ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 55 mpaka wa 60 wa hotuba ambayo mmegawiwa.

Mheshimiwa Spika, upande wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, wameendelea kutafuta wataalam wenye ujuzi na kuandaa mfumo wa Kanzidata za wataalam hao ili kurahisisha utaratibu wa ajira, kuandaa orodha ya wahitimu wa vyuo vikuu na wataalam wenye weledi ili kurahisisha rejea na ujazaji wa nafasi wazi za ajira katika utumishi wa umma. Pia wameweza kutangaza nafasi wazi za kazi zinazotokea katika utumishi wa umma na kufanya usaili na kuwashauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na mchakato wa ajira.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2016/2017, Sekretarieti ya Ajira ilidhinishiwa Jumla ya shilingi bilioni 2.205 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, mwaka huu 2017, shilingi bilioni 2.121 zilikuwa zimepokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Sekretarieti ya Ajira imehakiki vyeti vya waombaji kazi 39,511 na kati ya hao 1,951 walibainika kuwa na vyeti vya kughushi na wahusika wallondolewa katika mchakato wa ajira pamoja na vyeti hivyo kuchukuliwa na kuwasilishwa kwa mamlaka husika kwa ajili ya hatua zaidi. Taarifa kamili ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 60 mpaka wa 63 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Tume ya Utumishi wa Umma nao pia wameendelea kuhakikisha kwamba masuala ya rasilimaliwaitu katika utumishi wa umma yanatekelezwa kwa kuzingatia sheria, kanuni, miongozo na

taratibu zilizopo ili kuimarisha utendaji unaozingatia malengo na matokeo yanayopimika. Aidha, Tume ni mamlaka ya rufaa kwa watumishi wa umma dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka zao za nidhamu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017, Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa shilingi bilioni 3.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Machi, 2017 shilingi bilioni 3.738 zilikuwa zimeshapokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Umma katika Mwaka huu wa Fedha ilitekeleza majukumu yafuatayo kwa muhtasari:-

(1) Rufaa 75 ziliamuliwa, ambapo kati ya hizo 14 zilikubaliwa, 49 zilikataliwa na 12 zilitupiliwa mbali kwa kuwa zilikatwa nje ya muda.

(2) Vilevile, malalamiko 47 ya Watumishi wa Umma yalitolewa uamuvi pamoja na ukaguzi wa kawaida wa rasilimaliwater ulifanyika katika Taasisi 41 ambazo ni Idara Zinazojitegemea mbili, Sekretarieti za Mikoa tano, Wakala tatu, Taasisi ya Umma moja, pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa 30.

(3) Pia, ukaguzi maalum ulifanyika katika Manispaa ya Kinondoni. Taarifa kamili inaonekana katika ukurasa wa 63 mpaka wa 65.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma. Katika Mwaka wa Fedha wa 2016/2017, iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 1.859 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu, shilingi milioni 926.5 zilipokelewa na kutumika. Maeleo yanaonekana kwa kina katika ukurasa wa 65 na 66 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2016/2017, Bunge iliidhinisha shilingi bilioni 27.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo kwa Taasisi ya Ufutililaji wa Utekelezaji wa Miradi (*PDB*). Kati ya fedha hizi, shilingi

milioni 397.2 ni matumizi ya kawaida na bilioni 27.2 ni za miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2017 shilingi bilioni 3.4 za fedha za miradi ya maendeleo zilipokelewa na kutumika. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 kwa shughuli zilizotekelawa na *PDB* ni kama zinavyoonekana katika ukurasa wa 66 mpaka wa 68 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa wameendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa usimamizi wa Kumbukumbu na nyaraka za Taifa na kusimamia utekelezaji wa kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu. Kwa mwaka huu wa fedha 2016/2017, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka waliiidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 1.2 hadi kufikia Machi, mwaka huu 2017 shilingi milioni 990.7 ziliweza kupokelewa na kutumika kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka waliweza kuweka mfumo wa kuhifadhi taarifa, Kumbukumbu na Nyaraka kwa njia ya kielektroniki. Waliweza kuchambua, kuorodhesha na kuhamisha kumbukumbu kutoka katika baadhi ya taasisi za Serikali kwenda katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pia wameweza kutambua na kuratibu ukusanyaji wa vitu na kumbukumbu za Waasisi wa Taifa letu. Mwisho, wameweza pia kusimamia na kutoa mwongozo kwa taasisi za umma zilizohamia Makao Makuu ya Serikali Dodoma kuhusiana na namna bora ya kuhamisha kumbukumbu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi au *OGAB*. Wameendelea kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uchumi wa mafuta na gesi kwa Baraza la Mawaziri. *OGAB* wameweza kuidhinishiwa shilingi bilioni 1.036 kwa matumizi ya kawaida hadi kufikia Machi, mwaka huu shilingi milioni 141.9 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa mapendeleko ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 kwa Mafungu 20, 30, 32, 33, 67, 94, 09, 04 na 11 imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015, Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/2018 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoainishwa na Serikali ya Awamu ya Tano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(1) Kutoa huduma kwa Mheshimiwa Rais pamoja na familia yake pamoja na ushauri kwa Mheshimiwa Rais katika maeneo mbalimbali.

(2) Pia imepanga kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (*IMTC*) pamoja na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri.

(3) Aidha, Ikulu imepanga pia kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma na wananchi.

(4) Pia Ofisi ya Rais Ikulu imepanga kukarabati Ikulu Ndogo za Mwanza, Shinyanga, Mbeya na Moshi, pamoja na kukarabati nyumba 12 za watumishi katika Ikulu Ndogo ya Chamwino pamoja na nyumba moja iliyopo Dodoma Mjini na ujenzi wa Ikulu mpya ya Chamwino.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, TAKUKURU imepanga kuendelea na ukamilishaji wa uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza.

Pia wamepanga kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2007 ili kujumuisha makosa ya uhujumu uchumi na kutaifisha mali zilizopatikana na njia ya rushwa na ujisadi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa MKURABITA wamepanga kutekeleza kazi zifuatazo ikiwemo:-

(i) Kukamilisha uandaaji na utoaji wa hati za hati miliki za kimila 11,184,000 katika Halmashauri za Wilaya 14; na

(ii) Kufanya urasimishaji wa ardhi vijiji ni katika eneo la Chanjamjawiri, Wilaya ya Chake Chake - Pemba na Mahonda, Wilaya ya Kaskazini B - Unguja.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa *TASA* fimepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo yote ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ambapo matarajio ni kufikia kaya za walengwa 355,000 katika vijiji, mitaa na shehia 5,690;

(ii) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini zipatazo milioni 1.1 nchini kote;

(iii) Kufanya uhakiki ili kupata wanufaika wapya wa mpango na kuziondoa kaya za walengwa zilizoboreka baada ya kupokea ruzuku kwa miaka mitatu mfululizo na kwa wasiostahili kuwemo kwa sababu mbalimbali kwa kuzingatia miongozo na taratibu; na

(iv) Kutoa ajira za muda kwa jumla ya kaya za walengwa 298,970 zitakazohusika katika utekelezaji wa ajira za muda.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Taasisi ya Uongozi watatekeleza yafuatayo:-

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

- (i) Watatoa mafunzo ya "Stashahada ya Uzamili katika Uongozi ili kuwajengea uwezo viongozi wa kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimali watu pamoja na rasilimali nyingine;
- (ii) Watakeleza programu ya kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara na taasisi za Serikali kwa kufanya majadiliano ya mikataba yenyenye thamani kubwa na namna ya kuunda timu za majadiliano zilizo madhubuti; na
- (iii) Watatoa kozi 18 za mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam ili kuwajengea uwezo viongozi katika maeneo ya uongozi na maendeleo endelevu kutohana na mahitaji na maombi ya walengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*) wamepanga kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kutoa mikopo 3,600 yenyenye thamani ya shilingi bilioni 2.4 sambamba na kutoa mafunzo ya awali na endelevu kwa wanufaika 4,000 na 2,000 mutawalia; na
- (ii) Wataendelea kujenga uwezo wa watendaji wa Mfuko wa *PTF* ili kutoa huduma bora kwa wateja.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Ofisi ya Rais, Ikulu, inaomba shilingi 16,267,586,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, inaomba kuidhinishiwa shilingi 747,885,035,000. Kati ya fedha hizi, shilingi 368,314,145,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 379,570,890,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake ni kama yanavyoonekana katika ukurasa wa 74 - 87 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Wakala zake kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 itatekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuhakikisha kwamba utumishi wa umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba sera, sheria, kanuni na taratibu mbalimbali za utumishi wa umma zinazingatiwa;
- (ii) Kujenga uwezo wa Serikali katika kuratibu utungaji na utekelezaji sera unaowiana ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii au *policy coherence*;
- (iii) Kuanzisha na kuhuisha miundo na mgawanyo wa majukumu ya taasisi za umma kutekeleza malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano iliyodhamiria kuongeza ufanisi katika utendaji kazi;
- (iv) Kusimamia utumishi wa umma kwa kutoa vibali vya uhamisho na uteuzi kwa watumishi wanaopendekezwa na waajiri mbalimbali kushika nyadhifa za uongozi;
- (v) Kuwezesha uhamisho wa watumishi mionganini mwa waajiri na kushughulikia maombi yanayowasilishwa ya vibali vya likizo bila malipo, vibali vya kuazimwa pamoja na kushikizwa;
- (vi) Kushughulikia malalamiko yatokanayo na ukiukwaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya utumishi wa umma na kuchukua hatua stahiki dhidi ya waajiri wanaolalamikiwa;
- (vii) Kuboresha michakato ya utoaji wa huduma na kuimarisha usimamizi wa mifumo na viwango vya utendaji kazi kwa kufanya ufuatiliaji na kutoa ushauri wa kitaalamu katika taasisi za Serikali;
- (viii) Kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni mbalimbali za mafunzo pamoja na kuratibu fursa zinazopatikana kwa ajili ya kujenga uwezo wa watumishi wa umma kufanya kazi kwa ufanisi na kuziwezesha taasisi za umma kuandaa mipango ya rasilimali watu na urithishanaji wa madaraka;

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

(ix) Kufanya vikao vya kazi na Sekretarieti za Mikoa yote na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(x) Kuboresha mfumo wa taarifa za kiutumishi na malipo ya mishahara katika ngazi zote na kuhuisha mfumo huo ili uweze kuendana na mahitaji ya sasa na teknolojia iliyopo;

(xi) Kuratibu utekelezaji wa miradi inayohusiana na Serikali ya mtandao chini ya programu ya *RC/P* pamoja na kuendelea na usanifu na uidhinishaji wa Programu ya Maboresho ya Utumishi wa Umma;

(xii) Itasimamia pia ajira za watumishi wa umma ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Serikali inatarajia kuajiri watumishi wa umma kwa kuzingatia vipaumbele na kuimarisha maeneo yenye upungufu mkubwa; na

(xiii) Kufanya kampeni na ufuatiliaji wa uzingatiaji wa maadili, utekelezaji wa ahadi za uadilifu na uzingatiaji wa maadili kwa watumishi wa umma pamoja na kujenga uelewa wa mfumo wa mikataba ya utendaji kazi kwa viongozi wa kisiasa na watendaji wakuu wa taasisi za umma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, tumeponga kuendelea kutoa mafunzo na ushauri wa kitaalam, kufanya utafiti pamoja na kutelekeza kazi nyinezo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (*TaGLA*) imepanga kutoa mafunzo kwa washiriki 2,500 katika maeneo ya uongozi, utawala bora, maadili, anuai za jamii, mazingira, kupunguza umaskini, afya na TEHAMA. Vilevile wakala wa *TaGLA* utakuza mtandao wake kikanda ili kuwafikia wateja walioko mikoani kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa upande wa Wakala ya Serikali Mtandao (*eGA*) inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kusimamia na kuendesha vituo vya kuhifadhi taarifa pamoja na mifumo ya TEHAMA ya Serikalini (*Government Data Centres*) kwa lengo la kuongeza usalama, kupunguza gharama na kujikinga na majanga;

(ii) Kuunganisha taasisi 80 kwenye mfumo wa pamoja na salama wa barua pepe wa Serikali na hivyo kuwa na idadi ya taasisi 281 zinazotumia mfumo salama wa mawasiliano serikalini na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi;

(iii) Kutengeneza mfumo wa kuwezesha ubadilishanaji taarifa ili kuondoa udurufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma; na

(iv) Kukamilisha uunganishwaji wa taasisi 77 zinazojumuisha hospitali za mikoa 19, Ofisi za Halmashauri 38 pamoja na Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa 20 za Serikali za Mitaa kwenye mfumo wa mawasiliano wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza Mpango wa mwaka wa fedha wa 2017/2018 kwa ufanisi, katika Fungu 32, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 33,695,038,000. Kati ya fedha hizi, shilingi 26,695,038,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 7,000,000,000 kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kwa kazi zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Rais, Utumishi pamoja na Wakala wake wa *TPSC, TaGLA* pamoja na *eGA* ni kama zinavyoonekana katika ukurasa wa 87 - 99 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa mwaka huu wa fedha unaokuja imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kupokea malalamiko ya viongozi wa umma kuhusu rasilimali na madeni yaliyopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(ii) Kufanya uhakiki wa matamko ya rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma 1,000, pamoja na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma; na

(iii) Kuanzisha mchakato wa kutumia mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili (*Ethics Management Information System – EMIS*).

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa shilingi 8,640,422,004 na kati ya fedha hizi shilingi 6,990,422,004 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,650,000,000 ni fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka cha fedha wa 2017/2018, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenyewe sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

(ii) Kuimarisha kanzidata ya kutunza taarifa za waliopangienda vituo vya kazi, taarifa za kada zenye wataalam wenyewe ujuzi maalum (*rare profession*) pamoja na taarifa za wahitimu wa vyuo vikuu nchini; na

(iii) Kuendelea kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira Zanzibar ili kurahisisha mchakato wa ajira kwa ajira za Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 3,115,975,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,365,975,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 750,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kufanya ukaguzi wa kawaida kwa taasisi 150 na ukaguzi maalum kwa taasisi 10 ili kuangalia uzingatiaji wa sheria, kanuni, miongozo na taratibu za usimamizi wa rasilimali watu katika utumishi wa umma;

(ii) Kujadili na kutoa uamuzi kwa taarifa za ukaguzi, rufaa, malalamiko na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa na Tume;

(iii) Kuelimisha taasisi na watumishi wa umma kuhusu majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma, utekelezaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi wa umma kupitia ziara za makamishna, vikao vya kazi, vyombo vya habari, machapisho na tovuti; na

(iv) Kuandaa taarifa ya hali ya Utumishi wa Umma na utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2016/2017 na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2017/2018, Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kutumia kiasi cha shilingi 4,909,515,670 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma inatarajia kufanya utafiti wa namna ya kutoa motisha kwa kuzingatia utendaji katika utumishi wa umma (*pay for performance*). Ili kutekeleza Mpango wa Bajeti wa mwaka wa fedha wa 2017/2018, Bodi inaomba kuidhinishiwa shilingi 1,721,977,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, wataendelea kutekeleza yafuatayo:-

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(i) Kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Taasisi za Umma 25 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 kwenda katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu, Dodoma;

(ii) Kujenga uwezo wa taasisi za umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali; na

(iii) Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa pamoja na kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu katika Kanda ya Ziwa - Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa 2017/2018, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa Sh.4,375,726,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,375,726,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 2,000,000,000 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka ujao wa fedha, Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta na Gesi majukumu yake yatakayotekelawa ni kama yanavyoonekana katika ukurasa wa 199 - 110 ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Baraza la Mawaziri wenye matokeo ya tafiti mbalimbali katika masuala yanayohusu uchumi wa mafuta na gesi pamoja na mambo mengine yanayohusiana na majadiliano ya mikataba. Ofisi hii inaomba kuidhinishiwa shilingi 711,073,000 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Spika, ili kujumuisha, mipango na bajeti ya mwaka wa fedha wa 2017/2018 ya mafungu yaliyotajwa yamezingatia vipaumbele na matakwa ya Serikali ya Awamu ya Tano yenye kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika utumishi wa umma ili kuondokana na matumizi mabaya ya rasilimali, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na urasimu katika utoaji wa huduma kwa wananchi na kuwa mifumo thabiti ya usimamizi wa utekelezaji. Tunaamini kuwa utumishi wa umma

uliotukuka ni chachu ya maendeleo kwa Taifa lolote duniani. Hivyo kama Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora tumejipanga kikamilifu kuhakikisha kwamba ofisi yetu pamoja na taasisi zake zinatoa mchango wake ulio bora katika kufikia malengo yetu kama Taifa na kuiwezesha nchi yetu kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaunga mkono kwa dhati juhudzi za Mheshimiwa Rais za kupiga vita rushwa, ubadhirifu wa mali ya umma na ujisadi. Tunaunga mkono hatua zinazochukuliwa na viongozi katika ngazi mbalimbali kwa kuzingatia sheria na kanuni za utumishi wa umma ili kurejesha nidhamu ya utumishi wa umma na kuboresha huduma kwa wananchi wetu. Naomba Waheshimiwa Wabunge na watu wenye mapenzi mema kwa nchi yetu waendelee kuunga mkono juhudzi hizi. Tumeanza kuona mafanikio lakini bado tunayo kazi kubwa ya kufanya mbele yetu.

Aidha, tunaunga mkono kwa nguvu zote uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma na Ofisi yangu imeshaanza kutoa huduma zinazohusiana na sera, mipango, utawala wa utumishi wa umma na kuwezesha wananchi kuonana na Viongozi Wakuu wa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha wa 2016/2017, naomba kuwasilisha maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

A. Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu  
i. Matumizi ya Kawaida shilingi 16,267,586,000

B. Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri  
i. Matumizi ya Kawaida shilingi 368,314,145,000  
ii. Miradi ya Maendeleo shilingi 397,570,890,000

Jumla shilingi 747,885,035,000

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

- C. Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma
- i. Matumizi ya Kawaida shilingi 26,695,038,000
  - ii. Miradi ya Maendeleo shilingi 7,000,000,000
  - Jumla shilingi 33,695,038,000
- D. Fungu 33 - Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma
- i. Matumizi ya Kawaida shilingi 6,990,422,004
  - ii. Miradi ya Maendeleo shilingi 1,650,000,000
  - Jumla shilingi 8,640,422,004
- E. Fungu 67- Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma
- i. Matumizi ya Kawaida shilingi 2,365,975,000
  - ii. Miradi ya Maendeleo shilingi 750,000,000
  - Jumla shilingi 3,115,975,000
- F. Fungu 94 -Tume ya Utumishi wa Umma
- i. Matumizi ya Kawaida shilingi 4,909,515,670
- G. Fungu 09- Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma
- i. Matumizi ya Kawaida shilingi 1,721,977,000
- H. Fungu 4 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa
- i. Matumizi ya Kawaida shilingi 2,375,726,000
  - ii. Miradi ya Maendeleo shilingi 2,000,000,000
  - Jumla shilingi 4,375,726,000
- I. Fungu 11 - Ofisi ya Ushauri ya Mafuta na Gesi Asilia
- i. Matumizi ya Kawaida shilingi 711,073,000

Mheshimiwa Spika, jumla kuu ya bajeti nayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2017/2018 ni kama ifuatavyo:-

- i. Matumizi ya Kawaida shilingi 430,351,457,674
- ii. Miradi ya Maendeleo shilingi 390,970,890,000
- Jumla shilingi 821,322,347,674

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya, ili muweze kuyajadili na kuyaiddhinisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

(*Hoja ilitolewa lamuliwe*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA ANGELAH JASMINE KAIRUKI (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA WA 2017/18 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

1. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30), Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33), Ufutiliaji wa Utekelezaji wa Miradi (Fungu 06), Ushauri wa Mafuta na Gesi (Fungu 11), Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32), Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67), Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94), Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09), na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04). Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

2. *Mheshimiwa Spika*, Kwanza namshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuniamini katika nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Umma na Utawala Bora; ninamuahidi kuwa nitaendelea kutekeleza wajibu wangu kwa ufanisi wa hali ya juu na uadilifu. Aidha, nawashukuru Wajumbe wa Vyama vya Wafanyakazi na Wafanyakazi kwa ujumla kwa kuendelea kunipatia ushirikiano ninapoendelea kuwawakilisha. Vilevile, naishukuru familia yangu kwa dhati ya moyo wangu kwa ushirikiano wanaonipatia na kuwa wavumilivu ninapotekeleza majukumu yangu.

3. ***Mheshimiwa Spika***, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jasson Samson Rwekiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcchema, Mbunge wa Viti Maalum Tabora Mjini kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2016/17 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18. Maoni na ushauri wa Kamati hiyo umetuwezesha na utaendelea kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

4. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaohimiza uadilifu, uwajibikaji na utendaji wenye matokeo katika Utumishi wa Umma. Aidha, namponge kwa uamuzi wake wa kijasiri wa kuhamishia Serikali Dodoma, uamuzi ambao ulikuwa mgumu kufanyika kwa zaidi ya miaka arobaini. Pili, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

5. ***Mheshimiwa Spika***, Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, kwa uongozi wake shupavu wa Serikali ya Zanzibar na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa

Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa moyo wake wote.

6. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuwa nguzo muhimu ya utekelezaji, usimamiaji na uratibu wa kazi za kila siku za Serikali na kuwa Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni. Aidha, nampongeza kwa kusimamia vizuri utekelezaji wa uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma kwa awamu.

7. ***Mheshimiwa Spika***, naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa busara na hekima. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa umahiri na kazi nzuri wanayoifanya ya kuliongoza Bunge lako Tukufu.

8. ***Mheshimiwa Spika***, Nawapongeza pia Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio wanayoendelea kuyapata katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Kwa namna ya pekee, nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa George Boniface Simbachawene (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, na Naibu wake Mheshimiwa Selemani Said Jafo (Mb), kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais.

9. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ambao ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Kabudi (Waziri wa Mambo ya Katiba na Sheria) kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa msiba wa Mbunge Mheshimiwa Dkt. Elly Macha, tunaomba Mola aiweke roho ya marehemu pema peponi, Amina!

10. ***Mheshimiwa Spika***, nawashukuru Balozi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Bwana Alphayo Japani Kidata, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean J. Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Bi. Susan Paul Mlawi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Tume na Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati.

11. ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kushukuru na kuwataja wachache ambao ni:- China, Japan, Uingereza, India, Korea ya Kusini, Ujeruman, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Indonesia, Brazil, Italia, Malaysia, Misri, Pakistan, Singapore, Thailand, Ubelgiji, Ireland, Israel. Vilevile, nashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia, OFID-OPEC Fund for International Development, Japan (JICA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii wa Japan (Japanese Social Development Fund), DfID, KOICA, GIZ, DFATD, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, NORAD na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

12. ***Mheshimiwa Spika***, mwisho kabisa ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa, uzalendo wao, ari yao na imani yao kwa Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli; hayo yamewezezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwashudumia wananchi.

13. ***Mheshimiwa Spika***, naomba kulithibitishia Bunge lako tukufu kwamba Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaendelea kutekeleza maelekezo yaliyotolewa katika hotuba ya Rais wa Jamhuri

ya Muungano wa Tanzania wakati akifungua Bunge la 11 yaliyohusu kupunguza urasimu ili kuongeza kasi ya utekelezaji, kubana matumizi na kurejesha nidhamu ya Serikali na Utumishi wa Umma kwa kuongeza uwazi na kusimamia sheria, kanuni na taratibu za uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ili wawajibike kwa wananchi ambaa ndio wateja na waajiri wakuu wa watumishi wa umma. Vilevile, tunamuunga mkono Mheshimiwa Rais katika vita dhidi ya rushwa, ubadhirifu, ujisadi, uzembe, uvivu, ukiukwaji wa maadili na utumishi hewa kwa kuwawajibisha wanaodhihirika kujihusisha na vitendo hivyo. Hatua anazoendelea kuchukua Mheshimiwa Rais zinatakiwa kuungwa mkono na Bunge lako Tukufu pamoja na wale wote wanaoitakia mema nchi yetu. Dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwa na Serikali inayowahudumia wananchi wa kawaida itatimia kwa Watumishi wa Umma wote kufanya kazi kwa juhud, maarifa na uadili fu mkubwa. Tunaendelea kusisitiza utoaji wa huduma bora, kwa haraka na kwa staha ili kuwaondolea wananchi usumbu.

14. ***Mheshimiwa Spika***, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki yakiwemo Tetemeko lilitotokea Mkoa wa Kagera, ajali na mafuriko yaliyotokea katika sehemu mbalimbali nchini. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema, peponi. Amina.

15. ***Mheshimiwa Spika***, hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni: Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 pamoja na Mpango wa Utekelezaji na Maombi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18.

#### **B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA 2016/17**

16. ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa 2016/17 ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Mpango wa Maendeleo wa

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Miaka Mitano (2011/12 – 2015/16) na llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015. Shughuli zilizotekelawa na kila Taasisi ni kama ifuatavyo:-

**OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE**

17. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Fungu:20 Ofisi ya Rais, Ikulu liliidhinishiwa **Shilingi 14,962,054,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi 11,063,163,664** zilipokelewa na kutumika.

**OFISI YA RAIS NA SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI**

18. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri (Fungu 30) linalojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, liliidhinishiwa **Shilingi 793,164,600,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 362,715,571,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 430,449,029,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi 547,583,679,331** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 260,648,784,846** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 286,934,894,485** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**(a) Ikulu**

19. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatalia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, shughuli zifuatazo zilitkelezwaza:-

(i) Huduma kwa Rais na familia yake ziliendelea kutolewa;

(ii) Huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya uchumi, siasa, masuala ya jamii, sheria, mawasiliano na habari kwa umma, uhusiano wa kimataifa na maeneo mengine zilitolewa kwa ajili ya kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(iii) Mikutano 31 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, ambapo nyaraka 49 zilichambuliwa. Mikutano 17 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 26 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano 9 ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 28 zilijadiliwa na kufanyiwa maamuzi. Aidha, mikutano 14 ya kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika na mada mbalimbali ziliwasilishwa na kujadiliwa;

(iv) Mkutano wa Tathmini wa Mwaka kati ya Wakurugenzi wa Sera na Mipango/Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri kwenye Wizara na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ulifanyika tarehe 13-17 Februari, 2017, Dodoma. Katika Mkutano huo, Taasisi ya Uongozi ilitoa mafunzo yaliyohusu masuala ya uongozi na uchambuzi wa sera. Aidha, mafunzo kuhusu maandalizi ya Nyaraka mbalimbali za Baraza la Mawaziri yalitolewa;

(v) Hotuba 18 za Mheshimiwa Rais zilichapishwa na kutangazwa kwenye vyombo mbalimbali via habari nchini. Aidha, Vipindi Maalum via Televisheni 24 vinavyojulikana kwa jina la "Makala ya Rais" vilitengenezwa na kurushwa hewani kwenye vyombo mbalimbali via habari;

(vi) Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, Awamu ya Tatoo (2016–2022) ulizinduliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 10 Desemba, 2016 katika Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Duniani;

(vii) Vikao 5 vya Kamati ya Taifa ya Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (OGP) vilifanyika kwa ajili ya kutathmini utekelezaji wa Mpango Kazi wa OGP. Aidha, warsha ya wadau ya kujadili na kutoa maoni kuhusu Mpango huo ilifanyika mwezi Septemba, 2016, Dar es Salaam;

(viii) Rufaa 101 za Watumishi wa Umma na Mamlaka za Nidhamu zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa uamuzi ambapo kati ya hizo, Rufaa 89 zilitolewa uamuzi na wahusika kujulishwa. Aidha, malalamiko 600 ya Watumishi

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

wa Umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo;

(ix) Kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ilishiriki katika kutoa majibu na ushahidi kwenye kesi za madai 8 zinazohusu Watumishi wa Umma na wananchi wengine zilizoko Mahakama Kuu dhidi ya uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Katibu Mkuu Kiongozi;

(x) Vikao 4 vya uratibu na uendeshaji wa maboresho chini ya Katibu Mkuu Kiongozi kujadili mafanikio, changamoto na mipango ya baadae ya maboresho vilifanyika;

(xi) Ufutiliaji wa mifumo iliyosimikwa na Programu za Maboresho katika Ngazi za Wizara na Mikoa ya Shinyanga na Simiyu ulifanyika;

(xii) Zahanati ya Ikulu imetoa matibabu kwa watumishi 1,466. Kati ya hao, wanaume ni 847 na wanawake 619. Aidha, Watumishi wa Zahanati walifanya ziara katika Ikulu Ndogo 9 na kufanya upimaji wa afya za Watumishi na familia zao na kutoa ushauri nasaha. Ikulu Ndogo zilizotembelewa ni Chamwino, Dodoma, Mwanza, Lushoto, Tabora, Shinyanga, Arusha, Moshi na Tabora;

(xiii) Watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI na familia zao wamepata huduma muhimu za dawa, lishe na ushauri nasaha kupitia Zahanati ya Ikulu; na

(xiv) Ufutiliaji na ukaguzi wa Miradi ya TASAF na MKURABITA umefanyika katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe, Morogoro, Dodoma pamoja na Unguja na Pemba. Aidha, miradi ya utoaji wa mikopo kwa vijana na wanawake inayotekelizwa na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea katika Mikoa ya Njombe miradi 4 na Morogoro miradi 3 ilikaguliwa.

**(b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)**

20. *Mheshimiwa Spika*, TAKUKURU imeendelea kutekeleza jukumu lake kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329, ambalo ni kuelimisha umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya Sheria na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya rushwa. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Uchunguzi wa majalada 376 ulikamilika na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kuombewa kibali cha kuwafikisha watuhumiwa Mahakamani. Majalada 157 kati ya yaliyopelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani;

(ii) Kesi 706 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 227. Katika kipindi hiki, kesi 264 ziliamuliwa mahakamani ambapo kati ya hizo, kesi 161 watuhumiwa wake waliachiwa huru na kesi 103 watuhumiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini. Aidha, kesi 33 zillondolewa mahakamani kutokana na sababu mbalimbali. Kesi 409 zinaendelea mahakamani;

(iii) Shilingi bilioni 12.316 ziliokolewa kutokana na operesheni zilizofanywa na TAKUKURU na kurejeshwa Serikalini. Kati ya fedha zilizookolewa, Shilingi bilioni 8.009 zilitokana na ukwepaji ushuru (EFDs), Shilingi bilioni 2.6 zilitokana na ubadhirifu, Shilingi milioni 912.396 zilitokana na mishahara hewa na Shilingi milioni 794.182 ziliokolewa kutoka katika maeneo mengine. Aidha, nguvu kubwa imeelekezwa kudhibiti rushwa katika eneo la ukusanyaji mapato ya Serikali, uzuiaji wa malipo hewa na ukaguzi wa miradi ya maendeleo;

(iv) Kutokana na kuimarika kwa Kitengo cha ufuatiliaji na urejeshaji wa mali, TAKUKURU imefanikiwa kutaifisha nyumba 6 ambapo 5 ziko Buhongwa na moja iko

Ilemela Mkoani Mwanza pamoja na magari 4 ambayo ni Toyota Chaser 2, Toyota Land Cruiser 1 na Mitsubishi Fuso 1 zilizopatikana kwa njia ya rushwa;

(v) Utafiti wenyе lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mianya ya rushwa katika Sekta za Uhamiaji na Afya umefanyika. Kazi hizo ni uchambuzi wa mianya ya rushwa katika mfumo wa utoaji wa hati za kusafiria na tathmini ya uzingatiaji wa sheria na kanuni za uanzishajji na usimamizi wa maduka ya dawa muhimu;

(vi) Kazi 246 za uchambuzi wa mifumo na warsha/vikao 106 vya wadau kujadili matokeo ya kazi za utafiti na uchambuzi wa mifumo kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa viliifanyika katika maeneo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kilimo, Mifugo, Uchukuzi, Ardhi, Ujenzi, Mahakama, Blashara, Huduma za jamii, Fedha, Afya, Maji, Madini, Viwanda, Misitu, Nishati na Elimu. Aidha, kazi 18 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yatokanayo na mapendelekezo ya uchambuzi wa mifumo zilifanyika;

(vii) Elimu kuhusu athari za rushwa ilitolewa kuititia njia mbalimbali zikiwemo semina 1,912, mikutano ya hadhara/mijadala ya wazi 1,297, vipindi vya redio na televisheni 168, vipindi vya televisheni 8, maonesho 125 na taarifa kwa umma 57 zilitolewa kuititia vyombo vya habari. Aidha, habari/makala 185 ziliandaliwa kwa ajili ya wavuti na nakala za machapisho 16,000 zilisambazwa. Katika uelimishajji huo, wananchi 476,944 walifikiwa ana kwa ana. Idadi hiyo haihusishi walifikiwa kwa njia ya redio, runinga na machapisho;

(viii) Kundi la vijana limeendelea kuwa ajenda muhimu ambapo vijana walio shulen, vyuoni na walio nje ya shule walipatiwa elimu kuhusu rushwa na kuwasisitiza kuijunga na klabu za wapinga rushwa kwa lengo la kuwajenga kimaadili. Klabu mpya za wapinga rushwa 291 zilifunguliwa na 1,560 ziliimarishwa;

(ix) Kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Umma, TAKUKURU ilishiriki katika maadhisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa. Kauli mbiu ya maadhisho hayo ilikuwa kujenga na kukuza maadili, haki za binadamu, uwajibikaji, utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa ambapo wananchi walipata fursa ya kufahamishwa mambo mbalimbali kupitia midahalo, matembezi ya hiari na wiki ya kuwapatia huduma wananchi;

(x) Kampeni ya Longa Nasi iliyobuniwa kuwahamasisha wananchi kutoivumilia rushwa na namna ya kuifikia TAKUKURU kutoa taarifa za vitendo vya rushwa imeendelea katika Mikoa yote kupitia njia za mikutano ya hadhara, vipindi vya redio na runinga inayojazwa upepo vilifikia Mikoa ya Shinyanga, Geita na Simiyu;

(xi) Kituo cha Huduma kwa Mteja kimesaidia kutoa elimu na msaada wa haraka kwa wananchi hususan wanaoombwa rushwa au kucheleweshwa kupatiwa huduma kwa kuwa kinafanya kazi saa ishirini na nne. Wananchi wameweza kuifikia TAKUKURU kwa kupiga simu namba 113, kutuma ujumbe kwenda namba hiyo au kutoa taarifa kwa kupiga \*113# yaani mfumo wa USSD (*Unstructured Supplementary Service Data*). Katika kipindi husika, malalamiko 199,337 yamepokelewa ambapo malalamiko 35,804 yalikuwa kwa njia ya simu, 157,481 kupitia ujumbe mfupi wa simu na 6,052 kupitia USSD;

(xii) Watumishi 214 walipatiwa mafunzo ili kuwajengea uwezo wa kumudu majukumu yao kwa ufanisi. Kati ya hao, watumishi 199 walipata mafunzo ndani ya nchi na watumishi 15 walipata mafunzo nje ya nchi; na

(xiii) Ujenzi wa jengo la makazi ya Mkuu wa TAKUKURU Wilaya ya Bahi umekamilika. Jengo hili litatumika kama Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Bahi mpaka hapo jengo la ofisi litakapojengwa.

**(c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

21. *Mheshimiwa Spika*, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) unaendelea kuchukua hatua mbalimbali ili kuwawezesha wananchi wanaomiliki rasilimali na biashara nje ya mfumo rasmi kuwa na uwezo wa kurasimisha mali na hatimaye kushiriki katika uchumi wa soko unaoendeshwa kwa mujibu wa Sheria. Ili kufikia azma hii, MKURABITA inao wajibu wa kuwawezesha Watanzania kutumia mali zao zilizokwisharasmishwa kama dhamana katika kupata mikopo na fursa nyiningine katika uchumi wa soko. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitkelezwa:-

(i) Uandaaji wa Hati za Haki Miliki za Kimila 8,790 umefanya katika Halmashauri za Wilaya 7 za Buhigwe, Uvinza, Mpimbwe, Ikungi, Karagwe, Mkuranga na Nachingwea;

(ii) Ujenzi wa Masjala 2 za Ardhi za Vijiji vya Pwaga na Munguwi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa umekamilika. Aidha, MKURABITA imekamilisha ujenzi wa Masjala 1 ya Ardhi katika Shehia ya Kiungoni, Wilaya ya Wete, Pemba;

(iii) Kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Kituo kimoja cha kurasimisha biashara (one stop centre) kimeanzishwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ambapo huduma muhimu za utoaji wa leseni za biashara, utoaji wa Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi (TIN), usajili wa jina la biashara (BRELA), huduma za benki, na Mifuko ya hifadhi ya Jamii zinapatikana sehemu moja. Hadi kufikia Machi, 2017 Kituo kimesajili biashara 3,222 ambapo Shilingi milioni 343 zimekusanywa kutokana na ada za leseni;

(iv) Mafunzo ya kuwajengea uwezo wakulima kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kukuza mitaji yao yametolewa kwa wakulima 1,068 na Viongozi 219 wa vyama vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya za Mwanga (Vijiji

vya Kivulini na Kileo), Meru (Vijiji vya Maweni na Karangai), Mbinga (Vijiji vya Tanga na Tukuzi), Sumbawanga (Kijiji cha Mshani), Kalambo (Kijiji cha Katuka), Korogwe (Vijiji vya Mnyuzi na Kwagunda), Karagwe (Kijiji cha Nyakayanja), na Kilombero (Vijiji vya Idete A na B). Aidha, Mipango Kazi ya Jamii ya Vijiji imetekelезwa kwa kuanzisha vikundi 31 vya uzalishaji, mashamba darasa 4 na SACCOS 3;

(v) Uandaaji wa mwongozo kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Majaribio ya Urasimishaji kwa kutumia dhana ya Mfuko wa Dhamana katika Manispaa ya Iringa na Halmashauri 2 za Mkoa wa Songwe umekamilika;

(vi) Kwa kushirikiana na Ofisi za Taifa za Takwimu Tanzania Bara na Zanzibar, MKURABITA imeandaa Hadidu za Rejea pamoja na Zana za utafiti (Dodoso) ambazo zitatumika kwa ajili ya utafiti na tathminu ya sekta isiyo rasmi nchini. Aldha, MKURABITA imekamilisha uandaaji wa Dhana ya Andiko kwa ajili ya kutafuta fedha za utafiti;

(vii) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Elimu Tanzania, MKURABITA imeshiriki katika uchambuzi wa takwimu na kuandaa ripoti ya matokeo ya utafiti kwa ajili ya utangamano wa dhana za urasimishaji katika Mtaala wa Elimu ya Msingi ambapo washiriki wengi wanaona umuhimu wa kuingiza dhana ya urasimishaji katika Mitaala; na

(viii) MKURABITA iliwasilisha mada katika Vikao vya Kamati za Ushauri za Mikoa ya Singida na Dodoma kwa lengo la kuendelea kutoa elimu ya urasimishaji kwa wadau katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**(d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

22. ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya ukuzaji wa uchumi, kuongeza fursa na kupunguza umaskini wa kipato; kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na utawala bora na uwajibikaji.

23. *Mheshimiwa Spika*, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitkelezwa:-

(i) Jumla ya kaya maskini 1,358,268 zimetambuliwa tangu Mpango wa kunusuru kaya maskini uanz. Kati ya hizo, kaya maskini 1,110,377 zenyе jumla ya watu 5,895,230 zimeandikishwa. Kati ya kaya/watu wote waliomo katika Mpango, asilimia 54 ni wanawake. Mpango huu unatekelezwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa za Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar. Aidha, jumla ya Shilingi bilioni 202.2 zilihawilishwa kama ruzuku kwa kaya maskini;

(ii) Mpango wa kutoa ajira za muda umetekeleza jumla ya miradi 3,553 kutoka katika Vijiji 2,063, Mitaa 329 na Shehia 168 jumla yake ni 2,560 ambapo kaya za walengwa 298,970 zilipata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar. Miradi hiyo ina thamani ya Shilingi bilioni 32. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji, uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti, uchimbaji wa visima vifupi, uboreshaji wa barabara, uhifadhi wa vyanzo vya maji, na hifadhi ya mazingira. Aidha, jumla ya wawezeshaji 953 wa ngazi ya Halmashauri na 231 kwa upande wa Unguja na Pemba walipewa mafunzo ya uandaaji wa miradi na usimamizi;

(iii) Zoezi la uhakiki wa kaya maskini ambalo ni endelevu lilitanyika na kubaini kuwepo kwa kaya 68,914 nchini kote ambazo zilikosa sifa. Kaya hizi zote zimeondolewa kwenye Mpango. Mgawanyo wa kaya hizo ni kama ifuatavyo:

(a) Kaya zilizokuwa na mwanakaya mmoja ambaye alifariki au wote wamefariki ni 15,833;

(b) Kaya zilizohamia katika Vijiji/Mitaa/Shehia ambapo Mpango haujaanza kutekelezwa ni 8,436;

(c) Kaya ambazo hazikujitokeza mara tatu mfululizo kupokea ruzuku ni 20,914;

(d) Kaya ambazo wananchi walithibitisha kuwa siyo maskini ni 18,919; na

(e) Kaya ambazo baadhi ya wanakaya ni Wajumbe wa Kamati za Usimamizi za Jamii, Halmashauri za Vijiji/Kamati za Mitaa, Viongozi na Watendaji ni 4,812.

(iv) Ukusanyaji wa takwimu za hali halisi ya mahitaji ya miundombinu ya afya, elimu na maji kutoka katika maeneo yote ya utekelezaji 161 ulifanyika na uchambuzi wa takwimu unaendelea ili kutambua mahitaji ya kila eneo la utekelezaji. Jumla ya miradi 72 ya miundombinu ya elimu na afya yenye thamani ya Shilingi bilioni 4.8 imetekelezwa. Kati ya hiyo, miradi 70 imetekelezwa Tanzania Bara na miradi 2 imetekelezwa Zanzibar (Unguja 1 na Pemba 1). Aidha, mchakato wa kuibua miradi mipya umefanyika ambapo jumla ya Shilingi bilioni 1.9 zimeidhinishwa ili kutekeleza miradi 39 katika Mikoa ya Arusha na Njombe;

(v) Miongozo ya utekelezaji wa shughuli za kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya ilikamilika na kuanza kutumika katika utekelezaji. Miongozo hiyo ilitumika kutoa mafunzo ya stadi za ujasiriamali na mbinu za kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba kwa kaya za walengwa yametolewa kwa wawezeshaji 400 kutoka Halmashauri 18 za Tanzania Bara, Unguja na Pemba. Jumla ya vikundi 5,136 vya kuweka akiba na kuwekeza vyenye wanachama 73,914 viliundwa na jumla ya Shilingi milioni 572 zimetumika;

(vi) Mfumo wa Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Utambuzi, Uandikishaji, Malipo na Malalamiko ya Walengwa umekamilika na unatumika. katika Ofisi za TASAF zilizoko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 142 za Tanzania Bara pamoja na Unguja na Pemba zimeunganishwa na Makao Makuu ya TASAF kuititia mtandao wa mawasiliano wa TAMISEMI kwa Tanzania Bara na mtandao wa mawasiliano wa Kampuni ya Simu (TTCL) kwa Unguja na Pemba;

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

(vii) Katika kujenga uwezo wa wadau muhimu katika kutekeleza Mpango kwa ufanisi, mafunzo yalitolewa kwa Wakuu wa Mikoa 29; Makatibu Tawala 25 wa Mikoa; Wakuu wa Wilaya 134; Wakurugenzi 190 wa Halmashauri za Jiji/ Manispaa/Miji /Wilaya na Wasaidizi 9 wa Wakuu wa Mikoa. Kwa upande wa Zanzibar, mafunzo yalitolewa kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri 3; Wakuu wa Mikoa 5; Wakurugenzi 31 wa Uratibu; Maafisa Wadhamini 8, Makatibu 7 wa Baraza la Wawakilishi; Wakuu wa Wilaya 11, Wawakilishi 18, Makatibu Tawala 7 na Madiwani 5. Aidha, mafunzo yalitolewa pia kwa wawezeshaji 176,326 kutoka maeneo yote ya utekelezaji; Wajumbe 58,738 wa Kamati za Usimamizi za Jamii; watendaji 4,712 wa Vijiji, Mitaa na Shehia; Wenyevit 4,490 wa Vijiji, Mitaa na Shehia; walimu 5,174 wa shule za sekondari na msingi; wafanyakazi 2,464 wa afya, wajumbe 16,201 wa Halmashauri za Vijiji, Mitaa na Shehia; na washauri wafuatiliaji, waratibu na wahasibu wa Mpango 340. Pia, mafunzo ya stadi za maisha yametolewa kwa vijana 188 na wanajamii 986;

(viii) Tafiti mbalimbali zenye lengo la kupima ufanisi wa utekelezaji wa Mpango na matoeko yake zimeendelea kufanyika. Tafiti hizo zilihusu Tathmini ya Mpango; tathmini ya Mpango kwa maendeleo ya vijana; na tathmini kuhusu ushiriki na uwezeshwaji wa wanawake. Tafiti hizi ambazo ni za msingi zimekamilika kwa awamu ya kwanza. Awamu ya pili imepangwa kuanza Mwezi Aprili, 2017;

(ix) Mafunzo ya kujenga uelewa pia yamefanyika kwenye Sekretarieti za Mikoa ambapo wajumbe 512 wamejengewa uelewa kwenye Mikoa 26 ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhusu Mpango wa TASAF Awamu ya Tatu; na

(x) Ukaguzi wa ndani ulifanyika ili kuhakikisha endapo fedha zilitumika ipasavyo katika utekelezaji wa Mpango wa TASAF Awamu ya Tatu. Ukaguzi ulifanyika TASAF Makao Makuu pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa 46. Aidha, Wakaguzi wa Nje kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) walifanya ukaguzi wa uhawilishaji fedha kwa walengwa, manunuzi, uendeshaji na thamani ya fedha.

**(e) Taasisi ya UONGOZI**

24. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya UONGOZI imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha utaalam wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, Watumishi wa Umma na Mahakama.

25. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, shughuli zifuatazo zimetekelizwa:-

(i) Kozi 18 za muda mfupi zimetolewa kwa Viongozi wa Umma 631 ili kuimarisha utendaji wao. Kozi hizi ni kwenye maeneo ya Maadili, Utawala Bora na Uwajibikaji; Mawasiliano Fanisi na Mbinu za Uchambuzi Yakinifu; Mitazamo na Dira; Usimamizi wa Vihatarishi na Udhibiti wa Ndani; Uongozi wa Kimkakati; Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi; Ujuzi na Mbinu za Majadiliano ya Mikataba; Usimamizi wa Mipango yenye Matokeo; na Michakato ya Sera;

(ii) Maandalizi ya Programu ya "Stashahada ya Uzamili katika Uongozi" (Post Graduate Diploma in Leadership) yamekamilika. Programu hii inalenga kuwajengea viongozi uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimali watu na rasilimali nyingine na sifa binafsi za kiongozi. Programu hii itatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto kilichoko Helsinki, Finland. Awamu ya kwanza ya mafunzo/programu inatarajiwa kuanza mwezi huu wa Aprili, 2017 na itahusisha viongozi waandamizi wa Jeshi la Polisi ambapo awamu ya kwanza itahusisha viongozi 32;

(iii) Maandalizi ya Programu ya Mafunzo kuhusu "Majadiliano ya Mikataba ya Kimataifa ya Biashara" yatakayotolewa kikanda yamekamilika. Washiriki watatoka Tanzania, nchi nyingine Barani Afrika na Taasisi za Kikanda, zikiwemo Jumuuya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC)

na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). Utekelezaji wa Programu hii utaanza mwezi Aprili, 2017;

(iv) Kwa kushirikiana na Taasisi za ndani na nje ya nchi, mikutano 7 ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa ilifanyika kwa lengo la kukutanisha viongozi ili kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Jumla ya Viongozi 1,018 walishiriki kutoka Tanzania na nchi mbalimbali ndani na nje ya Afrika. Mikutano ifuatayo ilifanyika:-

(a) Kongamano la Kikanda la Viongozi wa Afrika juu ya "Namna ya Kuendeleza Biashara Barani Afrika" liliifanyika tarehe 28-29 Julai, 2016. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Mstaafu, Mhe. Benjamin William Mkaa;

(b) Kongamano la Kimataifa kuhusu "Sera zinazohusu Mabadiliko ya Tabia Nchi" liliifanyika tarehe 13-14 Julai, 2016. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya "Climate Strategies" ya Uingereza;

(c) Kongamano la Kimataifa juu ya namna ya "Kukuza Uwekezaji katika Sekta ya Misitu" liliandaliwa kwa kushirikiana na Serikali ya Finland na Taasisi ya Finn Fund. Kongamano hilo liliifanyika tarehe 15-16 Novemba, 2016;

(d) Kongamano la Kitaifa kuadhimisha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere liliifanyika tarehe 13 Oktoba, 2016. Mada kuu ilikuwa "Mafunzo kwa Viongozi wa Sasa na wa Kizazi cha Baadae". Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Ubalozi wa China hapa nchini na Taasisi ya Kukuza Urafiki kati ya China na Tanzania;

(e) Kongamano la kitaifa la viongozi juu ya "Nafasi ya Mashirika ya Umma katika Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano" liliifanyika tarehe 28 Februari, 2017. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina;

(f) Kongamano la Kitaifa kuhusu "Uhuru wa Nchi, Demokrasia na Maendeleo ya Jamii Afrika" lilitanyika tarehe 10 Machi, 2017. Kongamano hili liliandaliwa kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es salaam;

(g) Mkutano wa Kitaifa kujadili "Mikakati ya Tanzania katika kuelekea kwenye Uchumi wa Viwanda" ulifanyika tarehe 31 Machi, 2017. Mkutano huo uliandaliwa kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID).

(v) Vipindi 7 vya mahojiano na viongozi waandamizi na wataalam wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu viliandaliwa na kurushwa kwenye runinga na kuwekwa kwenye tovuti ya Taasisi na mitandao ya kijamii kwa nia ya kuimarisha na kujenga uwezo wa viongozi wa sasa na wanaochipukia. Vipindi hihi vinaoneshwa na kuonekana Bara zima la Afrika;

(vi) Programu Jumuishi juu ya masuala ya Maendeleo Endelevu imeanzishwa ili kuwezesha utekelezaji wa Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu. Programu hii inahusisha mafunzo, makongamano, na tafiti juu ya masuala ya maendeleo endelevu;

(vii) Maandalizi ya kuanzisha Programu ya utafiti juu ya "Masuala ya Uongozi Barani Afrika" yamekamilika;

(viii) Utafiti unaohusu "Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP)" umekamilika. Utafiti huu ulihuisha miradi 10 ya ubia katika Sekta za Nishati, Miundombinu na Mawasiliano Barani Afrika. Utafiti ulihuisha miradi kutoka Nchi za Tanzania, Nigeria, Ghana, Afrika ya Kusini na Kenya;

(ix) Utafiti kuhusu "Viwezeshi na Vikwazo vya Uongozi Barani Afrika" unaendelea kufanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Birmingham, Uingereza. Utafiti huu unazihusu nchi 5 ambazo ni Tanzania, Uganda, Afrika ya Kusini, Ethiopia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo;

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

(x) Chapisho kuhusu Maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mhe. Benjamin Mkapa liko katika hatua za mwisho, na linalohusu Maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mhe. Ally Hassan Mwinyi limeanza kuandaliwa. Lengo kuu ni kutoa machapisho (memoirs) kuhusu maisha binafsi na michango ya Marais wastaaufu;

(xi) Shindano la insha kwa vijana wa Afrika wenye umri kati ya miaka 18-25 lilifanyika kwa lengo la kuimarisha uwezo wa kujenga hoja na uelewa katika masuala ya Uongozi. Vijana 532 kutoka nchi 31 za Afrika walishiriki. Kati yao, vijana 111 walitoka Tanzania, sawa na asilimia 21 ya vijana wote walioshiriki. Washindi walikuwa 5, waliotoka Kenya 2, Nigeria 2 na Zimbabwe 1;

(xii) Zoezi kwa vijana wa Afrika kuhusu "Jinsi Teknolojia inavyoweza Kutumika Kuboresha Uwazi, Uwajibikaji na Ufanisi katika Taasisi za Umma" liliandaliwa kwa kushirikiana na Kituo cha Kikanda cha "*Young African Leadership Initiative*" (YALI). Lengo la zoezi hili ni kuwajengea uwezo wa uchambuzi wa masuala ya kisera na kiutendaji. Zoezi hili liliishirikisha vijana 13 kutoka Tanzania, Kenya, Rwanda, Sudani Kusini, Djibouti, Congo na Ethiopia. Matokeo ya zoezi hili yaliwasilishwa, na vijana husika walipatiwa mrejesho na wataalam;

(xiii) Programu Jumuishi ya Usimamizi wa Rasilimali za Taifa hususan katika Sekta ya Uziduaji (Mafuta, Gesi Asili na Madini) ilitekelezwa kama ifuatavyo:

(a) Mafunzo kwa ajili ya kuijengea uwezo Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mikataba ya Mafuta na Gesi Asili yalitolewa. Kozi 5 zilifanyika kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Columbia, Marekani;

(b) Maandalizi ya Programu ya mafunzo kuhusu "Majadiliano ya Mikataba katika Sekta ya Maliasili" yatakayofanyika kikanda yalikamilika. Programu hii itajikita katika masuala ya majadiliano ya mikataba katika maeneo ya Mabadiliko ya Tabia ya Nchi, Mafuta, Gesi na Madini;

- (c) Kongamano la Kikanda kuhusu jinsi ya kuongeza ushiriki wa makampuni ya ndani katika mnyororo wa thamani kwenye Sekta ya Uziduaji liliandaliwa kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kongamano hilo lilitifanyika tarehe 27-28 Oktoba, 2016 na kuhudhuriwa na viongozi na wataalam 93 kutoka ndani na nje ya Tanzania;
- (d) Tafiti 3 zinaendelea kufanyika ambazo ni Athari za Kimazingira katika Sekta ya Uziduaji; Uwekezaji na Matumizi Sawia ya Mapato ya Serikali yatokanayo na Sekta ya Mafuta na Gesi Asili; na Hali ya Sekta ya Uziduaji Nchini kwa mwaka 2016;
- (e) Makala 3 juu ya masuala ya uziduaji yaliandaliwa na kuchapishwa kwenye magazeti na tovuti ya Taasisi;
- (f) Uratibu na uwezeshaji wa shughuli za Timu ya Serikali ya Majadiliano ya Mikataba ya Mafuta na Gesi unaendelea kufanyika. Timu hiyo kwa sasa inaendelea na majadiliano na Makampuni ya Mafuta ya Kimataifa.

**(f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea**

26. ***Mheshimiwa Spika***, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umeendelea kutoa mikopo, mafunzo pamoja na ushauri wa kibiasahara kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Baadhi ya kazi zilizotekelze wa katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Mikopo 1,425 yenye thamani ya Shilingi milioni 907.30 imetolewa kwa vijana waliohitimu mafunzo katika Vyuo vya Ufundji Stadi vinavyotambuliwa na VETA na SIDO na wanawake wajasiriamali wa Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Njombe na Lindi;
- (ii) Walengwa 1,821 wa Mfuko walipata mafunzo ya ujasiriamali, namna ya kujitambua na taratibu za mikopo ya Mfuko;

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

- (iii) Tawi la Lindi limefunguliwa mwezi Novemba, 2016 ambapo Walengwa wa Mfuko 83 walipata mafunzo ya awali na walengwa 46 walipatiwa mikopo yenye thamani ya Shilingi milioni 17.5;
- (iv) Kwa kushirikiana na *Plan International*, mafunzo kwa vitendo kuhusu stadi mbalimbali za kazi kama vile ushonaji, utengenezaji wa batiki, n.k yamefanyika kwa vijana 104 wanaoishi katika mazingira magumu katika Mikoa ya Pwani na Morogoro;
- (v) Tafiti zilifanyika katika Mikoa ya Lindi na Njombe ambapo zilibaini utayari na uhitaji wa huduma za mikopo kwa kundi lengwa ni mkubwa na hivyo ni fursa nzuri kwa Mfuko kujipanua;
- (vi) Maofisa mikopo 10 walipata mafunzo ya utoaji huduma na sera za mikopo; na
- (vii) Maofisa 5 kutoka Matawi yote ya Mfuko walipata mafunzo yanayohusu uthibiti na usimamizi wa huduma za mikopo.

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZAKE**

27. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32) inayojumuisha Wakala zilizo chini yake liliidhinishwa jumla ya **Shilingi 30,341,137,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 22,791,137,000** ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 7,550,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 kiasi cha **Shilingi 18,704,565,589.28** zilikuwa zimepokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 18,014,565,589.28** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 690,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

28. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Wakala zake imeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakkisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Aidha, Watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi pale wanapotoa huduma mbalimbali kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa.

29. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

**a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

(i) Marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 yamefanyika ili kuiwezesha Serikali kutekeleza Sera ya Mishahara na Motisha katika Utumishi wa Umma ya Mwaka 2010 ambayo inalenga kuoanisha na kuwianisha mishahara mionganoni na baina ya watumishi wa Taasisi za umma;

(ii) Wizara zimeendelea kujengewa uwezo wa kuandaa Sera pamoja na kufanya tathimini ya utekelezaji wake katika sekta husika ambapo Timu ya Kitaifa ya Wataalam wa Sera inayoratibiwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilishirikiana na Wataalamu wa Wizara husika kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Aidha, Rasimu za Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki, Sera ya Taifa ya Serikali Mtandao na Sera ya Taifa ya Mazingira ziliandaliwa kwa mfumo huu;

(iii) Watumishi Housing Company - WHC imetekeliza jukumu la kujenga nyumba zenye gharama nafuu na kuwauzia Watumishi wa Umma kwa utaratibu wa mikopo. Chini ya WHC, Miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za watumishi inaendelea kutekelezwa katika maeneo ya Bunju (Mabwepande), Kigamboni (Gezaulole) na Watumishi Magomeni Flats (Dar es Salaam), Kisesa (Mwanza),

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

na Mizani Mkundi (Morogoro). Aidha, Kampuni inaendelea na maandalizi ya kujenga nyumba katika maeneo mbalimbali nchini; ambayo ni, Mailimoja Setelite City (Kibaha, Pwani), Njedengwa (Dodoma), Mangamba (Mtwara), Tunduma-Mpemba (Mbeya), Pongwe City (Tanga), Shinyanga (Shinyanga), Usa River (Arusha), na Mtwelo Beach (Lindi);

(iv) Vibali vya ajira mpya kwa nafasi 9,721 vimetolewa kwa waajiri ikijumuisha nafasi 3,174 kwa Jeshi la Polisi, 1,000 kwa Jeshilila Magereza, 852 kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, nafasi 297 kwa Jeshi la Uhamiaji pamoja na nafasi 50 kwa ajili ya ajira za wataalamu wa Afya katika Hospitali ya Mloganzila. Aidha, kibali cha ajira kwa nafasi 4,129 za walimu wa Masomo ya Sayansi na Hisabati pamoja na nafasi 219 kwa ajili ya kuajiri Mafundi Sanifu wa Maabara za shule vilitolewa na taratibu za ajira kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI;

(v) Uhakiki wa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 18,823 yenye thamani ya Shilingi 32,859,479,490.37 umefanyika na kuyaingiza kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mshahara kwa ajili ya malipo. Aidha, madai ya malimbikizo ya Mshahara ya Watumishi 12,973 yenye jumla ya Shilingi 21,615,565,432.71 bado yanaendelea kuhakikiwa;

(vi) Watumishi 19,708 wameondolewa kwenye Orodha ya Malipo ya Mshahara ya Watumishi wa Umma (Payroll) kutokana na kustaafuli, kuacha kazi, kufariki, kufukuzwa kazi na kumalizika kwa mikataba kwa lengo la kudhibiti watumishi hewa na mishahara batili;

(vii) Kufanya ukaguzi na uhakiki wa matumizi ya Rasilimaliwateri mionganoni mwa waajiri katika Mikoa yote Tanzania Bara kwa lengo la kuongeza uwajibikaji katika kusimamia rasilimaliwateri kwenye Taasisi za Umma;

(viii) Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili umefanyika katika Taasisi za Umma 30. Aidha, Ufuatiliaji umeonesha jumla ya makosa 313 kati ya 371 yaliyohusiana na ukiukwaji wa Maadili katika Taasisi hizo yalishughulikiwa.

Hii ni sawa na 84%. Kiwango cha jumla (overall annual score) cha ufuatilaji kwa Mwaka wa fedha wa 2016/17 kitatolewa baada ya kufanyika kwa ufuatilaji wa mwisho wa mwaka wa fedha 2016/17;

(ix) Mafunzo ya maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma yametolewa kwa Watumishi 9,763 kutoka katika Taasisi 20 za Umma. Aidha, viapo vya Ahadi ya Uadilifu kwa Watumishi wa Umma 165,481 kutoka katika Taasisi za Umma 172 vimematibowi;

(x) Elimu kuhusu Maadili ya Watumishi wa Umma imetolewa, ambapo jumla ya makala 2 zilitolewa na vipindi 2 vya Runinga vilirushwa kama sehemu ya maadhisho ya Kitaifa ya Wiki ya Uadilifu na Haki za Binadamu yaliyofanyika mwezi Disemba, 2016;

(xi) Ofisi imeendelea kusimamia na kuratibu mafunzo ya Watumishi wa Umma katika ngazi mbalimbali ili kuwajengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Watumishi wa Umma 654 walihudhuria mafunzo mbalimbali nje ya nchi kupitia ufadhili wa Serikali kama ifuatavyo:- India (302), Japan (91), China (44) Jamhuri ya Korea Kusini (66), Australia (36), Uhlanzi (106) na Misri (9);

(xii) Taasisi za Umma zimeendelea kuwezeshwa kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu na Mipango ya Urithishanaji Madaraka. Lengo ni kuziwezesha Taasisi hizo kutambua mahitaji ya sasa na ya baadae ya Rasilimaliwatu ili kuyatumia vizuri katika kutekeleza Mipango Mkakati yake. Taasisi zilizowezeshwa ni Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Chuo Kikuu cha Sayansi, na Teknolojia Mbeya (MUST), na Sekretarieti za Mikoa ya Geita, Shinyanga na Mbeya pamoja na Mamlaka zao za Serikali za Mitaa;

(xiii) Taasisi za Umma 4 zimewezeshwa kuhuishwa Mipango yao ya Mafunzo. Taasisi zilizowezeshwa ni:- Chuo cha Utalii, Wakala ya Serikali Mtandao (eGA), Bodi ya

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Wataalam wa Ununuzi (PSPTB), na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamin Tanzania (RITA).

(xiv) Usanifu wa Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma umeanza kufanyika kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Uingereza (DFID) na Benki ya Dunia. Usanifu wa Programu ya Maboresho umeanza kwa kufanya uchambuzi wa vikwazo vyta utendaji kazi nya Kitaasisi na Uchambuzi wa hali ya kiuchumi na kisiasa;

(xv) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Ofisi/ Wizara 20 na Taasisi za Umma 3 imehuishwa ili kuendana na mahitaji ya sasa kwa nia ya kupunguza ukubwa wa Serikali na kuimarissha utoaji wa huduma na uwajibikaji kama ilivyo dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano;

(xvi) Uandaaji wa Nyaraka za kuanzisha Wakala ya Barabara za Serikali za Mitaa (Tanzania Rural and Urban Agency (TARURA) umekamilika na Nyaraka hizo zimepelekwa kwenye Mamlaka za Serikali (Katibu Mkuu Kiongozi) kwa ajili ya kuidhinishwa;

(xvii) Kanzidata ya Fomu zinazotumika kwenye Taasisi za Serikali imeanzhishwa na mpaka sasa fomu 409 kutoka Taasisi 18 zimeshawekwa kwenye Mfumo. Ufuatiliaji kwa Taasisi zingine unaendelea;

(xviii) Mifumo mitano ilifuatiliwa kwenye Wakala za Serikali 35 na matokeo yanaonesha utekelezaji wake umeimarika. Mifumo hiyo ni: Mpango Mkakati, Mfumo wa Malalamiko, Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS), Mkataba wa Huduma kwa Mteja; na Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji;

(xix) Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango Mkakati, Bajeti na Utoaji Taarifa umehuishwa kwa kushirikisha wadau wakuu kwenye uandaaji wa mipango na bajeti serikalini. Ikjumuisha Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma,

Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu);

(xx) Ofisi kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Marekani kuititia Mradi wa PS3 ilifuutilia utekelezaji wa Mifumo ya Utendaji kazi kwa majoribio kwenye Mikoa 2 (Dodoma – Halmashauri ya Bahi na Chemba na Iringa – Halmashauri ya Iringa Vijijiini na Kilolo);

(xi) Elimu juu ya Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji kwa Wizara 12, Mikoa 25 na Halmashauri zote zilizo chini ya Mikoa hiyo ilitolewa kwa njia ya mtandao (video conference). Elimu hiyo ilitolewa katika vikao 3 ambapo washiriki 566 walifihiwa kwa gharama nafuu ikilinganishwa na gharama ambayo ingetumika endapo watumishi hao wangesafiri kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya mafunzo hayo.

(xii) Ukusanyaji na uhuishaji wa takwimu za watumishi wenyе ulemavu katika Utumishi wa Umma na kuzitunza takwimu hizo kwa maamuzi na matumizi mbalimbali ya Serikali umefanyika. Aidha, ufuatiliaji wa utekelezaji wa mwongozo wa VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza katika Taasisi za Umma umefanyika;

(xiii) Uratibu wa uhamisho na uteuzi katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia taarifa za kiutumishi, umeendelea kufanyika ambapo vibali 2,044 vya Uhamisho, 1,563 vya kuazimwa watumishi na 189 vya likizo bila malipo vilitolewa. Katika kipindi hiki Watumishi 306 wameteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali za Uongozi;

(xiv) Jumla ya malalamiko 1,346 kati ya 1,384 sawa na asilimia 97 yanayohusu ukiukwaji wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma yameshughulikiwa;

(xv) Huduma za Kawaida kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu 11 na wajane 5 zimeendelea kutolewa;

(xvi) Uratibu wa utekelezaji wa eneo la Serikali Mtandao chini ya Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

ya Kikanda, kwa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (RCIP) umeendelea kufanyika ambapo miradi inayotekelzeza katika Programu hiyo ipo katika hatua mbalimbali. Miradi hiyo ni Mfumo wa Taarifa za Usajili wa Vizazi na Vifo (Birth and Death Registration system); Mfumo wa Taarifa za Biashara (National Business Portal); Mfumo wa Taarifa za Kitabibu (Telemedicine); Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (Government Network); Mfumo wa Kielektroniki wa Nyaraka (e-Records Management and Preservations); na Mfumo wa Taarifa za Ununuzi kwa Njia ya Kielektroniki (e-Procurement);

(xxvii) Uainishaji wa mahitaji ya miundombinu katika Idara za Afya, Elimu, Mifugo na Kilimo katika Sekretariati za Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa ajili ya matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) umekamilika na mfumo huo umeboreshwa kufuatana na mahitaji hayo na taratibu za usimamizi wa masuala ya rasilimaliwaitu katika Idara hizo. Ufungaji wa Mfumo katika Idara hizo unaendelea kufuatia mafunzo kwa watumiaji wa mfumo kukamilika;

(xxviii) Mafunzo kwa Maafisa Elimu na Makatibu Afya 633 na Maafisa TEHAMA 116 kutoka Idara za Elimu, Afya na Kitengo cha TEHAMA katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa yamekamilika na walengwa wameanza kutumia mfumo huo. Hadi sasa, jumla ya Taarifa za Shule za Msingi 6,400, Shule za Sekondari 1,730 na Vituo vya Afya/Zahanati/Hospitali 1,881 zimeshaingizwa kwenye mfumo;

(xxix) Rasimu ya mwisho ya Sera ya Serikali Mtandao imekamilika na inaandaliwa kuwasilishwa kwenye mamlaka za maamuzi Serikalini.

**b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)**

30. ***Mheshimiwa Spika***, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala;

kutoa shauri za kitaalam kufanya utafiti na machapisho mbalimbali ya kitaalam katika Utumishi wa Umma.

31. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:

(i) Mafunzo ya kujandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma yalifanyika kwa Watumishi 476;

(ii) Mafunzo mbalimbali yalitolewa kwa Watumishi wa Umma, ambapo watumishi 594 walinufaika na mafunzo ya awali na watumishi 968 walipata mafunzo ya muda mfupi na wengine 13,990 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Cheti, na Stashahada katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Usimamizi wa Manunuzi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(iii) Maandiko 5 ya ushauri wa kitaalamu yameandalowiwa. Aidha, kazi ya kutoa ushauri kwenye eneo 1 la kitaalamu imefanyika;

(iv) Toleo la kwanza la Jarida la Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC Journal) lipo katika hatua ya uchapishaji. Aidha, makala 5 za kitaalam katika Utumishi wa Umma zimechapishwa katika majarida mbalimbali ndani na nje ya nchi;

(v) Mafunzo kwa Watumishi wa Chuo cha Utumishi wa Umma yamedhaminiwa kama ifuatavyo: 11 Shahada ya uzamivu; 10 Shahada ya uzamili, 9 Shahada ya kwanza, 2 Stashahada na watumishi wengine 70 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi, katika maeneo yafuatayo: Kuongeza stadi za kuandika ripoti za kitafiti; Udhhibit wa maambukizi ya VVU na UKIMWI mahali pa kazi pamoja na Magonjwa Sugu Yasiyoambulizwa;

(vi) Uhakiki wa wakazi wanaostahili kulipwa fidia kwenye eneo linalotarajiwa kujengwa Chuo cha Utumishi wa Umma Wilayani Rufiji unaendelea chini ya usimamizi wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Rufiji;

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(vii) Chuo kinashirikiana na Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida kukamilisha Mpango Kabambe (Master plan) ya eneo la Chuo la ekari 89; na

(viii) Kukamilisha malipo na umilikishwaji wa eneo la Chuo katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

**c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)**

32. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao imeendelea kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo maalum ya muda mfupi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

33. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zimetekelozwa:

(i) Mafunzo yametolewa kwa jumla ya washiriki 1,368 ambapo kati ya hao wanaume ni 842 na wanawake ni 526, katika maeneo ya Uongozi, Utawala Bora, Maadili, Anuai za jamii, TEHAMA na stadi za kuboresha utendaji kazi. Watumishi wa umma walikuwa ni asilimia 92 ya washiriki wote;

(ii) Wakala kwa kushirikiana na wadau wa ndani na nje ya nchi kwa kutumia Teknolojia ikiwemo Chuo cha Serikali cha Kenya, Chuo cha Menejimenti cha Uganda na "UNESCO Institute of Life Long Learning" kilichopo Hamburg – Ujerumanimepanua wigo wa kutoa mafunzo katika maeneo ya Uongozi na Menejimenti, ambapo watumishi wa umma watapata fursa za mafunzo kutoka kwa wataalam wa nje ya nchi bila ya kusafiri na kwa gharama nafuu;

(iii) Wakala imekamilisha ufungaji wa vifaa vya Mtandao na mawasiliano kwa njia ya video katika Ofisi yake ya Arusha;

(iv) Kuongeza ubora wa huduma kwa wateja kwa kuweka kompyuta za kisasa 10 kwenye maabara ya kompyuta ya Wakala;

(v) Watumishi 6 wa Wakala wamejengewa uwezo kwa kupewa mafunzo ya muda mfupi na wa kat;

(vi) Huduma ya mawasiliano kwa njia ya video imeendelea kutumika na Mahakama katika kuleta mashahidi. Aidha, Madaktari 88 kutoka Taasisi mbalimbali nchini, waliunganishwa na madaktari bingwa kutoka nchi 13 za Afrika, Amerika na Asia na kujadili changamoto za tiba ya malaria na uboreshaji wa tiba za mifupa; na

(vii) Wakala imefanya majoribio ya teknolojia ya mawasiliano kwa njia ya video inayotegemewa kutumia masafa ya intaneti "bandwidth" kidogo hivyo kuwezesha mawasiliano hata sehemu zenye upungufu wa masafa ya intaneti.

**d) Wakala ya Serikali Mtando (eGA)**

34. ***Mheshimiwa Spika***, Wakala ya Serikali Mtando imeendelea kutekeleza Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ya Mwaka 2016 katika Utumishi wa Umma ili kuongeza ufanisi, kupunguza gharama na kuimarisha uwajibikaji katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, Wakala ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kukuza matumizi ya TEHAMA serikalini kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma bora kwa wananchi kwa usalama, urahisi na kwa gharama nafuu.

35. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017, Wakala imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Awamu ya kwanza ya ujenzi wa vituo vikuu vyaa kuhifadhi taarifa na mifumo ya Serikali (Government Data Centre) imekamilika na vituo vimeanza kutumika. Lengo la vituo hivi ni kuongeza na kuimarisha usalama wa mifumo na taarifa za Serikali na kuongeza uhakika wa upatikanaji wa taarifa katika kutekeleza majukumu ya kila siku;

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(ii) Jumla ya Taasisi 63 za Serikali zimeunganishwa katika Mfumo wa Mawasiliano kwa Njia ya Barua pepe (Government Mailing System - GMS) na hivyo kufanya Taasisi zilizounganishwa kutumia mfumo huo kufikia 201. Mfumo huu umeimarisha mawasiliano kwa njia ya barua pepe na kuongeza usalama wa kubadilishana taarifa;

(iii) Jumla ya Taasisi 72 zimeunganishwa kwenye Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Government Network) kwa lengo la kuziunganisha Taasisi za Serikali katika mtandao mmoja wa mawasiliano ya kielektroniki (taarifa, sauti na video) ili kuboresha usalama wa taarifa na kupunguza gharama za mawasiliano. Uunganishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa 77 umekamilishwa kwa asilimia 50. Aidha, Uunganishaji wa mtandao kwa 'fiber' kwenye mikoa 20 ili kuiunga na Mkongo wa Tafifa kwa dhumuni la kurahisisha uunganishwaji wa mikoa hii kwenye mtandao wa mawasiliano serikalini umeendelea;

(iv) Kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali, mifumo mbalimbali ya TEHAMA imetengenezwa ikiwa ni pamoja na:-

a) Mfumo wa kielektroniki wa kufuatilia utekelezaji wa ahadi na maagizo ya viongozi wakuu wa nchi, na llani ya Chama Tawala;

b) Mfumo wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kufuatilia utekelezaji wa mipango kazi (Utumishi Dashboard);

c) Mfumo wa Vibali vya Kusafiri Nje ya Nchi (Travel Permit System),

d) Mfumo Mkuu wa Kusimamia Malipo na Maduhuli ya Serikali Kielektroniki (Government Payment Gateway);

- e) Mfumo unaotumiwa na wananchi kutoa taarifa za matukio ya rushwa kwa TAKUKURU kwa kutumia simu za mikononi na namba maalum (113 na \*113# );
  - f) Mfumo wa kuiwezesha Tume ya Utumishi wa Umma kutekeleza majukumu yake;
  - g) Mfumo wa Usimamizi na Uratibu wa Majengo ya Serikali unaotumiwa na Wakala wa Majengo (TBA);
  - h) Kuboresha Mfumo wa Kuhifadhi Taarifa za Bunge (POLIS); na
  - i) Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali na Miradi ya TEHAMA Serikalini.
- (v) Mfumo wa Kutoa Huduma kwa Njia ya Simu za Mkononi (Government Mobile Platform) umeboreshwa kwa kutengeneza miundo mbinu ya kutoa huduma ya Ujumbe Mfupi (SMS Gateway) na kwa Menyu (USSD Gateway) kuititia namba maalum \*152\*00# ambapo mpaka sasa jumla ya Taasisi 28 za Serikali zinatumia huduma hii; Mfumo huu umezirahisishia taasisi za Serikali kuweza kujenga mfumo wa kutolea huduma kwa njia ya simu za mikononi kwa muda mfupi ukilinganisha na ilivyokuwa hapo awali. (Kwa mfano mfumo uliokuwa unajengwa kwa miezi mitatu unaweza kujengwa ndani ya siku saba kukamilika;
- (vi) Mafunzo kwenye masuala ya Serikali Mtandao yametolewa kwa watumishi wa Taasisi 90 za Serikali ili kujenga uwezo wao wa kubuni, kujenga na kusimamia miundombinu na mifumo mbalimbali inayotumiwa na Taasisi husika;
- (vii) Mfumo wa Kielekroniki wa Masjala (e-Office) umetengenezwa ili kurahisisha ubadilishanaji wa nyaraka na utoaji wa maamuzi Serikalini. Mfumo huu unatumwiwa na Taasisi 6 za Serikali katika awamu ya majoribio. Taasisi hizo ni Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Wakala

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

ya Serikali Mtandao, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi wa Umma;

(viii) Mfumo/Dawati la Kielektroni la Huduma kwa Wateja umeboreshwa kuimarisha utoaji wa msaada wa kiufundi kwa wataalam wa TEHAMA wa Taasisi za Serikali. Hadi sasa, jumla ya Taasisi 154 zinatumia Mfumo huu unaopatikana kuititia <http://helpdesk.ega.go.tz>, [egov.helpdesk@ega.go.tz](mailto:egov.helpdesk@ega.go.tz) na simu namba 0764 292 299;

(ix) Usimamizi wa Viwango, Miongozo na Taratibu za Serikali Mtandao ulitekelezwa kwa kuthibitisha miradi/mifumo mbalimbali ya TEHAMA pamoja na kukagua mifumo mbalimbali ya Taasisi 12 za Serikali;

(x) Elimu kwa Umma kuhusu matumizi ya TEHAMA imetolewa kwa kuzalisha na kurusha vipindi vyta runinga kuititia Televisheni ya Taifa na Tovuti ya Wakala. Jumla ya vipindi 52 vinaandalialiwa ambapo vipindi vitatu vimesharushwa.

**SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

36. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **Shilingi 6,441,908,200**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 5,441,708,200** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi 3,292,716,100** za Matumizi ya Kawaida kilipokelewa na kutumika. Kwa upande wa Miradi ya Maendeleo, **Shilingi 123,441,000** zilipokelewa na kutumika.

37. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Malalamiko 186 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 130 yalihu Sheria ya Maadili ya Viongozi na malalamiko 56 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Malalamiko hayo

yanajumuisha maeneo ya migogoro ya ardhí, rushwa, jinai, nk. Uchunguzi wa awali umefanyika kwa malalamiko 9 yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Malalamiko 121 yaliyosalia yapo katika hatua mbalimbali za kiuchunguzi. Aidha, malalamiko 56 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, walalamikaji walipewa ushauri na mengine yalielekezwa kwenye mamlaka zinazohusika;

(ii) Viongozi wa Umma 15,881 walitumiwa Fomu za Tamko la Rasilimali na Madeni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Disemba, 2016. Hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya Viongozi wa Umma 15,346 ambaao ni sawa na asilimia 97.3 wamerejesha Fomu hizo. Viongozi walioshindwa kurejesha Matamko yao kwa wakati wamekumbushwa kufanya hivyo na watakaoshindwa kutoa sababu za msingi za kutorejesha kwa wakati watafikishwa katika Baraza la Maadili;

(iii) Viongozi 116 kati ya 500 kwa mwaka wa fedha 2016/17 walihakikiwa. Aidha, Viongozi 384 waliosalia watahakikiwa katika kipindi cha Aprili-Juni, 2017. Viongozi walioonekana kuwa na tofauti au kasoro katika matamko yao wametakiwa kutoa maelezo ya kasoro au tofauti hizo na wale ambaao hawatakuwa na maelezo yanayoridhisha watafikishwa kwenye Baraza la Maadili kwa uchunguzi wa kina;

(iv) Viongozi 15,524 walisaini Hati ya Ahadi ya Uadilifu na wale ambaao hawajasaini wanaendelea kupewa elimu ya umuhimu wa kusaini hati hiyo. Sekretarieti imekuwa ikitoa elimu mara kwa mara hasa pale viongozi wa kitaifa wanapoapishwa kuingia katika madaraka;

(v) Elimu ilitolewa kwa Viongozi wa Taasisi za Umma 1,056, pamoja na Watumishi wa Umma na wananchi 2,718 kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Aidha, Klabu 7 za Maadili zilianzishwa katika Shule za Msingi;

(vi) Siku ya Maadili Kitaifa iliadhishwa tarehe 10 Disemba, 2016 kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali

zinazosimamia masuala ya utawala bora, uwajibikaji, haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa na maadili. Aidha, elimu kwa viongozi wa Taasisi za Umma na wananchi wapatao 680 ilitolewa kuititia Wiki ya Huduma kwa Wateja (Viwanja vya Mnazi Mmoja Dar es Salaam), matembezi ya watumishi, midahalo 2 inayohusu maadili na kuititia vipindi vya redio, luninga na makala katika magazeti mbalimbali katika kuadhimisha siku hiyo;

(vii) Sekretarieti imeimarisha uwezo ambapo watumishi 80 walipatiwa mafunzo ya juu yaliyofanyika katika Chuo cha Maafisa wa Polisi, Kidatu Morogoro. Mafunzo hayo yalijumuisha namna bora ya kuhakiki mali na madeni ya viongozi wa umma, kufanya uchunguzi, uendeshaji wa kesi katika Baraza la Maadili, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, utakatishaji wa fedha haramu na Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili;

(viii) Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Maadili Kanda ya Kusini lililopo Mtwara ulikamilika mwezi Agosti, 2016 na Ofisi ilizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan mwezi Septemba, 2016;

(ix) Uzinduzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili ulifanyika tarehe 10 Machi, 2017. Mfumo huu utawezesha na kufanikisha kukusanya, kuchakata, kutunza taarifa na kumbukumbu mbalimbali kutoka kwa Viongozi wa Umma kuhusu mali na madeni walijonayo wao binafsi, familia zao, kwa kila mwaka na taarifa kuhusu malalamiko ya ukiukwaji wa maadili unaofanywa na Viongozi wa Umma dhidi ya wananchi. Taarifa na kumbukumbu hizo huchambuliwa na pale inapobidi hufanyika uhakiki unaoiwezesha Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kuchukua hatua stahiki dhidi ya Viongozi wasiokuwa waadilifu kama njia mojawapo ya kujenga na kuimarisha Utawala Bora na Uwajibikaji Serikalini na Taifa kwa ujumla;

(x) Maandalizi ya ujenzi wa Ofisi za Maadili Dodoma yameanza; na

(xi) Utafiti kuhusu hali ya Maadili ya Viongozi wa Umma ulifanyika. Matokeo ya utafiti huo yanaonesha kuwa yapo malalamiko ya matumizi mabaya ya madaraka kwa Viongozi wa Umma kwa asilimia 39 na matumizi mabaya ya mali za umma kwa asilimia 20. Aidha, asilimia 70 ya waliohojiwa wana uelewa kuhusu masuala ya Mgongano wa Maslahi. Kwa ujumla utafiti unaonesha kuwa hali ya maadili kwa Viongozi wa Umma ni nzuri ingawa zipo changamoto kadhaa ambazo ni lazima zifanyiwe kazi. Utafiti huo ulihusisha makundi mbalimbali wakiwemo Viongozi wa Umma 573, wananchi 1,625, makampuni binafsi 62 na AZAKI 50 na ulifanywa kwa ushirikiano kati ya Mshauri Mwelekezi na wataalam kutoka Sekretarieti ya Maadili. Utafiti ulifanyika katika Mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Mtwara, Arusha, Iringa, Mwanza, Singida na Shinyanga.

#### **SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

38. ***Mheshimiwa Spika***, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imeendelea kutafuta wataalam wenye ujuzi na kuandaa mfumo wa Kanzidata za Wataalam hao ili kurahisisha utaratibu wa ajira; kuandaa orodha ya wahitimu wa vyuo vikuu na wataalam wenye weledi kwa madhumuni ya kurahisisha rejea na ujazaji wa nafasi wazi za ajira katika Utumishi wa Umma; kutangaza nafasi wazi za kazi zinazotokea katika Utumishi wa Umma na kufanya usaili na kuwashauri waajiri kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na mchakato wa ajira.

39. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa Jumla ya **Shilingi 2,205,404,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, Jumla ya **Shilingi 2,121,650,583** zilikuwa zimepokelewa na kutumika.

40. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Sekretarieti imehakiki yeti nya waombaji kazi 39,511 ambapo kati ya hivyo yeti 1,951 vilibainika kuwa ni nya kughushi na watusika waliondolewa katika mchakato pamoja na yeti hivyo kuchukuliwa na kuwasilishwa kwa mamlaka husika kwa ajili ya hatua zaidi;

(ii) Sekretarieti ilisimamia na kuendesha mchakato wa ajira ya watendaji wakuu wa Taasisi za Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini na nafasi 1 ya Benki ya Azania. Aidha, ilishiriki pia kwa kutoa utaalamu katika kuendesha mchakato wa usaili wa nafasi 3 za Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, nafasi 1 ya Wakala wa Umeme Vijijini na nafasi 1 ya Shirika la Posta Tanzania;

(iii) Sekretarieti imeanza kutengeneza kanzidata ya Maafisa Waandamizi na wenye taaluma/ujuzi maalum ili kurahisisha mchakato wa kujaza nafasi wazi za juu katika Utumishi wa Umma endapo Serikali itahitaji. Hadi kufikia Februari 2017 taarifa za Maafisa Waandamizi 1,840 zimepokelewa kutoka Wizara 5, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri za Wilaya 45, Wakala 4, vyuo Vikuu 3 na Taasisi 14;

(iv) Umefanyika utafiti uliohusisha mahojiano kwenye jumla ya Taasisi 18 katika mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kupata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa michakato ya ajira pamoja na utendaji wa Sekretarieti. Taasisi zilizohusika ni Wizara 5, Ofisi za Wakuu wa Mikoa 2, Wakala wa Serikali 4, Idara Zinazojitegemea 2, Manispaa 3 na Halmashauri 2;

(v) Sekretarieti imekamilisha maandalizi ya kuunganisha mfumo wa maombi ya kazi na ule wa kutunza taarifa za wananchi unaomilikiwa na Mamlaka ya vitambulisho nya Taifa ili kuhakiki kuwa wanaoajiriwa wanakuwa na sifa stahiki;

(vi) Sekretarieti imefungua ofisi Zanzibar kwa ajili ya kurahisisha mchakato wa ajira katika taasisi za Muungano. Watumishi 3 wamehamishiwa katika ofisi hiyo ambayo tayari imewekewa samani na vitendea kazi;

(vii) Kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao, uboreshaji na uimarishaji unaendelea kwenye mfumo wa kielektroniki wa kuendesha mchakato wa ajira na utunzaji kumbukumbu za wasailiwa na wataalam mbalimbali;

(viii) Sekretarieti imeendelea kuwahudumia wananchi wanaohitaji msaada wa namna ya kutumia mfumo wa maombi ya kazi kwa njia ya kielektroniki (Recruitment Portal) ana kwa ana, barua pepe na kwa njia ya simu; na

(ix) Sekretarieti ya Ajira imewezesha watumishi 4 kupata mafunzo ya muda mrefu nchini na watumishi 4 mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi.

#### **TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

41. *Mheshimiwa Spika*, Tume ya Utumishi wa Umma imeendelea kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma yanaendeshwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo zinatumika vizuri kwa lengo la kuimarisha utendaji unaozingatia malengo na matokeo yanayopimika. Aidha, Tume ni Mamlaka ya Rufaa kwa Watumishi wa Umma dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka zao za nidhamu.

42. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2016/17 Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 3,717,876,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2017 kiasi cha **Shilingi 3,738,193,089** zilikuwa zimetolewa na kutumika.

43. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Tume ya Utumishi wa Umma ilitekeleza majukumu yafuatayo:-

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

- (i) Rufaa 75 ziliamuliwa ambapo 14 zilikubaliwa, 49 zilikataliwa na 12 zilitupiliwa mbali kwa kuwa zilikatwa nje ya muda;
- (ii) Malalamiko 47 ya Watumishi wa Umma yalitolewa uamuvi;
- (iii) Uguzi wa kawaida wa rasilimali watu umefanyika katika Taasisi 41 ambazoni Idara Zinazojitegemea 2, Sekretarieti za Mikoa 5, Wakala 3, Taasisi ya Umma 1 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 30;
- (iv) Uguzi Maalum ulifanyika katika Manispaa ya Kinondoni;
- (v) Wadau wa Tume walielimishwa kuhusu taratibu za rufaa katika Utumishi wa Umma na taratibu za kuwachukulia hatua za nidhamu Watumishi wa Umma kupitia utoaji wa makala 1, tovuti 1 ya Tume na mikutano 3 na waandishi wa habari na kupitia wiki ya maadili;
- (vi) Watumishi 69 wa Tume walielimishwa kuhusu VVU na UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na mapambano dhidi ya rushwa. Aidha, huduma kwa watumishi wa Tume wanaoishi na VVU na UKIMWI zilitolewa;
- (vii) Watumishi 19 wa Tume waliwezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi ya kuongeza ujuzi katika masuala ya rasilimali watu, na utunzaji wa kumbukumbu.

**BODI YA MISHAHARA NA MASLAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

44. *Mheshimiwa Spika*, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma imeendelea kufanya mapitio ya mara kwa mara ya mishahara na kupendekeza kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya viwango vya mishahara, posho na mafao katika Utumishi wa Umma kwa ujumla. Vile vile, Bodi ina wajibu wa kumshauri Rais wa

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya misingi ya miundo ya mishahara katika Utumishi wa Umma.

45. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2016/17, Bodi ya Mishahara iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,859,845,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 jumla ya **Shilingi 926,501,520** zilipokelewa na kutumika.

46. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2016/17 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

(i) Rasimu ya Tathmini ya Kazi inayolenga kuhuisha miundo ya mishahara ya Watumishi wa Umma imepitiwa na wataalam kutoka kwenye Wizara na Taasisi mbalimbali wanaounda Kamati ya Tathmini ya Kazi na kurejeshwa kwa Mtaalam Mwelekezi kwa ajili ya marekebisho ya mwisho; na

(ii) Bodi imefanya mapitio ya Mpango Mkakati wa Bodi wa mwaka 2013/14 hadi 2017/18 na kuanda Mpango Mkakati wa mwaka 2016/17 hadi 2020/21.

**UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI (PDB)**

47. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Bunge liliidhinisha **Shilingi 27,616,107,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 397,278,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 27,218,829,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi 3,499,096,330** fedha za Miradi ya Maendeleo zilipokelewa na kutumika.

48. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitokolezwa:-

(i) Kuwezesha upimaji wa udongo na uandaaji wa ramani za matumizi ya udongo katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini (SAGGOT Regions) kuititia Mradi wa *Tanzania Soil Information Service (TansIS)* ulio chini ya Wizara ya Kilimo,

## **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mifugo na Uvuuvi pamoja na Taasisi zake za utafiti. Ukusanyaji wa sampuli za udongo umefanyika na kazi ya uchunguzi inaendelea. Aidha, ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mradi unafanyika ili kuhakikisha matokeo yanapatikana kwa wakati;

(ii) Kuliwezesha Jeshi la Polisi katika Mpango wa Usalama wa Raia na Mali Zao kwa kufanya tathmini ya utayari katika Mikoa ya Kipolisi ya Ilala, Temeke, Mwanza, Arusha, Dodoma na Geita. Tathmini hiyo imefanyika mwezi Septemba, 2016 hadi Februari, 2017;

(iii) Kuratibu zoezi la upembizi yakinifu wa takwimu za Sekta ya Kilimo uliosaidia zoezi la kumalizia uandaaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo (ASDP II);

(iv) Kwa kushirikiana na Mahakama, Kikosi kazi cha Mahakama kimejengewa uwezo wa kusimamia vipaumbele kwa kutumia mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa (BRN);

(v) Kuliwezesha Jeshi la Polisi kuhamasisha wadau katika kusaidia Mkoa wa Kipolisi wa Kinondoni kujenga vituo vidogo vya polisi 3 vya muda katika matukio mengi ya uhalifu ya Manzese, Coco Beach na Masaki. Aidha, uwezeshaji wadau pia umefanyika katika ujenzi wa Kituo cha Polisi Madale pamoja na hanga la makazi la Kikosi cha Kuzuia Fujo (FFU) Kunduchi; na

(vi) Kuliwezesha Jeshi la Polisi kuhamasisha wadau katika kusaidia ujenzi wa Kituo cha kisasa cha mawasiliano katika Kituo cha Polisi cha Kati Dar es salaam ambacho kimefungwa vifaa vya kufuatilia mwenendo na matumizi ya magari ya doria. Kituo hicho kilizinduliwa Mwezi Julai, 2016.

## **IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA**

49. *Mheshimiwa Spika*, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za utunzaji

kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya Mwaka 2002. Aidha, Idara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

50. ***Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka wa fedha 2016/17, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,293,851,000**.

51. ***Mheshimiwa Spika***, Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi 990,762,300** zilipokelewa na kutumika kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

52. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Machi, 2017 Idara ya Kumbukumbu imefanikiwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Uwekaji wa Mfumo wa kuhifadhi taarifa, kumbukumbu na nyaraka kwa njia ya kielektroniki (Digital Records Management and Preservation System) umeanza. Vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya kufunga mfumo huu vimenunuliwa na kuwasilishwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma ambako ndipo kitakuwa kituo kikuu cha Mfumo. Mkandarasi anatarajiwaa kuanza kufunga vifaa hivyo ili kazi ya kuingiza nyaraka katika mfumo ianz;

ii. Kuchambua, kuorodhesha na kuhamisha kumbukumbu kutoka katika baadhi ya Taasisi za Serikali kwenda kwenye Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma. (Makasha 473 za iliyokuwa Kamati ya Ukombozi wa Bara la Afrika kutoka Jeshi la Wananchi Tanzania, Makasha 808 kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Makasha 295 kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Makasha 583 kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Makasha 291 Kutoka Wizara ya nishati na Madini, Makasha 449 kutoka Wzara ya Fedha na Mipango Makasha 1,291 kutoka TASAF, Makasha 138 kutoka Wizara ya

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano na Makasha 1,130 kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa) kazi hiyo ni endelevu;

iii. Machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya Nchi yetu kutoka katika Taasisi za Umma na watu binafsi yamekusanya. Machapisho haya ni pamoja na Taarifa rasmi za Bunge (Hansards), Ripoti, Hotuba, Majarida, Sera kutoka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali;

iv. Kukusanya na kufanya ujalidi magazeti 989 kutoka makampuni ya Business Times, Daily News, Habari leo, Nipashe, Mwanachi, The Guardian na Majira;

v. Waraka wa utekelezaji (implementation Circular) wa majukumu ya kuanzishwa na kuendeshwa Maktaba na Makumbusho ya Marais Wastaifu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeandaliwa;

vi. Watafiti 72 wamehudumiwa, kati ya watafiti hao 39 ni wa ndani na watafiti 33 ni wa nje. Idadi ya majalada yaliyosomwa ni 413;

vii. Kutambua na kuratibu ukusanyaji wa vitu na kumbukumbu mbalimbali za Waasisi wa Taifa kumefanyika. Jumla ya vitu na kumbukumbu 2,035 zimetambuliwa, kati yake vitu na kumbukumbu 1,837 zimekusanya na kuhifadhiwa na Wadau ambao ni pamoja na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Makumbusho ya Taifa, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, KAVAZI la Mwalimu Nyerere na Radio na Televisheni Zanzibar;

viii. Uandaaji wa Makala ya Kihistoria kuhusu Nyumba Kumbukizi aliyowahi kuishi Mwalimu Julius Kambarage-Magomeni. Makala hii inatunza historia ya Nyumba na vitu aliyowahi kutumia Muasisi wakati anaanza harakati zake za kuikomboa nchi yetu;

ix. Kipindi 1 cha Televisheni na kimoja cha Redio viliandaliwa, ili kuelimisha umma kuhusu mambo mbalimbali yanayohusu Waasisi wa Taifa ikiwa ni pamoja na utekelezaji

wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004;

x. Mafunzo ya utunzaji kumbukumbu kwa Waratibu wa masuala ya Utunzaji Kumbukumbu katika Taasisi za Umma yamefanyika Dodoma. Jumla ya waratibu 91 walihudhuria mafunzo haya kutoka katika Taasisi mbalimbali za Serikali. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo wa kusimamia masuala ya utunzaji kumbukumbu katika Taasisi zao;

xi. Taasisi za Umma zimeendelea kusaidiwa kutengeneza mwongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu. Katika kipindi hiki jumla ya Taasisi tatu ambazo ni Mkemia Mkuu wa Serikali, Energy and Water Utilities Regulatory Authority (EWURA), Parastatal Pensions Fund (PPF) na Tanzania Social Action Fund (TASAF) zimesaldiwa kuandaa mwongozo huo; na

xii. Kusimamia na kutoa mwongozo kwa Taasisi za Umma zilizohamia Makao Makuu ya Serikali Dodoma.

### **USHAURI WA MAFUTA NA GESI (OGAB)**

53. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi imeendelea kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu uchumi wa mafuta na gesi kwa Baraza la Mawaziri kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015.

54. Mheshimiwa ***Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2016/17 Bunge liliidhinisha **Shilingi 1,036,239,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2017 **Shilingi 141,973,550** fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika.

55. ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017 shughuli zifuatazo zilitkelezwa:-

(i) Ushauri ulitolewa katika masuala yanayohusu uchumi wa mafuta na gesi zikiwemo Sera za Kisekta, Sera ya

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Uwekezaji, Sheria na Kanuni zinazohusu masuala ya Uchumi wa Mafuta na Gesi na mambo mengine yanayohusiana na Uchumi wa Mafuta na Gesi;

(ii) Utafiti juu ya manufaa ya gesi asili iliyogunduliwa kwa wananchi na Taifa katika kukuza uchumi ulianza mwezi Julai, 2016 na umekamilika mwezi Februari, 2017. Ripoti ya matokeo ya utafiti huo inaandaliwa;

(iii) Ushauri ulitolewa kuhusu aina ya utaalam unaotakiwa kwenye majadiliano ya mikataba, ukubwa wa timu, mikakati na mbinu zitakazotumika na kushiriki kama waangalizi katika majadiliano ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika Sekta ya Mafuta na Gesi; na

(iv) Kushiriki katika Mikutano mbalimbali iliyofanyika ndani na nje ya nchi yetu ambayo ilijadili masuala yanayohusu mafuta na gesi.

**C. MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2017/18 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA**

56. *Mheshimiwa Spika*, baada ya kutoa maelezo kuhusu Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2016/17, sasa naomba kutoa Mapendeleko ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/18.

57. *Mheshimiwa Spika*, Mipango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/18 kwa Mafungu 20, 30, 32, 33, 67, 94, 09, 04 na 11 imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika llani ya Uchaguzi wa Mwaka 2015 ya Chama cha Mapinduzi, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha wa 2017/18 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoainishwa na Serikali ya Awamu ya Tano kama ifuatavyo:-

## **OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE**

### **(a) Ikulu**

58. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake;
- (ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya uchumi, siasa, masuala ya jamii, sheria, mawasiliano na habari kwa umma, mahusiano ya kikanda, kimataifa na maeneo mengine;
- (iii) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu;
- (iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;
- (v) Kuandaa mukutano wa tathmini wa mwaka kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;
- (vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;
- (vii) Kupokea, kuititia na kuchambua rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma na wananchi;
- (viii) Kuratibu na kuendesha mikutano 8 ya uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Maboresho katika Sekta ya Umma nchini;

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(ix) Kutengeneza na kurusha hewani Vipindi Maalum 60 vya Televisheni, kuchapisha na kutangaza Hotuba na Picha za Mheshimiwa Rais kwenye vyombo vya habari;

(x) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea;

(xi) Kuelimisha watumishi juu ya Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na Kujikinga na UKIMWI mahali pa kazi pamoja na kuwezesha watumishi wanaoishi na VVU na UKIMWI kupata huduma muhimu za dawa, lishe na ushauri nasaha;

(xii) Kusimamia utoaji wa huduma za afya kwa watumishi kupitia Zahanati ya Ikulu;

(xiii) Kukarabati nyumba 12 za watumishi katika Ikulu Ndogo ya Chamwino na nyumba 1 iliyopo Dodoma Mjini;

(xiv) Kuendelea na ujenzi wa Ikulu mpya Chamwino; na

(xv) Kukarabati majengo ya Ikulu Ndogo za Mwanza, Shinyanga, Mbeya na Moshi.

**(b) Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU)**

59. **Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea na ukamilishaji wa uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

(ii) Kuendelea na uendeshaji wa kesi 409 zinazoendelea na mpya zitakazofunguliwa Mahakamani;

(iii) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 ili kujumuisha makosa ya uhujumu uchumi na kutaifisha mali zilizopatikana kwa njia ya Rushwa na Ufisadi;

(iv) Kufanya Utafiti na Udhibiti wa Mianya ya Rushwa katika maeneo ya Vitalu vya Uwindaji, Usimamizi na Uendeshaji wa Serikali za Mitaa na Tathmini ya Uzingatiaji wa Matumizi ya Mashine za Kielektroniki katika Ukusanyaji wa Kodi;

(v) Kufanya uchambuzi wa mifumo katika Sekta na Idara mbalimbali katika ngazi ya Mikoa na Wilaya;

(vi) Kuweka mikakati kwa kushirikiana na wadau ili kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo;

(vii) Kufuatilia fedha zinazotolewa na Serikali na Washirika wa Maendeleo katika maeneo yote ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;

(viii) Kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa na ujisadi na juhudzi za Serikali katika kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;

(ix) Kufungua na kuimarisha Klabu za Wapinga Rushwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo pamoja na makundi ya vijana wasio shuleneni ili kuendelea kujenga jamii inayochukia rushwa;

(x) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika Taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za Wilaya, Mkoa na Makao Makuu; na

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(xi) Ujenzi wa majengo ya Ofisi za TAKUKURU katika Wilaya za Ruangwa, Mpwapwa, Masasi, Ngorongoro, Namtumbo, Manyoni na Chamwino.

**(c) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

60. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kukamilisha Uandaaji na utoaji wa Hati za Haki Miliki za Kimila 11,184 katika Halmashauri za Wilaya 14 za Rufiji, Musoma, Sikonge, Chamwino, Kiteto, Meru, Geita, Makete, Kahama, Njombe, Misenyi, Sumbawanga, Misungwi, na Magu;

(ii) Kufanya urasimishaji wa ardhi vijijini katika eneo la Chanjamjawiri, Wilaya ya Chake Chake Pemba na Mahonda, Wilaya ya Kaskazini B Unguja;

(iii) Kutoa mafunzo kuhusu fursa na matumizi bora ya Hati za Haki Miliki za Kimila kwa wakulima 800 waliorasimisha ardhi zao na viongozi 80 wa vyama vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya 4 za Mpwapwa, Misungwi, Ngara na Serengeti. Aidha, kwa kushirikiana na Halmashauri husika kusimamia utekelezaji wa Mipango Kazi ya jamii ya vijiji vilivyorasimishwa kwa kuanzisha mashamba darasa na kuunda vikundi vya uzalishaji;

(iv) Kutoa mafunzo kwa Wafanyabishara 3,000 kwa ajili ya urasimishaji wa biashara katika Manispaa ya Dodoma, pamoja na Halmashauri za Wilaya za Urambo na Bariadi. Kwa upande wa Zanzibar, urasimishaji wa biashara utafanyika katika Wilaya ya Kusini Unguja ambapo jumla ya wafanyabishara 100 watasajiriwa na kupewa mafunzo. Vituo vya Urasimishaji Biashara (One stop centers) vitaanzishwa katika maeneo hayo ili kuwawezesha wafanyabishara kupata huduma muhimu za usajili, namba ya mlipa kodi, leseni, ushauri wa biashara, pamoja na huduma za kibenki katika sehemu moja;

(v) Kufanya utafiti na tathmini ya ukubwa wa Sekta isiyo rasmi Tanzania Bara na Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi za Taifa za Takwimu Tanzania Bara na Zanzibar;

(vi) Kwa kushirikiana na TAMISEMI, MKURABITA itaratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya majaribio ya Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya katika Manispaa ya Iringa na Halmashauri 2 za Mkoa wa Songwe;

(vii) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya sheria za ardhi na biashara;

(viii) Kukamilisha uandaaji wa hati katika Halmashauri za Miji ya Njombe, Morogoro, Arusha, Tunduma, Iringa, Babati, Miji Midogo ya Tandala na Ikonda Tanzania Bara, ambako urasimishaji ardhi mijini ulifanyika;

(ix) Kufanya urasimishaji wa ardhi mjini katika Wilaya za Chake Chake, Pemba na Unguja Mjini;

(x) Kukamilisha ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji 12 katika Halmashauri za Wilaya 5 ambazo ni Mvomero, Manyoni, Nachingwea, Mbinga na Chamwino. Aidha, ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji 8 utaendelea na kufikia hatua ya kuezeka katika Halmashauri za Wilaya 8 za Sumbawanga, Kalambo, Meru, Mwanga, Masasi, Mbarali, Moshi na Makete;

(xi) Kununua kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za MKURABITA lenye ghorofa moja Dodoma. Aidha, taratibu za kumpata mzabuni wa usanifu wa michoro na wa ujenzi zitakamilishwa na kuanza ujenzi; na

(xii) Kushirikiana na Wizara ya Nishati na Madini kuanza urasimishaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini katika maeneo ya Mkoa wa Geita.

**(d) Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

61. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

- (i) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ya Vijiji, Mitaa na Shehia zote ambazo hazikufikiwa katika awamu ya kwanza. Utambuzi na uandikishaji huu unategemea kuwafikia kaya za walengwa 355,000 katika Vijiji, Mitaa na Shehia 5,690;
- (ii) Kuendelea kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini zipatazo 1,100,000 katika vipindi 6 vya mizunguko ya malipo katika Halmashauri zote za Tanzania Bara pamoja na Unguja na Pemba, Zanzibar. (Uhawilishaji wa fedha utafanywa kwa kufuata Kalenda ya Malipo ya kila baada ya miezi miwili);
- (iii) Kuziondoa katika Mpango, kaya za walengwa wenyewe hali zilizoboreka baada ya kupokea ruzuku kwa muda wa miaka mitatu mfululizo kwa kuzingatia taratibu na miongozo iliyoelekezwa katika Mpango;
- (iv) Kuendelea kufanya uhakiki wa walengwa wanaostahili kunufaika na Mpango na kuwaondoa wasiostahili kuwemo kwa sababu mbalimbali;
- (v) Kutoa ajira za muda kwa jumla ya kaya za walengwa 298,970 ambazo zitahusika katika utekelezaji wa kazi za ajira za muda kwa Kaya Maskini. Walengwa hawa watatoka katika Halmashauri 42 pamoja na Unguja na Pemba;
- (vi) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati na Miongozo ya Kuweka Akiba na kuwekeza katika maeneo ya utekelezaji. Wawezeshaji 200 watapatiwa mafunzo ya kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba kwa kaya za walengwa. Jumla ya vikundi 26,162 vya walengwa vitaundwa, kupewa mafunzo na vitendea kazi. TASAF imepanga kutoa ruzuku kwa vikundi 34,000 vitakavyofanya vizuri;
- (vii) Kutekeleza jumla ya miradi 143 ya afya, elimu, ujasiliamali na barabara za vijijini chini ya Mpango wa Kuendeleza Miundombinu. Wafanyakazi 850 wa Halmashauri na Sekretarieti za Mikoa na Wajumbe wa Kamati 143 za

Usimamizi za Jamii watapewa mafunzo juu ya namna ya kutekeleza na kusimamia miradi;

(viii) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu za walengwa, uendeshaji na utoaji taarifa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mpango hususan kuimarisha mawasiliano kati ya maeneo ya utekelezaji na TASAF Makao Makuu;

(ix) Kufanya utafiti shirikishi katika maeneo mbalimbali ya kijamii na kiuchumi ili kubaini fursa na vikwazo katika kufikia lengo la jamii kujipatia maendeleo. Hii itahusisha kukusanya takwimu mbalimbali katika ngazi za jamii kwa ajili ya utafiti huo;

(x) Kujenga uwezo wa watumishi katika ngazi mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na TASAF Makao Mkuu, Mikoa, Halmashauri na jamii ili kuweza kusimamia na kutekeleza shughuli za Mpango kwa ufanisi; na

(xi) Kuimarisha usimamizi, ufuutiliaji na tathmini za shughuli za Mpango pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji wa Mpango. Shughuli hii pia itahusisha kufanya tathmini ya kwanza ya Mpango ili kupima ni kwa kiasi gani Mpango umeweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**(e) Taasisi ya UONGOZI**

62. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kutoa mafunzo ya "Stashahada ya Uzamili katika Uongozi" (Post Graduate Diploma in Leadership), kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimali watu na rasilimali nyingine;

(ii) Kutekeleza Programu ya kuwajengea uwezo wataalam wa Wizara na Taasisi za Serikali wa kufanya

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

majadiliano ya mikataba yenyewe thamani kubwa na namna ya kuunda timu madhubuti za majadiliano;

(iii) Kutoa kozi 18 za mafunzo ya muda mfupi na ushauri wa kitaalam kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi katika maeneo ya uongozi na maendeleo endelevu, kutokana na mahitaji na maombi ya walengwa;

(iv) Kuandaa mikutano 4 ya Kimataifa na Kikanda, 3 ya Kitaifa na 10 ya faragha juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(v) Kuandaa vipindi vyatuhesheni 18 vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali ndani na nje ya nchi, juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Vipindi hivi vitarushwa kwenye runinga, tovuti na mitandao ya kijamii na kuonekana katika Bara zima la Afrika;

(vi) Kufanya tafiti 9 zinazohusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(vii) Kuandaa chapisho litakaloelezea maisha na uzoefu wa Kiongozi maarufu Mstaifu;

(viii) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo yanayohusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu pale utakapohitajika;

(ix) Kutekeleza Programu Jumuishi juu ya Usimamizi wa Rasilimali za Taifa katika sekta ya uziduaji; na

(x) Kushiriki katika uendeshaji wa Kituo cha Tathmini kwa lengo la kuboresha mfumo wa uteuzi wa viongozi wa kati na waandamizi katika Utumishi wa Umma.

**(f) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)**

63. *Mheshimiwa Spika*, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- (i) Kutoa mikopo 3,600 kwa walengwa yenyе thamani ya Sh. 2,415,000,000;
- (ii) Kutoa mafunzo ya awali kwa walengwa 4,000 na mafunzo endelevu kwa wanufaika 2,000;
- (iii) Kufanya tafiti na kutoa huduma katika Mikoa ya Dodoma (Wilaya ya Dodoma), Kagera (Wilaya ya Bukoba Vijijiini) na Iringa (Wilaya ya Kilolo); na
- (iv) Kuendelea kujenga uwezo wa watendaji wa Mfuko ili kutoa huduma bora kwa wateja.

64. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba **Shilingi 16,267,586,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 747,885,035,000**. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 368,314,145,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 379,570,890,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

#### **OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA WAKALA ZILIZO CHINI YAKE**

##### **a) Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

65. ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika mwaka wa fedha wa 2017/18 itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa.

66. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

- (i) Kujenga uwezo wa Serikali katika kuratibu utungaji na utekelezaji Sera unaowiana (Policy Coherence) ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii;
- (ii) Kuanzisha na kuhuisha Miundo na Mgawanyo wa Majukumu ya Taasisi za Umma kulingana na mahitaji ya Serikali ya Awamu ya Tano ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa wananchi;
- (iii) Kuendelea kutoa vibali vya uhamisho na uteuzi kwa watumishi wanaopendekezwa na waajiri mbalimbali kushika nyadhifa za uongozi. Aidha, Ofisi yangu itaendelea kuwezesha uhamisho wa watumishi miongoni mwa waajiri na kushughulikia maombi ya vibali vya likizo bila malipo, kuazimwa na kushikizwa yanayowasilishwa na waajiri na watumishi;
- (iv) Kuendelea kushughulikia malalamiko yatokanayo na ukiukwaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma na kuchukua hatua stahiki kwa waajiri wanaolalamikiwa kwa kutozingatia sheria, kanuni, miongozo na taratibu hizo;
- (v) Kuboresha michakato ya utoaji wa huduma na kuimarisha usimamizi wa mifumo na viwango vya utendaji kazi kwa kufanya ufuutiliaji na kutoa ushauri wa kitaalamu katika Taasisi za Serikali;
- (vi) Kuratibu tathmini ya utendaji kazi wa Wakala za Serikali ili kubaini tija iliyopatikana na changamoto za uendeshaji wa vyombo hivi vya Serikali;
- (vii) Kuratibu mapendekezo mbalimbali ya kuboresha mfumo wa ufuutiliaji na tathmini ili kuendelea kuhuisha mfumo uwe madhubuti ulioaanishwa ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa na matokeo yatakayosaidia kufanya maamuzi na kuboresha sera na mikakati ya Serikali kwa ujumla;

(viii) Kusimamia na kuratibu fursa za mafunzo kwa ajili ya kujenga uwezo wa Watumishi wa Umma kufanya kazi kwa ufanisi;

(ix) Kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni mbalimbali za mafunzo kwa Watumishi wa Umma;

(x) Kuziwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo (Training Needs Assessment) ili kuhakikisha kwamba Programu za mafunzo zinazotolewa zinakidhi mahitaji halisi ya mafunzo ya Taasisi;

(xi) Kuziwezesha Taasisi za Umma 10 zinazohitaji kuandaa mipango ya Rasilimali watu na Urithishanaji Madaraka;

(xii) Kuandaa mwongozo wa kuwezesha Taasisi za Umma kuwa na Mpango wa Rasilimali watu wa muda wa kati na muda mrefu katika Utumishi wa Umma;

(xiii) Kuhimiza watanzania wenyе sifa kuomba kazi katika mashirika ya kimataifa na kikanda pindi nafasi zinapoitokeza;

(xiv) Kuendelea kufanya vikao vya kazi na Sekretarieti za Mikoa yote na Mamlaka za Serikali za Mitaa kupitia huduma ya 'Video Conference' pamoja na kusambaza mwongozo wa matumizi ya huduma hiyo katika Taasisi za Serikali;

(xv) Kuendelea kuboresha Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara katika ngazi zote za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala ya Serikali; Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na kuhuisha mfumo huo kuendana na mahitaji ya sasa na teknolojia iliyopo;

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(xvi) Kuendelea na utekelezaji wa mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Malipo ya Mishahara katika Idara za Kilimo na Mifugo kwa kutoa mafunzo kwa watumishi wa Idara hizo, na kufuatilia utekelezaji wa mfumo huo katika Idara za Afya na Elimu katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa;

(xvii) Kuratibu Utekelezaji wa Miradi inayohusiana na Serikali Mtandao chini ya Programu ya Miundombinu ya Mawasiliano ya Kikanda, kwa Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika (RCIP);

(xviii) Kuendelea na usanifu na uidhinishaji wa Programu ya Uboreshaji wa Utumishi wa Umma;

(xix) Kusimamia ajira za Watumishi wa Umma ambapo katika mwaka wa fedha wa 2017/18 Serikali inatarajia kuajiri watumishi kwa kuzingatia vipaumbele na kuimarisha maeneo yenye upungufu mkubwa;

(xx) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa matumizi sahihi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara;

(xxi) Kufanya uhakiki wa mahitaji sahihi ya rasilimaliwatu katika Mikoa 5 na kutoa mafunzo kwa Maofisa Rasilimaliwatu 30 kutoka Taasisi za Umma;

(xxii) Kufanya Kampeni na ufuatiliaji wa uzingatiaji wa Maadili utekelezaji wa Ahadi za Uadilifu na uzingatiaji wa maadili katika (Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali) 20, Sekretarieti za Mikoa 2 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 13;

(xxiii) Kuhuisha Kanuni za Maadili na Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2005;

(xxiv) Kuratibu, kusimamia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo wa Anuai za Jamii, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY) katika Utumishi wa Umma;

(xxv) Kufuatilia utekelezaji wa Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu wa Mwaka 2008;

(xxvi) Kujenga uelewa wa Mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi kwa Viongozi wa Kisiasa na Watendaji Wakuu wa Taasisi za Umma;

(xxvii) Kuwezesha Menejimenti za Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, na Majopo ya Kitaalamu ya Serikali kufanya majadiliano juu ya utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji Kazi;

(xxviii) Kuzijengea uwezo Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma juu ya uandaaji na utekelezaji wa Mikataba ya Utendaji Kazi; na

(xxix) Kukamilisha kuandaa Sera ya Serikali Mtandao pamoja na Mpango Mkakati wake wa Utekelezaji, na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miongozo ya Serikali Mtandao katika taasisi za Umma;

**b) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC)**

67. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa 2017/18, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo ya kijiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi 840;

(ii) Kutoa Mafunzo ya Uongozi, Menejimenti na Utawala kwa Watumishi wa Umma 2,790;

(iii) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma kwa Watumishi wa Umma 2,010;

(iv) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 15,810 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili,

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, na Menejimenti ya Rasilimali Watu, Usimamizi wa Manunuvi ya Umma, Uongozi na Utawala Bora;

(v) Kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Taasisi za Umma 21;

(vi) Kufanya utafiti katika maeneo 6 yanayolenga kuboresha Utumishi wa Umma;

(vii) Kuanzisha Shahada ya Kwanza katika kozi za Uhazili na Utunzaji wa Kumbukumbu;

(viii) Kuandaa machapisho mbalimbali kama vile majarida, vitabu, na makala za kitaalamu katika Utumishi wa Umma katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala;

(ix) Kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 30 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi zifuatazo: 17 Shahada ya Uzamivu, 09 Shahada ya Uzamili na 04 Shahada ya Kwanza;

(x) Kugharamia mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 80 wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika maeneo ya Uongozi na Utawala Bora katika Utumishi wa Umma na maeneo mengine kulingana na taaluma zao;

(xi) Kuendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa jengo la ghorofa 2 litakalotumika kwa ajili ya madarasa, maktaba na ofisi katika Kampasi ya Tabora na kufanya ukarabati wa Hostel;

(xii) Kufanya maandalizi ya upanuzi wa maeneo au kampasi za kutolea mafunzo katika mikoa ya Mwanza, Singida na Dodoma kwa kuandaa Mpango Kabambe (Master Plan) wa eneo la Singida, kukamilisha umilikishwaji wa eneo la Mwanza na kununua eneo mkoani Dodoma kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania na kukarabati jengo la Chuo lilitopo Dodoma;

(xiii) Kufanya ukarabati wa mfumo wa umeme na kuweka mfumo wa mawasiliano ya ndani ya kielektroniki (LAN) katika majengo ya Kampasi ya Dar es Salaam; na

(xiv) Kuandaa mpango kazi wa utekelezaji wa ushirikiano na Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo.

**c) Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)**

68. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao imepanga kutekeleza kazi zifuatizo:-

(i) Kutoa mafunzo kwa washiriki 2,500 katika maeneo ya uongozi, utawala bora, maadili, anuai za jamii, mazingira, kupunguza umasikini, Afya na TEHAMA;

(ii) Kuongeza ushirikiano na taasisi za ndani na nje ya nchi ili kutoa mafunzo kwa kutumia teknolojia za kisasa na kwa gharama nafuu;

(iii) Kukuza mtandao wa Wakala kikanda ili kuwafikia wateja walioko mikoani kwa urahisi;

(iv) Kununua vitendea kazi kwa ajili ya Wakala ili kuongeza uwezo wa kutoa huduma bora zinazoendana na ukuaji wa mahitaji;

(v) Kufanya usanifu kwa ajili ya maandalizi ya kujenga ofisi za Wakala Dodoma;

(vi) Kuwapatia mafunzo wafanyakazi 18 wa Wakala ili kuwaongezea uwezo wa utendaji kazi;

(vii) Kuratibu mikutano ya kazi ya Wizara, Mamlaka za Serikaliza Mitaa, Idara, Wakala na taasisi nyingine za serikali kwa kutumia huduma ya daraja-video (bridging services) na kutoa ushauri wa kitaalamu; na

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

(viii) Kufanya utafiti na majaribio ya teknolojia rafiki na rahisi za mawasiliano ya video na mafunzo na kuziboresha.

**d) Wakala ya Serikali Mtandao (eGA)**

69. ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2017/18, Wakala ya Serikali Mtandao inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuendelea na usimamizi na uendeshaji wa Vituo vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya TEHAMA ya Serikalini (Government Data Centres) kwa lengo la kuongeza usalama, kupunguza gharama na kujikinga na Majanga;

(ii) Kuunganisha Taasisi 80 kwenye Mfumo wa Pamoja na Salama wa Barua Pepe wa Serikali na hivyo kuwa na idadi ya taasisi 281 zinazotumia mfumo salama wa mawasiliano serikalini na kuongeza ufanisi wa utendaji kazi;

(iii) Kutengeneza mfumo wa kuwezesha ubadilishanaji taarifa ili kuondoa udurufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma;

(iv) Kukamilisha kazi ya ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Masijala (e-Office) na kusambazwa kwenye Wizara zote na taasisi zitakazokuwa zimeunganishwa kwenye Mtandao wa Mawasiliano wa Serikali (Government Network) ili kuendelea kurahisisha ubadilishanaji wa nyaraka na utoaji wa maamuzi Serikalini.

(v) Kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali hususani Wizara ya Fedha na Mipango na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mfumo Mkuu wa Kusimamia Malipo na Makusanyo ya Maduhuli ya Serikali Kielektroniki (Government Payment Gateway) utakamilishwa na kuanza kutumiwa rasmi na taasisi mbalimbali za Serikali;

(vi) Kuongeza matumizi ya pamoja ya Miundombinu na Mifumo ya TEHAMA kwa kuongeza matumizi

ya Miundombinu iliyopo. Lengo ni kuhakikisha angalau Taasisi 100 za Serikali zinatumia rasilimali hizi pamoja na kuongeza huduma za Serikali zinazotolewa kuititia miundombinu hii;

(vii) Kutoa mafunzo ya Serikali Mtando kwa Viongozi, Wasimamizi wa TEHAMA na Watumishi wa kada mbalimbali kutoka taasisi 150 ili kuongeza uelewa na uwezo wa Taasisi za Umma katika kutumia TEHAMA, kuongeza ufanisi wa kiutendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi;

(viii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi ya Serikali Mtando kwa njia mbalimbali ikiwemo vipindi vyta runinga, redio, machapisho na kwenye mitando;

(ix) Kutoa ushauri wa kitaalam na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa Taasisi 300 za Serikali;

(x) Kukamilisha kuunganisha Taasisi 77 (Hospitali za Mikoa 19, Ofisi za Halmashauri 38 na Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa 20) za Serikali za Mitaa kwenye Mfumo wa Mawasiliano wa Serikali;

(xi) Kuwezesha watumishi 40 wa Wakala kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi, 10 mafunzo ya kitalaam (professional training) na watumishi 2 mafunzo ya muda mrefu; na

(xii) Kutoa elimu kwa watumishi wa Wakala kuhusu VVU na UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na mapambano dhidi ya rushwa.

70. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18 kwa ufanisi, Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 33,695,038,000**. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 26,695,038,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 7,000,000,000** kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

**SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

71. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:

- (i) Kupokea Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni linalopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (ii) Kupokea na kushughulikia malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa Maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka kwa wananchi;
- (iii) Kuchunguza tuhuma yoyote ya ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;
- (iv) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 1,000;
- (v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (vi) Kuelimisha Viongozi wa Umma na Wananchi kwa ujumla kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Hati ya Ahadi ya Uadilifu;
- (vii) Kuandaa taarifa ya Mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;
- (viii) Kuanzisha na kuendeleza Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini; na
  
- (ix) Kuanzisha mchakato wa kutumia mfumo wa ujazaji wa fomu za matamko ya rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa njia ya mtandao (online application) baada ya kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa

Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili (Ethics Management Information System – EMIS).

72. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 8,640,422,004**. Kati ya fedha hizi **Shilingi 6,990,422,004** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,650,000,000** ni fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

#### **SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

73. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka cha fedha wa 2017/18, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia na kuendesha mchakato wa ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenyе sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

(ii) Kuimarisha kanzidata ya kutunza taarifa za waliopangiwa vituo vya kazi, taarifa za kada zenye wataalam wenyе ujuzi maalum (rare profession) na taarifa za wahitimu wa vyuo vikuu nchini;

(iii) Kuendelea kufanya utafiti kwa waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kupata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa michakato ya ajira pamoja na utendaji wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(iv) Kuboresha mfumo wa kielektroniki wa maombi ya kazi (recruitment portal) ili uwasiliane na mifumo mingine kwa lengo la kuwapata watumishi wenyе sifa;

(v) Kuendelea kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira Zanzibar ili kurahisisha mchakato wa ajira kwa ajira za Muungano;

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

- (vi) Kwa kushirikiana na Wakala ya Serikali Mtandao, kuendelea kuboresha na kuimarisha mfumo wa kielektroniki wa kuendesha mchakato wa ajira na utunzaji kumbukumbu za wasailiwa na wataalam mbalimbali na mfumo wa kutuma ujumbe mfupi wa simu za kiganjani (bulk sms);
- (vii) Kushiriki kama Wataalam waalikwa kwenye usaili unaoendeshwa na Taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa kwao;
- (viii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani ya nchi kwa watumishi 5. Aidha, mafunzo pia yatatolewa kwa watumishi wengine kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa watumishi hao;
- (ix) Kuboresha mifumo ya uendeshaji wa usaili kwa kutumia mbinu za kisasa, ikiwemo matumizi ya “psychometric tests”;
- (x) Kutoa taarifa na elimu kwa umma ili kukuza uelewa katika shughuli zinazotekelezwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- (xi) Kusimamia mashauri yahusuyo waombaji wa ajira wanaogushi vyeti; na
- (xii) Kuimarisha miundo mbinu ya TEHAMA itakayosaidia uboreshaji wa utendaji kazi wa Taasisi.

74. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha wa 2017/18, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa Jumla ya Shilingi **3,115,975,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Shilingi **2,365,975,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **750,000,000** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo.

## TUME YA UTUMISHI WA UMMA

75. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha wa 2017/18, Tume ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya Ukaguzi wa kawaida kwa Taasisi 150 na Ukaguzi Maalum kwa Taasisi 10 kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kufanya mikutano ya kisheria ya Tume kujadili na kutolea uamuzi taarifa za ukaguzi, rufaa, malalamiko na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

(iii) Kuelimisha Taasisi za Umma na Watumishi wa Umma kuhusu majukumu ya Tume na utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma kupitia, ziara za Makamishna, vikao vya kazi, vyombo vya habari, machapisho na Tovuti;

(iv) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2016/17 na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais;

(v) Kutoa elimu na mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wapya 24 wa Tume;

(vi) Kutoa huduma kwa watumishi wa Tume wanaoishi na VVU na UKIMWI; na

(vii) Kutoa elimu kwa watumishi wa Tume kuhusu VVU, UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa na mapambano dhidi ya rushwa.

76. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Fungu 94 Tume ya Utumishi wa Umma inatarajia kutumia kiasi cha **Shilingi 4,909,515,670** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

## BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

77. ***Mheshimiwa Spika***, kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/18, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya utafiti wa namna ya kutoa motisha kwa kuzingatia utendaji katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kutoa elimu kwa wadau kuhusu vigezo vinavyotumika kupanga mishahara na masilahi katika Utumishi wa Umma;

(iii) Kuandaa taarifa za gharama za chini za maisha kama msingi wa kukadiria kiwango cha mshahara wenye staha; na

(iv) Kuwajengea uwezo wajumbe 7 na watumishi 20 wa Bodi kuhusu masuala ya mishahara na masilahi.

78. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 1,721,977,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

## IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

79. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Taasisi za Umma 25 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 kwenda Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu, Dodoma;

ii. Kusaidia taasisi za umma 6 kutengeneza miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu;

- iii. Kujenga uwezo wa taasisi za umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano kazi kwa Menejimenti za taasisi za umma na Mafunzo kazi kwa Waratibu na watunza kumbukumbu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za serikali;
- iv. Kukusanya taarifa na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka taasisi za umma na watu binafsi;
- v. Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu yya Waasisi wa Taifa;
- vi. Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali 20 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;
- vii. Kuanzisha na kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Taifa kwa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa kwa kuanzisha Mfumo wa Kidijitali wa Kuhifadhi Nyaraka (Digital Records Management and Preservation System) ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi;
- viii. Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Masjala (e-Filing) kwa lengo la kuboresha huduma, kupunguza gharama na kurahisisha zoezi la Serikali kuhamia Dodoma;
- ix. Kuendeleza ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu katika Kanda ya Ziwa- Mwanza;
- x. Kuimarisha uwezo wa utendaji wa watumishi wa Idara; na
- xi. Kufanya uhakiki (appraisal) wa kumbukumbu tuli za taasisi 3 za umma zilizohifadhiwa katika Kituo cha Taifa

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

cha Kumbukumbu Dodoma ili kubaini zenyе umuhimu wa kuendelea kuhifadhiwa na zile ambazo umuhimu wake umekoma ili kuteketezwa.

80. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa Shilingi **4,375,726,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya Fedha hizo, Shilingi **2,375,726,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **2,000,000,000** ni kwa ajili ya mradi wa Maendeleo.

**OFISI YA RAIS, USHAURI WA MAFUTA NA GESI (OGAB)**

81. ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka wa Fedha wa 2017/18, shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:-

(i) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Baraza la Mawaziri katika masuala yanayohusu uchumi wa mafuta na gesi zikiwemo Sera za Kisekta, Sera ya Uwekezaji, Sheria na Kanuni zinazohusu masuala ya uchumi wa mafuta na gesi na mambo mengine yanayohusiana na uchumi wa mafuta na gesi;

(ii) Kufanya tafiti mbalimbali za uchumi wa mafuta na gesi na kulishauri Baraza la Mawaziri ili kuchocheara maendeleo endelevu kwa faida ya Watanzania wote;

(iii) Kutoa ushauri wa kitaalam kuhusu aina ya utaaliam utakaohusika kwenye majadiliano ya mikataba, ukubwa wa timu ya majadiliano, mikakati na mbinu zitakazotumika na kushiriki kama waangalizi katika majadiliano ya uwekezaji wa kimkakati katika sekta ya mafuta na gesi; na

(iv) Kuwajengea uwezo wataalam wa ushauri wa mafuta na gesi kwa kuwapa mafunzo nje na ndani ya nchi.

82. ***Mheshimiwa Spika***, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Ofisi ya Rais, Ushauri wa Mafuta

na Gesi inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 711,073,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

### **MAJUMUISHO**

83. ***Mheshimiwa Spika***, Mipango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2017/18 ya mafungu yaliyotajwa imezingatia vipaumbele na matakwa ya Serikali ya Awamu ya Tano yenye kusudio la kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika Utumishi wa Umma ili kuondokana na matumizi mabaya ya rasilimali, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na urasimu katika utoaji wa huduma kwa wananchi na kuwa mifumo thabiti ya usimamizi wa utekelezaji. Tunaamini kuwa Utumishi wa Umma uliotukuka ni chachu ya maendeleo kwa Taifa lolote duniani. Hivyo nasi pia tumejipanga kikamilifu kuhakikisha kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake inatoa mchango wake maridhawa katika kufikia malengo yetu kama Taifa na kuiwezesha Nchi yetu kuwa ya uchumi wa kati ifikapo Mwaka 2025.

84. ***Mheshimiwa Spika***, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaunga mkono kwa dhati juhudzi za Mheshimiwa Rais za kupiga vita rushwa, ubadhirifu wa mali ya Umma na ujisadi. Tunaunga mkono hatua stahiki zinazochukuliwa na viongozi katika ngazi mbalimbali ili kurejesha nidhamu ya Utumishi wa Umma na kuboresha huduma kwa wananchi. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge na watu wenyewe mapenzi mema kwa Nchi yetu waendelee kuunga mkono juhudzi hizi. Tumeanza kuona mafanikio lakini bado tunayo kazi kubwa ya kufanya mbele yetu. Aidha, tunaunga mkono kwa nguvu zote uamuzi wa Serikali kuhamia Dodoma, kwa kuanzia Ofisi yangu imeshaanza kutoa huduma ikiwa Makao Makuu kama ilivyoamuliwa.

85. ***Mheshimiwa Spika***, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha wa 2016/17 na mipango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha wa 2017/18, naomba kuwasilisha maombi

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

**a. Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu**

- i. Matumizi ya Kawaida

Jumla	Sh. 16,267,586,000
	<b>Sh.16,267,586,000</b>

**b. Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

i. Matumizi ya Kawaida	Sh. 368,314,145,000
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.379,570,890,000
Jumla	<b>Sh.747,885,035,000</b>

**c. Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

i. Matumizi ya Kawaida	Sh.26,695,038,000
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh. 7,000,000,000
Jumla	<b>Sh. 33,695,038,000</b>

**d. Fungu 33: Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

i. Matumizi ya Kawaida	Sh. 6,990,422,004
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.1,650,000,000
Jumla	<b>Sh.8,640,422,004</b>

**e. Fungu 67: Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

i. Matumizi ya Kawaida	Sh.2,365,975,000
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.750,000,000
Jumla	<b>Sh. 3,115,975,000</b>

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

**f. Fungu 94: Tume ya Utumishi wa Umma**

Matumizi ya Kawaida	Sh. 4,909,515,670
Jumla	Sh.4,909,515,670

**g. Fungu 09: Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma**

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>1,721,977,000</u>
Jumla	Sh. <u>1,721,977,000</u>

**h. Fungu 04: Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Matumizi ya Kawaida	Sh.2,375,726,000
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh. <u>2,000,000,000</u>
Jumla	Sh. <u>4,375,726,000</u>

**j. Fungu 11: Ofisi ya Ushauri ya Mafuta na Gesi Asilia**

Matumizi ya Kawaida	Sh. <u>711,073,000</u>
Jumla	Sh. 711,073,000

86. *Mheshimiwa Spika*, Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2017/18, ni kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida	Sh. 430,351,457,674
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo	Sh.390,970,890,000
Jumla kuu kwa Mafungu yote	Sh.821,322,347,674

87. *Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge*, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

88. *Mheshimiwa Spika*, naomba kutoa hoja.

**ANGELLAH J. KAIRUKI (MB)  
WAZIRI WA NCHI  
OFISI YA RAIS - MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA  
UTAWALA BORA**

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante sana Waheshimiwa Mawaziri. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Angellah Kairuki.

Waheshimiwa Wabunge, kama mlivyoshuhudia wakati Waheshimiwa Mawaziri wanawasilisha hotuba zao hapa, vipaza sauti vyetu havikuwa vizuri sana. Kwa hiyo, naomba mvumilie kwa dakika kama tano hivi, wanataka ku reboot, watazima na kuviwasha lakini endeleeni kukaa hapo hapo mlipo. Haya, watu wa *IT* muendelee sasa.

*(Hapa mfumo wa vipaza sauti ulizimwa kwa muda wa dakika tano na kuwashwa kuruhusu Bunge kuendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Jasson Rweikiza.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Utawala na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa mujibu wa kifungu cha 6(4) kikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais,

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yalipitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya uchambuzi wa bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1), kwa kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Baada ya kutimiza masharti hayo, Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Taarifa hiyo inahusisha jumla ya mafungu 28 kama ifuatavyo:-

- (i) Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.
- (ii) Fungu 2 - Tume ya Utumishi wa Walimu; na
- (iii) Mafungu 26 ya Mikoa ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba baada ya uchambuzi wa taarifa ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii, taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais – TAMISEMI inajikita katika maeneo manne yafuatayo:-

- (i) Matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- (ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017;
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na
- (iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha na kutekelezwa kwa

### **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

mwaka wa fedha 2016/2017. Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Katika mwaka wa fedha 2016/2017 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilitengewa jumla ya shilingi 1,630,731,452,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia sharti la kipindi kisichozidi siku saba ambalo limewekwa na Kanuni, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelizwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Baadhi ya miradi hiyo, inahusu Mpango wa Miji Mkakati Tanzania (*Tanzania Strategic Cities Project*), Mfuko wa Barabara (*Road Fund*), Mfuko wa Maendeleo ya Vijana na Wanawake (asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri) na Ukarabari na Uendelezaji wa Hospitali za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, ufanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo; Mradi Namba 6403 – *Tanzania Strategic Cities Project (TSCP)*. Mradi huu ilitengewa jumla ya shilingi 8,042,405,000 na ulipangwa kutekelezwa chini ya kifungu 8071 cha Fungu 86 – Mkoa wa Tanga na Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya. Utekelezaji wa mradi huu umefikia 55% na unalenga kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga kwa kiwango cha lami ngumu, kuweka taa za barabarani, kujenga vituo vya mabasi na mifereji ya maji taka katika Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mbeya. Aidha, mradi unaendelea na ujenzi wa dampo kubwa la kisasa la kukusanya taka ngumu katika Jiji la Mbeya na Maabara ya Vifaa vya Ujenzi katika Jiji la Tanga. Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo sita kwenye Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 4170 – Mfuko wa Barabara (*Road Fund*). Mradi huu ilitengewa jumla ya shilingi 12,395,296,399 na unatekelezwa kupitia Akaunti Maalum ya Mfuko wa Barabara katika Fungu Namba 86 – Mkoa wa Tanga, Fungu Namba 73 – Mkoa wa Iringa na Fungu Namba 79 – Mkoa wa Morogoro. Mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya barabara, matengenezo ya barabara za

kawaida na sehemu korofu kwa kujenga kwa kiwango cha lami, kujenga vituo vya mabasi, mifereji ya majitaka, madaraja na kuwajengea uwezo wataalam wa barabara waliopo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ili kujiridhisha na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo sita yaliyoko kwenye Mikoa ya Tanga, Morogoro na Iringa.

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 4946 – *Local Government Own Source Projects*. Mradi huu ilitengewa jumla ya shilingi 460,589,216,216 na unatekelezwa chini ya kifungu 8091 cha Fungu Namba 78 – Mkoa wa Mbeya, Fungu Namba 54 – Mkoa wa Njombe na Fungu Namba 86 – Mkoa wa Tanga. Mradi unalenga kusaidia vikundi vya wanawake na vijana kupitia Halmashauri kwa kutenga 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri, kwa ajili Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake. Ili kujiridhisha na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo matano katika Mikoa ya Tanga, Mbeya na Njombe.

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 5402 – Ukarabati na Uendelezaji wa Hospitali za Mikoa (*Regional Hospital Rehabilitation*). Mradi huu ilitengewa shilingi 1,342,700,000 na unatekelezwa chini ya Kifungu Namba 3001 cha Fungu Namba 86 – Mkoa wa Tanga na Fungu Namba 78 – Mkoa wa Mbeya. Kwa mujibu wa taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, Mradi huu umekuwa ukilenga kukarabati na kuendeleza majengo ya Hospitali za Mikoa ili kuziwezesha kutoa huduma ya rufaa katika hospitali hizo. Ili kujiridhisha kuhusiana na hatua ziliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo mawili katika mikoa ya Tanga na Mbeya.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi. Ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni muhimu kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya ukaguzi huo. Kwa

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na majedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi illyo chini ya Ofisi ya Rais. Ufafanuzi huu wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 6403 – *Tanzania Strategic Cities Project*. Katika maeneo sita yaliyoko kwenye Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mbeya ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mafanikio ni:-

(i) Kuongezeka kwa kilomita za barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami. Mfano, katika Jiji la Mbeya barabara hizo zimeongezeka kutoka kilometa 29 zilizokuwepo kabla ya kuanza kwa mradi huu hadi 52.1 sawa na 79.6%;

(ii) Kuboreshwa kwa mandhari ya Majiji ya Mbeya na Tanga;

(iii) Kupanda kwa thamani ya viwanja na majengo yaliyo jirani na mradi wa *TSCP*;

(iv) Dampo la kukusanya taka limechangia kuweka maeneo ya Jiji la Mbeya katika hali ya usafi.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni:-

(i) Kukosekana kwa mifereji ya kuondoa maji ya mvua kwenye barabara zilizojengwa na mradi huu na hivyo kusababisha maji kutuama kwa muda mrefu na kuharibu barabara;

(ii) Baadhi ya madereva wasio waaminifu wamekuwa wakipitisha magari yenye uzito zaidi ya unaotakiwa kwenye barabara zilizojengwa. Mfano, barabara ya Kabwe – Block T, Kisanji na Sae – Ituha za Jijini Mbeya zimejengwa kwa ajili

ya magari yasiyozidi tani 10. Hata hivyo, madereva wa magari wasiozingatia alama za barabaranii wamekuwa wakipitisha magari yenye uzito zaidi ya huo; na

(iii) Wizi wa karatasi ngumu katika eneo linalosaidia kuhifadhi taka kwenye dampo la kisasa katika Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 4170 – Mfuko wa Barabara (*Road Fund*). Katika maeneo sita ya Mikoa ya Tanga, Morogoro na Iringa ambayo Kamati iliyatembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huo, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ni:-

(i) Kuongezeka kwa mtando wa barabara za lami na changarawe katika mikoa husika;

(ii) Kuwezesha barabara za maeneo korofi kuitika katika muda wote wa mwaka;

(iii) Kutengeneza mifereji kwa ajili ya maji ya mvua na hivyo kuepusha uharibifu wa barabara unaosababishwa na maji kutuama;

(iv) Kufungua mawasiliano ya barabara kwa kujenga madaraja katika maeneo ambayo mvua zinaharibu barabara na kuvunja madaraja. Mfano, katika Mkoa wa Iringa, madaraja 11 yamejengwa katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuchelewa kwa fedha za Mfuko wa Barabara na hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi mradi huu;

(ii) Upungufu wa wahandisi wa barabara katika Halmashauri, jambo linalosababisha usimamizi hafifu na kukosekana kwa ushauri wa kitaalam katika mradi. Mfano, Mkao wa Iringa una wahandisi 12 tu katika 20 wanaohitajika;

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(iii) Uchache wa mitambo ya kutengenezea barabara kwenye Halmashauri nyingi nchini jambo linalosababisha utegemezi wa mitambo ya kukodi na hivyo kuongeza gharama za mradi; na

(iv) Baadhi ya miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

Mheshimiwa Spika, Mradi Namba 4946 – *Local Government Own Source Projects*. Kwa upande wa mradi huu, katika maeneo matano ambayo Kamati iliyatembelea kwenye Mikoa ya Tanga, Mbeya na Njombe, mambo kadhaa yilibainika yakijumuisha mafanikio na changamoto. Ufanuzi zaidi unatolewa katika jedwali namba 01 la taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, mafanikio ni kama ifuatavyo:-

(i) Wanawake na vijana wamewezeshwa kupata elimu ya ujasiriamali na mikopo ya kuanzisha miradi ya kiuchumi;

(ii) Baadhi ya vikundi vimeanzisha vyama vya ushirika na kuweka *SACCOS* kuitia fedha hizi na kukuza mtaji ili kuongeza wigo wa mikopo katika jamii. Mfano ni kikundi cha Nyombo katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambacho kilianzisha *SACCOS* mwaka 1999 kwa mtaji wa shilingi milioni 1.4 na hadi mwezi Februari, 2017 mtaji huo ulikuwa umeongezeka hadi kufikia shilingi billioni 1.58; na

(iii) Kupungua kwa uhalifu kwani vijana wamepata mitaji inayowawezesha kuanzisha shughuli za kuwaingizia kipato.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni kama ifuatavyo:-

(i) Kukosekana kwa sheria inayosimamia utekelezaji wa Agizo la Serikali la kuzitaka Halmashauri kutenga kikamilifu asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake;

(ii) Halmashauri kutumia sehemu ya mapato yanayotokana na asilimia kumi ya mapato ya ndani kufanya shughuli nyingine na hivyo kuwanyima vijana na wanawake fursa ya kupata mikopo; na

(iii) Baadhi ya vikundi vya wanawake na vijana kutorejesha fedha kikamilifu ili kutoa fursa kwa wengine kukopeshwa.

Mheshimiwa Spika, Ukarabati wa Hospitali za Mikoa (*Regional Hospital Rehabilitation*), katika Hospitali mbili za Mikoa ambazo Kamati ilitembelea katika Mikoa ya Tanga na Mbeya ili kukagua utekelezaji wa mradi huu, mambo yafuatayo yalijiri:-

Mheshimiwa Spika, mafanikio ni kama ifuatavyo:-

(i) Kujengwa kwa baadhi ya majengo muhimu kama vile jengo la */ICU* (Hospitali ya Mkoa wa Tanga);

(ii) Ukarabati wa majengo chakavu na kuanza kutumika. Mfano, Hospitali ya Mkoa wa Tanga imekarabati jengo la *grade one* kwa shilingi milioni 28 na sasa linatumika; na

(iii) Hospitali ya Mkoa wa Mbeya imefanikiwa kujenga mita 429 za njia za kupitia wagonjwa (*patients walk ways*) na zote hizi zimeezekwa.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti finyu inayotengwa na kutopatikana kikamilifu;

(ii) Kukosekana kwa huduma muhimu za tiba na ukosefu majengo. Mfano, Hospitali ya Mkoa wa Mbeya haina majengo ya huduma muhimu za tiba yapatayo tisa. Miiongoni mwa hayo ni jengo la huduma ya dharura (*casualty*) na upasuaji (*theatre*); na

(iii) Kutokupatikana kikamilifu kwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya hospitali hizo. Mfano, kati ya shilingi milioni 467 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya upasauji katika Hospitali ya Mkoa wa Mbeya ni shilingi milioni 200 tu ndiyo zilikuwa zimetolewa hadi mwezi Februari, 2017. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 42.8 ya kiasi kilichotengwa.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2015/2016. Kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba:-

(i) Miradi ya maendeleo ingetekelezwa kikamilifu na kukamilika kwa wakati iwapo fedha zilizotengwa zingetoka kwa wakati na kiasi cha kutosha;

(ii) Uelewa wa kutosha juu ya uendeshajji wa miradi pamoja na ushirikishwaji wa wananchi utasaidia wananchi kuanzisha miradi na kuifanya kuwa endelevu;

(iii) Kukosekana kwa umakini na upembuzi yakinifu wa kutosha kwenye miradi ya maendeleo kunaisababishia Serikali hasara kutokana na kuongezeka kwa gharama za miradi;

(iv) Matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato yamechangia kuongezeka kwa makusanyo ya Serikali na kudhibiti mianya ya upotevu; na

(v) Kukosekana kwa maeneo maalum ya kufanya biashara na shughuli za uzalishajji, kunakwamisha juhudzi za kuwakwamua kiuchumi vijana na wanawake.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili

ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kwa kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati pamoja na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati vikao nya Kamati. Kwa ufanuzi wa ziada kuhusu uchambuzi huu, Kamati imetumia majedwali ili kurahisisha maelezo yake wakati wa kuonesha taarifa, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa kuhusu ukusanyaji maduhuli. Ofisi ya Rais – TAMISEMI - Fungu 56 ilitarajiva kukusanya jumla ya shilingi 16,880,839,976.00 kutoka vyanzo nya ndani. Hadi kufikia Februari, 2017 jumla ya shilingi 4,750,262,451.03 zillikuwa zimekusanya na Fungu 56. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 28.13 ya mapato yaliyokadiriwa kukusanya katika mwaka wa fedha 2016/2017. Kamati ilielezwa kwamba sababu za makusanyo kidogo ni pamoja na:-

(i) Mauzo machache ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu nya ofisi; na

(ii) Ukusanyaji mdogo wa mapato kutoka vyanzo vingine tofauti na makadirio ya awali.

Mheshimiwa Spika, ingawa mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli siyo mzuri, hata hivyo, kiasi kilichokusanya kimeongezeka kwa zaidi ya asilimia 16 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 12 kilichokusanya katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/2016. Kamati inatarajia kuwa, mwenendo huu wa ukusanyaji mapato utaendelea kuimarika katika mwaka ujao wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba:-

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo kuliko ilivyokusudiwa; na

(ii) Fedha zinazopaswa kutolewa na Hazina hazipatikani kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2017 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na taasisi zilizo chini yake ilikuwa imepokea shilingi 202.29 kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 57 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii. Ulingenisho wa Kamati kuhusiana na hali hiyo ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2016/2017 na mwaka 2015/2016 ulibaini kwamba, kiasi hicho cha fedha ni ongezeko la asilimia nane tu ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2015/2016 ambapo ulikuwa ni asilimia 48 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa kwa kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida kilikuwa shilingi 18.62 ambacho ni sawa na asilimia 64 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi hayo. Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa asilimia 18 ikilinganishwa na fedha iliyokuwa imepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawada katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/2016 ambayo ilikuwa ni asilimia 46 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2017 Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zake ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 183.66 kutoka Hazina kiasi ambacho ni sawa na asilimia 56 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa asilimia nane ikilinganishwa na kiasi kilichokuwa kimepokelewa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ajili ya maendeleo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, namuongezea Mwenyekiti nusu saa ili aweze kumaliza hotuba yake. Mheshimiwa Mwenyekiti unaweza ukaendelea. (*Makof*)

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa asilimia nane ikilinganishwa na kiasi kilichokwu kimepokelewa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/2016 kwa ajili ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba bado upatikanaji fedha kwa ajili ya maendeleo umeendelea kuwa chini ikilinganishwa na fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Tafsiri ya mwenendo huu ni kwamba utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaendelea kusuasua katika kipindi cha mwaka wa fedha kilichosalia.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa uwiano wa fedha iliyoidhishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na fedha iliyopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2017 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Ufafanuzi zaidi wa ulinganisho huu umeoneshwa kupitia Jedwali Namba 02.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa ushauri wa Kamati, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri katika mambo 15 kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa iliweza kuzingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kufanya hivyo kwa maoni mengine yaliyosalia. Baadhi ya maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha Halmashauri na Mikoa inatumia kikamilifu Mifumo ya Kielektroniki katika ukusanyaji wa

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

mapato. Hadi Februari mwaka huu jumla ya Halmashauri 175 kati ya 185 ambazo ni sawa na asilimia 95 zinatumia mfumo wa *LGR CIS*. Aidha, Hospitali 19 za Rufaa za Mikoa, Hospitali 43 za Wilaya, Vituo vya Afya 38 na Zahanati moja zimefungiwa Mfumo wa *GoT – HOMIS*;

(ii) Uhakiki wa watumishi hewa na kuwaondoa katika mfumo wa malipo ya mishahara (*payroll*) ambapo hadi mwishoni wa Februari, 2017 jumla ya watumishi 13,369 waliondolewa katika orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali kutokana na sababu za utoro, kustaafu na vifo. Aidha, kati ya watumishi hao 4,968 walibainika kuwa watumishi hewa na wameisababishia Serikali hasara ya shilingi bilioni 25.36; na

(iii) Kukamilisha mfumo wa ukusanyaji nauli kwa njia ya kielektroniki na kupanga nauli ili Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (*DART*) uanzo kutoa huduma kwa wakazi wa Jiji la Dar es Salaam. Mfumo huo ulikamilika na kuanza kutumika katika ukusanyaji wa nauli tangu tarehe 16 Mei, 2016.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maoni ambayo yanaendelea kuzingatiwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuhakikisha Halmashauri zinatenga kikamilifu asilimia kumi ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi wanawake na vijana; na

(ii) Kuhakikisha fedha za maendeleo hazichelewi kutoka Hazina. Bado zinachelewa kwani hadi Februari, 2017 ni asilimia 56 tu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo hayo ndio zilikuwa zimetolewa na Hazina.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa mpango wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; taarifa ya mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inayojumuisha Mafungu 28 (Fungu 56; Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) imeandaliwa kwa kuzingatia

vipaumbele vilivyoanishwa katika llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020; Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals*); Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI uliofanyiwa mapitio mwaka 2016; Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa kitaifa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inapanga kutekeleza malengo yanayoonekana kwenye taarifa Kamati.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi triliioni 6.57; katи ya fedha hizo, shilingi triliioni 4.54 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi triliioni 1.78 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika fedha za Matumizi ya Kawaida shilingi triliioni 4.27 sawa na asilimia 89.15 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 519.447 sawa na asilimia 10.8 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Jedwali Na. 03 la taarifa hii linafafanua zaidi kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio na mapato; katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, inakadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 713.189. Mapato hayo yameongezeka kwa shilingi bilioni 30.58 sawa na asilimia 4.48 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa mgawanyo utakaooneshwa katika Jedwali Na. 04 la taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchambuzi, sehemu kubwa ya makusanyo inatarajiwa kupatikana kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na mfumo wa Serikali za Mitaa kuwa na watu wengi na kumiliki vyanzo

vingi vya mapato. Aidha, kuanza kutumika kwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kieletroniki kumeonekana kusaidia ongezeko la makusanyo. Aidha, Mikoa licha ya kuwa na ongezeko kubwa la makusanyo (asilimia 843.63) bado imeendelea kuwa na makusanyo kidogo ikilinganishwa na Halmashauri na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa makadirio na matumizi; katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaombewa kuidhinishiwa jumla ya shilingi triliuni 6.57 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo zinazombwa, shilingi triliuni 4.79 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi triliuni 1.78 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, katika fedha hizo zipo shilingi billioni 12.42 kwa ajili ya mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu.

Mheshimiwa Spika, kiasi cha fedha kinachoombwa kimeongezeka kwa shilingi billioni 516.240 sawa na asilimia 8.52% ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake, kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Hata hivyo, ongezeko la mwaka huu ni dogo ikilinganishwa na lillopita katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambalo lilikuwa asilimia 12.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi umebaini kwamba, katika fedha za miradi ya maendeleo, kuna ongezeko la shilingi billioni 148.39 kutoka shilingi 1.63 za mwaka wa fedha 2015/2016 hadi shilingi 1.78 katika mwaka wa fedha 2017/2018. Ongezeko hili ambalo ni sawa na asilimia 9.10 ni dogo sana kwani limepungua kwa zaidi ya mara saba, ikilinganishwa na ongezeko lilloshuhudiwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambalo lilikuwa ni asilimia 74. 83.

Mheshimiwa Spika, ni jambo lisilopingika kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ndiyo inayoongoza kwa kuwa na bajeti kubwa dhidi ya Wizara nyingine ikilinganishwa na bajeti ya Taifa. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2017/2018 bajeti

ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefikia asilimia 20.72 ya Bajeti ya Taifa ambayo ni takribani shilingi trilioni 31.699. Hilo ni ongezeko la asilimia 0.2 ikililinganishwa na mwaka wa fedha 2016/2017 ambapo ongezeko lilikuwa asilimia 20.5. Hata hivyo...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mwenyekiti, kwa kengele hiyo maana yake ni kwamba uwe unamalizia ripoti ya kwanza ili uanze ripoti ya pilii.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo na taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita ina maoni kama ifuatavyo:-

- (i) Serikali isimamie na kuhakikisha Halmashauri zinaandaa na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na vikundi vya wanawake na vijana;
- (ii) Halmashauri zibuni vyanzo vipyta vya mapato ili kuepuka kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu;
- (iii) Mikoa iandae vipaumbele vichache kulingana na uwezo wa bajeti;
- (iv) Halmashauri ziwatumiie Maafisa wa Maendeleo ya Jamii kutoa elimu ya ujasiriamali kwa vijana na wanawake;
- (v) Halmashauri zishirikiane na Mpango wa MKURABITA ili kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi;
- (vi) Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati;

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(vii) Serikali iandae utaratibu utakaowezesha Halmashauri kukusanya kikamilifu mapato yatokanayo na huduma za minara ya simu;

(viii) Serikali iongeze kasi ya kuajiri wataalam wa afya na upatikanaji wa dawa;

(ix) Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo hazijaanza kutumia mfumo wa kielektroniki zianze kufanya hivyo; na

(x) Serikali ipeleke kikamilifu fedha za ukarabati na uendelezaji wa hospitali za Mikoa ili kuziwezesha kukamilisha matengenezo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, napenda kutoa pongezi za dhati kwako binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge. Aidha, nitumile fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcemba, kwa kuchaguliwa na Wajumbe wa Kamati, kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Hiyo inaonesha kwamba wana imani kubwa na yeye pamoja na kutambua kwamba mchango wake wa Kamati kwa kipindi chote alichokuwa akinisaidia kabla hajachaguliwa rasmi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kamati hii ina mafungu mengi sana, nawashukuru wajumbe wa Kamati kwa kujitolea muda wao mwangi sana, kufanya kazi kwa muda mwangi hadi usiku na siku za mwisho wa juma bila kudai malipo ya ziada.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, naomba nitaje Wajumbe hao kama ifuatavyo...

**SPIKA:** Hao waruke tu Mwenyekiti, muda kwenye ripoti ya pili utakuwa mdogo usipoangalia.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI WA KAMATI YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, sawa nairuka hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio

ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hotuba ya pili ataisoma Makamu Mwenyekiti.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA  
NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU  
YA OFISI YA RAIS, UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KWA  
MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAONI YA  
KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, yalipitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya uchambuzi wa Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1), kwa kutembelea na

## *NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2015/16. Baada ya kutimiza sharti hilo, Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa fedha 2016/2017. Taarifa hiyo inahusisha jumla ya Mafungu Ishaarini na Nane (28) kama ifuatavyo:-

- i. Fungu 56: Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- ii. Fungu 02: Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC); na
- iii. Mafungu 26 ya Mikoa yote ya Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya uchambuzi wa Taarifa ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii yaliyowasiliishwa, Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais – TAMISEMI inajikita katika maeneo manne yafuatayo:-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## **2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

### **2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ilitengewa

jumlah ya **Shilingi 1,630,731,452,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuzingatia sharti la kipindi kisichozidi siku Saba (7) ambalo limewekwa na Kanuni, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelizwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI. Baadhi ya miradi hiyo, inahusu Mpango wa Miji Mkakati Tanzania (*Tanzania Strategic Cities Project – TSCP*); Mfuko wa Barabara (*Road Fund*); Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri) na Ukarabari na Uendelezaji wa Hospitali za Mikoa. Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

#### **2.1.1 Mradi Na. 6403 - Tanzania Strategic Cities Project (TSCP).**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ultengewa jumla ya **Shilingi 8,042,405,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 8071 cha **Fungu 86** – Mkao wa Tanga, na **Fungu 78** – Mkao wa Mbeya. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 55 na unalenga kuboresha miundombinu ya barabara kwa kujenga kwa kiwango cha lami ngumu, kuweka taa za barabarani, kujenga vituo vya Mabasi na mifereji ya maji taka katika Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mbeya. Aidha, mradi unaendelea na ujenzi wa Dampo kubwa la kisasa la kukusanya taka ngumu katika Jiji la Mbeya, na Maabara ya Vifaa vya Ujenzi katika Jiji la Tanga.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa, mradi huu unatekelezwa katika Miji Saba nchini ambayo ni Arusha, Mwanza, Mbeya, Tanga, Dodoma, Mtwara Mikindani, na Kigoma (Ujiji) na Ustawishaji wa Makao Makuu Dodoma (CDA). Ili kujiridisha na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo Sita (6) kwenye Halmashauri za Majiji ya Tanga na Mbeya.

### **2.1.2 Mradi Na. 4170 – Mfuko wa Barabara (Road Fund).**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ilitengewa jumla ya **Shilingi 12,395,296,399** na unatekelezwa kupitia Akaunti Maalum ya Mfuko wa Barabara katika Fungu 86: – Mkao wa Tanga; Fungu 73: – Mkao wa Iringa na Fungu 79: – Mkao wa Morogoro. Mfuko huu ulianzishwa mwaka 1992 kwa lengo la kukarabati, kuboresha na kutengeneza barabara muhimu za Mikoa, Wilaya na Mijini, kwa kutumia vyanzo vya ndani vya mapato kama vile tozo na ushuru katika matumizi ya barabara na mafuta, leseni na usajili wa magari. Mfuko huu umekuwa ukisimaiwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI pamoja na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi huu unalenga kuboresha miundombinu ya barabara, matengenezo ya barabara ya kawaida na sehemu korofii kwa kujenga kwa kiwango cha lami, kujenga vituo vya mabasi, mifereji ya maji taka, madaraja na kuwajengea uwezo wataalam wa barabara walipo katika sekretarieti za Mkao na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Ili kujiridhisha na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo Sita yaliyoko kwenye Mikoa ya Tanga, Morogoro na Iringa.

### **2.1.3 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects.**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ilitengewa jumla ya **shilingi 460, 589, 216, 216** na unatekelezwa chini ya kifungu 8091 cha Fungu 78: - Mkao wa Mbeya; Fungu 54: Mkao wa Njombe na Fungu 86: Mkao wa Tanga. Mradi unalenga kusaidia Vikundi vya Wanawake na Vijana kupitia Halmashauri kwa kutenga asilimia kumi (10%) ya mapato ya Ndani ya Halmashauri, kwa ajili Mfuko wa Maendeleo wa Vijana na Wanawake.

Ili kujiridhisha na hatua ya utekelezaji iliyofikiwa katika mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo matano (5) katika Mikoa ya Tanga, Mbeya na Njombe.

#### **2.1.4 Mradi Na.5402 – Ukarabati na Uendelezaji wa Hospitali za Mikoa (Regional Hospital Rehabilitation)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ultengewa **shilingi 1,342,700,000** na unatekeleza chini ya Kifungu cha 3001 cha Fungu 86 – Mkoa wa Tanga, na Fungu 78: - Mkoa wa Mbeya. Kwa mujibu wa Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, Mradi huu umekuwa ukilenga kukarabati na kuendeleza majengo ya Hospitali za Mikoa ili kuziwezesha kutoa huduma ya rufaa katika hospitali hizo.

Ili kujiridhisha kuhusiana na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo mawili (2) katika Mikoa ya Tanga na Mbeya.

#### **2.2 Matokeo ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni muhimu kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya ukaguzi huo. Kwa madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na majedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi iliyio chini ya Ofisi hii. Ufafanuzi wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:

##### **2.2.1 Mradi Na. 6403 - Tanzania Strategic Cities Project (TSCP).**

**Mheshimiwa Spika**, katika maeneo Sita yaliyoko kwenye Halmashauri za Majiji ya Mbeya na Tanga, ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa Mradi huu wa Miji ya Kimkakati (*Tanzania Strategic Cities Project*), mambo

kadhaa yilibainika kuhusiana na utekelezaji huo, ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto:

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitokeza. Kutokana na ukaguzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

**a) Mafanikio;**

i) Kuongezeka kwa kilomita za barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami. Mfano; katika Jiji la Mbeya barabara hizo zimeongezeka kutoka kilomita 29 zilizokuwepo kabla ya kuanza kwa mradi huu hadi 52.1 (ongezeko hilo ni sawa na asilimia 79.65);

ii) Kuboreshwa kwa mandhari ya Majiji ya Mbeya na Tanga;

iii) Kupanda thamani kwa viwanja na majengo yaliyo jirani na miradi ya TSCP;

iv) Vituo vya Mabasi ambavyo vimejengwa kupitia mradi huu, vimesaidia kuondoa kero ya usafiri kwa kupunguza msongamano wa mabasi;

v) Fursa za biashara, kwa maeneo yaliyo kando na miradi ya TSCP;

vi) Dampo la kukusanya Taka, limechangia kuweka maeneo ya Jiji la Mbeya katika hali ya usafi;

**b) Changamoto;**

(i) Kukosekana kwa mifereji ya kuondoa maji ya mvua kwenye barabara zilizojengwa na mradi huu, na hivyo kusababisha maji kutuama kwa muda mrefu na hivyo kuharibu barabara;

(ii) Baadhi ya madereva wasio waaminifu wamekuwa wakipitisha magari yenye uzito zaidi ya

unaotakiwa kwenye barabara zilizojengwa. Mfano; barabara za Kabwe – Block T, Kisanji na Sae – Ituha, za Jijini Mbeya zimejengwa kwa ajili ya magari yasiyozidi Tani 10. Hata hivyo, madereva wa magari wasiozingatia alama za barabarani wamekuwa wakipitisha magari yenye uzito zaidi;

(iii) Kupasuka mara kwa mara kwa mabomba yaliyokatisha kwenye barabara, kunasababisha uharibifu kwenye maeneo hayo ya barabara. Mfano ni barabara ya Ilomba – Isyesye na Airport – Samora, katika Jiji la Mbeya; na

(iv) Wizi wa karatasi ngumu katika eneo linalosaidia kuhifadhi taka kwenye Dampo la kisasa, katika jiji la Mbeya.

#### **2.2.2 Mradi Na. 4170 – Mfuko wa Barabara (Road Fund).**

**Mheshimiwa Spika**, katika maeneo Sita (6) ya Mikoa ya Tanga, Morogoro na Iringa, ambayo Kamati iliyatembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto.

##### **(a) Mafanikio;**

i. Kuongezeka kwa mtandao wa barabara za lami, na changarawe katika mikoa husika. Mfano; katika Jiji la Tanga, Mfuko wa Barabara umetengeneza kilomita Tisa za barabara kwa kiwango cha changarawe;

ii. Kuwezesha barabara za maeneo korofii kupitika katika muda wote wa mwaka;

iii. Kutengeneza mifereji kwa ajili ya maji ya mvua na hivyo kuepusha uharibifu wa barabara unaosababishwa na maji kutuama;

iv. Wataalam wa barabara katika Sekretarieti ya Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, wamejengewa uwezo;

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

vii) Kufungua mawasiliano ya barabara kwa kujenga madaraja katika maeneo ambayo mvua zinaharibu barabara na kuvunja madaraja. Mfano; katika mkoa wa Iringa, madaraja 11 yamejengwa katika mwaka wa fedha 2015/16.

**(b) Changamoto;**

i. Kuchelewa kwa fedha za mfuko wa barabara na hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa;

ii. Kusuasua kwa utekelezaji wa miradi ya mfuko wa barabara, kutopteka na urasimu wa kuhamisha miundombinu ya maji safi na mati taka, pamoja na nguzo za Umeme;

iii. Upungufu wa Wahandisi wa barabara, katika halmashauri, jambo linalosababisha usimamizi hafifu na kukosekana kwa ushauri wa kitaalam, katika miradi. Mfano; Mkoa wa Iringa una Wahandisi 12 tu kati ya 20 wanaohitajika. Upungufu huo ni sawa na asilimia 60 ya mahitaji.

iv. Uchache wa mitambo ya kutengenezea barabara kwenye halmashauri nyingi nchini, jambo linalosababisha utegemezi wa mitambo ya kukodi na hivyo kuongeza gharama za miradi;

v. Uharibifu wa mara kwa mara wa miundombinu unaosababishwa na mvua na hivyo kuhitaji ukarabati wa mara kwa mara; na

vi. Baadhi ya miradi kutekelezwa chini ya kiwango.

**2.2.3 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi huu, katika maeneo matano maeneo matano (5) ambayo Kamati iliyatembelea kwenye Mikoa ya Tanga, Mbeya na Njombe,

maumbo kadhaa yalibainika yakijumuisha mafanikio na changamoto. Ufafanuzi zaidi unatolewa kuititia **Jedwali Na.01**

**Jedwali Na.01:** Mikoa na Vikundi vilivyopata mikopo kutoka Asilimia Kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri.

M k o a	F u n g u	V i k u n d i v i l i v y o k o p e s h w a	F e d h a i l i y o t o l e w a
T a n g a	8 6	2 7	6 6 , 0 0 0 , 0 0 0
M b e y a	7 8	5 2	1 0 1 , 6 0 0 , 0 0 0
N j o m b e	5 4	1 9 7	2 9 2 , 9 8 9 , 2 1 6
J u m l a		2 7 6	4 6 0 , 5 8 9 , 2 1 6

Chanzo: Taarifa za Mikoa ya Tanga, Mbeya na Njombe.

**(a) Mafanikio;**

i. Wanawake na Vijana wamewezeshwa kupata elimu ya ujasiriamali na mikopo ya kuanzisha miradi ya kiuchumi;

ii. Wanufaika wameweza kuongeza kipato na hivyo kuboresha hali ya maisha;

iii. Baadhi ya vikundi vimeanzisha vyama vyaya kuweka na kukopa (SACCOs) kuititia fedha hizi, na kukuza mtaji ili kuongeza wigo wa mikopo katika jamii. Mfano ni Kikundi cha Nyombo, katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe ambacho kilianzisha SACCOs mwaka 1999 kwa mtaji wa **shilingi milioni 1.4** na hadi mwezi Februari, 2017 mtaji huo ulikuwa umeongezeka hadi kufikia **shilingi bilioni 1.58**; na

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

iv. Kupungua kwa uhalifu kwani Vijana wanapata mitaji inayowawezesha kuanzisha shughuli za kuwaingizia kipato;

**(b) Changamoto;**

(i) Kukosekana kwa sheria inayosimamia utekelezaji wa Agizo la Serikali la kuzitaka Halmashauri kutenga kikamilifu asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya Mfuko wa Vijana na Wanawake;

(ii) Halmashauri kutumia sehemu ya mapato yanayotokana na asilimia kumi (10%) ya Mapato ya ndani, kutekeleza shughuli nyingine, na hivyo kuwanyima Vijana na Wanawake fursa ya kupata mikopo;

(iii) Baadhi ya Vikundi vya Wanawake na Vijana kutorejesha fedha kikamilifu ili kutoa fursa kwa wengine kukopeshwa;

(iv) Baadhi ya Vijana na Wanawake kukosa elimu ya ujasiriamali na hivyo kushindwa kuendesha miradi wanayoianzisha;

(v) Halmashauri kukosa Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa kutosha kwa ajili ya kuelimisha Vijana na Wanawake wanaonufalka na mikopo hii; na

(vi) Vijana na Wanawake kukosa maeneo rasmi ya kuendeshea shughuli wanazoanzisha kutohana na mikopo wanayopewa na mpango huu.

**2.2.4 Ukarabati wa Hospitali za Mikoa “*Regional Hospital Rehabilitation*”**

**Mheshimiwa Spika**, katika Hospitali mbili za Mikoa ambazo Kamati ilitembea katika Mikoa ya Tanga na Mbeya, ili kukagua utekelezaji wa mradi huu, mambo yafuatayo yalijiri:-

**(a) Mafanikio;**

- i. Kujengwa kwa baadhi ya majengo muhimu kama vile jengo la ICU (Hospitali ya Mkoa wa Tanga);
- ii. Ukarabati wa majengo chakavu na kuanza kutumika. Mfano; Hospitali ya Mkoa wa Tanga imekarabati jengo la Grade One kwa **shilingi milioni 28** na sasa linatumika;
- iii. Hospitali ya Mkoa wa Mbeya imefanikiwa kujenga mita 429 za njia za kupitia wagonjwa (*walk ways*); na
- iv. Ununuzi wa gari la kubebea wagonjwa mahututi kwa hospitali ya Mkoa wa Tanga.

**(b) Changamoto;**

- i. Bajeti finyu inayotengwa na kutopatikana kikamilifu;
- ii. Hospitali kukabiliwa na msongamano mkubwa wa wagonjwa;
- iii. Kukosekana kwa huduma muhimu za tiba kwa ukosefu majengo. Mfano; Hospitali ya Mkoa wa Mbeya, haina majengo ya Huduma muhimu za tiba Tisa, mionganini mwa hayo ni jengo la huduma ya dharura (*casualty*) na upasuaji (*theatre*);
- iv. Barabara za kikamilifu kwa fedha hizo. Mfano; katи ya **shilingi milioni 467** zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa Wodi ya Upasuaji katika hospitali ya Mkoa wa Mbeya, ni **shilingi milioni 200** tu ndiyo ilikuwa imetolewa hadi mwezi Februari, 2017. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 42.82** ya kiasi kilichotengwa.
- v. Uchakavu wa majengo;
- vi. Ukosefu wa vifaa kama Ct Scan, Echo na vitendanishi vyaa maabara;

- vii. Bajeti finyu kwa ajili ya dawa; na
- viii. Ukosefu wa Wodi ya Wagonjwa mahututi.

### **2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2015/2016**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba:-

(i) Miradi ya maendeleo ingetekelizwa kikamilifu na kukamilika kwa wakati iwapo fedha zilizotengwa zingetoka kwa wakati na kiasi cha kutosha;

(ii) Urasimu katika Halmashauri unachelewesha hatua muhimu za utekelezaji wa miradi;

(iii) Uelewa wa kutosha juu ya uendeshaji wa miradi pamoja na ushirikishwaji wa Wananchi utasaidia Wananchi kuanzisha miradi na kuifanya kuwa endelevu;

(iv) Kukosekana kwa umakini na upembizi yakinifu wa kutosha kwenye miradi ya maendeleo, kunaisababishia Serikali hasara kutokana na kuongezeka kwa gharama za miradi;

(v) Kukosekana kwa ufanisi wa kitaalam katika usimamiaji wa miradi ya maendeleo kunasababisha miradi hiyo kutekeleza chini ya kiwango;

(vi) Matumizi ya mfumo wa kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato, yamechangia kuongezeka kwa makusanyo ya Serikali na kudhibiti mianya ya upotevu;

(vii) Kukosekana kwa maeneo maalum ya kufanya biashara na shughuli za uzalishaji, kunakwamisha juhudzi za kuwakwamua kiuchumi Vijana na Wanawake;

(viii) Kukosekana kwa elimu ya usajiri amali kwa Vijana na Wanawake, kunawakwamisha kujikwamua kiuchumi;

### **3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

#### **3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kwa kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati, pamoja na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati vikao vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, kwa uafanuzi wa ziada kuhusu uchambuzi huu, Kamati imetumia majedwali ili kurahisisha maelezo yake wakati wa kuonesha taarifa, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji.

##### **3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli**

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56) ilitarajiwa kukusanya jumla ya Shilingi **16,880,839,976.00** kutoka vyanzo vya ndani. Mapato haya ilitarajiwa kutokana na mauzo ya nyaraka za zabuni pamoja na vifaa chakavu, na kwa upande wa Taasisi mapato ilitarajiwa kutokana na tozo mbalimbali, ukusanyaji wa madeni, makusanyo ya mapato yatokanayo na nauli za mabasi, ada za Wanafunzi katika Vyuo, ushuru wa mauzo ya bidhaa mbalimbali, kodi ya pango zinazotozwa kwa wapangaji wa majengo mbalimbali ya taasisi, na mapato yatokanayo na uchangiaji wa huduma za Afya katika hospitali.

Hadi kufikia Februari, 2017 jumla ya **Shilingi 4,750,262,451.03** zilikuwa zimekusanywa na Fungu 56. Kiasi

hicho ni sawa na **asilimia 28.13** ya mapato yaliyokadiriwa kukusanya katika mwaka wa fedha 2016/17. Kamati ilitaka kujua ni kwanini kumekuwa na kiwango kidogo cha Makusanyo ya maduhuli, na sababu zilizotolewa ni pamoja na:-

- (i) Mauzo machache ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu vya ofisi, na
- (ii) Ukusanyaji mdogo wa mapato kutoka vyanzo vingine tofauti na makadirio ya awali.

**Mheshimiwa Spika**, ingawa mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli siyo mzuri, hata hivyo, kiasi kilichokusanya kimeongezeka kwa zaidi ya **asilimia 16** ikilinganishwa na kiwango cha **asilimia 12** kilichokuwa kimekusanya katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/16. Kamati inatarajia kuwa, mwenendo huu wa ukusanyaji mapato utaendelea kuimarika katika mwaka ujao wa fedha, 2017/18.

Aidha, ni vyema Ofisi ya Rais – TAMISEMI, ikakadiria makusanyo kwa kuzingatia hali halisi ya vyanzo vya mapato vinavyotarajiwa, ili kuепusha kutofikiwa kwa malengo yaliyowekwa, jambo ambalo linatoa taswira ya kutowajibika ipasavyo kwa mamlaka zinazohusika na ukusanyaji wa mapato.

### **3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, umebaini kwamba, hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/17 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba:-

- i. Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo kuliko ilivyokusudiwa katika Mpango wa upatikanaji fedha (*cash flow plan*); na

ii. Fedha zinazopaswa kutolewa na Hazina hazipatikani kwa wakati, jambo linaloathiri utekelezaji wa Mpango kazi uliowekwa ili kutekeleza malengo ya bajeti ya Ofisi hii;

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2017 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea **Shilingi 202, 297,842,072/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 57 ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii.

Ulingenisho wa Kamati kuhusiana na hali hiyo ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2016/17 na mwaka 2015/16 ulibaini kwamba, kiasi hicho cha fedha ni ongezeko la **asilimia 8** ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2015/16 ambapo ulikuwa ni **asilimia 48** ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa kwa kipindi hicho.

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho kiasi cha fedha kilichokuwa kimepokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kilikuwa **Shilingi 18,629,656,339** ambacho ni sawa na asilimia 64 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi hayo. Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa asilimia 18 ikilinganishwa na fedha iliyokuwa imepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawada katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/16 ambayo ilikuwa ni asilimia 46 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2017, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zake, ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 183,668,185,733.00** kutoka Hazina, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 56 ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa **asilimia 8** ikilinganishwa na kiasi kilichokuwa kimepokelewa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/16 kwa ajili ya maendeleo ambacho kilikuwa ni **asilimia 48** ya kiasi chote kilichokuwa kimeidhinishwa na Bunge lako tukufu katika mwaka huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, ingawa mwenendo wa upatikanaji fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) katika mwaka wa fedha 2016/17 umeonekana kuwa mzuri (**wastani wa asilimia 60.5**) ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2015/16 ambao ulikuwa na **wastani wa asilimia 47**, bado lengo tarajiwa halikufikiwa kikamilifu.

Kwa matarajio ya kawaida upatikanaji wa fedha hadi kufikia robo ya tatu ya utekelezaji wa bajeti unapaswa kuwa zaidi ya asilimia 70, kwa mgawanyo wa angalau asilimia 25 ya upatikanaji fedha katika kila robo.

Aidha, bado upatikanaji fedha kwa ajili ya maendeleo umeendelea kuwa chini ikilinganishwa na fedha zinazotolewa kwa ajili ya matumizi ya Kawaida. Tafsiri ya mwenendo huu ni kwamba, tutaendelea kushuhudia ucheleweshwaji katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na ongezeko la gharama za miradi hiyo kwa kipindi cha mwaka kilichosalia.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya ulinganisho wa uwiano wa fedha iliyoidhishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na fedha iliyopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2017, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Ufanuzi zaidi wa ulinganisho huu umeoneshwa kupitia **Jedwali Na. 02**

**Jedwali Na.02:** Bajeti iliyoidhinishwa dhidi ya Fedha zilizopatikana hadi Februari, 2017

Mgawanyo	Bajeti ya Mwaka wa fedha 2016/17	Fedha zilizotolewa hadi Februari, 2017	Asilimia ya fedha iliyopokelewa hadi Februari, 2017
OC	6,396,357,000	4,236,929,183	66.24
Mshahara	22,516,917,000	14,392,727,155	63.92
Maendeleo	325,469,218,000	183,668,185,733	56.43
<b>Jumla</b>	<b>354,382,492,000</b>	<b>202,297,842,072</b>	<b>100</b>

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI

### 3.1.3 Mapito ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2016/17, Kamati ilioita ushauri katika mambo Kumi na Tano (15) kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliweza kuzingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati, na inaendelea kufanya hivyo kwa maoni mengine yaliyosalia. Baadhi ya maoni na ushauri uliozingatiwa ni kuhusu:-

i. Kuhakikisha Halmashauri na Mikoa inatumia kikamilifu Mifumo ya Kielektroniki katika Ukusanyaji wa Mapato ambayo ni *Local Government Revenue Collection Information System (LGRCIS)* na Got - HOMIS ambao ni mahususi katika mapato yanayotokana na uchangiaji katika Sekta ya Afya. Hadi Februari 2017 jumla ya Halmashauri 175

kati ya 185 ambazo ni sawa na asilimia 95 zinatumia mfumo wa LGRCIS, na zilizosaliana ziko katika hatua mbalimbali za ufungaji wa mfumo. Aidha, Hospitali 19 za Rufaa za Mikoa, Hospitali 43 za Wilaya, Vituo vya Afya 38 na Zahanati moja (1) zimefungiwa Mfumo wa GoT – HOMIS;

ii. Uhakiki wa Watumishi hewa na kuwaondoa katika mfumo wa malipo ya mishahara (*Payroll*) ili kuepusha upotevu wa fedha za umma. Hadi mwishoni wa Februari, 2017 jumla ya Watumishi 13,369 waliondolewa katika orodha ya malipo ya mishahara ya Serikali kutokana na sababu za utoro, kustaafu na vifo. Aidha, kati ya Watumishi hao 4,968 walibainika kuwa Watumishi hewa na wameisababishia Serikali hasara ya Shilingi bilioni 25.36. Juhudi za Ofisi ya Rais – TAMISEMI zimefanikiwa kufuatilia na kurejesha Shilingi bilioni 2.7 (sawa na asilimia 11 ya fedha zote) na juhudzi zinaendelea ili kurejesha zillizosalia; na

iii. Kukamilisha mfumo wa ukusanyaji nauli kwa njia ya kielektroniki na kupanga nauli ili Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka, Dar es Salaam (DART) uanze kutoa huduma kwa Wakazi wa Jiji la Dar es Salaam. Mfumo huo ulikamilika na kuanza kutumika katika ukusanyaji wa nauli tangu tarehe 16 Mei, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, baadhi ya maoni ambayo yanaendelea kuzingatiwa ni pamoja na:-

i. Kuhakikisha Halmashauri zinatenga kikamilifu asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani kwa ajili ya kuwawezesha kiuchumi Wanawake na Vijana. Serikali inaendelea na utekelezaji wa agizo hili kwa kuliingiza katika mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kuipa nguvu ya kisheria Mifuko ya Maendeleo ya Vijana na Wanawake. Rasimu ya kwanza ya mapendekezo hayo imefikishwa katika Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, na inasubiri kuendelea na hatua zinazofuata; na

ii. Kuhakikisha fedha za maendeleo hazinelewi kutoka Hazina. Bado jambo hili halijatekelezwa kikamilifu kwani fedha za maendeleo zinaendelea kuchelewa. Hadi mwezi Februari 2017, ni asilimia 56 tu ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya maendeleo ndiyo zilikuwa zimetolewa na Hazina.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

##### **4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, taarifa ya mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inayojumuisha Mafungu 28 (Fungu 56; Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015 – 2020; Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals*); Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI uliofanyiwa mapitio mwaka 2016; Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa.

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inapanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha amani na utulivu nchini na kusimamia shughuli za utawala bora na kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma (D by D)

ii. Kusimamia matumizi ya rasilimali katika ngazi zote za Ofisi ya Rais – TAMISEMI;

iii. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi (Core Business) ya kila Taasisi yaliyoainishwa kwenye Mipango Mikakati yao;

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

iv. Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya Wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda;

v. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikiwa ni pamoja kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Serikali na miradi katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vi. Kuratibu shughuli za usimamizi na uendeshaji wa elimu, afya na sekta nyingine;

vii. Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa Watumishi wa Serikali katika Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri, pamoja na kuendeleza rasilimali watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi; na

viii. Kusimamia, kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa Taasisi, programu na miradi iliyo chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 6, 568, 841, 586,637**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4, 535, 390, 860,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 1, 779, 128, 523,846** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 4,270,265,560,000**, sawa na asilimia 89.15 ni kwa ajili ya mishahara, na **Shilingi 519,447,430,791**, sawa na asilimia 10.85 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. **Jedwali Na. 03** linafafanua zaidi juu ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

**Jedwali Na. 03** Mgawanyo wa Bajeti ya Ofisi ya Rais –  
TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI

#### **4.2 Uchambuzi wa makadirio ya Mapato**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, inakadiria kukusanya jumla ya shilingi **713,187,789,615**. Mapato hayo yameongezeka kwa **Shilingi 30,575,512,826** sawa na **asilimia 4.48** ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa mgawanyo utakaooneshwa katika **Jedwali Na. 04** hapo chini.

**Mheshimiwa Spika**, makusanyo hayo yanatarajiwa kutokana na kuuza vifaa chakavu pamoja na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, marejesho ya masurufu na mishahara. Aidha, kwa upande wa Halmashauri, makusanyo yatatokana na ushuru na kodi mbalimbali na vyanzo vingine vya mapato vilivyopo kwa mujibu wa sheria.

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

**Jedwali Na. 04 Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo ya ndani**

Ofisi/Taasisi	Bajeti 2016/17	Bajeti 2017/18	Ongezeko	Asilimia
CR-TAMSEM naTaasisi	16,867,336,976	22,766,063,908	5,898,726,932	34.97
Mkoa	330,111,813	3,115,064,707	2,784,952,894	843.63
Halmashauri (MM)	665,744,939,813	687,306,661,000	21,891,833,000	3.29
<b>JUMAKU</b>	<b>682,612,276,789</b>	<b>713,187,789,615</b>	<b>30,575,512,826</b>	<b>4.48</b>

**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa uchambuzi, sehemu kubwa ya makusanyo inatarajiwa kupatikana kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Sababu kubwa kuhusiana na kiasi hicho kikubwa cha makusanyo ni kwamba, Mfumo wa Serikali za Mitaa, ndio wenyewe watu wengi na unamiliki vyanzo vingi vya mapato. Aidha, kuanza kutumika kwa mfumo wa ukusanyaji wa Mapato kwa njia ya Kieletroniki kumeonekana kusaidia ongezeko la makusanyo.

Aidha, Mikoa licha ya kuwa na ongezeko kubwa la Makusanyo (asilimia 843.63) bado imeendelea kuwa na makusanyo madogo ikilinganishwa na Halmashauri, na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake.

#### **4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinaombewa kuidhinishiwa

jumlah ya **Shilingi 6,568,841,568,673** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Tawala za Mikoa na katika Serikali za Mitaa. Kati ya fedha hizo zinazoombwa, **Shilingi 4,789,713,062,791** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,779,128,523,846** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Aidha, katika fedha, hizo zipo **Shilingi 12,422,291,495** kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).

**Mheshimiwa Spika**, kiasi cha Fedha kinachoombwa kimeongezeka kwa **Shilingi 516,240,633,637**, sawa na asilimia 8.52% ikilinganishwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake, Mikoa na MSM katika mwaka wa fedha 2016/2017. Hata hivyo, ongezeko la mwaka huu ni dogo ikilinganishwa na liliopita, katika mwaka wa fedha 2016/17 ambalo lilikuwa asilimia 12.

Uchambuzi umebaini kwamba, katika fedha za miradi ya maendeleo, kuna ongezeko la **Shilingi 148,397,071, 846** kutoka **Shilingi 1,630,731,452,000** za mwaka wa fedha 2015/2016 hadi **Shilingi 1,779,128,523,846** katika mwaka wa fedha 2017/2018. Ongezeko hili ambalo ni sawa na **asilimi 9.10** ni dogo sana kwani limepungua kwa zaidi ya mara Saba, ikilinganishwa na ongezeko lilloshuhudiwa katika mwaka wa fedha 2016/17 ambalo lilikuwa ni **asilimia 74. 83**

**Mheshimiwa Spika**, ni jambo lisilopingika kwamba, Ofisi ya Rais – TAMISEMI ndiyo inayoongoza kwa kuwa na bajeti kubwa dhidi ya Wizara nyingine, zikilinganishwa na bajeti ya Taifa. Kwa mfano; katika mwaka wa fedha 2017/2018 bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI imefikia asilimia 20.72 ya Bajeti ya Taifa ambayo ni takribani **Shilingi Triliioni 31. 699**. Hilo ni ongezeko la **asilimia 0.23** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/17 ambapo ongezeko lilikuwa **asilimia 20. 49**. Hata hivyo, kiwango hicho kinaendelea kuwa pungufu ikilinganishwa na uwiano wa namna hiyo katika mwaka wa bajeti 2015/16 ambapo bajeti ya TAMISEMI lilikuwa ni asilimia 24 ya bajeti yote.

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

**Mheshimiwa Spika**, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni kama unavyooneshwa katika **Jedwali Na. 05:-**

**Jedwali Na 5: Mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya OR- TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha 2017/ 2018 ikilinganishwa na Mwaka 2016/17**

AINA YA MATUMIZI	2016/17	2017/18	Ongezeko	Asilimia
Matumizi ya kawaida				
OR - TAMISEMI				
Mishahara Makao Makuu	8,130,978,000	8,491,975,000	360,997,000	4.43
Mishahara ya Taasisi	14,385,939,000	15,318,027,000	932,088,000	6.47
Matumizi Mengineyo Makao Makuu	3,835,054,000	6,384,732,000	2,549,678,000	66.48
Matumizi Mengineyo Taasisi	2,561,303,000	1,827,564,296	-733,738,704	-28.64
<b>JUMLA</b>	<b>28,913,274,000</b>	<b>32,022,296,296</b>	<b>3,109,022,296</b>	<b>10.75</b>

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Tume ya Utumishi wa Walimu				
Mshahara	6,442,019,000	7,800,146,000	1,358,127,000	21.08
Matumizi Mengineyo	3,605,773,000	4,622,145,495	1,016,372,495	28.19
Jumla	10,047,792,000	12,422,291,495	2,374,499,495	23
<b>Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mtaa</b>				
Mikoa: (Mafungu 26)				
Mshahara	153,036,181,000	168,579,832,000	15,543,651,000	10.16
Matumizi Mengineyo	37,786,227,000	41,297,783,000	3,511,556,000	9.29
Jumla	190,822,408,000	209,877,615,000	19,055,207,000	9.98

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mamlaka za Serikali za Mitaa				
Mishahara	3,593,880,663,000	4,070,075,580,000	476,194,917,000	13.25
Matumizi Mengineyo	598,205,364,000	465,315,280,000	-132,890,084,000	-22.21
<b>JUMLA</b>	<b>4,192,086,027,000</b>	<b>4,535,390,860,000</b>	<b>343,304,833,000</b>	<b>8.18</b>
<b>Mpango wa Maendeleo</b>				
OR- TAMISEMI	325,469,218,000	413,178,629,846	87,709,411,846	26.95
Mikoa	64,701,480,000	75,259,322,000	10,557,842,000	16.32
Halmashauri	1,240,560,754,000	1,290,690,572,000	50,129,818,000	4.04
<b>JUMLA</b>	<b>1,630,731,452,000</b>	<b>1,779,128,523,846</b>	<b>148,397,071,846</b>	<b>9.10</b>
<b>JUMLA KUU</b>	<b>6,052,600,953,000</b>	<b>6,568,841,586,637</b>	<b>516,240,633,637</b>	<b>8.52</b>

### **Chanzo: Randama ya TAMISEMI**

#### **5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

- i. Serikali isimamie na kuhakikisha Halmashauri zinaandaa na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na Vikundi vya Wanawake na Vijana, na jinsi vinavyopokea na kurejesha fedha zinazotokana na Asilimia Kumi (10%) ya Mapato ya

Ndani ya Halmashauri. Aidha, Halmashauri zitekeleze kwa ukamilifu utengaji wa fedha hizo na kuzipeleka kwa wahusika kwani ni Agizo la Serikali na siyo hiyari;

ii. Serikali iangalie uwezekano wa kurejesha sehemu ya mapato yatokanayo na Kodi ya Majengo (*property tax*) katika Halmashauri za Manispaa Thelathini (30) nchini ambazo zimeathirika kutokana na chanzo hicho cha mapato kuchukuliwa na Mamlaka ya Mapato (TRA);

iii. Serikali iruhusu Halmashauri kukata asilimia 30 ya mapato yatokanayo na Kodi ya Ardhi na Asilimia 25 ya Mapato yatokanayo na Kodi katika Huduma za Misitu, kabla ya kuwasilisha fedha hizo Serikali Kuu, kwani uzoefu unaonesha Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imekuwa hairejeshi fedha hizo kwenye Halmashauri;

iv. Halmashauri zibuni vyanzo vipyta vya mapato ili kuepuka kutegemea ruzuku kutoka Serikali Kuu. Aidha, vyanzo hivyo vipyta vitaziba pengo la mapato yaliyokuwa yakitokana na ushuru mdogo mdogo ulioondolewa na Serikali kutokana na kuwa kero kwa wananchi;

v. Mikoa iandae vipaumbele vichache kulingana na uwezo wa bajeti na kusimamia kikamilifu utekelezaji wake, badala ya kuwa na msururu wa vipaumbele ambavyo havitekelezeki kutokana na ufinyu wa Bajeti;

vi. Halmashauri ziwatumiie Maafisa wa Maendeleo ya Jamii kutoa elimu ya ujasiriamali kwa Vijana na Wanawake, ili kuwajengea uwezo wa kuendesha kwa ufanisi miradi ya maendeleo inayoanzishwa na vikundi hivyo na hatimaye kuepusha upotevu wa mitaji wanayopatiwa;

vii. Halmashauri zishirikiane na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ili kuandaa mpango wa matumizi bora ya Ardhi, kwa kuanisha maeneo ya kilimo, ufugaji na matumizi mengine, jambo litakalosaidia kuepusha migogoro ya ardhi baina ya Wakulima na Wafugaji;

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

viii. Serikali itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati ili kuziwezesha Halmashauri kulipa madeni ya Wazabuni na Wakandarasi kwa wakati na hivyo kuепusha ongezeko la madeni katika miradi inayotekeliza;

ix. Serikali iandae utaratibu utakaowezesha Halmashauri kukusanya kikamilifu mapato yatokanayo na huduma za minara ya simu pamoja na mabango ya biashara;

x. Serikali iongeze kasi ya kuajiri Wataalam wa Afya na upatikanaji wa Dawa, Vifaa Tiba na Vitendanishi katika Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali za Serikali, ili kuwezesha Wananchi kupata huduma stahiki za afya;

xi. Serikali ihakikishe Halmashauri ambazo hazijaanza kutumia mfumo wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki, zinafanya hivyo haraka iwezekanvyo ili kuепusha upotevu wa mapato unaotokana na ukusanyaji wa kutumia vitabu. Aidha, halmashauri ambazo hazitumi mfumo huo kikamilifu kutokana na kutokuwa na mashine za kutosha, zihimizwe kununua mashine za kutosha na kuzitumia katika ukusanyaji wa mapato; na

xii. Serikali ipeleke kikamilifu fedha za ukarabati na uendelezaji wa hospitali za Mikoa ili kuziwezesha kukamilisha matengenezo yaliyokusudiwa na kuanza kutoa huduma za afya kikamilifu kwa lengo la kupunguza msongamano wa wagonjwa uliopo.

## **6.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi za dhati kwako binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkiendesha shughuli za Bunge vizuri. Aidha, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Mwanne Ismail Mchemba, kwa kuchaguliwa na Wajumbe wa Kamati, kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Hii inaonesha imani kubwa walijonayo kwake, pamoja na kutambua mchango wake kwa Kamati katika kipindi chote alichokuwa akinisaidia

majukumu ya Kamati kabla ya kuchaguliwa rasmi. Ninamshukuru sana kwa ushirikiano wake, na nina imani tutaendelea kushirikiana katika kuitumikia vyema Kamati.

Vilevile, kwa heshima na unyenyekevu mkubwa, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa weledi na ushirikiano mkubwa waliouonesha wakati wa utekelezaji wa majukumu ya Kamati, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa kina wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, 2017/2018.

Kamati hii ina Mafungu mengi ya Bajeti ambayo inayashughulikia, na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi ikiwa ni pamoja na siku za mwisho wa wiki. Mazingira hayo magumu hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, na badala yake walijitao kikamilifu na kukabili majukumu yaliyokuwa mbele yao, kwa moyo na weledi wa hali ya juu wakiashiria utayari wao katika kulitumikia Bunge na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu mkubwa, napenda niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe.Mwanne Ismail Mchemba,Mb –M/Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb
6. Mhe.Ester Alexander Mahawe,Mb
7. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
8. Mhe.Halima Ali Mohamed,Mb
9. Mhe.Hamad Salim Maalim,Mb
10. Mhe.Waitara Mwita Mwikwabe,Mb
11. Mhe.Innocent Sebba Bilakwate,Mb
12. Mhe.Josephine Tabitha Chagula,Mb
13. Mhe.Khamis Ali Vuai,Mb
14. Mhe.Maida Hamad Abdallah,Mb
15. Mhe.Hamoud Abuu Jumaa,Mb
16. Mhe.Khalifa Mohamed Issa,Mb
17. Mhe.Hussein Ibrahim Makungu,Mb
18. Mhe.Mariam Ditopile Mzuzuri,Mb

19. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
20. Mhe.Ruth Hiyobi Mollel,Mb
21. Mhe.Saada Mkuya Salum,Mb
22. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
23. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
24. Mhe.Zacharia Paulo Isaay,Mb
25. Mhe.Saed Ahmed Kubenea,Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ningependa kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Seleman Said Jafo (Mb), pamoja na Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, hiyo wakiongozwa na Eng. Musa Iyombe, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati wakati wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kwa usimamizi na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha unaoisha, na kwa kuwasilisha vyema mbele ya Kamati, Taarifa za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Vilevile, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Jumla, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Mariam Ally, kwa uratibu wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S.Rweikiza (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA  
NA SERIKALI ZA MITAA**

18 Aprili, 2017

**SPIKA:** Ahsante sana. Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Mwanne Mcemba, karibu sana Mheshimiwa. Umebakiwa na kama dakika ishirini hivi jitahidi kwenye ripoti yako ya Utumishi na Utawala Bora ui-cover hasa maoni na ushauri wa Kamati. (*Makofi*)

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA - MAKAMU MWENYEKITI**

**WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI  
ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, utangulizi, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 6(4) kikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1)(a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yalipitiwa na

kuchambuliwa na Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kabla ya uchambuzi wa bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 98(2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1), kwa kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Baada ya kutimiza sharti hilo, Kamati ilichambua taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya ofisi hii kwa mwaka 2016/2017 na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Taarifa hiyo inahusisha jumla ya mafungu tisa kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa baada ya uchambuzi wa taarifa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii yaliyowasilishwa, taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi hii inajikita katika maeneo manne yafuatayo:-

- (i) Matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- (ii) Mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017;
- (iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2017/2018; na
- (iv) Maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2016/2017; ufanuzi wa miradi ya maendeleo iliyolengwa kukaguliwa. Katika mwaka wa fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa shilingi 466,217,858,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kupitia mafungu manne kama inavyoonekana katika taarifa.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia sharti la kipindi kisichozidi siku saba ambalo limewekwa na Kanuni, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelawa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Miradi hiyo inahusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (*MKURABITA*), Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (*TPSC*). Ufanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi namba 6220 – *Support to Tanzania Social Action Fund*, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 416,362,198,000 na ulipangwa kutekelezwa chini ya kifungu 1003 cha Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa hadi sasa takribani Watanzania milioni 5.9 wameandikishwa ili kunufaika na mpango huu ambao umesaidia sana kaya maskini kuboresha maisha kwa kumudu kupata chakula, kuwezesha watoto kwenda kuhudhuria shule pamoja na kliniki kwa wale walio chini ya umri wa miaka mitano. Miradi iliyotembelewa ni mikoa ya Morogoro, Tanga, Mbeya Njombe na Iringa.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (*MKURABITA*). Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi bilioni 2 na unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 kiitwacho *Policy and Planning* cha Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Mpango huu unaandaa na kusimamia Mfumo wa Kitaifa wa Umiliki wa Raslimali na Uendeshaji wa Biashara unaotambulika na kukubalika kisheria na kwa mantiki hiyo kuwasaidia wanyonge kurasimisha ardhi na biashara ili wajikwamue kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mradi namba 6576 - Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*); utekelezaji wa shughuli za mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi milioni 500 chini ya kifungu 1003 kiitwacho *Policy and Planning* cha Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Taarifa ziliainisha majukumu ya msingi katika mradi huo ambayo ni kutoa mikopo, ushauri na mafunzo ya kibiashara kwa wajasiriamali

wadogowadogo na wa kati, katika Mikoa ya Njombe na Morogoro kwa kutembelea jumla ya vikundi sita.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma (*TPSC*) kilianzishwa ili kutoa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala, kutoa ushauri wa kitaalam, kufanya utafiti na kutoa machapisho ya kitaalam katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, matokeo ya ukaguzi. Ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni muhimu kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya ukaguzi huo. Kwa madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na majedwali na asilimia, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya ofisi hii. Ufanuzi wa matokeo ya ukaguzi huo na kwa kuokoa muda naomba nisiyasome, lakini yaingizwe kwenye *Hansard* kama yalivyo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (*Support to Tanzania Social Action Fund*) katika maeneo sita yaliyoko kwenye mikoa mitano ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, mambo kadhaa yalibainika kuhusiana na utekelezaji huo. Mafanikio ni kama ifuatavyo:-

(i) Malipo yamefanyika kwa wastani wa awamu 11 hadi Februari, 2017 ambapo shilingi milioni 216 zimelipwa;

(ii) Mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mpango;

(iii) Watoto wa walengwa wanapata mahitaji ya shule na hivyo kuhudhuria shuleni kikamilifu na kliniki kwa walio chini ya umri wa miaka mitano; na (*Makofi*)

(iv) Walengwa wengi wamewezeshwa kuijunga na Bima ya Afya ya Jamii (*CHF*).

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Mheshimiwa Spika, changamoto ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti finyu ya mpango ikilinganishwa na idadi ya kaya maskini;

(ii) Malalamiko ya uonevu kutoka kwa Walengwa walioondolewa katika mpango kwa madai ya kukosa sifa;

(iii) Zipo Kaya maskini nyingi hazijaingizwa katika mpango wa ruzuku; (*Makofi*)

(iv) Sehemu kubwa ya walengwa ni wazee hivyo hutumia ruzuku wanayopata kwa ajili ya mlo tu;

(v) Walengwa wa mpango waliojiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (*CHF*) kukosa huduma ya afya katika zahanati binafsi kwani haziko tayari kuwahudumia wateja wenye aina hiyo ya bima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), naomba nisisome hicho kifungu niende moja kwa moja kwenye mafanikio ambayo ni pamoja na:-

(i) Baadhi ya wananchi wamekuza mitaji ya biashara zao kutohana na mikopo waliyoipata kwa kutumia Hati Miliki za Kimila kama dhamana. Mfano, wanufaika wanne katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, wamekopa kati ya shilingi milioni 50 hadi 500; (*Makofi*)

(ii) Kuongezeka thamani kwa maeneo yaliyorasimishwa; na

(iii) Wanawake kumilikishwa Hati Miliki za ardhi peke yao au pamoja na wenza wao.

Mheshimiwa Spika, changamoto za mpango huu ni kama ifuatavyo:-

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

- (i) Bajeti ndogo ya MKURABITA inaathiri utekelezaji wa mpango huu;
- (ii) Baadhi ya wananchi kushindwa kugomboa Hati za Miliki za Kimila za maeneo waliyopimiwa; na
- (iii) Baadhi ya taasisi za fedha haziko tayari kutoa mikopo kwa dhamana ya Hati za Hakimiliki za Kimila.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*); naomba niende moja kwa moja kwenye mafanikio ambayo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Vikundi vya vijana viwili na wanawake vikundi 14 wamepata mafunzo ya ujasiriamali pamoja na mikopo bila kuwa na dhamana;
- (ii) Vijana na wanawake wajasiriamali wamewezeshwa kujiajiri; na
- (iii) Makundi maalum ya walemaru yamepatiwa mikopo, mfano watu wenyе ulemamu 16 pamoja na wanaoishi na VVU wamekopeshwa shilingi milioni saba mkoani Morogoro. (*Makofi*)

Changamoto za mfuko huu ni pamoja na:-

- (i) Bajeti ndogo ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (*PTF*) hivyo kushindwa kuwafikia walengwa wengi;
- (ii) Mtandao (*network*) mdogo wa shughuli za mfuko nchini; na
- (iii) Shughuli za mfuko zimejikita zaidi maeneo ya mjini, jambo ambalo linawanyima fursa ya mikopo wananchi wa vijijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Chuo cha Utumishi wa Umma, naomba nisisome, niende kwenye changamoto ambazo ni pamoja na:-

(i) Majengo yanayotumiwa ni ya kukodi kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya, jambo linalogharimu chuo hicho kwa shilingi milioni 22 kwa mwezi, sawa na shilingi milioni 264 kwa mwaka;

(ii) Pamoja na kukosa majengo yake, Chuo cha Utumishi wa Umma, *campus* ya Mbeya kimeendelea kufanya vizuri katika kutimiza malengo yake; na

(iii) Bado chuo kinatumia walimu wa mkatuba badala ya kuwa na watumishi wa ajira ya kudumu.

Mheshimiwa Spika, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kutokana na matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba:-

(i) Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini uongeweza kufanikiwa zaidi iwapo fedha za ndani zingetumika kwa kiasi kikubwa kama ilivyo kwa fedha za wafadhili. Tangu kuanza kwa mpango huu katika mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imechangia shilingi bilioni 3.6 katи ya shilingi bilioni 60.5 ilizopaswa kuchangia hadi sasa, kiasi ambacho ni kama asilimia 5.9 tu;

(ii) Itikadi za kisiasa walizonazo viongozi na watendaji zinaweza kusababisha mgawanyiko miongoni mwa wananchi hivyo kuathiri utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini;

(iii) Kwa kuwa wazee walio katika vituo vya kulelea wazee nchini wanakidhi sifa na vigezo vya kusaidiwa, ni jambo jema kutekeleza mpango wa ruzuku kwa kaya maskini katika vituo hivyo na kwamba utekelezaji huo utasaidia wazee hao kumudu maisha;

(iv) Dhamira ya kuwataka wanufaika wa Mpango wa Ruzuku kwa Kaya Maskini wajunge na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (*CHF*) itafanikiwa zaidi iwapo Serikali itawezesha zahanati binafsi kutoa huduma kwa walengwa hao;

(v) Halmashauri zikishirikiana na MKURABITA, zinaweza kuandaa na kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi na hivyo kuepusha migogoro ya ardhi;

(vi) Huduma ya mikopo kwa vijana na wanawake kutoka Mfuko wa Rais wa Kujitegemea itafanikiwa zaidi iwapo mfuko huo utawezeshwa kifedha na kufungua matawi mengine mengi hapa nchini; na

(vii) Iwapo Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kitamilikishwa majengo kinayoyatumia kwa ajili ya Kampasi ya Mbeya, hatua hiyo itasaidia kuepusha gharama kubwa za pango zinazolipwa kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Kama nillivyosema awali, naomba taarifa hii iingie kwenye *Hansard*, naomba niende tu moja kwa moja kwenye mafanikio.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti ya ofisi hii umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutohana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo kuliko ilivyokusudiwa katika Mpango wa Upatikanaji Fedha (*Cash Flow Plan*) na fedha kutoka Hazina hazipatikani kwa wakati na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya bajeti ya ofisi hii. Maeleo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na mafungu yake kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2017 (katikati ya robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2016/2017) na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi unabainisha kuwa hadi mwezi Februari, 2017, ofisi hii pamoja na mafungu yaliyo chini yake ilikuwa imepokea shilingi bilioni 527.1 kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi

hiki ni sawa na asilimia 59.75 ya fedha iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kamati ililinganisha hali hiyo ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2016/2017 na mwaka 2015/2016 na kubaini kuwa kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa asilimia 23.11 ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2015/2016 ambapo ni sawa na asilimia 82.86 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa kwa mwaka huo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi umebaini kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2017, ofisi hii na mafungu yake, ilikuwa imepokea shilingi bilioni 246.8 tu kutoka Hazina, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 52.93 ya fedha ya maendeleo iliyoidhinishwa. Kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa asilimia 21.28 ikilinganishwa na fedha ya 2015/2016 ambayo ilikuwa na upungufu wa asilimia 74.21 ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Wakati wa kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri katika mambo tisa kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa maoni na ushauri vilizingatiwa kikamilifu na baadhi yake ni kuhusu:-

(i) Uhakiki wa watumishi hewa na kuwaondoa katika mfumo wa mishahara ambapo katika kipindi cha Machi hadi Agosti, 2016 watumishi 19,708 walibainika na kuondolewa; na

(ii) Tathmini kwa lengo la kubaini wanufaika wa mpango wa ruzuku wa kaya maskini wasio na sifa na kuwaondoa ambapo hadi mwezi Machi, 2017 kaya za walengwa 63,819 zilikuwa zimebainika na kuondolewa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; taarifa ya mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018, kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa

Umma na Utawala Bora, inayojumuisha mafungu tisa (Fungu 20, 30, 32, 33, 67, 94, 04 na 11) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika llani ya Uchaguzi ya mwaka 2015 ya Chama Tawala, mwongozo wa Taifa wa kuandaa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na maeneo muhimu ya kuzingatia kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano. Kwa ujumla Ofisi hii pamoja na mafungu yake imepanga kutekeleza malengo 186 na baadhi ya hayo ni malengo kama yanavyoonekana kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, ili iweze kutekeleza malengo hayo yalivyoanishwa, Ofisi hii inaomba kuidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 821.32; kati ya fedha hizo shilingi bilioni 430.35 ni kwa ajili ya matumizi ya kawada na shilingi bilioni 390.95 ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, shillingi billioni 23.214 sawa na asilimia 5.39 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 407.13 sawa na asilimia 94.61 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba bajeti inayoombwaa kwa mwaka ujao wa fedha imepungua kwa shilingi bilioni 60.79 sawa na asilimia 6.89 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 ambayo ilikuwa ya shilingi bilioni 882.11. Kwa upande wa bajeti ya maendeleo, kiasi kinachoombwa kimeitungua kwa shilingi bilioni 75.24 sawa na asilimia 16.13 ikilinganishwa na shilingi bilioni 466.21 zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati illifanya uchambuzi wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kufanya ulinganisho na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/2018 na kubaini mambo yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka 2017/2018 ambayo ni shilingi bilioni 821 ni sawa na asilimia 2.59 ya bajeti yote Serikalini ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2017/2018 ni shilingi trilioni 31.699.

(ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 unaonyesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 7.31 ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti wa mwaka 2017 lakini bajeti ya ujumla ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018 imepungua kwa asilimia 6.89 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2016/2017; na

(iii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 38, imepungua kwa asilimia 16.13.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa ya utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapendekeza kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Serikali itoe kikamilifu mchango wake katika Mpango wa Ruzuku kwa Kaya Maskini. Tangu kuanza kwa mpango huu katika mwaka wa fedha 2015, Serikali imechangia shilingi bilioni 3.6 tu badala ya bilioni 60.

(ii) Walengwa kutoka kaya maskini waelimishwe juu ya mpango huu; na

(iii) Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka mpango wa ruzuku kwenye kaya maskini hususani kambi za wazee.

Hitimisho, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa namna mnavyoendesha shughuli za Bunge. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa kushiriki kikamilifu kutekeleza shughuli za Kamati. Kamati hii ina mafungu mengi ya bajeti ambayo inayashughulikia na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi ikiwa ni pamoja na siku za mwisho wa wiki. Mazingira hayo magumu hayakuwa kikwazo walijitua kikamilifu na kukabili majukumu yaliyokuwa

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

mbele yao kwa moyo na weledi wa hali ya juu katika kulitumikia Bunge na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu mkubwa na kwa ridhaa yako, naomba Wajumbe hawa waingie kwenye *Hansard*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati, pia namshukuru Mheshimiwa Angella Kairuki, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na watendaji wa ofisi hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu-Utumishi, Dkt. Lauren Ndumbaro kwa jinsi walivyoshiriki katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kufanikisha kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2017/2018. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt.Thomas Kashilllah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein...

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa malizia sasa.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI YA MITAA:** ...Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Jumla, Ndugu Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndugu Chacha Nyakega, Ndugu Victor Leonard Mhagama na Ndugu Eunice Shirima, wakisaidiwa na Ndugu Mariam Ally, kwa uratibu wa shughuli za Kamati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kama yalivowasilishwa na mtoa hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum

kutoka kule Tabora. Tunakushukuru sana sana kwa hotuba hiyo ya Kamati na nichukue nafasi hii kwa kweli kuwashukuru saa Wajumbe wa Kamati hii kwa jinsi ambavyo wamefanya kazi kubwa sana na kwa muda mfupi sana kuchambua mafungu yote ya TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora.

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA  
NA SERIKALI ZA MITAA, KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU  
YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA  
UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017;  
PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA  
MAPATO NA MATUMIZI, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **1.0      UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) na 117 (11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) (a) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, yalipitiwa na kuchambuliwa na Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

**Mheshimiwa Spika**, kabla ya uchambuzi wa Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98 (1), kwa kutembelea na kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Baada ya kutimiza sharti hilo, Kamati ilichambua taarifa ya

utekelezaji wa Bajeti ya ofisi hii kwa mwaka 2016/17 na kufanya ulinganisho wa makadirio ya matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Taarifa hiyo inahusisha jumla ya Mafungu Tisa (9) yafuatao:-

- i) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;
- ii) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
- iii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma;
- iv) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- v) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- vi) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;
- vii) **Fungu 09:** Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma;
- viii) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; na
- ix) **Fungu 11:** Ofisi ya Ushauri wa Mafuta na Gesi

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa baada ya uchambuzi wa Taarifa na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii yaliyowasilishwa, Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi hii inajikita katika maeneo manne yafuatayo:-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

**2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

**2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyolengwa kukaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa Fedha 2016/2017, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora ilitengewa **Tsh. 466, 217, 858, 000/=** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kupitia Mafungu Manne kama ifuatavyo:-

- i) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – Tshs. 430,449,029,000/=
- ii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma – **Tshs .7,550,000,000/=**
- iii) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – **Tshs. 1,000,000,000/=**
- iv) **Fungu 6:** Ofisi ya Rais, Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Miradi - Tshs. **27,218,829,000/=**

**Mheshimiwa Spika**, katika kuzingatia sharti la kipindi kisichozidi siku Saba (7) ambalo limewekwa na Kanuni, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelzwa na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Miradi hiyo, inahusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC). Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

### **2.1.1 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ultengewa jumla ya Shilingi **416,362,198,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1003 cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Katika utekelezaji wake, Mradi huu umefikia Awamu ya Tatu, inayojikita katika kusaidia jamii ya Watanzania kwa kukuza uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii, pamoja na kuhamasisha utawala bora na uwajibikaji.

Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, hadi sasa takribani Watanzania milioni 5.9 wameandikishwa ili kunufaika na Mpango huu ambao umesaidia sana kaya maskini kuboresha maisha kwa kumudu kupata chakula, kuwezesha Watoto kuhudhuria shulen i pamoja na Kliniki kwa wale walio chini ya umri wa miaka mitano.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa zaidi kuwa kwa familia zenye Watoto wanaopaswa kupata huduma ya elimu na afya, mahudhurio ya shulen na kliniki, vimekuwa vigezo vikuu vya kuzingatiwa ili walengwa waendelee kunufaika na utaratibu wa kupoakea fedha. Sababu ya vigezo hivyo ilitajwa kuwa ni kutokana na Watoto kutoka Kaya maskini nchini kuwa waathirika wakubwa wa kukosa huduma za elimu na afya. Ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi huu Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wake katika maeneo Sita yaliyoko kwenye Mikoa Mitano nchini. Mikoa hiyo ni Morogoro, Tanga, Mbeya, Njombe na Iringa.

### **2.1.2 Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ultengewa jumla ya Shilingi **2,000,000, 000/=** na unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 kiitwacho *“Policy and Planning”* cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Mpango huu unaandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa raslimali na uendeshaji wa biashara unaotambulika na kukubalika kisheria nchini, na kwa mantiki hiyo kuwasaidia

Wanyonge kurasimisha mali walizonazo (ardhi na biashara) ili ziwawezeshe kujikwamua kiuchumi.

Kwa mujibu wa Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati, mpango huu umekuwa ukihamasisha na kuchangia ujenzi wa Masijala ya Ardhi katika Vijiji/Mitaa, kwa ajili ya uhifadhi madhubuti na salama wa nyaraka (Hati za Hakimiliki za Kimila na nyaraka nyingine) pamoja na matumizi mengine ya Serikali za Vijiji au Mitaa katika maeneo mbalimbali ya nchi. Napenda kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitembelea jumla ya maeneo Kumi na Moja (11) yaliyoko katika Mikoa Minne (4) ambayo ni Njombe, Morogoro, Dodoma na Mbeya kwa lengo la kujiridhisha kuhusu hali ya utekelezaji.

#### **2.1.3 Mradi Na. 6576 - Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)**

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa shughuli za mradi huu ultiengewa jumla ya **Shilingi 500, 000, 000/=** chini ya Kifungu 1003 kliitwacho "*Policy and Planning*" cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Taarifa ziliainisha majukumu ya msingi katika Mradi huo ambayo ni kutoa mikopo, ushauri na mafunzo ya kibiashara kwa Wajasiriamali Wadogo na wa Kat, katika sehemu mbalimbali nchini. Kamati ilikagua utekelezaji wa mradi huu katika Mikoa miwili ya Njombe na Morogoro, kwa kutembelea jumla ya Vikundi Sita (6).

#### **2.1.4 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika**, chuo hiki kilianzishwa ili kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala, kutoa ushauri wa kitaalam, kufanya utafiti na kutoa machapisho ya kitaalam katika utumishi wa Umma. Kamati ilijulishwa kuwa, chuo hiki kinazo jumla ya Kampasi Sita (6) katika maeneo mbalimbali ya nchi. Kamati ilitembelea kampasi mbili kati ya sita sawa na asilimia 33.3% ya idadi ya kampasi za chuo hicho. Kampasi zilizotembelewa ni za Mbeya na Tanga.

### **2.2. Matokeo ya Ukaguzi**

**Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyo tengewa fedha chini ya Ofisi ya

## NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha unaoisha, ni muhimu kulijulisha Bunge lako Tukufu kuhusu matokeo ya ukaguzi huo. Kwa madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na majedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Ofisi hii. Ufafanuzi wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

### 2.2.1 Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini “Support to Tanzania Social Action Fund”

**Mheshimiwa Spika**, katika maeneo Sita yaliyoko kwenye Mikoa Mitano ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini, mambo kadhaa yalibainika kuhusiana na utekelezaji huo, ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto. **Jedwali Na. 01** linafafanua zaidi kuhusu hali ya Mradi huu.

**Jedwali Na. 01:** Hali ya Utekelezaji wa Mpango wa Ruzuku kwa Kaya Maskini katika maeneo yaliyotembelewa na Kamati

Mkoa	Mtaa (M) Kijiji (K)	Awamu za Malipo	Fedha iliyolipwa katika Awamu zote	Kaya nufakira	Kaya zilizoodolewa	% ya Kaya zilizondolewa
Morogoro	Kilongo (M)	11	50,066,699	106	13	10.92
Tanga	Makuyuni (K)	10	39,179,000	115	7	5.73
Mbeya	Lumbila (M)	10	27,600,000	71	0	0
Iringa	Mlanda (K)	10	31,372,000	86	3	3.48
Iringa	Isakkililo (M)	11	17,016,000	236	55	18.90
Njombe	Uwemba (K)	11	51,676,000	139	0	0

**Chanzo:** Taarifa za TASAF kuhusu Mpango za Ruzuku kwa Kaya Maskini nichini

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaka kujua hatua iliyofikiwa katika utekelezaji, mafanikio yaliyopatikana na changamoto zilizojitekeza. Kutohana na ukaguzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

**a) Mafanikio;**

(i) Malipo yamefanyika kwa wastani wa Awamu 11 hadi Februari, 2017 ambapo jumla ya Shilingi Milioni 216 zimelipwa katika kipindi hicho;

(ii) Mwenendo mzuri wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mpango;

(iii) Walengwa wa mpango wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile, kilimo, ufugaji na biashara;

(iv) Watoto wa Walengwa wanapata mahitaji ya shule na hivyo kuhudhuria shulenii kikamilifu na Kliniki kwa walio chini ya umri wa miaka mitano; na

(v) Walengwa wengi wamewezeshwa kujiunga na Bima ya Afya ya Jamii (CHF).

**b) Changamoto;**

(i) Bajeti finyu ya mpango ikilinganishwa na idadi ya Kaya maskini;

(ii) Malalamiko ya uonevu kutoka kwa Walengwa walioondolewa katika mpango kwa madai ya kukosa sifa. Mfano, Kaya Tatu katika Kijiji cha Mlanda, Mkoani Iringa, zimekata rufaa katika ngazi ya Wilaya kupinga kuondolewa katika mpango;

(iii) Zipo Kaya maskini nyingi hazijaingizwa katika Mpango wa ruzuku;

(iv) Sehemu kubwa ya walengwa ni Wazee hivyo hutumia ruzuku wanayopata kwa ajili ya mlo tu, kwani hawana nguvu za kujishughulisha na uzalishaji;

(v) Walengwa wa mpango waliojunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) kukosa huduma ya afya katika Zahanati binafsi kwani haziko tayari kuwahudumia wateja wenye aina hiyo ya bima;

(vi) Ukosefu wa Zahanati au Vituo vya Afya, unakwamisha baadhi ya Walengwa kutimiza masharti ya afya (kupeleka Kliniki Watoto walio chini ya umri wa miaka mitano).

#### **2.2.2 Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika**, katika maeneo Kumi na Moja (11) ya Mikoa Minne 94) ambayo Kamati iliyatembelea na kukagua utekelezaji wa MKURABITA, mambo kadhaa yalibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto. **Jedwali Na. 02** linatoa muhtasari wa hali utekelezaji wa mpamgu huo.

**Jedwali Na. 02:** Hali ya utekelezaji wa MKURABITA katika maeneo yaliyotembelewa na Kamati

Mkoa	Mtaa (M) Kijiji (K)	Urasimishaji Ardhi/Biashara	Fedha ili yotumika (Tsh)	Hali Milliki zili zoandalisha	Hati Milliki zili zo chukuliwa	% ya Hali zili zo chukuliwa na Wananchi
Morogoro	<ul style="list-style-type: none"> <li>Tuelewane</li> <li>Kihonda (B)</li> </ul>	Viwanja 822	-	822	132	16.05
Njombe	<ul style="list-style-type: none"> <li>Joshoni (M)</li> <li>Melinze (M)</li> <li>Mpechi (M)</li> <li>Nazareti (M)</li> <li>Idundilaga (M)</li> </ul>	Viwanja 1003	Milio ni 62	650	602	92.61
Njombe	Kambarage (M)	Wiwanja 632	Milio ni 34	80	10	12.5
Dodoma	Pwaga (K)	Mashamba 1,277	-	1,031	1,031	100
Dodoma	Pwaga (K)	Masijala ya Ardhi	Milio ni 32	-	-	-

**Chanzo:** Taarifa za MKURABITA kuhusu urasimishaji wa ardhi na biashara.

**a) Mafanikio**

(i) Baadhi ya Wananchi wamekuza mitaji ya biashara zao kutokana na mikopo waliyoipata kwa kutumia

***NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

Hati Miliki za Kimila kama dhamana. Mfano; Wanufaika wanne (4) katika Halmashauri ya Wilaya ya Njombe, wamekopa katи ya Shilingi Milioni 50 hadi 500;

(ii) Mpangilio mzuri wa maeneo, na hivyo kuepusha au kuondoa migogoro katika maeneo yaliyopimwa na kurasi mishwa;

(iii) Kuongezeka thamani kwa maeneo yaliyorasimishwa;

(iv) Wanawake kumilikishwa Hati Miliki za ardhii peke yao au pamoja na Wenza wao;

**b) Changamoto;**

(i) Bajeti indogo ya MKURABITA inaathiri utekelezaji wa mpango huu;

(ii) Baadhi ya Wananchi kushindwa kugomboa Hati za Miliki za Kimila za maeneo waliyopimiwa; Mfano, katika maeneo yaliyotembelewa mkoani Morogoro katи ya Hati 822 zilizoandalisha ni 132 tu (sawa na asilimia 16.05) ndiyo zimechukuliwa na Wananchi;

(iii) Wafanyabiashara wengi kukosa mwamko wa kurasi mishwa biashara zao;

(iv) Baadhi ya Taasisi za fedha haziko tayari kutoa mikopo kwa dhamana ya Hati za Hakimiliki za Kimila;

**2.2.3 Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF).**

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mradi huu, katika vikundi Sita (6) ambavyo Kamati ilitembelea kwenye Mikoa ya Morogoro na Njombe, mambo kadhaa yaliyiri yakijumuisha mafanikio na changamoto. Ufanuzi zaidi unatolewa kupitia **Jedwali Na. 03**

**Jedwali Na. 03:** Mikoa na Vikundi vilivyokopeshwa fedha na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

Mkoa	Jina la Kikundi	Shughuli ya Kikundi	Thamani ya Mkopo	Muda wa Mkopo
Njombe	Vijana Gaurage	Uchomeleaji (Welding)	Milioni 2.5	Miezi 6
Njombe	Upendo	Ukamuaji wa Mafuta ya Alizeti	Milioni 2.5	Miezi 6
Njombe	Women Handcraft Group	Ufumaji	Milioni 2.4	Miezi 6
Njombe	Lumumba Group	Ufugaji Nguruwe, Ng'ombe & Kuku	Milioni 2.5	Miezi 6
Morogoro	Mwale Cleaners	Uzoaji Taka	Milioni 10	Miezi 6
Morogoro	Women Bakery Group	Uokaji Mikate	Milioni 5	Miezi 6

**Chanzo:** Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF)

**a) Mafanikio**

- i) Vikundi vya Vijana (2) na Wanawake (14) vimepata mafunzo ya ujasiriamali pamoja na mikopo bila kuwa na dhamana;
- ii) Vijana na Wanawake wajasiriamali wamewezeshwa kujajiri; na
- iii) Makundi Maalum ya Walemvu yamepatiwa mikopo. Mfano; Watu wenye Ulemavu 16 pamoja na Wanaoishi na VVU wamekopeshwa **Shilingi Milioni Saba (7)** Mkoani Morogoro.

b) **Changamoto;**

i) Bajeti ndogo ya Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) hivyo kushindwa kufikia walengwa wengi;

ii) Mtandao (Network) mdogo wa shughuli za Mfuko nchini; na

iii) Shughuli za Mfuko zimejikita zaidi maeneo ya mjini, jambo linalowanyima fursa ya mikopo Wananchi wa vijijini.

#### **2.2.4 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza utendaji wa Chuo hiki kwani kimekuwa nguzo muhimu ya mafunzo ya kiutumishi kwa Watumishi wa Umma, hasa kwa kuzingatia ukweli kwamba, hakuna Taasisi nyingine yenyewe jukumu la kutoa mafunzo hayo. Katika ziara yake, kwenye Kampasi ya Mbeya kamati ilibaini yafuatayo:-

i) Majengo yanayotumiwa ni ya kukodi kutoka Halmashauri ya Jiji la Mbeya, jambo linalokigharimu chuo **Shilingi Milioni 22** kwa Mwezi, sawa na **Shilingi Milioni 264** kwa Mwaka. Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ilizopata Kamati kuna mazungumzo yanayoendelea baina ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), kuhusu uwezekano wa chuo kumilikishwa majengo hayo;

ii) Pamoja na kukosa majengo yake, Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Mbeya kimeendelea kufanya vizuri katika kutimiza malengo yake, kwa kutoa Mafunzo na ushauri wa kitaalamu katika Utumishi wa Umma; na

iii) Bado chuo kinatumia Walimu wa Mkataba badala ya kuwa na Watumishi wa ajira za kudumu;

### **2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba:-

i) Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini ungeweza kufanikiwa zaidi iwapo fedha za ndani zingetumika kwa kiasi kikubwa kama ilivyo kwa fedha za Wafadhili. Tangu kuanza kwa mpango huu katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imechangia **Shilingi bilioni 3.6** kati ya **Shilingi bilioni 60.5** ilizopaswa kuchangia hadi sasa, kiasi ambacho ni sawa na asilimia **5.9** ya kiasi kilichotakiwa;

ii) Itikadi za kisiasa walizonazo Viongozi na Watendaji zinaweza kusababisha mgawanyiko mionganoni mwa Wananchi na hivyo kuathiri utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini;

iii) Uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa Walengwa wa Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini kuchukua fedha zao wenyewe utasaidia kufanikisha utekelezaji wa mpango na kufikiwa kwa lengo la kutoa elimu ya afya kwa walengwa;

iv) Kwa kuwa Wazee walio katika Vituo vya kulelea Wazee nchini wanakidhi sifa na vigezo vya kusaidiwa, ni jambo jema kutekeleza mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini katika vituo hivyo na kwamba utekelezaji huo utasaidia wazee hao kumudu maisha;

v) Dhamira ya kuwataka Wanufaika wa Mpango wa Ruzuku kwa kaya maskini wajunge na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) itafanikiwa zaidi iwapo Serikali itawezesha Zahanati binafsi kutoa huduma kwa walengwa hao;

vi) Uendeshaji wa Zoezi la kuhakiki na kuziondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini ni muhimu na utakuwa na tija zoezi hilo likifanyika kwa kuzingatia taratibu na kwa haki ili kuепusha kuibuka kwa

malalamiko kuhusu uonevu na kutotendewa haki kwa baadhi ya waliokuwa wanufaika.

vii) Uhaba wa fedha unachangia kukwamisha Zoezi la kupima na kurasimisha ardhi na biashara za Wananchi linalotekeliza na MKURABITA.

viii) Halmashauri zikishirikiana na MKURABITA, zinaweza kuandaa na kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi, jambo litakalosaidia kuepusha migogoro ya ardhi, na kuwezesha Wananchi kutumia Hati za Haki Miliki wanazopata kama dhamana ya mikopo kutoka taasisi za fedha.

ix) Uelewa wa kutosha juu ya umuhimu wa Wanufaika wa MKURABITA kulipia na kuchukua Hati Miliki za Kimila kwa wakati, ni jambo muhimu katika kufanikisha ukusanyaji wa fedha na kuendeleza zoezi hilo katika maeneo mengine;

x) Huduma ya mikopo kwa Vijana na Wanawake kutoka Mfuko wa Rais wa Kujitegemea, itafanikiwa zaidi iwapo mfuko huo utawezeshwa kifedha na kufungua matawi maeneo mengine ya nchi;

xi) Iwapo Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, kitamilikishwa majengo kinayoyatumia kwa ajili ya Kampasi ya Mbeya, hatua hiyo itasaidia kuepusha gharama kubwa za pango zinazolipwa kila mwaka;

### **3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017**

#### **3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili

ya shughuli zilizopangwa. Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

### **3.1.1    Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa:-

- i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo kuliko ilivyokusudiwa katika mpango wa upatikanaji fedha (cash flow plan); na
- ii) Fedha zinazotolewa kutoka Hazina hazipatikana kwa wakati jambo ambalo linaathiri utekelezaji wa Mpango kazi wa kuyaende malengo ya Bajeti ya Ofisi hii.

Maelezo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (na mafungu yake) kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari (katikati ya robo ya Tatu ya mwaka wa fedha 2016/17) na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi zaidi unabainisha kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2017 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake, ilikuwa imepokea Shilingi **527, 116, 217, 512/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho cha fedha ni sawa na asilimia **59.75** ya fedha yote ilioidhinishwa na Bunge lako Tukufu.

Kamati ililinganisha hali hiyo ya upatikanaji wa fedha kwa mwaka 2016/2017 na mwaka 2015/2016 na kubaini kuwa Kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa asilimia **23. 11** ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2015/16 ambapo upatikanaji wa fedha ulikuwa ni sawa na asilimia **82. 86** ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa kwa mwaka huo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umebainisha kwamba, hadi kufikia Mwezi Februari, 2017, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mafungu yake, ilikuwa imepokea jumla ya Shilingi **246, 780, 369, 584/=** kutoka Hazina, kiasi ambacho ni sawa na Asilimia **52. 93** ya fedha yote iliyoidhinishwa kwa ajili ya maendeleo.

Kiasi kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa asilimia **21.28** ikilinganishwa na kiasi kilichokuuwa kimepatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2015/16 kwa ajili ya maendeleo ambacho kilikuwa ni sawa na asilimia **74.21** ya fedha iliyokuwa imeidhinishwa kwa mwaka huo.

Kamati imebaini kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha (ie. Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa ujumla haukuwa mzuri, kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani Asilimia **59.75** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Tafsiri inayoweza kuelezwa hapa ni kwamba, kiwango kilichokadriwa kwa ajili ya kila robo ya mwaka wa fedha hakikupatikana, kwani ilitakiwa katika kipindi hicho upatikanaji wa fedha uwe zaidi ya Asilimia **70** ya fedha iliyoidhinishwa.

Aidha, katika kipindi hicho jumla ya fedha ya Matumizi ya Kawaida Shilingi **280,335,847,928/=** ilikuwa imepokelewa kiasi ambacho ni sawa na Asilimia **67.41** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hii inaonesha kwamba, kiasi cha fedha za Matumizi ya Kawaida kilikuwa kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo zilizopatikana katika kipindi kama hicho.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, mtiririko wa fedha umeendelea kudorora ikilinganishwa na miaka iliyopita na bado ile kasumba ya kwamba, fedha za matumizi ya kawaida ni lazima ziwe juu ikilinganishwa na fedha za maendeleo imeendelea kutamalaki.

### **3.1.2 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kuchambua bajeti ya Ofisi ya Rais - Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka 2016/2017, Kamati ilitoa ushauri katika mambo Tisa (9) kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa Ofisi ya Rais Menejementi ya Utumishi wa Umma, na Utawala Bora, iliweza kuzingatia kikamilifu maoni na ushauri wa Kamati. Baadhi ya Maoni na ushauri uliozingatiwa ni kuhusu:-

i) Uhakiki wa Watumishi hewa na kuwaondoa katika mfumo wa mshahara ili kuepusha upotetu wa fedha za Umma, ambapo katika kipindi cha Machi hadi Agosti, 2016 jumla ya **Watumishi hewa 19,708** walibainika na kuondolewa katika Mfumo wa Mshahara; na

ii) Tathmini kwa lengo la kubaini Wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini wasio na sifa, na kuwaondoa katika utaratibu huo, ambapo hadi mwezi Machi, 2017 jumla ya Kaya za **Walengwa 63,819** zilikuwa zimebainika na kuondolewa katika utaratibu huu kutakana na sababu mbalimbali.

#### **4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018**

##### **4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Mpango na Bajeti ya Mwaka wa fedha 2017/2018, kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayojumuisha Mafungu Tisa (20; 30; 32; 33; 67; 94; 04 na 11) imeandalisha kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika llani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 ya Chama Tawala, Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 na maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla ofisi hii pamoja na mafungu yake imepanga kutekeleza malengo **186** na baadhi ya hayo ni malengo yafuatayo:-

- i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake, pamoja na ushauri kwa Rais katika maeneo ya Uchumi, Siasa, Masuala ya Jamii, Sheria, Mawasiliano na Habari kwa Umma, Mahusiano ya Kikanda, Kimataifa na maeneo mengine;
- ii) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Mfuko wa Rais wa Kujitegemea;
- iii) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya 2007 ili kujumuisha makosa ya uhujumu uchumi na kutakatisha mali zilizopatikana kwa njia ya Rushwa na Ufisadi;
- iv) Kutumia Wakala wa Serikali Mtandao (eGA) kuunganisha Taasisi za Serikali 80 kwenye mfumo wa pamoja na salama wa barua Pepe wa Serikali ili kufikisha taasisi 281 zinazotumia mfumo;

v) Kuanzisha mchakato wa kutumia mfumo wa ujazaji wa fomu za matamko ya raslimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa njia ya mtandao (*online application*) baada ya kukamilika kwa Mfumo wa Kielektroniki wa Menejimenti ya Taarifa za Kimaadili (Ethics Management Information System - EMIS).

vi) Kuandaa taarifa za gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kiwango cha mshahara wenyе staha; na kutafiti namna ya kutoa motisha kwa kuzingatia utendaji katika Utumishi wa Umma, na

vii) Kuendelea kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika Taasisi za Umma 25 na Mamlaka za Serikali za Mitaa 18 kwenda Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu, Dodoma; na kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Masijala (e-Filing) ili kuboresha huduma na kurahisisha zoezi la Serikali kuhamia Dodoma;

viii) Kutoa ushauri wa kitaalam kwa Baraza la Mawaziri katika masuala yanayohusu uchumi wa mafuta na gesi zikiwemo Sera za Kisekta, Sera ya Uwekezaji, Sheria na Kanuni zinazohusu masuala ya uchumi wa mafuta na gesi;

**Mheshimiwa Spika**, ili iweze kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 821,322,347,674**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 430,351,457,674** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kaiwada, na **Shilingi 390,970,890,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 23,214,791,000** (sawa na asilimia 5.39) ni kwa ajili ya Mishahara, na **Shilingi 407,136,666,674** (sawa na asilimia 94.61) ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwaa kuidhinishiwa katika mwaka ujao wa fedha imepungua kwa **Shilingi 60,788,585,326** (sawa

na **asilimia 6.89**) ikilinganishwa bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa fedha 2016/17 ambayo ilikuwa **Shilingi 882, 110, 933, 000**.

Kwa upande wa bajeti ya maendeleo, kiasi kinachoombwa kuidhinishwa kimepungua kwa **shilingi 75,246,968,000** (sawa na **asilimia 16.13**) ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 466,217,858,000** kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2016/17.

#### **4.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kufanya ulinganisho na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018. Uchambuzi wa Kamati ulilenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la Bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelozwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji, na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Mambo yaliyobainika ni haya yafuatayo:-

i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/18 ambayo ni **shilingi biliioni 821** ni sawa na **asilimia 2.59** ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2017/18 ni **shilingi biliioni 31,699**:

ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/18 unaonesha ongezeko la bajeti kwa **asilimia 7.31**, ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2016/17; lakini bajeti ya jumla ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2017/18 imepungua kwa **asilimia 6.89** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika Mwaka wa fedha 2016/17;

iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la **asilimia 38** katika fedha za maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2017/18, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo ni sawa na asilimia 3.25 ya Bajeti ya Taifa, imepungua kwa **asilimia 16.13** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2016/17. Aidha, **Jedwali Na. 04** linafafanua zaidi juu ya ulinganisho baina ya maeneo hayo mawili.


**Jedwali Na. 04:** Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais(UUB) dhidi ya Bajeti ya Taifa, kwa Mwaka 2017/18

BAJETI KUU YA TAIFA 2017/2018			BAJETI YA OFISI YA RAIS – UUB 2017/2018		
Mgawanyo	Bajeti Kuu (Tsh.Milioni)	Asilimia ya Jumla ya Bajeti kuu	Mgawanyo	Bajeti ya Wizara	Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara
OC	3,032,954	9.57	OC	407,136,666,674	49.57
Deni la Taifa	9,461,433	29.85	-	-	-
Mishahara	7,205,768	22.73	Mishahara	23,214,791,000	2.83
Maendeleo	11,999,592	37.85	Maendeleo	390,970,890,000	47.60
Jumla	<b>31,699,748</b>	<b>100</b>	Jumla	<b>821,322,347,674</b>	<b>100</b>

**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa, na Randama ya Ofisi ya Rais – UUB


Matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma yanaweza kuoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01** na **Na. 02** kama ifuatavyo:-

**Chati Na. 01: Bajeti ya Taifa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Mishahara, Denila Taifa na Maendeleo, Mwaka 2017/18**



**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

Chati Na.02: Bajeti ya Ofisi ya Rais - UUB kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, Mishahara na Maendeleo kwa Mwaka 2017/18



**Chanzo:** Randama ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

i) Serikali itoe kikamilifu mchango wake katika Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini ungeweza kufanikiwa zaidi iwapo fedha za ndani zingetumika kwa kiasi kikubwa kama ilivyo kwa fedha za Wafadhili. Tangu kuanza kwa mpango huu katika Mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali imechangia **Shilingi bilioni 3.6** kati ya **Shilingi bilioni 60.5**

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

ilizopaswa kuchangia hadi sasa, kiasi ambacho ni sawa na asilimia **5.9** tu.

ii) Viongozi na Watendaji waache kuingiza itikadi za kisiasa katika utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, kwani unaleta mgawanyiko usio na msingi kwa Wananchi na hivyo kuathiri utekelezaji wa mpango;

iii) Walengwa wa Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini waelimishwe juu ya umuhimu wa kuchukua fedha zao wenyewe badala ya kutuma watu, ili waweze kunufaika na malengo mengine ya mpango ikiwa ni pamoa na kupata elimu ya afya;

iv) Serikali iangalie uwezekano wa kupeleka Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini, kwenye vituo vyatutenzia Wazee nchini, kwani Wazee walioko katika vituo hivyo wanazo sifa na vigezo vyatutenzia kunufaika na mpango huo;

v) Serikali iandae utaratibu utakaowezesha Wanufaika wa Mpango wa Ruzuku kwa kaya maskini ambao wamejiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ya Jamii (CHF) kupata huduma ya matibabu katika Zahanati binafsi. Kwa sasa Zanahati binafsi hazikubali kutoa huduma ya afya kwa walengwa hao;

vi) Serikali ihakikishe zoezi la kuhakiki na kuziondoa katika mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini, kaya zisizo na sifa linatekelezwa kwa haki na kufuata taratibu ili kuepusha malalamiko ya uonevu na kutotendewa haki kutoka kwa waathirika;

vii) Serikali iongeze fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa kupima na kurasi misha ardhi na biashara za Wananchi, unaotekelawa na MKURABITA ili kutoa fursa kwa Wananchi kutumia ardhi na biashara walizonazo kujikwamua kiuchumi;

viii) Serikali ihamashe Halmashauri kushirikiana na MKURABITA, katika kuandaa na kutekeleza mpango bora wa

matumizi ya ardhi, ili kupunguza au kuepusha migogoro ya ardhi, na kuwezesha Wananchi kutumia Hati za Haki Miliki wanazopata kama dhamana ya mikopo kutoka taasisi za fedha;

ix) Wanufaika wa MKURABITA nchini wahamasishwe kulipia kulipia na kuchukua Hati Miliki za Kimila kwa wakati, ili kuwezesha fedha iliyotumika katika upimaji na uandaaji wa hati itumike kuendeleza zoezi hilo katika maeneo mengine;

x) Mfuko wa Rais wa Kujitegemea (PTF) uwezeshwe kifedha ili kutanua wigo wa shughuli zake nchini na kuongeza huduma ya mikopo kwa Vijana na Wanawake; na

xi) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, kiwezeshwe kumiliki majengo kinayoyatumia katika Kampasi ya Mbeya ili kuepuka gharama za pango ambazo ni kubwa;

## **6.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkiendesha shughuli za Bunge.

Aidha, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa kushiriki kikamilifu kutekeleza shughuli za Kamati. Kamati hii ina Mafungu mengi ya Bajeti ambayo inayashughulikia, na kwa kuzingatia muda mfupi uliokuwa umetengwa wakati wa uchambuzi wa bajeti, Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi ikiwa ni pamoja na siku za mwisho wa wiki. Mazingira hayo magumu hayakuwa kikwazo kwa Wajumbe, na badala yake walijitoa kikamilifu na kukabili majukumu yaliyokuwa mbele yao, kwa moyo na weledi wa hali ya juu wakiashiria utayari wao katika kulitumikia Bunge na Taifa kwa ujumla. Kwa umuhimu mkubwa, napenda niwatambue kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

2. Mhe.Mwanne Ismail Mcemba,Mb –Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb
6. Mhe.Ester Alexander Mahawe,Mb
7. Mhe.George Malima Lubeleje,Mb
8. Mhe.Halima Ali Mohamed,Mb
9. Mhe.Hamad Salim Maalim,Mb
10. Mhe.Waitara Mwita Mwikwabe,Mb
11. Mhe.Innocent Sebba Bilakwate,Mb
12. Mhe.Josephine Tabitha Chagula,Mb
13. Mhe.Khamis Ali Vuai,Mb
14. Mhe.Maida Hamad Abdallah,Mb
15. Mhe.Hamoud Abuu Jumaa,Mb
16. Mhe.Khalifa Mohamed Issa,Mb
17. Mhe.Hussein Ibrahim Makungu,Mb
18. Mhe.Mariam Ditopile Mzuzuri,Mb
19. Mhe.Mwatum Dau Haji,Mb
20. Mhe.Ruth Hiyobi Mollel,Mb
21. Mhe.Saada Mkuya Salum,Mb
22. Mhe.Salum Khamis Salum,Mb
23. Mhe.Venance Methusela Mwamoto,Mb
24. Mhe.Zacharia Paulo Isaay,Mb
25. Mhe.Saed Ahmed Kubenea,Mb

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. Angellah Kairuki, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na Watendaji wa Ofisi hiyo wakiongozwa na Katibu Mkuu Utumishi, Dr. Lauren Ndumbaro kwa jinsi walivyoshiriki katika kujibu hoja za Wajumbe wa Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, na kufafanua kwa kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Aidha, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt. Thomas Kashililah, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Jumla, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Victor Leonard na Eunike

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Mariam Ally, kwa uratibu wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jasson S. Rweikiza (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA  
NA SERIKALI ZA MITAA**

18 Aprili, 2017

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tutaendelea na upande wa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Ofisi zote mbili kwa maana TAMISEMI na Utawala Bora na ninyi pia mtapa saa moja, nusu saa kwa kila Ofisi.

Nimepata viji-note vingi vya Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na makubaliano yetu ya wakati ule wa semina ile ya mara ya mwisho ya yale mambo ya zile hisa, nafikiri mnakumbuka Waheshimiwa?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Nimekuwa bado nafanya kazi lile jambo najua muda unakimbia lakini nadhani *byleo* jioni tutakuwa tumefika

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

mahali pa kuelewana, lakini kuna ugumu fulani. Lakini kuna ugumu wenyewe ni kwamba, nitajaribu kusema kidogo kwa lugha za alama, kama mambo yatabakia yalivyo kama yalivyo sasa, mkumbuke hesabu za mwisho zinategemeana na mambo yatakavyokuwa pale mwisho, lakini kwa hesabu ya sasa ingekuwa ndiyo pale 2020, hesabu yetu ni kama 170. Ukiiondoa ile kodi tuliojitatikia inashuka kidogo kuja hapo kwenye 150 hivi kitu kama hicho. (*Kicheko*)

Sasa hiyo ni mkono wa kwaheri ambayo ni kidogo sana kwa Mbunge unayeondoka kwenda kwenye mapambano, kwa wale ambao mnapanga kupambana tena. Wengine kwa kweli hata hapo hawana kitu cha maana, tayari walishaingia huko, tayari walishachotachota.

Kwa hiyo, hali si nzuri kihivyo na Spika ambaye naye anaendekeza tena muendelee kuingia huko ili mtoke vibaya zaidi atakuwa kidogo hawatakii mema. Sasa hapo ndiyo *dilemma* yangu ilipo hapo, *whether nikiwakubalia nitakuwa nawasaidieni au nawatumbukiza kwenye matatizo zaidi.* (*Makofi*)

Basi baada ya maelezo hayo, naomba sasa nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni tutakapoanza na upande wa Upinzani, ahsanteni.

(*Saa 7.32 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni*)

(*Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Tunaendelea na *session* ya jioni ya Mkutano wetu wa Saba, Kikao chetu cha Nane. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais,  
Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais,  
Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, majadiliano yanaendelea na naomba sasa moja kwa moja nimuite Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Karibu sana Mheshimiwa, muda wako si zaidi ya nusu saa.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMADI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2017/2018 chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Spika, naomba hotuba yangu yote iingie kwenye *Hansard* ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, Naibu Waziri Kivuli wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, TAMISEMI na Waheshimiwa Wabunge wote ambao wameshiriki katika kuchangia hotuba hii. Pia nichukue fursa hii kutoa pole kwa familia ya Mheshimiwa Dkt. Elly Macha, nikupe pole wewe na pia nitoe pole kwa familia ya Mheshimiwa Tahir, Mbunge wa Dimani ambaye alitutoka. Mungu awaweke mahali pema peponi hawa wapendwa wetu ambao wametutoka.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, Ibara ya 145 na 146, Serikali za Mitaa ni

## **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

vyombo vya wananchi ambavyo vipo katika ngazi za chini za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vyombo hivi huundwa, huendeshwa, husimamiwa na kuwajibika kwa wananchi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa miaka ya 1970 na mwanzoni mwa miaka ya 1980 Serikali ilirejea dhamira yake ya kuwa na Serikali za Mitaa zilizo imara ili kutimiza azma yake ya kupeleka madaraka kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuzipa mamlaka ya kukusanya mapato kutohama na vyanzo mbalimbali vya mapato.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vimeainishwa katika vifungu namba sita hado tisa vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 yaani (*The Local Government Finance Act, No. 9 of 1982*). Kulingana na Sheria ya Fedha Na.9 ya mwaka 1982 ya Serikali za Mitaa iliyorekebishwa na Sheria ya Fedha Na.15 ya mwaka 2003 yaani (*The Finance Act No. 15 of 2003*), Serikali za Mitaa hazitozi kodi ya mapato. Jukumu hili hufanywa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (*Tanzania Revenue Authority*) kwa kushirikiana na Hazina kwa viwango mbalimbali kwa mujibu wa sheria na kanuni husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhusiano kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Serikali Kuu ni chombo ambacho kwa misingi maalum kimepewa mamlaka ya kuendesha utawala wa nchi nzima. Maeneo ya Serikali Kuu yanaanza Taifa, Mkoa, Wilaya na Taraifa. Serikali za Mitaa ni vyombo vya Serikali Kuu katika ujenzi wa utawala bora, demokrasia na kuleta maendeleo nchini.

Kufanikiwa kwa Serikali za Mitaa kunategemea zaidi uhusiano na ushirikiano kati yake na Serikali Kuu kwa kujenga mazingira mazuri ya kiutendaji. Ibara ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na marekebisho yake inaweka misingi ya uhusiano kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Ili kuwezesha kufanya kazi kwa uhusiano huo, Sheria mbalimbali zimetungwa kuhalalisha uhusiano huo. Sheria hizo ni pamoja na:-

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(a) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Namba 7 ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 6 ya mwaka 1999;

(b) Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Namba 8 ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na Sheria Namba 6 ya mwaka 1999; na

(c) Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa kwa mujibu wa kifungu cha 174A cha Sheria Namba 7 ya mwaka 1982 na marekebisho ya Sheria Namba 13 ya mwaka 2006 kifungu cha 54A cha Sheria Namba 8 ya mwaka 1982, majukumu 10 ya Serikali Kuu kwa Serikali yameainishwa katika sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Sheria hiyo Na.19 ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ya mwaka 1997 imetaja majukumu na mipaka ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri mwenye dhamana kuwaelekeza Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kufanya kazi kwa kuzingatia mipaka yao ya kisheria. Wakuu wa Mikoa na Wilaya waepuke kufanya maamuzi yanayorudisha nyuma utekelezaji wa majukumu ya Madiwani na Watendaji wa Halmashauri nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani haiamini katika tabia iliyojengeka sasa ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ya kuwanyanyasa watumishi wa Halmashauri kinyume cha sheria za Tanzania za utumishi wa umma. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maboresho ya Serikali za Mitaa; Serikali za Mitaa huwawezesha wananchi kuwa na sauti katika maamuzi mbalimbali kwa mujibu wa Ibara ya 8(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali inapata madaraka na mamlaka yake kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 1998, Sera ya Taifa ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa (*Policy Paper on Local Government Reform 1998*) iliandaliwa na kuweka bayana umuhimu wa kugatua madaraka ya Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa (*Decentralization by Devolution*) au kwa jina lake maarufu *D by D*. Chini ya Sera hii, Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa (*Local Government Reform Programme - LGRP*) ilianzishwa kwa dhamira ya kuziimarishe Serikali za Mitaa ili kusukuma mbele utekelezaji wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini yaani *Poverty Reduction Strategy* na baadaye MKUKUTA na vilevile kuhakikisha kuwa Halmshauri za Miji na Wilaya zinatoa huduma bora kwa wananchi wake hususan huduma za afya, maji, elimu na huduma za ughani na kadhalika (angalia mpango wa *LGRP Medium Term Plan and Budget July 2005 – June 2008*, Ofisi ya Rais – TAMISEMI: Juni 2005 ).

Mheshimiwa Spika, malengo maalum ya programu hiyo yalikuwa ni:-

(i) Kugatua madaraka ya Serikali Kuu kuyapeleka kwenye Serikali za Mitaa (*LGAs*) ili ziwe na madaraka kamili yaani *to create more autonomous Local Government Authorities* kuitia *political decentralization*;

(ii) Kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kuitia watumishi wa umma wanaowajibika kwa Serikali za Mitaa zenyewe (*de-linking of local authority staff from the respective line-ministries, making them accountable to the LGA who will be their employer, fully responsible for all human resource management* yaani *Administrative Decentralization*; na

(iii) Kuziwezesha Halmashauri kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake na kuwa na mfumo wa mgawanyo wa mapato kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa yaani *financial decentralisation*.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa kipekee maboresha pia yalikuwa na dhamira kuu ya kubadilisha

mfumo wa mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kutoka mfumo wa Serikali Kuu wa kuwa na *control role* na hivyo kuwa na wajibu wa kutunga sera na kuweka vigezo vya ubora wa huduma na kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza Sera kwa kuwajengеа uwezo na kuwapatia raslimali fedha na utaalamu ili ziweze kutoa huduma inayolingana na ubora uliowekwa na kukubalika. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa, Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ilitekelezwa sambamba na programu nyingine za uboreshwaji wa sekta za umma na sekta binafsi. Moja kati ya nyanja muhimu za uboreshaji wa sekta ya umma ni Uboreshaji wa Utumishi wa Umma yaani *Civil Service Reform Programme (CSRP 1998)* ambayo baadaye iliboreshwa na kutengeneza programu maalum ya miaka kumi na mitano yaani *Public Service Reform Programme* ya 2000 to 2015. Maboresho haya maboresho hayo yalidhamiria kuimarisha utawala na utoaji huduma mambo ambayo ni muhimu sana katika kuiondoa nchi yetu kwenye umaskini na pia kufikia vigezo vya mpango wa Maendeleo ya Millenia wa kupunguza umaskini wa kipato na nchi yetu kuwa na uchumi wa kati.

Mheshimiwa Spika, awamu za kwanza za maboresho hayo ya Serikali ya Mitaa yalichukua miaka kumi, kuanzia mwaka 1998 – 2008. Katika kadhia hiyo, sera ya *D by D (Decentralization by Devolution)* ndiyo ilipata umaarufu sana. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba uwekezaji wote huo uliofanywa na Serikali za Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne umekuwa ni kazi bure kwa vile katika uhalisia madaraka yamerudishwa Serikali Kuu. Awamu ya Tano ambayo wananchi walikuwa na matumaini makubwa kwayo katika kugatua madaraka kwa lengo la kukuza demokrasia na ushirikishwaji wa wananchi katika mipango yao ya maendeleo na utawala bora inafanya kinyume kabisa na matarajio ya wananchi. (*Makofі*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini ugatuaji wa madaraka ni jambo la msingi sana katika kutekeleza ustawi wa maendeleo ya wananchi. Hivyo,

### **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

inaishauri Serikali ya Awamu ya Tano isimamie na kutekeleza dhana ya ugatuaji madaraka. Kwa msingi na muktadha huo, kama Serikali haitakuwa makini katika kutekeleza hilo, itegemee kupata matatizo kama iliyopata matatizo kwenye sera ya ubinafsishaji ambapo leo mnaanza kupambana kurudisha viwanda ambavyo mliviuwa kwa sera zenu mbovu za Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu Halmashauri kukosa mamlaka kamili inayolingana na dhamira halisi ya kuanzishwa Serikali za Mitaa, ni kweli kwamba Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa ndio msimamizi mkuu wa Serikali za Mitaa. Kwa njia hii Serikali za Mitaa zinawajibika moja kwa moja kwa Wizara hii kwa chochote kile kinachofanywa na Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majji. Kwa lolote lile, Waziri Mwenye dhamana anaweza kuamua kuivunja Halmashauri ya Wilaya, Manispaa au Jiji na kuteua Tume ya kusimamia uendeshaji wa Halmashauri ya Wilaya, Manispaa au Jiji husika. Aidha, Waziri ana mamlaka ya kumhamisha au kumsimamisha kazi Mtendaji Mkuu au Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, mfumo mzima wa kuwawajibisha viongozi wa kisiasa katika ngazi za Halmashauri nao unaingiliwa sana na maamuzi ya Serikali Kuu. Mambo haya yote kwa ujumla wake ndio yanaondoa mamlaka kamili (*autonomy*) ya Serikali za Mitaa na kufanya maboresho ya miaka kumi na sera nzima ya *D by D*kuwa ni bure na ni hasara kwa walipa kodi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, mamlaka ni kuwa na uwezo wa kuajiri na kufukuza (*hire and fire*). Kukosa mamlaka hayo maana yake ni kiini macho cha mamlaka hivyo basi Serikali za Mitaa sio Serikali kamili kama inavyotamkwa ndani ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali za Mitaa zilikuwa na sheria yake ya kuwa na uwezo wa kuajiri na kufukuza watumishi wake (*hire and fire*) ambayo ni Sheria Namba 10 ya mwaka

1982 (*The Local Government Service Act, No. 10 of 1982*). Hata hivyo, Serikali Kuu kwa kufikiri kuwa Halmashauri zitakuwa na nguvu za kuweza kuwatumikia Watanzania kwa kiwango cha juu na kuweza kuwaondolea umaskini, mwaka 2002 illifuta sheria hiyo na kutunga Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 (*The Public Service Act. No.8 of 2002*). Sheria hii ilipoka madaraka ya Halmashauri kuhusu utumishi na kurejesha madaraka hayo chini ya Ofisi ya Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuzipunguzia mamlaka Halmashauri ya kusimamia watumishi wake hasa Mkurugenzi na Wakuu wa Idara kunasababisha ubunifu wa watumishi wa Halmashauri kuwa wa chini sana kwa vile wamekuwa wakiendesha Halmashauri kwa mipango ama ya zimamoto au maagizo na miongozo kutoka ngazi za Serikali Kuu, bila kujali hali halisi ndani ya Halmashauri zao.

Aidha, nidhamu ya Wakurugenzi na watumishi wa Halmashauri kwa Madiwani ambao ndio wenye Halmashauri kwa niaba ya wananchi imekuwa ya chini mno hivyo kufanya maagizo mengi ya Mabaraza ya Madiwani katika Halmashauri kutotekelezwa kwa kuwa Wakurugenzi na Menejimenti za Halmashauri wanaweza wakaamua kupuuza maagizo hayo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wamekuwa tena sio washauri na waangalizi wa mienendo ya utendaji wa Halmashauri bali wamekuwa wafanya maazimio ya shughuli za kila siku za Halmashauri badala kuheshimu maazimio ya vikao vya kisheria vya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa vile wao wana kofia ya kumwakilisha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamekuwa wakitumia mamlaka yao kuwalazimisha Wakurugenzi kutekeleza maagizo yao na kupuuza maazimio ya Baraza la Madiwani, jambo ambalo limekuwa likileta mivutano mikubwa kati ya Madiwani na Wakurugenzi katika Halmashauri hapa nchini hivyo kudumaza maendeleo ya watu wetu.

### **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuangalia upya Sheria hii ya Utumishi na Ajira katika Serikali za Mitaa ili kuwe na utaratibu wa ajira za Wakurugenzi na Wakuu wa Idara ambao mchakato wake utaanzia kwenye vikao vya kisheria vya Halmashauri hata kama itakuwa ni kutoa mapendekezo kwa Waziri mwenye dhamana kwa watu wenyе sifa watakaokuwa wameomba ajira hizo za Ukurugensi na Ukuu wa Idara ili Waziri atue kutokana na mapendekezo ya Halmashauri husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, uwezo wa Halmashauri kukopa au kuingia ubia na sekte binafsi (*Private Public Partnership*). Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982 inaziruhusu Halmashauri kukopa katika taasisi za fedha ili kuwekeza katika miradi ya maendeleo. Jambo la kusikitisha ni pale ambapo Waziri mwenye dhamana anapoamua kuinyima kwa makusudi kibali cha kukopa Halmashauri ambayo imetimiza vigezo vyote vya kukopa katika taasisi za fedha ili kuwekeza katika miradi ya maendeleo ambayo inajиidesha yenye kwa faida. Kuna kila dalili kwamba kuna ubaguzi wa kisasa unaofanywa ama na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI au Serikali nzima ya Awamu ya Tano kwa kuzibagua Halmashauri zinazoongozwa na vyama vya upinzani kama vile za Jiji la Arusha, Jiji la Mbeya, Manispaa ya Iringa, Manispaa ya Moshi na kadhalika ili kuzifanya zishindwe kutimiza wajibu wake wa kuwalettea wananchi maendeleo na hatimaye wananchi wapoteze imani na vyama vya upinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni uamuzi wa Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI kuamua kwa makusudi ama kuchelewesha au kukataa kutoa kibali cha kukopa kwa Manispaa ya Moshi kwa mradi wa ujenzi wa *stand* ya kisasa ya mabasi yaendayo mikoani (*Modern Terminal Bus Stand*) ambapo Benki ya Rasilimali ya Tanzania (*TIB*) iko tayari kuwekeza kwenye mradi huo kwa kutoa zaidi ya shilingi bilioni ishirini kwa mfumo wa *Design Build, Operate and Transfer (BOT)*. Mradi huo ambao kuufanya upembuzi na uchambuzi yakinifu umetumia takribani shilingi milioni 300 fedha ya walipa kodi na ikathibitika kwamba ni wa faida kiuchumi

unanyimwa kibali ili kuwakomoa wananchi wa Manispaa ya Moshi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, imani ya kwamba kuna kila dalili ya ubaguzi wa kisiasa unaofanywa na ama na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI au na Serikali kwa ujumla wake ni kutokana na Waziri huyo huyo kutoa kibali cha miradi ya aina hiyo kwa Manispaa ya Morogoro na Jiji la Tanga. Huo ni upendeleo mbaya sana na matumizi mabaya ya madaraka (*double standards*) yanayofanywa na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali lazima itambue kwamba ina wajibu wa kuwatumikia wananchi wote bila ubaguzi wowote kwa vile Watanzania wote kwa namna moja ama nyingine wanalipa kodi, hivyo Serikali kuwapelekea maendeleo sio hisani bali ni wajibu. Aidha, wananchi wasiadhibiwe kwa vile wamechagua wawakilishi kupitia vyama vyaya upinzani kwa kuwa wamefanya uamuzi halali wa kikatiba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kurejea kwenye azma yake ya maboresho ya Serikali za Mitaa ili kuzifanya Halmashauri zijitegemee kwa kiwango kisichopungua 35% kwa kubuni miradi ya uwekezaji na kutafuta vyanzo vipyta vyaya mapato visivyo na kero kwa wananchi. Pia Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI awatumikie Watanzania wote bila ubaguzi wa kisiasa wala kikanda. Nategemea kwamba Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana atatoa kibali kwa Manispaa ya Moshi ili ujenzi wa standuendelee. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba chanzo kikubwa cha matatizo ya mapato yanazozikabili Halmashauri zote kwa ujumla ni kutokana na udhibiti unaofanywa na Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa. Hivyo basi, ili kurekebisha kasoro hizo ni kuifanyia marejeo Sheria za Fedha hasa kifungu cha 60 kinachoruhusu Halmashauri kukopa na kuondoa sharti la ridhaa ya Waziri mwenye dhamana ili Halmashauri ziweze kukopa kwenye

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

taasisi mbalimbali za fedha bila kisingizio wala kikwazo chochote.

Mheshimiwa Spika, jukumu la utoaji huduma za jamii katika Manispaa na Majiji; Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kuishauri Serikali kuona namna ya kufanya marejeo ya Sheria Namba 8 ya mwaka 1982 ili iweze kuwafanya Mameya wa Manispaa na Majiji wawe Mameya Watendaji (*Executive Mayors*) wenyewe mamlaka kamili na ikiwezekana sheria itamke kwamba watapigiwa kura na wananchi wote wa eneo husika ili wawe na wigo mpana wa kuwahudumia wananchi wote kwenye maeneo yao ya utawala. Hii itasababisha Halmashauri, hasa Mameya wa Majiji wawe na uwezo wa kuendesha miradi mikubwa ya maendeleo bila kuingiliwa na Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu muingiliano wa maagizo na maelekezo katika Halmashauri; katika mwendelezo huo wa kupoka madaraka ya Serikali za Mitaa, katika marekebisho ya Sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa ya mwaka 2006 inaonesha kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri ambao ni wateule wa Serikali Kuu wanalazimika kupeleka taarifa za utekelezaji kwa Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa ambao ni sehemu ya Serikali Kuu, rejea kifungu cha 9(b) cha Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Serikali za Mitaa kinachorekebisha kifungu cha 174 cha sheria mama ya *Local Government District Authorities Act*. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona huu ni udhibiti badala ya ushauri ili kudhibiti taarifa za Serikali za Mitaa zinazotakiwa kupelekwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali kwamba kama nchi hii inataka kufikia maendeleo ya haraka ni lazima iondoe huu muingiliano wa maagizo na maelekezo kwenye Halmashauri za nchi hii ambapo kwa upande mmoja kuna Madiwani na upande wa pili kuna Wakuu wa Mikoa ,Wilaya na Waziri mwenye dhamana na hata viongozi wa chama tawala wote wakitoa maagizo na maelekezo kwa Wakurugenzi na menejimenti ya Halmashauri jambo linalowakwaza sana Wakurugenzi na watumishi wengine kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kodi ya majengo (*propert tax*); kwa kuwa Halmashauri hapa nchini zimekuwa zikikusanya mapato kwa ajili ya kuendesha miradi yake ya maendeleo na shughuli nyingi za kawaida kutoka kwenye vyanzo vyake vya mapato kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Halmashauri (*Local Government Finance Act, 1982*) haukuwa uamuzi sahihi kutunga sheria ya kuondoa chanzo cha mapato cha kodi ya majengo kutoka katika Halmashauri nchini.

Mheshimiwa Spika, kufutwa kwa kifungu kilichokuwa kinazipa Halmashauri jukumu la kukadiria na kukusanya kodi za majengo na kulihamishia *TRA* kuititia Sheria ya Fedha ya mwaka 2016, kifungu cha 38 baada ya kufanya marekebisho kwa kuvifuta vifungu vya 31A na 31B vya Sheria ya Fedha ya Serikali ya Mitaa Sura 290 kumeziyumbisha sana Halmashauri katika kutekeleza majukumu yake kutokana na ukweli kwamba chanzo cha kodi ya majengo kilikuwa ni mojawapo ya chanzo kikubwa cha mapato hususani katika Manispaa na Majiji hapa nchini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali inaonyesha kodi ya majengo iliyokusanywa mpaka sasa ni shilingi milioni 4,762.37 kati ya shilingi milioni 29,004 sawa na asilimia 17.4 tu yaani Serikali imekusanya shilingi bilioni nne kati ya shilingi bilioni 29. Sababu ya makusanyo hayo madogo imeelezwa kuwa ni pamoja na kutokamilisha maandalizi ya yatakayowezesha ukusanyaji ikiwa ni pamoja na kuandaa sheria na kanuni za ukusanyaji, kutengeneza mfumo wa ukusanyaji wa kodi, kuunda kitengo na kuweka wafanyakazi na vitendeza kazi.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote kwa muda wa miaka zaidi ya 30 ya uhai wa Serikali za Mitaa zimeimarisha miundombinu ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato na rasilimali watu ambapo ilikuwa inahitaji marekebisho ya kawaida kuongeza ufanisi hususani kuziruhusu Halmashauri ziajiri watumishi zaidi kwenye Idara za Fedha za Halmashauri. Maoni ya Wabunge wengi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye hotuba ya bajeti mwaka 2016/2017 yalikuwa ni kutoondoa chanzo hicho cha kodi ya majengo katika

### **NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Halmashauri lakini Serikali ikakataa ushauri huo kwa msisitizo kwamba *TRA* ina uwezo wa kukusanya.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kwamba baada ya kukusanya itarejesha fedha hizo kwenye Halmashauri jambo ambalo halijafanyika mpaka sasa kwa Halmashauri nyingi nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kama kweli tunahitaji kuendelea na sera ya *D by Dambayo* ina lengo la kutoa mamlaka kamili kwa Serikali za Mitaa ni lazima Serikali ipitie upya Sheria ya *Property Tax* ili jukumu la kukusanya kodi hiyo liendelee kufanywa na Halmashauri kwa vile ukweli uko wazi kwamba *TRA* wanajukumu kubwa sana la kupanua wigo wa walipa kodi na jukumu kubwa la kuvisimamia vyanzo vyake ambavyo bado havijakusanya kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na zoezi linaloendeshwa na Serikali Kuu la kubaini watumishi hewa. Ni ukweli kwamba vyeo vya *RAS, DAS* na *DED* sio nafasi za kisiasa na mtumishi kufikia nafasi hizo ni dhahiri kwamba amepitia ngazi mbalimbali katika utumishi wa umma. Ngazi hizo huendana na marupurupu na mshahara na ni ukweli pia mtumishi katika nafasi hiyo akiondolewa kwa mujibu wa sheria haina maana kwamba na mshahara wake unaondolewa.

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kubana matumizi, hivyo ungetegemea mabadiliko yaliyofanywa ya Makatibu Tawala wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri ambao wote ni viongozi wa kitaaluma yazingatie nia hiyo ya kubana matumizi badala ya kutengeneza watumishi hewa ambao wanalitia Taifa hasara kubwa. Kwa mfano, kati ya Wakurugenzi 184 wa Halmashauri hapa nchini, Wakurugenzi 120 wa zamani hawakuteuliwa kwa nafasi hizo katika Serikali ya Awamu ya Tano ambapo hata wale wapya walioteuliwa walitoka nje ya mfumo wa Utumishi wa Umma wengi wao wakiwa ni makada wa CCM. Baada ya kutenguliwa kwa Wakurugenzi hao 120 kutoka Halmashauri mbalimbali nchini walielekezwa kuhudhuria kwa Makatibu Tawala wa Mikoa waliyotoka kwa ajili ya kupangiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, ni zaidi ya mwaka mmoja sasa Wakurugenzi hao takribani wote wanahudhuria kwa Makatibu Tawala wa Mikoa ambapo kimsingi hawana kazi za kufanya kwa kuwa ikama ya watumishi haionyeshi nafasi zao katika ngazi ya Katibu Tawala wa Mkoa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba Wakurugenzi hawa bado wanalipwa mishahara yao pamoja na stahiki zao zingine za kiutumishi kama vile nyumba, umeme, simu, matibabu na kadhalika. Wastani wa mshahara wa Mkurugenzi mmoja ni shilingi 3,820,000 mpaka 4,000,000 kwa mwezi. Hivyo malipo kwa Wakurugenzi 120 ni takribani shilingi 480,000,000 kwa mwezi na hivyo kwa mwaka ni takribani shilingi 5,760,000,000. Tafsiri sahihi ya jambo hili linaloendea ni kuwepo kwa *double payment* ya Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa zamani waliokuwa wameshafikia ngazi hizo za madaraka na wale wapya ambaao ndio waliofugaji.

Aidha, Serikali inaweza ikawa imejiingiza katika ubadhirifu kwa matumizi ya zaidi ya shilingi bilioni 5.76 kinyume cha fedha iliyopitishwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kutokana na ikama ya Wakurugenzi wa hapa nchini.

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**SPIKA:** Kengele ya kwanza tayari.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu sahihi juu ya sintofahamu hiyo ya waliokuwa Wakurugenzi wa Halmashauri, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya ambaao bado wanapokea mishahara na stahiki zingine za madaraka kwa nafasi ambaao walishaondolewa.

Mheshimiwa Spika, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na maumivu ya kisaikolojia (*psychological*

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

*torture) waliyopata Wakurugenzi wa zamani kutokana na chuki, ubaguzi na matumizi mabaya ya madaraka ya mamlaka za uteuzi yaliyosababishwa na matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 ambapo maeneo ambayo upinzani ulishinda Wakurugenzi wake hawakupata uteuzi kwa nafasi hizo kwa Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa kisingizio kwamba hawajakisaidia Chama cha Mapinduzi kupora ushindi halali wa wapinzani. (Makof)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ya Awamu ya Tano ijisahihishe ili isije ikiwafanya wananchi wakaamini kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inahalalisha vitendo vya wasimamizi wa uchaguzi kuharibu uchaguzi kwa kutangaza matokeo batili bila kuelewa kwamba vitendo hivyo vinahatarisha amani na utulivu wa nchi ya Tanzania. Kwa maana hiyo kwa Serikali ya CCM ni heshima kwa msimamizi wa uchaguzi kutotenda hakili aliyoapa kuisimamia kwa mujibu wa Katiba ya nchi kwa kutumia vitabu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu huku akilipwa fedha za walipa kodi wa Tanzania. (Makof)

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa elimu ya msingi na sekondari; TAMISEMI ndiyo wasimamizi wakuu wa elimu ya msingi na elimu ya sekondari hapa nchini lakini wanaotoa miongozo ya jinsi ya kuendesha elimu hiyo ni Serikali Kuu. Kwa maana hiyo mamlaka inayotoa leseni na vibali vya uanzishwaji wa shule ni Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imeazimia kutoa na kutekeleza dhana ya elimu bure kwa elimu ya msingi na sekondari. Pamoja na dhana hiyo hakuna ufanuzi wa kutosha au unaoeleweka. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali:-

(i) Kuweka wazi kwa umma wa Tanzania vipengele vyote ambavyo havitachangiwa na wananchi ili kuondoa mkanganyiko uliopo na kuwezesha bajeti za ukweli kuandaliwa.

(ii) Ili kuwezesha upatikanaji wa elimu bora vijijini na mijini katika ngazi ya msingi na sekondari, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupeleka bajeti kamili kwa ajili ya kujenga shule zilizokamilika yaani pasiwe na shule inayojengwa bila kukamilisha darasa, sambamba na uwiano wa madawati na vyoo vinavyoendana na idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa.

(iii) Kwa kuwa Serikali imeweka vigezo/viwango stahili kwa ajili ya kusajili shule za msingi na sekondari basi bajeti inayopelekwa katika Halmashauri ni lazima itosheleze kujenga miundombinu ya shule za umma katika viwango vilivywerekwa na Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba katika enzi hizi za maendeleo ya viwanda kuelekea Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati haitawezekana watoto wetu katika shule za msingi na sekondari waende katika shule zisizokidhi viwango hususani ukosefu wa matundu ya vyoo na madawati. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba ni muda muafaka sasa kwa Serikali kuangalia chombo ambacho kitasimamia kwa haki mfumo wa utoaji wa elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa huduma ya afya; Dira ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 ni kuwa na jamii yenye afya ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo binafsi na ya Taifa kwa ujumla. Pia sera hiyo inakusudia kutoa huduma muhimu za afya zenye uwiano wa kijiografia, viwango vya ubora unaokubalika, gharama nafuu na zilizo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inakadiriwa kuwa na takriban zahanati zipatazo 4,679, vituo vya afya 481 pamoja na hospitali 219. Zahanati na vituo vya afya ndizo nguzo kuu za huduma za afya ya msingi kwani hutoa huduma za awali kwa Watanzania kati ya 10,000 kwa zahanati na 50,000 kwa kituo cha afya. Hata hivyo, kasi ya ongezeko la idadi ya watu, upungufu wa watumishi wenye sifa, upungufu wa nyenzo, dawa, umbali wa vituo vya kutolea huduma, ubovu wa barabara za vijijini pamoja na tatizo la usafiri wenye uhakika

*NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

ni changamoto kubwa zinazokabili utoaji wa huduma za afya ya msingi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika utoaji wa huduma za afya, sekta binafsi ina mchango mkubwa. Kwa sasa asilimia 40 ya vituo vyote vya huduma za afya nchini, vinamilikiwa na watu binafsi. Changamoto kubwa kwa sasa ni kuwa zaidi ya asilimia 90 ya vituo binafsi vipo mijini na kuacha asilimia kubwa ya Watanzania takribani asilimia 80 inayoishi vijiji ni kukosa huduma muhimu ya afya.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha ni muhimu kuelewa kwa undani dhana ya *all development are local*. Katika muktadha wa Halmashauri zetu pamoja na Serikali za Mitaa kuleta maendeleo kwa wananchi ni lazima yawe kwa watu.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa ni kengele ya pili.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI**  
**ZAMITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba dakika moja.

**SPIKA:** Malizia malizia.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI**  
**ZAMITAA:** Mheshimiwa Spika, uelewa na ufahamu wa mahitaji ya mamlaka ya Serikali za Mitaa na jamii inayoishi hapo na kutoa msaada wa hali na mali ili kuwa na

maendeleo shirikishi, ndio njia pekee itakayohakikisha jamii ya Kitanzania inakuwa na maendeleo endelevu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inaitaka Serikali Kuu kama kweli inataka ustawi na maendeleo ya wananchi (*economic development*) kuzirejeshea Halmashauri zetu uhuru wa kuamua jinsi rasilimali zake zitakavyotumika kama ambavyo lengo la maboresho ya Serikali za Mitaa (*LGRP*) lilivyokuwa likihitaji. Ila kama Serikali inahitaji *economic growth* basi iendelee na utaratibu uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha, ahsante sana. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*. (*Makof!*)

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Raphael Michael. Ahsante kwa hotuba yako. Wakati mwingine huwa najuliza bado sina majibu kwa nini hotuba za Upinzani huwa hazina maoni na ushauri kama zillivo hotuba za Kamati, yaani za Upinzani lazima usome yote ndio uanze kupata kidogo, huwezi ukafungua mahali ukaona hasa wanashauri kitu gani kama ni vitano, sita, ni kitu gani hasa unachoshauri. (*Makof!*)

Ni lazima ufungue, ufungue, ufungue lakini nafikiri siku zijazo, maana hizi ripoti za Kamati na ninyi mnashiriki kuzitengeneza, kwa hiyo, ni vizuri mazuri mkayaiga sio lazima lakini ni ushauri tu wa jumla. (*Makof!*)

**HOTUBA YA MHESHIMIWA JAPHARY RAPHAEL MICHAEL  
(MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA  
UPINZANI BUNGENI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA  
MATUMIZI KATIKA OFISI YA RAIS – TAMISEMI KWA MWAKA  
WA FEDHA 2017/18 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za  
Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

## **I. UTANGULIZI**

- 1. Mheshimiwa Spika,** Napenda kuchukua fursa hii, kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2017/18.
- 2. Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima kubwa naomba kuwashukuru wananchi wote hasa viongozi wangu wa chama wa Jimbo la Moshi Mjini pamoja na viongozi wote wa chama wa Kanda ya Kaskazini kwa ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kuhakikisha majukumu yangu ya kuwashukuru wananchi yanatekelezwa.
- 3. Mheshimiwa Spika,** Niwashukuru waheshimiwa wabunge wenzangu wote kwa ushirikiano walionipa katika maandalizi ya hotuba hii, hasa wale wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Aidha, ni mshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wangu Mhe Joseph Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe kwa ushirikiano wake usio na kipimo katika mchakato mzima wa maandalizi ya Hotuba hii.
- 4. Mheshimiwa Spika,** Mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa familia yangu kwa uvumilivu mkubwa walionao pale ninapokuwa kwenye shughuli za kichama na za kibunge, nasema natambua upweke

wanaokuwa nao kwa mimi kutokuwepo pale ninapohitajika kuwepo.

**5. Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake,Ibara ya 145 na 146, Serikali za Mitaa ni vyombo vyta wananchi ambavyo viro katika ngazi za chini za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vyombo hivi huundwa, huendeshwa, husimamiwa na kuwajibika kwa wananchi wenyewe.

**6. Mheshimiwa Spika**,Katika kipindi kati ya mwaka 1962 na 1972 Serikali za mitaa zilipata mafanikio machache na matatizo kuwa mengi. Majukumu ya ya halmashauri yalionezekwa kama vile usimamizi wa elimu ya msingi, matibabu, barabara na maji.Uwezo wa halimashauri za miji na wilaya katika kutekeleza majukumu yake ulikuwa mdogo sana kutokana na kuwa na vyanzo vichache vyta mapato hivyo kuifanya serikali ione kwamba dhana ya serikali za mitaa haikuwa na tija.

**7. Mheshimiwa Spika**, Mwishoni mwa miaka ya sabini na mwanzoni mwa miaka ya themanini serikali ilirejea dhamira yake ya kuwa na serikali za mitaa zilizo imara ili kutimiza azma ya kupeleka madaraka kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kuzipa Mamlaka ya kukusanya mapato kutokana na vyanzo mbali mbali vyta mapato.

**8. Mheshimiwa Spika**, Vyanzo vyta mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vimeainishwa katika vifungu Na. (6) hadi (9) vyta Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 yaani (The Local Government Finance Act, No. 9 of 1982).Kulingana na Sheria ya Fedha Na. 9 ya mwaka 1982 ya **Serikali za Mitaa** iliyorekebishwa na Sheria ya Fedha Na. 15 ya mwaka 2003 yaani (The Finance Act No. 15 of 2003), Serikali za Mitaa hazitozi kodi ya Mapato. Jukumu hili hufanywa na Mamlaka ya Mapato ya Tanzania yaani (Tanzania Revenue Authorities - TRA) kwa kushirikiana na HAZINA kwa viwango mbalimbali kwa mujibu wa Sheria na kanuni husika.

**II. UHUSIANO KATI YA SERIKALI ZA MITAA NA SERIKALI KUU**

**9. Mheshimiwa Spika,** Serikali Kuu ni chombo ambacho kwa misingi maalum kimepewa mamlaka ya kuendesha utawala wa nchi nzima. Maeneo ya Serikali Kuu yanaanza Taifa, Mkoa, Wilaya na Tarafa. Serikali za Mitaa ni vyombo madhubuti vyta Serikali Kuu katika ujenzi wa utawala bora, demokrasia na kuleta maendeleo nchini. Kufanikiwa kwa Serikali za Mitaa kunategemea zaidi uhusiano na ushirikiano kati yake na Serikali Kuu kwa kujenga mazingira mazuri ya kiutendaji. Ibara ya 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na marekebisho yake inaweka misingi ya uhusiano kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Ili kuwezesha kuwapo na kufanya kazi kwa uhusiano huo, sheria mbalimbali zimetungwa kuhalalisha uhusiano huo. Sheria hizo ni pamoja na:-

**a.** Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Namba 7 ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na sheria Namba 6 ya mwaka 1999;

**b.** Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) Namba 8 ya mwaka 1982 kama ilivyorekebishwa na sheria Namba 6 ya mwaka 1999;

**c.** Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997.

Majukumu ya Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa Kwa mujibu wa kifungu cha 174A cha Sheria Namba 7 ya mwaka 1982, na marekebisho ya sheria namba 13 ya mwaka 2006 kifungu cha 54A cha Sheria Namba 8 ya mwaka 1982, majukumu ya Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

**i.** Kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu na mamlaka yake kwa kutambua uhuru wake kisheria;

- ii. Kubuni na kuweka sera za kitaifa, sheria, kanuni na taratibu kuhusu uendeshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa;
- iii. Kutoa ushauri wa kitaalam;
- iv. Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa sera za kitaifa, sheria, kanuni, taratibu, miongozo na viwango vilivywewekwa kitaifa;
- v. Kutoa ruzuku kwa Serikali za Mitaa;
- vi. Kuendeleza taaluma;
- vii. Kudhibiti mambo ya kisheria na ukaguzi wa fedha na rasilimali za Serikali za Mitaa. Hii inaweza kutekelezwa kwa kutoa mafunzo, kutayarisha taratibu na kanuni mbalimbali na kukusanya takwimu za kitaifa;
- viii. Kuweka mazingira yatakayowezesha mamlaka za serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ipasavyo;
- ix. Kuhakikisha watumishi na Mamlaka za Serikali za Mitaa wanatoa maamuzi na miongozo sahihi wanapotekeleza majukumu yao katika mfumo wa Serikali za Mitaa;
- x. Kufanya mambo mengine yatakayowezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya kisheria na majukumu mengine kwa ufanisi na kwa kuzingatia sheria.

### **III. MADARAKA YA MKUU WA MKOA**

**10. Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 5 (3) cha sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997 kinaelezea wajibu wa Mkuu wa Mkoa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa ni kuziwezesha na kuzijengea mazingira ya kutekeleza majukumu yao kisheria. Dhana hii

ya uhuru wa mamlaka za Serikali za Mitaa inaegemea katika sharti kuwa, mamlaka hizo zitakuwa zinajиendesha kisheria.

#### **IV. MADARAKA YA MKUU WA WILAYA**

**11. Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tawala za Mikoa Namba 19 ya mwaka 1997, kinampa Mkuu wa Wilaya majukumu ya kuziwezesha na kuzijengea mazingira mazuri mamlaka za Serikali za Mitaa zilizomo ndani ya eneo lake ili ziweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Aidha, kifungu cha 78A cha sheria namba 8 ya mwaka 1982, kama vile ilivyo kwa Mkuu wa Mkoa, vimetoa uwezo kwa Mkuu wa Wilaya kuchunguza uhalali wa vitendo na maamuzi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa katika eneo lake.

**12. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka Waziri Mwenye dhamana kuwaelekeza wakuu wa Mikoa na wakuu wa Wilaya kufanya kazi kwa kuzingatia mipaka yao ya kisheria. Wakuu wa Mikoa na wilaya waepuke kufanya maamuzi yanayorudisha nyuma utekelezaji wa majukumu ya madiwani na watendaji wa halmashauri nchini.

**13. Mheshimiwa Spika,** Ni muhimu kuwe na semina elekezi kwa Wakuu wa Mikoa, wakuu wa wilaya, madiwani na watendaji wa halimashauri ili kujua namna bora ya kutekeleza majukumu yao kwa ajili ya kuleta mahusiano mazuri ya kikazi yenye tija na ufanisi

Kambi Rasmi ya Upinzani haiamini katika tabia iliyojengeka sasa ya wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya kuwanyanya watumishi wa halmashauri kinyume cha sheria za Tanzania za utumishi wa Umma.

#### **V. MABORESHO YA SERIKALI ZA MITAA**

**14. Mheshimiwa Spika,** Serikali za Mitaa huwawezesha wananchi kuwa na sauti katika maamuzi mbalimbali ama kwa kushiriki moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi wao katika shughuli za maendeleo na utawala. Serikali za Mitaa zinatokana na dhana ya madaraka kwa

umma. Dhana na madhumuni ya madaraka kwa umma ni kuwapa wananchi (wanaume na wanawake) wote uwezo na fursa sawa ya kushiriki kikamilifu katika masuala ya siasa, uchumi na utawala katika nchi yao. Kwa mujibu wa Ibara ya 8 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali inapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi.

**15. Mheshimiwa Spika**, Mwaka 1998, Sera ya Taifa ya Uobreshaji wa Serikali za Mitaa '**Policy Paper on Local Government Reform 1998**' iliandaliwa na kuweka bayana umuhimu wa KUGATUA madaraka ya Serikali Kuu kwenda SERIKALI ZA MITAA (decentralisation by devolution au kwa jina lake maarufu D by D ).

**16. Mheshimiwa Spika**, Chini ya Sera hili, Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa (Local Government Reform Programme- LGRP) ilianzishwa kwa dhamira ya kuziimarishe Serikali za Mitaa ili kusukuma mbele utekelezaji wa Mikakati ya Kupunguza Umaskini yaani Poverty Reduction Strategy na baadaye MKUKUTA, na vile vile kuhakikisha kuwa Halmshauri za Miji na Wilaya zinatoa huduma bora kwa wananchi wake hususan huduma za Afya, Maji, Elimu, na huduma za ughani n.k. (angalia mpango wa "LGRP Medium Term Plan and Budget July 2005 – June 2008" OR – TAMISEMI: Juni 2005 )

**17. Mheshimiwa Spika**, Malengo maalum ya Programu hiyo yalikuwa ni:

i. Kugatua madaraka ya Serikali kuu na kuyapeleka kwenye Serikali za Mitaa (LGAs) ili ziwe na madaraka kamili (to create more autonomous Local Government Authorities), kupitia 'political decentralisation'

ii. kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kupitia watumishi wa umma wanaowajibika kwa Serikali za Mitaa zenyewe (*'de-linking of local authority staff from the respective line-ministries, making them accountable to the LGA who will be their employer, fully'*

*responsible for all human resource management'-  
Administrative Decentralisation)*

iii. Kuziwezesha Halmashauri kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake na kuwa na mfumo wa mgawanyo wa mapato kati ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa (financial decentralisation)

iv. Kwa umuhimu wa kipekee maboresha pia yalikuwa na dhamira kuu ya kubadilisha mfumo wa mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kutoka mfumo wa Serikali Kuu wa kuwa na '**control role**' na hivyo kuwa na wajibu wa kutunga sera na kuweka vigezo vya ubora wa huduma; na kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza sera kwa kuwajengea uwezo na kuwapatia raslimali fedha na utaalamu ili ziweze kutoa huduma inayolingana na ubora ulliowekwa na kukubalika.

**18. Mheshimiwa Spika**, Ikumbukwe kuwa, Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ilitekelezwa sambamba na programmu nyingine za uboreshaji wa Sekta za Umma na Sekta Binafsi. Moja kati ya nyanja muhimu za uboreshaji wa Sekta ya Umma ni uboreshaji wa Utumishi wa Umma yaani Civil Service Reform Programme (CSRP 1998), ambayo baadaye iliboreshwa na kutengeneza programu maalum ya miaka kumi na mitano Public Service Reform Programme (2000 -2015) yenye malengo makuu yafuatayo:

i. Kuboresha utendaji

ii. Kuweka tabia ya kufuutilia, kupima na kutathmini utendaji katika utumishi wa umma na utoaji wa huduma za umma

iii. Kuweka mifumo ya kuinua kiwango cha ubora wa huduma (quility improvement cycles).

**19. Mheshimiwa Spika**, Maboresho hayo yalidhamiria kuimarisha utawala na utoaji huduma. mambo ambayo ni muhimu sana katika kuiondoa nchi yetu kwenye

umasikini na pia kufikia vigezo vya mpango wa Maendeleo ya Millenia wa kupunguza umasikini wa kipato na nchi yetu kuwa na uchumi wa kati.

**20. Mheshimiwa Spika**, Awamu za kwanza za Maboresho hayo ya Serikali ya Mitaa yalichukua miaka kumi, kuanzia mwaka 1998 -2008, katika kadhia hiyo sera ya D by D (Decentralization by Devolution) ndiyo ilipata umaarufu sana. Kwa masikitiko makubwa ni kwamba uwekezaji wote huo uliofanywa na Serikali za awamu ya tatu na awamu ya nne umekuwa ni kazi bure, kwa vile katika uhalisia madaraka yamerudishwa Serikali Kuu.

**21. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya awamu ya tano ambayo wananchi walikuwa na matumaini makubwa kwayo katika kugatua madaraka kwa lengo kukuza Demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi katika mipango yao ya maendeleo na utawala bora inafanya kinyume kabisa na matarajio ya wananchi.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaanini ugatuaji wa madaraka ni jambo la msingi sana katika kuleta ustawi wa maendeleo ya watu hivyo inaishauri serikali ya awamu ya tano isimamie na kutekeleza dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa vitendo.

#### **VI. HALMASHAURI KUKOSA MAMLAKA KAMILI YANAYOLINGANA NA DHAMIRA HALISI YA KUANZISHWA SERIKALI ZA MITAA**

**22. Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli kwamba Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa ndio msimamizi mkuu wa Serikali za Mitaa. Kwa njia hii Serikali za Mitaa zinawajibika moja kwa moja kwa wizara hii kwa chochote kile kinachofanywa na Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Majiji.

Kwa lolote lile Waziri Mwenye dhamana anaweza kuamua kuivunja halmashauri ya wilaya, manispaa au jiji na kuteua Tume ya kusimamia uendeshaji wa halmashauri ya

wilaya, manispaa au jiji husika. Aidha, waziri ana mamlaka ya kumhamisha au kumsimamisha kazi mtendaji mkuu au Mkurugenzi wa Halmashauri. Mfumo mzima wa kuwawajibisha viongozi wa kisiasa katika ngazi za halmashauri nao unaingiliwa sana na maamuzi ya Serikali kuu. Mambo haya yote kwa ujumla wake ndiyo yanaondoa Mamlaka kamili ("autonomy") ya Serikali za Mitaa na kufanya maboresho ya miaka kumi na sera nzima ya D by D kuwa ni bure na ni hasara kwa walipa kodi wa Tanzania.

**23. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ni kuwa na uwezo wa kuajiri na kufukuza (*hire and fire*) kukosa mamlaka hayo maana yake ni kiini macho cha Mamlaka hivyo basi Serikali za mitaa sio Serikali kamili kama inavyotamkwa ndani ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977.

**24. Mheshimiwa Spika**, Serikali za Mitaa zilikuwa na sheria yake ya kuwa na uwezo wa kuajiri na kufukuza watumishi wake (*hire and fire*) *ambayo* ni sheria namba 10 ya mwaka 1982 (The Local Government Servise Act, No.10 of 1982), Lakini Serikali kuu kwa kufikiri kuwa Halmashauri zitakuwa na nguvu za kuweza kuwatumikia watanzania kwa kiwango cha juu na kuweza kuwaondolea umasikini, mwaka 2002 iliifuta sheria hiyo na kutunga sheria ya Utumishi wa Umma namba 8 (The Public Service Act. No.8 of 2002. Sheria hii ilipoka madaraka ya Halmashauri kuhusu utumishi na kurejesha madaraka hayo chini ya Ofisi ya Rais.

**25. Mheshimiwa Spika**, Kuzipunguzia mamlaka halmashauri ya kusimamia watumishi wake hasa Mkurugenzi na Wakuu wa Idara kunasababisha ubunifu wa watumishi wa halmashauri kuwa wa chini sana kwa vile wamekuwa wakiendesha halmashauri kwa mipango ama ya zimamoto au maagizo na miongozo kutoka ngazi ya Serikali Kuu, bila kujali hali halisi ndani ya halmashauri zao.

Aidha, nidhamu ya Wakurugenzi na watumishi wa halimashauri kwa Madiwani ambao ndio wenyewe halmashauri kwa niaba ya wananchi imekuwa ya chini mno hivyo kufanya maagizo mengi ya mabaraza ya madiwani katika

halmashauri kutotekelizwa kwa kuwa Wakurugenzi na manejimenti za halmashauri wanaweza wakaamua kupuuza maagizo hayo.

**26. Mheshimiwa Spika**, Baadhi ya wakuu wa Mikoa na wakuu wa Wilaya wamekuwa tena sio washauri na waangalizi wa mienendo ya utendaji wa halmashauri bali wamekuwa wafanya maazimio ya shughuli za kila siku za halmashauri badala kuheshimu maazimio ya vikao vya kisheria vya halmashauri zetu.

**27. Mheshimiwa Spika**, Na kwa vile wao wana kofia ya kumwakilisha Mh Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wamekuwa wakitumia mamlaka yao kuwalazimisha Wakurugenzi kutekeleza maagizo yao na kupuuza maazimio ya Baraza la Madiwani, jambo ambalo limekuwa likileta milutano mikubwa kati ya madiwani na wakurugenzi katika halmashauri hapa nchini hivyo kudumaza maendeleo ya watu wetu.

**28. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri serikali kuangalia upya sheria hii ya utumishi na ajira katika serikali za mitaa ili kuwe na utaratibu wa ajira za Wakurugenzi na wakuu wa idara ambao mchakato wake utaanzia kwenye vikao vya kisheria vya halmashauri hata kama itakuwa ni kutoa mapendekezo kwa Waziri mwenye dhamana kwa watu wenye sifa watakaokuwa wameomba ajira hizo za ukurugenzi na ukuu wa idara ili waziri atue kutokana na mapendekezo ya halmashauri husika.Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba kwa kuzipa Mamlaka Halmashauri kutoa mapendekezo ya ajira za Wakurugenzi na wakuu wa Idara kuteta nidhamu ya uwajibikaji katika halmashauri nchini.

## **VII. UWEZO WA HALIMSHAURI KUKOPA AU KUINGIA UBIA NA SEKTA BINAFSI-PRIVATE PUBLIC PARTNERSHIP(PPP)**

**29. Mheshimiwa Spika**, Sheria ya fedha ya Serikali za mitaa ya mwaka 1982 inaziruhusu halmashauri kukopa katika taasisi za fedha ili kuwekeza katika miradi ya maendeleo.

Jambo la kusikitisha ni pale ambapo Waziri mwenye dhamana anapoamua kuinyima kwa makusudi kibali cha kukopa halmashauri ambayo imetimiza vigezo vyote vya kukopa katika taasisi za fedha ili kuwekeza katika miradi ya maendeleo ambayo inajиendesha yenewe kwa faida.

**30. Mheshimiwa Spika**, Kuna kila dalili kwamba kuna ubaguzi wa kisasa unaofanywa ama na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI au Serikali nzima ya awamu ya tano kwa kuzibagua Halimashauri zinazoongozwa na vyama vya upinzani kama vile za jiji la Arusha, jiji la Mbeya, Manispaa ya Iringa, Manispaa ya Moshi, n.k ili kuzifanya zishindwe kutimiza wajibu wake wa kuwaletea wananchi maendeleo na hatimaye wananchi wapoteze imani na vyama vya upinzani.

**31. Mheshimiwa Spika**, Mfano mzuri ni uamuzi wa Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI kuamua kwa makusudi ama kuchelewesha au kukataa kutoa kibali cha kukopa kwa Manispaa ya Moshi kwa mradi wa ujenzi wa stendi ya kisasa ya mabasi ya endayo mikoani (modern Terminal Bus Stand) ambapo Benki ya Rasilimali ya Tanzania (TIB) iko tayari kuwekeza kwenye mradi huo kwa kutoa zaidi ya bilioni ishirini kwa mfumo wa ‘Design Build, Operate and Transfer’ (BOT). Mradi huo ambao kuufanyia upembizi na uchambuzi yakinifu umetumia takribani milioni mia Tatu fedha ya walipa kodi na ikathibitika kwamba ni wa faida kiuchumi unanyimwa kibali ili kuwakomoa wananchi wa Manispaa ya Moshi.

**32. Mheshimiwa Spika**, Imani ya kwamba kuna kila dalili ya ubaguzi wa kisasa unaofanywa na ama na waziri mwenye dhamana na TAMISEMI au na Serikali kwa ujumla wake ni kutokana na Waziri huyo huyo kutoa kibali cha miradi ya aina hyo kwa manispaa ya Morogoro na jiji la Tanga. Huo ni upendeleo mbaya sana na matumizi mabaya ya madaraka (double standards) yanayofanywa na Waziri mwenye dhamana na TAMISEMI.

**33. Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli kwamba Karibu miji yote ambayo inaongoza kwa kuwa walipakodi wazuri

na hivyo kuchangia vyema katika pato la Taifa, kwa mujibu wa taarifa za Benki Kuu, miji hiyo inaongozwa na vyama tofauti na chama Tawala, na miji hiyo ukiondoa jiji la mwanza(GDP 4.09 trillion) ipo katika mikoa ya Dar es Salaam (GDP 7.5 trillion), Mbeya (GDP3.2 trillion), Arusha (GDP 2.1 trillion), Tanga (GDP 2.09 trillion), na Kilimanjaro (GDP 2.03 trillion). Hivyo kwa msingi huo, sio sahihi kabisa kuibagua miji hiyo katika kuigawia keki ya Taifa hasa pale wawakilishi wa wananchi wanapotaka kutumia fursa za kiuchumi walizo nazo ili waharakishe maendeleo ya watu wao.

**34. Mheshimiwa Spika**, Serikali lazima itambue kwamba ina wajibu wa kuwatumikia wananchi wote bila ubaguzi wowote kwa vile watanzania wote kwa namna moja ama nyngine wanalipa kodi hivyo serikali kuwapelekea maendeleo sio hisani bali ni wajibu.Aidha, uamuzi wa uchaguzi wa vlongozi wanaowakilisha wananchi ni wa kikatiba ambao tumejipangia wenyewe kama Taifa. Hivyo wananchi wasiadhibiwe kwa vile wamechagua wawakilishi kuititia vyama vya upinzani kwa kuwa wamefanya uamuzi halali wa kikatiba.

**35. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kurejea kwenye adhima yake ya maboresho ya Serikali za Mitaa ili kuzifanya halimashauri zijitegemee kwa kiwango kisichopungua asilimia 35 kwa kubuni mlradi ya uwekezaji na kutafuta vyanzo vipyta vya mapato vlsivyo na kero kwa wananchi. Pia Waziri mwenye dhamana ya TAMISEMI awatumikie watanzania wote bila ubaguzi wa kisiaza wala kikanda.

**36. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba chanzo kikubwa cha matatizo ya mapato yanazozikabili halmashauri zote kwa ujumla ni kutokana na udhibiti unaofanywa na Serikali Kuu kwa Serikali za Mitaa. Hivyo basi ili kurekebisha kasoro hizo ni kuifanyia marejeo sheria za fedha hasa kifungu cha 60 kinachohusu halimashauri kukopa, na kuondoa sharti la ridhaa ya ya Waziri mwenye dhamana ili halmashauri ziweze kukopa kwenye taasisi mbali mbali za fedha

**VIII. JUKUMU LA UTOAJI HUDUMA ZA JAMII KATIKA  
MANISPAA NA MAJII**

**37. Mheshimiwa Spika**, Manispaa na majii makubwa Duniani yanakabiliwa na Changamoto za kuongezeka kwa wakaazi wake,jambo hilo limesababisha uwepo wa mahitaji makubwa ya huduma za kijamii na za kiuchumi kama vile Afya,Elimu, Maji, Huduma za uokozi,Usalama wa raia na Huduma za usafiri.

**38. Mheshimiwa Spika**, Baada ya kupitia nyaraka mbali mbali zinazosimamia kazi zinazofanywa na Mameya wa Manispaa na majii mbali mbali Duniani kuhusiana na utoaji wa Huduma za kijamii na za kiuchumi kwa wakazi wa Majiji na Manispaa imeonekana kwamba Mameya na Kamati zao ndio wenye Mamlaka ya mwisho ya kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo ihusuyo manispaa zao na majii yao ikiwemo wao kuwa maafisa masuhuli na watendaji wakuu (accounting officer and executive mayors ) wa Manispaa zao na majii yao.

**39. Mheshimiwa Spika**, Dhamira ya Kambi rasimi ya upinzani kwenye hoja hii ni kuishauri serikali namna bora ya kusimamia huduma ya usafiri katika majii hususani usafiri wa Umma, Uendeshajl wake na miundo mbinu yake kama mabasi madogo na makubwa ya mwendo kasi,tax,Pikipiki, Treni na vivuko katika majii husika ndani ya nchi ya Tanzania. Lengo kuu likiwa ni kuangalia namna ambavyo sheria namba 8 ya mwaka 1982 inayounda mamlaka za miji,Manispaa na Majiji inavyoweza kufanyiwa marekebisho ili uendeshajl na umiliki wa miundombinu ya usafirishajji wa abiria,matengenezo na ukarabati wa miundombinu yawe jukumu la msingi la uongozi wa Majiji.

**40. Mheshimiwa Spika**, Majiji yaliyoangaliwa kama ya mfano ni;

1) Jiji la London ambalo limeanza mamlaka inayoitwa 'Great London Authority'ambayo ipo chini ya Meya wa

London na ina jukumu la kusimamia Mfumo mzima wa usafiri wa jiji la London.

2) Jiji la Cape Town ambalo jukumula usafiri wa abiria lipo chini ya Ofisi ya Meya ambapo kimeanzishwa chambo kinachoitwa Transport for Cape Town(TCT)ambacho kinaendesha mrdl unaitwa 'MyCITY bus service'. Chombo hiki kina mamlaka ya ya kupanga,kusimamia na kuratibu shughuli zote za usafiri katika jiji la Cape Town ikiwa ni Pamoja kutengeneza na kukarabati miundo mbinu ya usafiri yaani planning costing, contracting, regulating, monitoring, evaluating, communicating, managing, and maintaining the city of Cape Town's Transport infrastructure, systems,operation ,facilities and network'.

3) Jiji la Johannesburg ambalo waliunda chombo kinachoitwa Rea VAYA chenyé maana ya the City of Johannesburg's revolutionary Bus Rapid Transit System kikiwa na lengo la kutoa usafiri wa haraka,salama na unaohimlika kwa Wananchi yaani 'Offering fast, safe and affordable public transport on a network of bus routes across Johannesburg'

**41. Mheshimiwa Spika**, imetulazimu kuonyesha jinsi majjii makubwa yanavyotoa huduma kwa wananchi wake na jinsi Ofisi za Meya na kamatl zao zinavyofanya kazi.

**42. Mheshimiwa Spika**, kwa Muktadha huo Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kitendo cha serikali kuingia mikataba ya mikopo kwa ajili ya jiji la Dar es salaam ili Kujenga miundo mbinu ya usafiri ni kuifedhesha hadhi na nguvu ya Meya wa jiji lakini pia ni kuibebesha mizigo mikubwa serikali kuu kwa majukumu ambayo ni ya Halimashauri ya jiji la Dar es salaam chini ya Meya wa jiji na Mameya wenzake wa manispaa za Dar es salaam ambapo serikali kuu ingekuwa mdhamini tu(Guarantor).

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kuishauri serikali kuona namna ya kufanya marejeo ya sheria namba 8 ya mwaka 1982 ili iweze kuwafanya Mameya wa Manispaa

na majiji wawe Mameya watendaji (executive Mayors) wenye Mamlaka kamili na ikiwezekana sheria itamke kwamba watapigwiwa kura na wananchi wote wa eneo husika ili wawe na wigo mpana wa kuwahudumia wananchi wote kwenye maeneo yao ya utawala.

#### **IX. MUINGILIANO WA MAAGIZO NA MAELEKEZO KATIKA HALIMASHAURI**

**43. Mheshimiwa Spika,** Katika muendelezo huo wa kupoka madaraka ya Serikali za Mitaa, katika marekebisho ya sheria mbalimbali za Serikali za Mitaa ya mwaka 2006, inaonesha kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri ambao ni wateule wa Serikali Kuu wanalazimika kupeleka taarifa za utekelezaji kwa Mkuu wa wilaya na Mkuu wa Mkoa ambao ni sehemu ya Serikali Kuu, rejea kifungu cha 9(b) cha marekebisho ya sheria mbalimbali za Serikali za mitaa kinachorekebisha kifungu cha 174 cha sheria Mama ya Local Government District Authorities Act.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaona huu ni udhibiti badala ya ushauri ili kudhibiti taarifa za Serikali za mitaa zinazotakiwa kupelekwa Serikali Kuu.

**44. Mheshimiwa Spika,** Ni ukweli kwamba marekebisho hayo yaliyofanyika badala ya kutoa madaraka zaidi kwa Serikali za Mitaa ndiyo yanazidisha kupokwa madaraka kwa Serikali za Mitaa. Hii ni hatari sana na inaonyesha kwamba marekebisho hayo yalikuwa na agenda ya siri kwani ilionekana wazi kwamba Vyama shindani na Chama Tawala vinaweza kushinda uchaguzi katika ngazi za halmashauri na kuendesha Halmashauri. Hivyo marekebisho hayo yalifanyika kwa nia ovu ya kuendelea kudhibiti halmashauri na kutawala kwa mlango wa nyuma. Ni muda mwafaka sasa kurekebisha mfumo wetu wa utawala wa Serikali kuu kutoka kwenye udhibiti na kuwa usaidizi na uangalizi zaidi.

**45. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri serikali kwamba kama nchi hii inataka Kufikia

maendeleo ya haraka ni lazima iondoe huu muingiliano wa maagizo na maekekezo kwenye halimashauri za nchi hii ambapo kwa upande mmoja kuna Madiwani na upande wa pili kuna wakuu wa mikoa ,wilaya na Waziri mwenye dhamana na hata viongozi wa chama tawala wote wakitoa maagizo na Maelekezo kwa Mkurugenzi na manejimenti yake ya halimashauri jambo linalowakwaza sana wakurugenzi na watumishi wengine kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

## X. KODI YA MAJENGO (PROPERT TAX)

**46. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa halmashauri hapa nchini zimekuwa zikikusanya mapato kwa ajili ya kuendesha miradi yake ya maendeleo na shughuli nydingine za kawaida kutoka kwenye vyando vyake vya mapato kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Halmashauri (Local Government finance Act, 1982) haukuwa uamuzi sahihi kutunga sheria ya kuondoa chanzo cha mapato cha kodi ya majengo kutoka katika halimashauri nchini.

**47. Mheshimiwa Spika**, Kufutwa kwa kifungu kilichokwuwa kinazipa Halmashauri jukumu la kukadiria na kukusanya kodi za majengo na kulihamishia TRA kupitia sheria ya fedha ya mwaka 2016, kifungu cha 38 baada ya kufanya marekebisho kwa kuvifuta vifungu vya 31A na 31B vya sheria ya fedha ya Serikali ya Mitaa sura 290 kumeziyumbisha sana halimashauri katika kutekeleza majukumu yake kutohana na ukweli kwamba chanzo cha kodi ya majengo kilikuwa ni mojawapo ya chanzo kikubwa cha mapato hususani katika Manispaa na majiji hapa nchini.

**48. Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Serikali inaonyesha kodi ya Majengo iliyokusanywa ni shilingi milioni 4,762.37 kati ya milioni 29,004 sawa na asillmia 17.4 tu. Sababu ya makusanyo hayo madogo imeelezwa kuwa ni pamoja na kutokamilisha maandalizi ya yatakayowezesha ukusanyaji ikiwa ni pamoja na kuandaa sheria na kanuni za ukusanyaji ,kutengeneza Mfumo wa ukusanyaji wa kodi ,kuunda kitengo ,kuweka wafanyakazi na vitendea kazi.

**49. Mheshimiwa Spika**, Halmashauri zote kwa muda wa miaka zaidi ya 30 ya uhai wa serikali za mitaa zimeimarisha miundombinu ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato na rasilimali watu ambapo ilikuwa inahitaji marekebisho ya kawaida kuongeza ufanisi hususani kuziruhusu halimashauri ziajiri watumishi zaidi kwenye idara za fedha za halimashauri.

Maoni ya wabunge wengi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwenye hotuba ya bajeti mwaka 2016/17 yalikuwa ni kutoondo chaanzo hlcho cha kodi ya majengo katika halmashauri lakini serikali ikakataa ushauri huo kwa msisitizo kwamba TRA ina uwezo Wa kukusanya.

Serikali illiahidi kwamba baada ya kukusanya itarejesha Fedha hizo kwenye halmashauri jambo ambalo halijafanyika mpaka sasa kwa halmashauri nyingi nchini.

**50. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kama kweli tunahitaji kuendelea na Sera ya D by D ambayo ina lengo la kutoa mamlaka kamili kwa Serikali za mitaa ni lazima serikali ipitie upya sheria ya Property tax ili jukumu la makusanyo ya kodi hiyo liendelee kufanywa na halimashauri kwavile ukweli uko wazi kwamba TRA wanajukumu kubwa sana la kupanua wigo wa walipa kodi na jukumu kubwa la kuvisimamia vyanzo vyake ambavyo bado havijakusanya kwa ufanisi.

## XI. ANWANI ZA MAKAZI NA POSTIKODI KATIKA MIJI YA TANZANIA

**51. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na uchukuzi-Sekta ya mawasiliano imefanya kazi kubwa ya Kuandaa Mfumo wa Anwani za makazi na Postikodi na kufanyia majariblo baadhi ya maeneo katika halimashauri hapa nchini,

Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwenye sekta ya mawasiliano ambayo ndio inaratibu program hii na pla kuzielekeza halimashauri kutenga fedha kwenye bajeti zake ili mradii huu wa Anwani za makazi

na Postikodi ukamilike kwa haraka kwa lengo la kurahisisha mawasiliano na ukusanyaji wa mapato kwa Serikali kuu na seriSerikali za mitaa.

## **XII. WATUMISHI HEWA TAMISEMI**

**52. Mheshimiwa Spika**, Kumekuwepo na zaoezi linaloendeshwa na Serikali kuu la kubaini watumishi ambaao wanapokea fedha bila ya kufanya kazi kwa maana rahisi na illyozoleka wanaitwa watumishi hewa. Zoezi hili la kuhakiki watumishi hewa limepelekea kusitishwa kwa ajira mpya.

**53. Mheshimiwa Spika**, Ni ukweli kwamba vyeo vya RAS, DAS na DED sio nafasi za kisasa na mtumishi kufikia nafasi hizo ni dhahiri kwamba amepitia ngazi mbalimbali katika utumishi wa Umma. Ngazi hizo huendana na marupurupu na mshahara, na ni ukweli pia mtumishi katika nafasi hiyo akiondolewa kwa mujibu wa sheria haina maana kwamba na mshahara wake unaondolewa.

Nia ya serikali ya awamu ya tano ni kubana matumizi hivyo Ungetegemea mabadiliko yaliyofanywa ya Makatibu Tawala wa mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halimashauri ambaao wote ni viongozi wa kitaaluma yazingatie nia hiyo ya kubana matumizi badala ya kutengeneza watumishi hewa ambaao wanalitia taifa hasara kubwa.

Kwa mfano kati ya Wakurugenzi 184 wa Halimashauri hapa nchini, wakurugenzi 120 wa zamani hawakuteuliwa kwa nafasi hizo katika serikali ya awamu ya tano ambapo hata wale wapya walio teuliwa walitoka nje ya mfumo wa Utumishi wa Umma wengi wao wakiwa ni makada wa CCM. Baada ya kutenguliwa kwa wakurugenzi hao 120 kutoka halimashauri mbali mbali nchini walielekezwa kuhudhuria kwa Makatibu Tawala wa Mikoa waliiyotoka kwa ajili ya kupangiwa kazi.

Ni zaidi ya Mwaka mmoja sasa Wakurugenzi hawa takribani wote wanahudhuria kwa Makatibu Tawala wa

Mikoa ambapo kimsingi hawana kazi za kufanya kwa kuwa ikama ya watumishi haionyeshi nafasi zao katika ngazi ya Katibu Tawala wa Mkoa.

Ikumbukwe kwamba Wakurugenzi hawa bado wanalipwa Mishahara yao pamoja na stahiki zingine za kiutumishi kama Nyumba, Umeme, simu , matibabu, n.k. Wastani wa mshahara wa Mkurugenzi ni Tsh, 3,820,000 mpaka Tsh,4,000,000kwa mwezi hivyo Malipo kwa wakurugenzi 120 ni takribani Tsh ,480,000,000 kwa mwezi na hivyo kwa mwaka ni takribani Tsh , 5,760,000,000.

Tafsiri sahihi ya jambo hili linaloendea ni kuwepo kwa Double' Payment' ya Wakurugenzi wa Halmashauri na Makatibu Tawala wa zamani waliokuwa wameshafikia ngazi hizo za madaraka na Wale wapya ambao ndio walioteuliwa.

Aidha Serikali inaweza ikawa imejiingiza katika Ubadhirifu kwa matumizi ya zaidi ya Shilingi bilioni 5.76 kinyume cha fedha iliypitishwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kutokana na ikama ya Wakurugenzi wa hapa nchini.

**54. Mheshimiwa Spika**,Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa majibu sahihi juu ya sintofahamu hiyo ya waliokuwa Wakurugenzi wa Halimashauri,Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya ambao bado wanapokea Mishahara na stahiki zingine za madaraka kwa nafasi ambazo walishaondolewa.

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na maumivu ya kisaikolojia (psychological toucher) waliyopata wakurugenzi wa zamani kutokana na Chuki,Ubaguzi na matumizi mabaya ya madaraka ya Mamlaka za uteuzi yaliyosababishwa na Matokeo ya Uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 ambapo maeneo ambayo upinzani ulishinda Wakurugenzi wake hawakupata uteuzi kwa nafasi hizo kwa serikali hii ya awamu ya tano kwa kisingizio kwamba hawajakisaidia chama cha mapinduzi kupora ushindi halali Wa wapinzani.

**55. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali ya awamu ya tano ijiisahihishe ili ilsije ikiwafanya wananchi waamini kwamba Serikali ya Chama cha mapinduzi inahalisha vitendo vya wasimamizi wa Uchaguzi kuharibu uchaguzi Kwa kutangaza matokeo batili bila kuelewa kwamba vitendo hivyo vinahatarisha amani na utulivu wa nchi ya Tanzania. Na kwa maana hiyo kwa Serikali ya CCM ni heshima kwa msimamizi wa Uchaguzi kutotenda haki alioapa kuisimamia kwa mujibu wa Katiba ya nchi kwa kutumia vitabu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu huku akilipwa fedha za Walipa kodi wa Tanzania.

### XIII. TAARIFA YA LAAC

**56. Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ya mitaa kama ilivyofanyia uchambuzi Taarifa ya Mdhilbiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/14 na mwaka 2014/15 imeonesha maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za serikali za mitaa kama ifuatavyo:

- a) Manunuzi yasiyozingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011,
- b) Kutotekeleza Mapendekezo ya Kamati kwa kipindi cha nyuma na kutojibu Hoja za Ukaguzi za Mdhilbiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa wakati, na
- c) Usimamizi mbovu wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unaopelekea kuwepo kwa Miradi ya Maendeleo isiyo kamilika kwa muda mrefu, miradi inayokamilika lakini haitumiki kama ilivyokusudiwa, na baadhi ya miradi kukamilika ikiwa katika ubora wa hali ya chini kinyume na matakwa ya mkataba.

**57. Mheshimiwa Spika**, Maeneo mengine yenye matatizo sugu ni pamoja na:

- a) Baadhi ya Halmashauri kutochangia kabisa na nyingine kutochangia kikamilifu na kwa wakati, asilimia kumi

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

(10%) ya fedha kutoka katika mapato ya vyanzo vya ndani (own sources revenue) kwa ajili ya Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake na Vijana,

b) Baadhi ya Halmashauri kutokupeleka kabisa na nyingine kutopeleka kikamilifu asilimia ishirini (20%) ya ruzuku inayopokelewa kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya Mamlaka za Chini (Vijiji na Serikali za Mitaa);

c) Uzembe katika ukusanyaji wa Mapato ya Ndani ya Halmashauri na upotevu usio na maeleo ya kuridhisha wa Vitabu vya Wazi vya kukusanya mapato;

d) Fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kuchelewa kutolewa na Hazina au kutotolewa kabisa;

e) Mfumo dhaifu wa udhibiti wa ndani (weak internal control system);

f) Watumishi kukaimu Nafasi zao bila kuthibitishwa kwa muda mrefu; na

g) Kubadili matumizi ya fedha kinyume na bajeti kwa kutumia kivuli cha maagizo kutoka ngazi za juu.

**58. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri serikali kwamba panahitajika jitihada za ziada katika kuboresha matumizi ya fedha za umma na kuzingatia sheria ya fedha na manunuzi.

**XIV. HATI ZINAZOTOLEWA BAADA YA KUFANYIKA KWA UKAGUZI WA MAHESABU**

**59. Mheshimiwa Spika**, Hati zinazotolewa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali mara nyingi ni kuonesha ni jinsi gani fedha zilivyotumika. Hati zinazoridhisha, Hati zenyeh shaka, Hati zisizoridhisha na Hati Mbaya.

**60. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba mbali ya juhudii nyingi zinazofanywa na

Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na matumizi makubwa na mabaya ukweli ni kwamba mara nyingi ukaguzi huo unafanyaika wakati tayari fedha zimekwishatumiaka.

**61. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani ina imani kwamba kitengo cha ukaguzi wa ndani kikiimashwa ni dhahiri ndicho kitakachosaidia kuzuia wizi badala ya kutafuta jinsi fedha zilivyoibwa.

Aidha itakuwa vizuri sana kama wakaguzi wa ndani watakuwa wanahamishwa vituo vyao vya kazi mara kwa mara badala ya kuwa katika kituo kimoja kwa muda mrefu kwani jambo hilo linatengeza mahusiano ya karibu sana na Maafisa masuhuli na wasaidizi wao jambo ambalo linahatarisha umakini katika usimamizi wa raslimali za hallmashauri.

#### **XV. UTEKELEZAJI WA ELIMU YA MSINGI NA SEKONDARI**

**62. Mheshimiwa Spika**, Tamisemi ndio wasimamizi wakuu wa elimu ya msingi na elimu ya sekondari hapa nchini, lakini watoa miongozo ya jinsi ya kuendesha elimu hiyo ni serikali kuu. Kwa maana hiyo mamlaka inayotoa leseni na vibali vya uanzishwaji wa shule ni Serikali kuu.

**63. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba matatizo wanayokumbana nayo Tamisemi kuhusu uendeshaji wa elimu katika ngazi hiyo chimbuko lake ni Serikali kuu. Tunasema hivyo kwa sababu, shule zinapewa vipi vibali vya kutoa elimu kwa wanafunzi bila ya kuwa na vyoo, madarasa na madawati, viwanja vya michezo n.k? Kwa kuwa shule hizo zinamilikiwa na Halmashauri zetu hivyo ni jukumu la msingi la halmashauri hizo kuweka miundombinu tajwa hapo juu ili kukidhi matakwa ya usajili wa shule hizo. Hivi ni kwa nini shule binafsi hazina tatizo la vyoo, madarasa, madawati na viwanja vya michezo?

**64. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya awamu ya tano imeazimia kutoa/kutekeleza dhana ya elimu bure kwa elimu ya msingi na sekondari, pamoja na dhana hiyo hakuna ufanuzi wa kutosha au unaoelewaka. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali:-

**Kwanza**, kuweka wazi kwa umma wa Tanzania vipengele vyote ambavyo havitachangiwa na wananchi ili kuondoa mkanganyiko uliopo na kuwezesha bajeti za ukweli kuandaliwa.

**Pili**, ili kuwezesha upatikanaji wa elimu bora vijiji na mijini katika ngazi ya msingi na sekondari, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kupeleka bajeti kamili kwa ajili ya kujenga shule zilizokamilika, yaani pasiwe na shule inayojengwa bila kukamilisha darasa, sambamba na uwiano wa madawati na vyoo vinavyoendana na idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa.

**Tatu**, Kwa kuwa Serikali imeweke vigezo/viwango (**standards**) stahili kwa ajili ya kusajili shule za msingi na serikali basi bajeti inayopelekwa katika halmashauri ni lazima itosheleze kujenga miundombinu ya shule za umma katika viwango vilivyowekwa na serikali yenyewe.

**65. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisisitiza kwamba, katika enzi hizi za maendeleo ya viwanda kuelekea Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa Kati haitawezekana watoto wetu katika shule za msingi na sekondari waende katika shule zisizokidhi viwango hususani ukosefu wa matundu ya vyoo na madawati.

**66. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba, ni muda mwafaka sasa kwa Serikali kuangalia chombo ambacho kitasimamia kwa haki mfumo wa utoaji wa elimu hapa nchini.

### **ELIMU YA MSINGI**

**67. Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Elimu na ile ya TAMISEMI kuititia (LGDG) inajumuisha fedha kwa ajili ya

utekelezaji wa programu za Elimu ya Elimu ya Msingi na Sekondari katika ngazi za Halmashauri. Taarifa ya utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Bunge ya Utawala na S/Mitaa kwa kipindi cha 2016/17 inaonesha kuwa kuna ongezeko kubwa la uandikishaji wa wanafunzi katika shule za Msingi na Sekondari katika mwaka huo wa fedha ikiwa ni ongezeko la takriban wanafunzi 509,085 wa Msingi na katika shule za sekondari ongezeko la wanafunzi 64,562 nchi nzima.

**68. Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Elimu Bure ulianza Jan 2016, hivyo kati ya Jan-June 2016, Serikali ilijipanga kushughulikia upungufu uliokuwepo kwa kuhakikisha kwamba Halmashauri na wadau wengine wa sekta ya Elimu wanachangia kwa hali na mali kupunguza makali ya upungufu huo. Taarifa inaonesha wazi kuwa kwa ujumla wake, Serikali na wadau wamefanikisha kuwepo kwa "ziada ya Madawati 66,042 (msingi) na 45,015 sekondari katika baadhi ya Halmashauri na Mikoa" Lakini wakati huo huo taarifa hiyo bila kutaja mikoa yenye ziada, inaonesha upungufu wa madawati 28,922 (msingi) na 3,875 (sekondari), na kuelezea bayana kwamba upungufu huo unaendelea kufanyiwa kazi.

**69. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuna kukosekana kwa umakini katika mifumo ya uratibu na ufuatiliaji kuliko sababisha kuwa na ongezeko kubwa la madawati "katika baadhi ya halmashauri na mikoa" kitu ambacho kimesababisha usumbufu mkubwa na matumizi yasiyokuwa na lazima ya fedha kutengeneza madawati ambayo hayakuhitajika na kwa sasa hayatumiki.

**70. Mheshimiwa Spika**, Sambamba na hilo, ni utaratibu uliotumiwa na Ofisi ya Bunge kutengeneza madawati kwa kulitumia jeshi la Magereza na kuwagawia waheshimiwa wabunge, haukuwa mzuri na umezitia hasara kubwa halmashauri zetu. Mfano, Halmashauri za Tarime, Ukerewe, Moshi Vijijiini, Bukoba Mjini na zinginezo za Ukanda wa Ziwa kutakiwa kufuata madawati mkoa wa Ruvuma na Lindi kwa ghamama ambazo zingeweza kutengeneza mara mbili madawati hayo kwenye maeneo yao, Jambo hili

lilongeza matumizi yasiyokuwa kwenye bajeti za Halmashauri nyingi hapa nchini.

**71. Mheshimiwa Spika**, Utengenezaji wa madawati kwa kutumia takwimu za ujumla za ongezeko la uandikishaji linaweza kupotosha bajeti za mpito na hata bajeti kuu, kwani uhalsia haupo kama inavyofikiriwa kinadharia. Inasikitisha kuona katika Halmashauri na mikoa mingine madawati yaliyogharimu fedha nyingi yakipigwa jua au yakinyeshewa mvua kwa kukosa mahali pa kuyahifadhi.

#### **XVI. KUIMARISHA MICHEZO NA UTAMADUNI KATIKA HALMASHAURI**

**72. Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Michezo na utamaduni katika halimashauri zinakuwa chini ya idara ya Elimu ya Msingi ambayo ina majukumu makubwa sana ya kushughulikia elimu ya Msingi na sehemu kubwa ya bajeti yake ya matumizi ya kawaida inatoka serikali kuu.

Kitengo cha Michezo na utamaduni kinakuwa kimemezwa na shughuli za Elimu ya Msingi hivyo kushindwa kutimiza majukumu yake kwa ufanisi.

**73. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri serikali kuunda idara mpya ya Michezo na utamaduni katika halimashauri hapa nchini ili kuinua na kuhamasisha shughuli za Michezo na utamaduni katika nchi yetu kwavile zitalazimisha serikali kuu na Halimashauri kutenga fedha za kutosha katika bajeti kwa ajili ya idara hiyo ya Michezo na utamaduni.

#### **XVII. UTOAJI WA HUDUMA YA AFYA**

**74. Mheshimiwa Spika**, Dira ya Sera ya Afya ya mwaka 2007 ni kuwa na jamii yenyewe afya ambayo itachangia kikamilifu kati ka maendeleo binafsi na ya taifa kwa ujumla. Pia sera hiyo inakusudia kutoa huduma muhimu za afya zenyewe uwiano wa kijiografia, viwango vya ubora unaokubalika, għarama nafuu na zilizo endelevu.

**75. Mheshimiwa Spika**, Tanzania inakadiriwa kuwa na takriban zahanati zipatazo 4679, vituo vya afya 481 pamoja na hospitali 219. Zahanati na vituo vya afya ndizo nguzo kuu za huduma za afya ya msingi kwani hutoa huduma za awali kwa watanzania kati ya elfu kumi (10,000) kwa Zahanati na elfu hamsini (50,000) kwa kituo cha afya. Hata hivyo kasi ya ongezeko la idadi ya watu, upungufu wa watumishi wenyе sifa, upungufu wa nyenzo, madawa, umbali wa vituo vya kutolea huduma, ubovu wa barabara za vijijini pamoja na tatizo la usafiri wenyе uhakika ni changamoto kubwa zinazokabili utoaji wa huduma za afya ya msingi hapa nchini.

**76. Mheshimiwa Spika**, katika utoaji wa huduma za afya, sekta binafsi inamchang'o mkubwa, Kwa sasa asilimia arobaini (40%) ya vituo vyote vya huduma za afya nchini, vinamilikiwa na watu binafsi. Changamoto kubwa kwa sasa ni kuwa zaidi ya asilimia 90% ya vituo binafsi vipo mijini na kuacha asilimia kubwa ya watanzania takribani 80% inayoishi vijijini kukosa huduma muhimu za afya.

### XVIII. MFUKO WA BIMA YA AFYA YA JAMII-CHF

**77. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuboresha mfumo wa Bima ya Afya ya jamii -CHF ili kuwezesha wanachama wa mfuko huu waweze kinufaika kwa kupata huduma mahali popote hata nje ya eneo analoishi. Mfano; Mwanachama aliyeo Kibakwe au Kongwa, aweze kupata huduma hata akiwa Peramiho au Ukerewe n.k Pia suala la huduma ya afya kwa wazee litiliwe mkazo na Halmashauri zote ziwekewe muda maalum kuhakikisha kuwa wazee wote wanapata vitambulisho na kupata huduma za afya.

### XIX. MASLAHI YA WATUMISHI KATIKA SEKTA YA AFYA NA ELIMU

**78. Mheshimiwa Spika**, kushuka kwa ari ya kazi kwa watumishi katika halmashauri zetu inachangiwa na mambo

kadhaa na hivyo kupunguza kasi ya ubunifu na bidii katika kutoa huduma kwa wananchi, baadhi ya mambo hayo ni:

- a. Kutopandishwa madaraja kwa watumishi mbalimbali hasa walimu na watumishi wa afya
- b. Kutokopata nyongeza ya mishahara kwa wakati,
- c. Kukaimishwa kwenye nafasi mbalimbali kwa muda mrefu bila kuthibitishwa licha ya kuwa na sifa stahiki.

**79. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha mapungufu haya na mengine ambayo hatukuyataja yanafanyiwa kazi kwa haraka ili kwenda sambamba na Dira ya Sera ya Afya ya mwaka 2007.

## **XX. UMASKINI NA VIASHIRIA VYA UMASIKINI**

**80. Mheshimiwa Spika**, Umaskini ni hali ya maisha isiyoridhisha. Ni hali ya kuwa na uwezo mdogo wa kumudu mahitaji ya maisha ya mwanadamu ya kila siku. Hali hii inajidhihirisha; kwa kuwa na kipato duni, kuishi katika mazingira duni, kusumbuliwa na maradhi na ujinga.

Kambi Rasmi ya Upinzani imelazimika kuweka hiyo tafsiri ya umasikini kwa sababu kubwa kwamba, utendaji wa Serikali za Mitaa ndio chombo au mamlaka pekee ya kisheria inayoweza kuiondoa jamii ya kitanzania katika umasikini nasio serikali kuu.

**81. Mheshimiwa Spika**, Nchi yetu kinadharia ina muundo (**Structure**) mzuri sana wa Serikali za Mitaa ambapo mfumo wake unaanzia ngazi za kamati za mitaa, mikutano ya mltaa, mikutano ya vitongoji, Halmashauri za vijiji na mikutano ya vijiji.

Kuna ngazi ya Kamati ya maendeleo ya Kata na hatimaye ngazi ya halmashauri kabla ya ngazi ya Serikali Kuu ambayo ni pamoja na Tarafa, Wilaya, Mkoa na Wizara yenye dhamana na Serikali za Mitaa.

**82. Mheshimiwa Spika**, Mfumo huu ukiratibiwa vizuri kwa maana ya kuruhusu kwa vitendo maamuzi kutoka chini kwenda juu (Bottom-Up) maendeleo ya nchi hii yatapatikana kwa haraka sana.

Ni ukweli kwamba maendeleo hayo yatagusa watu katika nyanja za kluchumi,kisiasa na kijamii. Hivyo Taifa litawenza kuvipunguza sana viashiria vya umasikini.

## **XXI. VIASHIRIA VYA UMASKINI**

**83. Mheshimiwa Spika**, Viashiria vinavyoonyesha hali halisi ya umaskini hapa Tanzania ni pamoja na:

- i. kutojua kusoma na kuandika,
- ii. Kutokuwa na uhakika wa kupata chakula, mavazi na malazi.
- iii. Uhaba wa maji safi na salama,
- iv. Huduma duni za afya,
- v. Vifo vingi vya wananchi,
- vi. Muda mfupi wa maisha,
- vii. Utapiamlo kwa watoto na watu wazima,
- viii. Uchakavu wa mazingira,
- ix. Ukosefu wa ajira na kipato duni,
- x. Kutofahamu masuala muhimu ya jamii.

**84. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini na kuendelea kusitiza kwamba Serikali za Mitaa ndio mamlaka sahihi yenye uwezo wa kupamba na umasikini kutokana na mfumo wake wa kiutendaji, vilevile ndio mamlaka inayoweza kutoa takwimu sahihi kwa ajili ya

kupanga jinsi ya kugawa raslimali (planning and allocation of resources) katika suala zima la kupambana na umasikini. Hivyo ni vyema Serikali ya awamu ya Tano ikatengeneza mkakati thabiti wa kuimarisha Serikali za Mitaa kama mpango ulivyobainishwa katika Programu ya maboresho ya Serikali za mitaa.

## **XXII. UMUHIMU WA KUTUMIA MAWAKALA KATIKA KUKUSANYA MAPATO**

**85. Mheshimiwa Spika**, Serikali za Mitaa zinakusanya mapato kuitia ada, ushuru, faini na kodi mbalimbali kutokana na vyanzo vyake vya mapato kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa na Mamlaka husika kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Namba 9 ya mwaka 1982,

Baadhi ya masuala yanayozungumziwa katika sheria hii ni pamoja na vyanzo vya mapato, taratibu za kutoza kodi na ukusanyaji wa mapato, matumizi ya fedha, usimamizi wa fedha pamoja na ukaguzi wa vitabu. Kwa ujumla, sheria hii inakazia juu ya usimamizi na udhibiti wa mali za Halmashauri ambazo zinahusisha fedha taslimu na rasilimali nyingine.

**86. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa kukusanya kodi na ushuru ni kwa mujibu wa sheria ya fedha kama ilivyonukuliwa hapo awali, vivo hivyo na utoaji wa huduma za msingi kwa wananchi pia ni jukumu la halmashauri.

**87. Mheshimiwa Spika**, Utaratibu wa kukusanya mapato katika halimashauri kwa kutumia mawakala ulifanyiwa utafiti kwa Msaada wa benki ya Dunia kwa miaka kadhaa ambapo ulienda sambamba na sera ya maboresho ya serikali za mitaa. Utaratibu huu kwa baadhi ya halimashauri za Manispaa na majiji hapa nchini umeshatumika kwa zaidi ya miaka kumi.

Mwaka hadi mwaka kumekuwa na mafanikio makubwa katika kuongeza mapato ya halimashauri kwa kutumia utaratibu huo, hivyo usingetegemea Serikali makini

ikurupuke kutaka kufuta utaratibu huo kutokana na changamoto ambazo ni rahisi kukabiliana nazo.

**88. Mheshimiwa Spika**, Utaratibu wa awali wa kuwapa mawakala viwango vya kuleta katika halimashauri ulikuwa na faida kwa halimashauri na serikali kwasababu zifuatazo:

- i. Gharama zake zake za ukusanyaji zilikuwa zenye tija (cost effective)
- ii. Halmashauri zilikuwa zinapata fedha za dhamana kabla ya wakala kuanza kazi hivyo hata kama wakala akishindwa katikati Halimashauri ilikuwa haipati hasara.
- iii. Utaratibu wa kulipa commission kwa mawakala unakuwa hauna uhakika kwa mzabuni kumaliza mkataba wake. Vilevile kunakuwa na visingizio vingi vya wazabuni kutoa taarifa ya hasara na hivyo ama kutishia kujitao au kujitao kabisa jambo ambalo linaziweka halimashauri katika wakati mgumu sana wa mapato.
- iv. Ushindani wa wazabuni katika tenda ulikuwa mkubwa kiasi kwamba halimashauri makini zilikuwa zinaongeza mapato mwaka hadi mwaka.
- v. Halimashauri zilikuwa zinapata msingi wa kutengeneza 'data base' za mapato kupitia katika ushindani wa wazabuni katika tenda.
- vi. Utaraibu wa mwanzo umesaidia sana kutengeneza ajira kwa kuimarisha sekta binafsi hivyo kuzipunguzia halimashauri mzigo wa kuajiri vibarua wengi ambao wangefanya matumizi ya mishahara yawe makubwa sana katika halimashauri zetu.

**89. Mheshimiwa Spika**, Kuna vyanzo katika halimashauri havikusanyiki kabisa katika Mfumo huu wa kutumia 'commission' kwa asilimia isiyozidi ishirini jambo

ambalo limeathiri ukusanyaji wa mapato kulingana na bajeti za halimashauri.

**90. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inalshauri Serikali kwamba kutokana na uzoefu ilioupata kutoka kwenye halimashauri zilizo chini yake ni muhimu Ofisi ya Rais TAMISEMI ifanyie mapitio maagizo na miongozo yake kuhusiana na utaratibu mpya wa kutumia mawakala katika kukusanya mapato.

Pia ni vizuri Ofisi ya Rais TAMISEMI ikazipitia changamoto zote zilizopatikana kwa kipindi cha mwaka mmoja katika utaratibu mpya wa kutumia mawakala kwa kuwalipa ‘commission’ isiyozidi asilimia ishirini kutokana na mapato yaliyokusanywa katika Halimashauri ili waone haja ya kurudi kwenye utaratibu wa zamani wa kuwapa mawakala kiwango cha kulipa katika halimashauri baada ya kushindanishwa katika taratibu za zabuni bila kujali kwamba wakala ametumia kiasi gani cha gharama katika ukusanyaji.

#### **XXIII. FEDHA ZA OC NA FEDHA ZA MAENDELEO KUTOFIKA KWA WAKATI**

**91. Mheshimiwa Spika**, General purpose grant (Ruzuku ya serikali kuu kwa vyanzo vilivyofutwa) ni muhimu iletwe kwenye halimashauri kwa wakati ili asilimia ishirini iweze kuelekezwa kwenye vijiji na mitaa. Pia fedha za Ruzuku kwa miradi ya Maendeleo laziima zifike kwa wakati. Hii ruzuku sio hisani bali ni kwa mujibu wa sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa kifungu cha 10, kuchelewa kutolewa kwa fedha hizo maana yake ni kuchelewesha maendeleo kwenye maeneo husika. Hivyo basi ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuitaka Serikali kuhakikisha ruzuku husika inapelekewa kwa wakati ili iwe na maana zaidi kiutendaji, kwani kuchelewesha fedha hizo kunazidisha uwezekano wa ubadhirifu wa fedha hizo pindi zinapotolewa kwa kuchelewa.

**92. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali Kujenga imani kwa wananchi kwa

kuhakikisha bajeti ya miradi ya Maendeleo inatekelezwa kwa wakati katika halimashauri hapa nchini ili kuwafanya wananchi wawe na moyo katika kushiriki vikao vya kuibua miradi katika ngazi za nchini.

#### **XXIV. AKAUNTI MAALUMU KWA FEDHA ZA MFUKO VIJANA NA KINAMAMA**

**93. Mheshimiwa Spika**, Katika kuhakikisha kuwa Halmashauri inatenga asilimia kumi (10%) ya mapato yake yote kwa ajili ya mfuko wa maendeleo wa wanawake (5%) na wa vijana (5%) na kuhakikisha fedha hizo zinakopeshwa kwa walengwa baada ya kujiridhisha kuwa walengwa wana sifa za kukopeshwa kwa sababu mfuko huo ni endelevu (revolving fund).

**94. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa kila Halmashauri ifungue akaunti maalum ili fedha hizo ziwekwe huko ili zisiwekwe kwenye General akaunti ambapo wakati mwingine fedha hizo zinaweza kutumika kama matumizi mengineyo (OC) na hivyo kushindwa kubainika matumizi yake. Kwa kuwa na Akaunti Maalum kutasaidia marejesho ya fedha hizo kutoka kwa wanufaikaji kurejeshwa kwenye akaunti hiyo na itakuwa rahisi kuiratibu au kuifanya ukaguzi.

Kwa hali illvyo sasa ni vigumu kutenganishwa fedha zilizotengwa kwenye bajeti ya mwaka na zile ambazo ni marejesho ya wakopajl.

#### **XXV. POSHO KWA VIONGOZI WA KUCHAGULIWA**

**95. Mheshimiwa Spika**, Kumekuwa ni kilio cha muda mrefu kwa viongozi wa kuchaguliwa kutaka ama kuongezewa posho au wengine kuingizwa kwenye mfumo rasmi wa kupata posho.

Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali iijitahidi kuboresha posho za madiwani kufikia kiasi kisichopungua laki nane( Tshs 800,000)kwa mwezi ikiwa ni pamoja na posho za

vikao kufikishwa elfu sabini(Tshs 70,000), Aidha Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali izielekeze Halimashauri kutenga fedha katika bajeti zao ili ziweze kuwalipa wenyeviti wa vijiji mitaa na vitongoji posho isiyopungua elfu hamsini(Tshs 50,000) kwa mwezi na elfu ishirini(Tshs 20,000)kwa wajumbe wa halimashauri za vijiji na wajumbe wa kamati za mitaa.

**96. Mheshimiwa Spika**, Tunatoa pendekezo hilo kutokana na ukweli kwamba, ngazi hii ya kiutendaji ndiyo muhimu sana katika maendeleo ya nchi kwani ndiko maendeleo yanakotakiwa kutekelezwa na ndipo umasikini ulipo. Hivyo kiasi hicho cha fedha ni kutoa motisha kwa viongozi wetu ili waongeze bidii Katika kutekeleza majukumu yao. Tukumbuke kwamba watendaji wa vijiji na mitaa hawawezi kufanya kazi zao bila kuwategemea viongozi hao waliochaguliwa na wananchi. Watendaji (VEO na WEO) ni waajiriwa wa Serikali lakini wenyeviti na wajumbe wanafanyakazi katika mazingira magumu na hivyo kupelekea uwezekano wa kuwepo na rushwa ndogo ndogo ambazo zinazidisha kero kwa wananchi badala ya kutatua kero za wananchi

## **XXVI. USAFI WA MAZINGIRA**

**97. Mheshimiwa Spika**, Hoja ya usafi wa mazingira kwa miji yetu limekuwa ni jambo ambalo kwa kiasi kikubwa likitia doa halmashauri zetu, kutokana na ukweli kwamba Halmashauri nyingi zimeshindwa kuwa na utaratibu unaoleweka wa kushughulika na taka ngumu.

**98. Mheshimiwa Spika**, Tunaposema uwezo maana yake ni Halmashauri kutokuwa au kuwa na fedha kidogo kwa ajili ya kuthibiti taka hizo.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali izielezekeze halimashauri kutenga bajeti kwa ajili ya kuendesha program ya kudhibiti taka ngumu (solid waste management) ikiwa ni pamoja ni kuelimisha wananchi namna ya kutenga taka taka katika vyanzo vya kukusanya taka hizo (separation at source). Programu hii itahusisha mpango wa kutenganisha taka

kulingana na matumizi kwa aina ya taka (Renewal, Reuse and Recycling -3Rs). Lengo kubwa la programu hii ni kubadilisha mtazamo ya wananchi wanaoamini kwamba taka taka ni uchafu badala yake kuwa rasilimali.

**99. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba kama mpango huu ukitekelezwa vizuri utasaidia miji yetu kuwa safi kwa gharama nafuu zaidi na pili halimashauri zetu kuwekeza kwenye 'Recycling plants' 'Composite manure plants', 'Methane gas na Bio gas plants' ambacho kitakuwa chanzo cha mapato na pia kuwa na uhakika wa kutoa ajira kwa vijana wetu.

**100. Mheshimiwa Spika**, Aidha Kamati za mazingira za Halmashauri zikiwemo za kwenye kata ni muhimu ziimarishwe ili jukumu la kukabiliana na uchafuzi wa mazingira lilekelezwe vizuri kwenye ngazi za chini ambapo ndipo wananchi wapo.

#### **XXVII. BUGHUDHA NA MAPAMBANO DHIDI YA WAFANYABIASHARA WADOGO (WAMACHINGA) KATIKA MIJI, MANISPAA NA MAJIFI**

**101. Mheshimiwa Spika**, Swala la Wamachinga katika nchi ya Tanzania linatakiwa lipate mtazamo mpya kutoka kwa viongozi wa serikali. Kutokana na kukosekana kwa ajira rasmi watu wengi wanawake na wanaume wameamua kujajiri wenyewe kwenye biashara ndogo ndogo ili kukidhi mahitaji yao ikiwemo chakula, Malazi, mavazi, Elimu, matibabu n.k

Utashi huo wa wananchi kujishughulisha na biashara ndogo ndogo kwanza unaongeza pato la Taifa na pili unasaidia sana kundi kubwa haswa la vijana kutojihusisha na vitendo vya uhalifu kama wizi, ujambazi, uzuzuraji n.k

Vitendo vya uhalifu vinapopungua inakuwa ni faraja kwa kundi la matajiri, watu wa kipato cha kati ,na hata viongozi wetu. Pia inasaidia utulivu wa nchi hivyo vyombo

vya ulinzi na usalama navyo vinakuwa na kazi ndogo ya kupambana na uhalifu.

**102. Mheshimiwa Spika,** Jambo muhimu sana ambalo viongozi mbali mbali wanapaswa kulifahamu ni kwamba kundi hili ndilo ambalo baadaye linazalisha watu wanaopata mafanikio makubwa kimitaji na hatimaye kuwa wawekezaji mashuhuri na muhimu katika uchumi wa nchi. Mifano ipo mingi nje na ndani ya nchi ambapo Wajasiriamali wa sekta isiyo rasmi ndio baadhi yao walirasimishwa kutokana na kukuwa kwa Mitaji yao na leo ni matajiri wakubwa sana katika nchi zao wakiwa wanamiliki mitaji mikubwa sana.

**103. Mheshimiwa Spika,** Ni muhimu sana serikali ya Tanzania ikiwa ni pamoja na serikali za mitaa kubadili mitazamo yao juu ya Wamachinga ili iwatengenezee mazingira rafiki kwa biashara zao badala ya kuwa kikwazo kwao. Pia Viongozi mbali mbali wakiwemo Mawaziri, Makatibu wa Wizara Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri lazima wabadili mitazamo yao ya kuwaona Wamachinga kama watu wanaovunja sheria za mipango miji hivyo kila wakati kutoa maagizo ya kuwakamata na kuwasumbua tena kwa kuwanyanganya Mali zao.

**104. Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri serikali kutoa maagizo yenye msImamo wa pamoja, unaoeleweka na kuaminika kwa Wamachinga kuzielekeza halimashauri zote hapa nchi wakiwemo Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kwamba zoezi lolote la kuwabughudhi Wamachinga kwa kutumia nguvu nyingi ni unyanyasaji usiozingatia haki na utu wa watu wanaojitafutia riziki yao halali haswa katika nchi ambayo kuna upungufu mkubwa wa ajira ulisababishwa kwa kiwango kikubwa na sera mbovu za ubinafisishaji za Serikali ya CCM .

#### **XXVIII. SHERIA NDOGO ZA HALIMASHAURI**

**105. Mheshimiwa Spika,** Halmashauri lazima ziongezewe uwezo wa viwango vya faini kwa baadhi ya

makosa. Kwa mfano uharibifu wa barabara kwa magari makubwa yanayoharibu barabara za lami katika halimashauri zetu lazima udhibitiwe kwa kutozwa faini inayozidi elfu hamsini.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri serikali kupitia upya sheria ndogo na adhabu zake ili izifanye ziende na wakati kutokana na mazingira halisi ya miji yetu bila kuleta bughudha kwa wananchi.

## **XXIX. MATUMIZI MABAYA YA MADARAKA YA WAKURUGENZI WA HALIMSHAURI NA MANISPAA ZA MIJI**

**106. Mheshimiwa Spika**, Kumekuwa na malalamiko mengi sana kutoka kwa waheshimiwa madiwani kwamba watumishi wa Halmashauri kusimamishwa kazi bila ya kufuata sheria na taratibu, jambo ambalo halmashauri inashtakiwa na kulazimika kuwalipa fidia, hivyo kuiingizia halmashauri hasara. Watendaji wa vijiji takriban 30 ambaao ni watumishi wa umma kusimamishwa kazi kwa hisia za kisasa, na hivyo kuathiri shughuli za maendeleo, hii imetokea katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru.

**107. Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na tabia ya wakurugenzi kutoa maelekezo ya kuwarudisha kazini watumishi waliopatikana na makosa mbalimbali ya kinidhamu bila kuwapa adhabu yoyote pamoja na ushahidi wa wazi wa ubadhirifu. Na wanarudishwa kazini bila mchakato wa kinidhamu wa kisheria, hii ni kudharau mamlaka zilizowafanya mchakato na hadi kuonekana kuwa makosa yametendeka. Mfano ni Mkurugenzi wa Hanang' na pia Meru.

**108. Mheshimiwa Spika**, Aidha, kumekuwa na utaratibu unaotumiwa na wakurugenzi wa kubadilisha matumizi ya fedha kama ambazo tayari zimepangiwaa matumizi kwa bajeti zinazopitishwa na vikao vya baraza la madiwani bila ya kufuata utaratibu. Tukumbuke kwamba taratibu za operations zinazozuka toka juu zinakuwa hazina bajeti yoyote ya utekelezaji wake katika ngazi za chini.

**109. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema vitendo hivi vya wakurugenzi vinakwenda kinyume na sheria na miongozo ifuatayo:

1. Sheria ya madaraka Mikoani (The Regional Administration Act, sura 97 na marejeo ya 2002)

2. Sheria Na.7 Sura 287 ya mwaka 1982 (marejeo ya 2002)

3. Kifungu cha 43(5),(6) na (8) cha sheria ya fedha za mitaa Na.9 ya mwaka 1982 na marejeo yake ya 2002

4. Kifungu cha 5 na 6 cha mwongozo wa fedha za Serikali za mitaa (*local Government financial memorandum*) 2009

**110. Mheshimiwa Spika**, Utaratibu wa Tume ya Uchaguzi kuwatumia wakurugenzi wa halmashauri wakati wa Uchaguzi wa wakilishi wa wananchi wakati wakurugenzi hao wameteuliwa katika misingi yenye harufu za itikadi za kisiasa unakandamiza misingi ya Haki na Demokrasia katika nchi yetu.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka serikali kuitengeta tume ya Uchaguzi fedha za kutosha katika bajeti ili iajiri watumishi wa kutosha watakaoweza kusimamia haki wakati wa chaguzi mbali mbali hapa nchini.

### **XXX. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2016/17 NA MPANGO WA MAENDELEO 2017/18 TAMISEMI (fungu 56)**

**111. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ndio taasisi inayohusika moja kwa moja na maisha ya kila siku ya watanzania kwa ngazi zote. Kwa mwaka wa fedha 2016/17 taasisi hii ilikadiriwa kukusanya maduhuli yapatayo shilingi triliioni 16.881 na katiki ya fedha hizo hadi mwezi Februari, 2017 ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 4.75 tu, sawa na 28%. Na ukiangalia fedha hizo zimetokana na marejesho ya mshahara, na kuuza vifaa

chakavu na zabuni makao makuu. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema vyanzo hivi sio vyanzo vya uhakika kuweza kutegemewa na taasisi kubwa kama hii ya Tamisemi inayogusa maisha ya watu ya kila siku. Kama mishahara isiporejeshwa na vyuma chakavu vikimalizika? Maana yake hakuna fedha zitakazopatikana!!!!!!!!!!!!!!.

**112. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi ya kawaida na maendeleo Tamisemi ilipangiwa kiasi cha shilingi billioni 354.383 katи ya hizo shilingi billioni 325.469 ni kwa ajili ya mpango wa maendeleo, ikiwa shilingi bilioni 256.739 zikiwa fedha za ndani na shilingi bilioni 68.730 zikiwa fedha za nje.

**113. Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa uwekezaji muhimu ni ule ambao utasaidia kuwa chanzo cha mapato kwa halmashauri, miradi ya ujenzi wa vituo vya mabasi 11, vituo 5 vya maegesho ya malori, machinjio 7 na masoko 9 katika miji 7 mradi huo haukupewa hata shilingi. Na miradi yenye muonekano wa kuwa vyanzo vya mapato kwa halmashauri ni mingi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kama kweli tunataka Serikali za mitaa kutimiza majukumu yao ni lazima miradi inayoweza kuwa vyanzo vya mapato itekelezwe kwa ukamilifu wake.

**114. Mheshimiwa Spika**, mpango wa utekelezaji miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/18 programu ya uendelezaji wa miji 18 kasma 6405 imetengewa shilingi billioni 12.610 wakati mwaka jana walitengewa bilioni 10.47 na hakuna hata shilingi iliyotolewa, na mbaya sana ile miradi iliyotakiwa kutekelezwa mwaka jana, mwaka huu haipo kwenye program ya utekelezaji badala yake itatekelezwa mradi mipyä, na fedha zote za program hii ni kutoka nje. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kunakosekana umakini wa "consistence" katika upangaji na utekelezaji wa miradi yake. Kwa mwendo huu ni dhahiri hatuwezi kupiga hatua yoyote katika kuendeleza Halmashauri zetu.

## XXXI. HITIMISHO

**115. Mheshimiwa Spika**, katika kuhitimisha ni muhimu kuelewa kwa undani dhana ya “**all development are local**”, katika muktadha wa halimashauri zetu pamoja na Serikali za mitaa katika kulete maendeleo kwa wananchi, na maendeleo ni lazima yawe kwa watu. Uelewa wa na ufahamu wa mahitaji ya mamlaka ya serikali za mitaa na jamii inayoishi hapo na kutoa msaada wa hali na mali ili kuwa na maendeleo shirikishi, ndio njia pekee itakayohakikisha jamii ya kitanzania inakuwa na maendeleo endelevu.

**116. Mheshimiwa Spika**, dhana ya “**all development are local**”, ni kwamba maendeleo endelevu yanapatikana kwa ushirikishwaji wa wananchi na sio kutokana na maelekezo na matamko ya viongozi na Serikali za mitaa ndiko wananchi walipo na sio Serikali kuu. Aidha tukumbuke kaulli ya Mwalimu Nyerere kwamba; “Maendeleo ni ya watu na sio ya vitu”. Ukweli ni kwamba sasa hivi maendeleo ni kwa vitu na jambo hilo wananchi wengi sasa hivi wanakula bombardier badala ya kula ugali na wali. “You cannot develop people, you must allow people to develop themselves”

**117. Mheshimiwa Spika**, “THE 2030 AGENDA FOR SUSTAINABLE DEVELOPMENT” malengo ya Milenia mapya endelevu ya Umoja wa Mataifa hasa lengo la 16. Kuwa na maendeleo shirikishi kwa jamii, na haki kwa wote, na kujenga taasisi inayowajibika kwa ngazi zote.

*“Promote peaceful and inclusive societies for sustainable development, provide access to justice for all and build effective, accountable and inclusive institutions at all levels”*

Kama ambavyo alisema Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kuwa ni lazima kuwepo na ushirikishaji wa jamii ambayo ndiyo injini ya uchumi wa nchi na jamii hiyo inaishi vijijini.

**118. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi inaitaka Serikali kuu, kama kweli inataka ustawi na maendeleo ya wananchi "economic Development" kuzirejeshea halmashauri zetu uhuru wa kuamua jinsi raslimali zake zitakavyotumika kama ambavyo lengo la maboresho ya Serikali za Mitaa (LGRP) lilivyokuwa likihitaji. Ila kama Serikali inahitaji "economic Growth" basi iendelee na utaratibu uliopo sasa.

**119. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
**Japhary Raphael Michael (Mb)  
Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-  
Ofisi ya Rais- TAMISEMI  
18.04.2017**

**SPIKA:** Baada ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Utumishi na Utawala Bora, wachangiaji watakaoanza ni Mheshimiwa Bonnah Kaluwa...

**MBUNGE FULANI:** Bado mmoja.

**SPIKA:** Bado nini?

**MBUNGE FULANI:** Bado wa Utawala Bora.

**SPIKA:** Nimesema baada ya huyo ili wajiandae.

**MBUNGE FULANI:** Uko sawasawa.

**SPIKA:** Akimaliza nusu saa atakayemalizia hapa watakaokuwa wachangiaji ili wajiandae, ataanza Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, Mheshimiwa Dkt. Rashid Chuachua, Mheshimiwa Elias Kwandikwa halafu Mheshimiwa Kasuku Bilago na tutaendelea na wengine.

Tunaendelea, bado tuko upande wa Upinzani ambako sasa anakuja Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya

**NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Upinzani kuhusu Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Ruth Mollel, karibu sana. Karibu sana Mheshimiwa usome hotuba yako na una nusu saa. (*Makofi*)

**MHE. RUTH H. MOLLEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari 2016.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kutoa salamu za rambirambi kwako wewe binafsi Mheshimiwa Spika, kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kwa Waheshimiwa Wabunge wote, Ofisi ya Bunge na familia ya Macha kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu Marehemu Dkt. Elly Macha. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kulaani kwa nguvu zote vitendo vinavyoendelea kutokea katika nchi yetu vya utekaji, utesaji na uuaji wa raia na polisi wasio na hatia hapa nchini. (*Makofi*)

*Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana kwamba wakati matukio haya yanaeendalea kutokea, Serikali nzima pamoja na vyombo vyake vya ulinzi na usalama, imekaa kimya na hajatoa tamko lolote juu ya jitihada zinazofanyika kukabiliana na matukio haya yanayoikumba nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa pia na Kiti cha Spika kiliviyotumika vibaya kuzuia Wabunge ambaao ni wawakilishi wa wananchi na ambaao baadhi yao wamelalamika kuwa wametishiwa maisha, kujadili jambo*

*hilo kwa kujificha nyuma ya kivuli cha Kanuni za Bunge.  
(Makof)*

*Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshushwa pia kuona Waziri anayehusika na Utawala Bora kukataa masuala yanayohusu utawala bora kujadiliwa Bungeni...[Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ruth naomba ukae kidogo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika,  
Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi amesimama,  
Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,  
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika,  
kuhusu utaratibu na Kanuni ya utaratibu ni 68(1) lakini  
najielekeza kwenye Kanuni ya 64(1)(e).

Mheshimiwa Spika, Kanuni yetu ya (e) inatuambia kabisa kwamba Mbunge anakatazwa kabisa kuzungumzia mwenendo wa viongozi kadhaa ikiwemo Mheshimiwa Spika.  
(Makof)

Mheshimiwa Spika, kifungu hiki anachokisoma Msemaji wa Kambi ya Upinzani anataka kutuhumu maamuzi ya Kiti cha Spika ambayo yalikwishafanyika na anataka kushawishi Bunge hili na wananchi wote kwamba maamuzi yale yalifanyika kwa kuvunja Kanuni za Bunge. (Makof)

Mheshimiwa Spika, Kanuni za Bunge zinatuongoza kama Mbunge anaona kabisa kwamba jambo fulani

lililofanyiwa maamuzi ndani ya Bunge na Spika halijaenda sawasawa zipo Kanuni zinazotuongoza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba mwongozo wako ni kwa nini kifungu hiki kisiondolewe kabisa kisije kikabakia kwenye *Hansard* kwa sababu hakielezi maana halisi na ukweli wa jambo lenyewe ambalo lilikuwa limetokea Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ili nisisimame tena, ukurasa wa tatu, *paragraph* ya tatu kutoka mwisho, naomba kuiombea mwongozo kwa sababu *paragraph* hii, wakati Kiongozi wa Upinzani akisoma hotuba yake Bungeni maneno yaliyoandikwa kwenye *paragraph* hii tulishafanyia maamuzi na yallondolewa kwenye *Hansard* lakini yamerudishwa tena.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba mwongozo wako, huu ni utaratibu wa Kibunge wa kuleta taarifa ndani ya Bunge ambazo zinakinzana na Kanuni za Bunge tulizonazo ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, hoja anayoitoa *Chief Whip* wa Serikali tulijadili na tulipingana nayo kwamba inakiuka Ibara ya 100 ya Katiba ambayo inazungumzia uhuru wa mawazo ndani ya Bunge ambayo ni pamoja na kujadili, kuhoji, mwenendo wa viongozi wetu wanavyofanya kazi. Hiki kipengele anachokisoma, Ibara ya 100 haipaswi kuathiriwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa *Chief Whip* anachokisema, anaithiri Ibara ya 100 ambayo inatupa haki ya kujadili mwenendo na ndiyo kazi yetu Upinzani kuikosoa, kuielekeza Serikali na kuishauri. Kwa hiyo, anajaribu kulifunga Bunge lisifanye kazi yake na kutokutoa nafasi kwa sisi kama Wapinzani kutimiza majukumu yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tutende haki ili tuisimamie Serikali badala ya kutufunga midomo tusifanye kazi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ruth, kama una cha kusema kuhusu hilo, ili tuweze kuendelea kutoka hapa. Tumia tu *microphone* hiyo hiyo.

Ni vifungu viwili, kuna kifungu ulichokuwa umekifikia kinachomhusu Mheshimiwa Spika na kuna kifungu cha ukurasa wa tatu, mwisho pale; mistari kama sita ya mwisho, ukurasa wa tatu pale. Moja, mbili, tatu, nne; mitano au sita hivi.

**MHE. RUTH H. MOLLEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nafikiri Mheshimiwa Msigwa amelizungumzia hili jambo na kwamba sisi kama Wabunge, kazi yetu ni kuisimamia Serikali na kutoa mawazo yetu kwa Serikali na ninafikiri ndicho tunachokifanya, wala siyo nia mbaya. (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote kwenye ukumbi, watu wanaposoma hivi vitu na kila mmoja wetu amewekewa kwenye dawati pale, ni vizuri tukawa pamoja.

**WABUNGE FULANI:** Hatujapata hiyo hotuba. Hakuna hotuba.

**SPIKA:** Haiwezekani ikawa hakuna. Makatibu wangu! Vimegawiwa tangu asubuhi hivi. Wengine mlikuwa nje, kwa hiyo, labda hamkuwepo.

Makatibu, hebu piteni; ninyi ambao mnagawa hivyo vitabu nanyi saidieni, kama viro wapatiensi; lakini vitabu vimegawanywa kwa uhakika. Kwa kila aliyekuwepo asubuhi alipata, labda kama mtu hakuwepo.

Sasa lengo letu ni kuokoa muda kwa sababu wachangiaji watapungua katika orodha ile ambayo nimeizungumzia mapema.

Tukianza na ukurasa wa pili, hotuba hii ya Kambi Rasmi ambayo Mheshimiwa Ruth ndio anaisoma kwa niaba yenu, anasema hivi, na mimi namnukuu: *"Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa pia na Kiti cha Spika kilivyotumika vibaya kuzuia Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi na ambao baadhi yao wamelalamika kuwa wametishiwa maisha, kujadili jambo hilo kwa kujificha nyuma ya kivili cha Kanuni za Bunge."*

Sasa sijui yaani katika *Commonwealth* maana tunafanya vitu kwa utamaduni, kumlaumu Spika kwa vitu vya aina hii na moja kwa moja kiasi hicho, lazima hotuba hii haiandikwi na Mbunge. Kuna mtu anawaandikieni huko labda au sijui vipi hata sielewi, ambaye hajui taratibu hizi. Hatufanyi hivyo.

Huwezi kuwa Mahakmani pale, wewe mwenyewe ni Hakimu halafu unam-*shoot* Jaji. Yaani mimi ni kiongozi wenu ninyi; mnapokuwa mnaniwekea maneno ya ajabu ajabu, sijui kama hiki chombo kitaheshimika, mimi sielewi! Yaani maneno haya kweli ni ya lazima? (*Makofii*)

Hivi aliyesema kwamba ametishiwa maisha, labda anataka kuuawa; niwaulizeni ninyi Wabunge, aliyeniletea taarifa ama kwa kuniandikia ama kwa kuniambia kwamba mimi Mbunge wako natishiwa maisha hivi na hivi na hivi; jina lake nani? (*Makofii*)

Kwa hiyo, vitu vingine siyo lazima. Mheshimiwa Bashe yuko hapa; Mheshimiwa Bashe, umewahi kumwona Spika ukamwambia chochote? Haya nitajieni ninyi hao

waliotishiwa. Ni akina nani? Kwa hiyo, Mbunge ye yote akisema tu hapa, basi; Bunge zima tunakwenda na upepo? Kusema ni kusema kama huyu alivyosema sasa hivi hapa. Kwani ni kweli hii? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Ruth, tunakwenda ya pili ile, inaanza na neno; “*kwamba kuna kudhibiti Wabunge na hasa wa Upinzani kutoa mawazo yao kwa uhuru.*”

Mnadhibitiwaje? Hivi kwa nini wewe unajiweka katika hali fulani ya kuona kama wewe unaonewa tu? Unaonewa na nani? Kanuni ni za wote, taratibu ni za wote, hakuna anayedhibitiwa chochote. Kila mtu anatoa mawazo yake kwa uhuru wake. Sasa kama ninyi hamuwezi kutoa kwa uhuru kwa kweli, siyo vizuri kuandika vitu kama hivyo.

“*Kuingilia mhimili wa Mahakama*” tulishasema siku ile ya Kiongozi wa Upinzani, sentensi ambazo ni *sweeping* kama hizi ni sentensi ambazo siyo lazima sana, *unless u-qualify* basi, mtu anayesoma aone *what are you talking about*, kuliko ki-sentensi tu; “*kuingilia uhuru wa Mahakama.*” Mahakama ni chombo chenye heshima yake. Mkishamdharau Spika mnaenda na kwa Mahakama tena? Si inatisha ikaishia hapa hapa!

“*Kupuuza utawala wa sheria wa kuruhusu wahalifu kuuawa, haya polisi na kadhalika.*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** (*Alizungumza bila kutumia kipaza sauti*).

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul, nakusikia vizuri! Yaani ninyi na hasa baadhi ya watoto wa kike, wanapenda kweli kunipanda panda mgongoni. Nawaheshimu sana, lakini sijui kwa nini ninyi mnapenda kukosa heshima. Sijui ndivyo mlivyo? Sijui mlikosa malezi mahali? (*Makofi/Kicheko*)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Ruth unafahamu jinsi ninavyokuheshimu, wewe umekuwa kiongozi wangu, umekuwa kiongozi wetu kwa *level* kubwa kabisa. Mafungu

haya mawili naomba tu uyaache, uendelee na kusoma hotuba yako. Tumlindie muda wake. Lile fungu la kwanza ambalo ulishalisoma kwenye *Hansard* tunalitoa, linalomshutumu Spika na hili la mwisho la ukurasa wa tatu, mistari sita hivi ya mwisho. Mengine unaweza ukaendelea nayo.

**MHE. RUTH H. MOLLEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kuna usemi usemao kwamba vyombo vyombi na usalama vinapoilinda Serikali, basi vinakuwa adui wa wananchi. Hicho ndicho kinachotokea sasa katika nchi yetu. Mtazamo wa kuilinda Serikali usipobadilika, basi usalama upo mashakani, kwani ni dhahiri kwamba vyombo hivyo vinategemea taarifa kutoka kwa wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri wahusika wajitafakari kwa amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, msingi wa utawala wa sheria; dhana ya utawala bora imejengwa katika misingi ya Katiba ya nchi inayoheshimu mgawanyo wa madaraka katika mihimili mikuu ya dola, demokrasia, utawala wa sheria, haki za binadamu na uhuru wa kutoa maoni na kupata habari, uhuru wa kukusanya na kujunga na mashirika au vyama mbalimbali katika jamii na kadhalika.

Aidha, utawala bora una sifa za uwazi, uwajibikaji, ushirikishwaji watu, ufanisi, tija, uadilifu, usawa na kuzingatia taratibu za kisheria, kanuni, katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tukijipima kama Taifa kwa maana hiyo ya utawala bora na kwa sifa hizo za utawala bora, utaona kwamba nchi yetu iko nyuma sana katika utekelezaji wa misingi ya utawala bora. Kwa mujibu wa hotuba ya Kiongozi wa Upinzani Bungeni aliyoitoa hapa Bungeni tarehe 6 Aprili, 2017 ni kwamba matukio yaliyofanywa na yanayoendelea kufanywa na Serikali hii ya Awamu ya Tano ya kupiga marufuku mikutano ya vyama vyaa siasa, kupiga

marufuku urushwaji wa moja kwa moja wa mijadala ya Bunge kuitia vyombo vya habari, kudhibiti Wabunge na hasa wa Upinzani kutoa mawazo yao...

**SPIKA:** Kuanzia hapo ndiyo nimekuzuia Mheshimiwa Ruth.

**MHE. RUTH H. MOLLEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nimefuta hiyo. (*Makof*)

**SPIKA:** Kuanzia hapo ndiyo nimekuzuia.

**MHE. RUTH H. MOLLEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, aah, *okay!*

**SPIKA:** Endelea na 2.1. (*Makof/Kicheko*)

**MHE. RUTH H. MOLLEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivoyeleza hapo awali, dhana ya utawala bora ina sifa ya uwajibikaji wa pamoja. Tofauti na awamu zilizopita za utawala, sifa hii muhimu ya utawala bora ya uwajibikaji wa pamoja imeanza kupotea katika Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu tumeshuhudia kwa nyakati tofauti kauli zinazokinzana za Serikali hiyo hiyo moja. Kwa mfano, matukio ya hivi karibuni ya Mkuu wa nchi kutengua hadharani agizo la aliyekuwa Waziri wake wa Katiba na Sheria juu ya sharti la kuwa na cheti cha kuzaliwa ili mtu aweze kufunga ndoa. Vilevile Waziri wa Afya kutofautiana na Makamu wa Rais juu ya upungufu wa dawa na vifaa tiba nchini; vilevile Mkuu wa nchi kupinga taarifa za njaa alizopewa na baadhi ya Wakuu wa Wilaya na Mikoa; Waziri wa Ardhi kupinga mchakato wa kumpatia

ardhi Mkoo wa Mkoa wa Dar es Salaam na mengine yanayofanana na hayo ni ishara tosha kwamba kuna tatizo kubwa la mawasiliano na uwajibikaji wa pamoja katika Serikali. Aidha, ni dalili mbaya kwamba Serikali inaelekeea kushindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na kutokuwa na msimamo wa pamoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri na kupendekeza kwamba Serikali irudi katika misingi ya uwajibikaji wa pamoja ambayo ni sifa muhimu ya utawala bora. Serikali izungumze lugha moja, Waziri mmoja anapotoa tamko, tamko hilo liwe ni kwa niaba ya Serikali nzima. Kwani kwa kutofanya hivyo, Serikali itawachanganya wananchi.

Aidha, Mkoo wa nchi awaache mawaziri wake wafanye kazi kwa kujamini ili wawe na tija katika majukumu yao. Kuwaingilia kila wakati au kuwapinga hadharani kunawavunja moyo na kuwafanya wafanye kazi kwa uoga wakihofia kutumbuliwa na kuumbuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, usawa wa jinsia na ushirikishwaji katika vyombo vya uamuzi ni mionganini mwa nguzo muhimu za utawala bora. Kumekuwa na tatizo duniani la ushirikishwaji hasa wa wanawake katika vyombo vya maamuzi. Kutokana na hali hiyo, kumekuwa na vuguvugu katika mataifa mbalimbali duniani ya kuhakikisha kuwa wanawake wanawakilishwa vya kutosha katika vyombo vya uamuzi ili kukidhi matakwa ya utawala bora.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Bara la Afrika, vuguvugu la kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya maamuzi lilipelekea nchi wanachama wa Jumuiya ya SADC kuazimia kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vya maamuzi kufikia angalau asilimia 50. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya SADC na iliridhia mkataba huo. Kulikuwa na jitihada za kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vya maamuzi hapa nchini katika Serikali ya awamu iliyopita, lakini

takwimu zinaonyesha kwamba nafasi za wanawake katika Awamu hii ya Tano zimepungua.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Mtandao wa Jinsia (*TGNP*) ni kwamba hadi kufikia Julai, 2016 uteuzi wa Baraza la Mawaziri ulionesha kushuka kwa idadi ya wanawake ukilinganisha na kipindi cha Serikali ya Awamu ya Nne. Wakati Serikali ya Awamu ya Nne iliteua Mawaziri wanawake 10 sawa na asilimia 33.3 ya Baraza lote, Serikali ya Awamu ya Tano iliteua Mawaziri wanawake wanne tu kati ya Mawaziri 19, sawa na asilimia 21.1 na hivyo kufanya uteuzi wa wanawake Mawaziri kushuka kwa asilimia 12.2. (*Makofi*)

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Taarifa.

**MHE. RUTH H. MOLLEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, taarifa ya *TGNP* inaonyesha pia kwamba, kati ya Makatibu Wakuu 29...

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Taarifa.

**MHE. RUTH H. MOLLEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** ...walioteuliwa, 26 walikuwa ni wanaume, sawa na asilimia 89.7...

**SPIKA:** Mheshimiwa Ruth, kuna taarifa muhimu sana. Utulie hapo hapo tu, usiende kukaa. Utulie hapo hapo tu Mheshimiwa Ruth.

Mheshimiwa Mollel, kuna nini? Ni Taarifa ya Mheshimiwa Mollel kwenda kwa Mheshimiwa Mollel, kwa hiyo, tulieni. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Ruth baki hapo hapo, usiondoke. Baki tu hapo hapo. Mheshimiwa Mollel!

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nasimama kwa Kanuni ya 68(1).

Mheshimiwa Spika, napingana na Taarifa ya Kambi ya Upinzani ambapo nitanukuu, anasema kwamba; "Kwa upande wa Bara la Afrika vuguvugu la kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya maamuzi lilipelekea nchi wanachama wa Jumuiya ya SADC kuazimia kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vya maamuzi angalau katika asilimia 50." Ibara ya 12 ya Mkataba wa SADC inasema kwamba, *Parties shall endeavour that 2015 at least fifty percent of decision making positions in Public...*"

Mheshimiwa Spika, nilichotaka kusema ni kwamba, wao wenyewe ndiyo ambao kwa namna moja au nyingine wameonesha... (*Kicheko/Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Waambie.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Wamekuwa wakizipunguza hizi asilimia na kwa mfano dhahiri ambao umetokea hivi karibuni, ni katika uchaguzi wa Bunge la Afrika Mashariki... (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Taarifa. (*Makofi*)

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Hawakuleta mwanamke hata mmoja.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa. (*Makofi*)

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Kwa hiyo, wao ni wa kwanza wanasingana haki za wanawake...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa!

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Halafu hapa wanakuja kuilaumu Serikali. Ahsante.

**SPIKA:** Basi, basi jamani!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** *Order! Order! Order!* Mheshimiwa Ruth Mollel, Taarifa ni ya kwako.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Ukiipokea sawa, utajua cha kufanya, halafu endelea kusoma. Wengine wote tulieni sasa. Mnamvuruga sana Mheshimiwa Ruth Mollel.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa!

**SPIKA:** Mheshimiwa Silinde ukae! Ukae! Endelea Mheshimiwa Ruth!

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, Ila hakuna Taarifa katika hotuba.

**SPIKA:** Wewe unawasha ndiyo maana anashindwa kuwasha aliyeko huku mbele, eeh!

**MHE. RUTH H. MOLLEL – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, siipokei taarifa. (*Makofii*)

Nataka ninukuu Ibara ya 12 ya Mkataba wa SADC, inasema: “*Parties shall endeavour that, 2015 at least fifty percent of decision making positions in Public and Private sector are held by women including the use of affirmative action measures as provided for in article 5.*” (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, taarifa ya TGNP inaonesha kwamba katika Makatibu Wakuu 29 walioteuliwa 26 walikuwa ni wanaume sawa na asilimia 89.7 huku wanawake wakipungua kutoka watano sawa na asilimia 21.7 ya mwaka 2014 hadi kufikia watatu sawa na asilimia 10.3 kwa sasa na hivyo kufanya uteuzi wa wanawake katika nafasi hizo kupungua kwa asilimia 10.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Wakuu wa Mikoa, idadi ya wanawake imeshuka zaidi. Kati ya Wakuu wa Mikoa 26 ya Tanzania Bara, 21 ni wanaume sawa na asilimia 80 na wanawake ni watano tu, sawa na asilimia mbili. Hali kadhalika idadi ya Wakuu wa Wilaya imezidi kuporomoka ikilinganishwa na awamu iliyopita. Hali hii ya kushuka kwa uteuzi wa wanawake inaonekana pia kwa nafasi za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wakati Tanzania ni kati ya mataifa duniani yaliyordhia na kusaini mikataba mbalimbali ya Kimataifa na ya kikanda inayoweka misingi ya usawa wa binadamu ikiwamo ushiriki katika ngazi zote za maamuzi, lakini haitekelezi mikataba hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaikumbusha Serikali kwamba ni sera ya dunia ya kuhakikisha kwamba kuna ushirikishwaji katika ngazi za maamuzi kwa sababu makundi ya wanawake, wale mavu na kadhalika, yana mahitaji tofauti, hivyo uwakilishi wao ni muhimu sana. Aidha, Serikali itambue pia kwamba kundi la wanawake ndiyo kundi la uhakika la wapiga kura. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mafunzo ya watumishi wa umma; watumishi ni rasilimali ya msingi katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Serikali katika ngazi ya Taasisi na Taifa kwa ujumla. Nguvu na mafanikio ya Taasisi yoyote na Taifa lolote inategemea aina ya watumishi waliopo kwenye taasisi au Taifa husika. Kwa msingi huo hawana budi kuendelezwa ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini wa mwaka 2010 mpaka 2014 (MKUKUTA – II) ulipangwa utatekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, unasisitiza suala la kujenga uwezo, weledi upangaji na matumizi mazuri ya rasilimali watu kuwa ni moja ya njia muhimu ya kuliwezesha Taifa kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, kimsingi utumishi wa Umma hauwezi kuwa na watumishi bora wenye upeo wa kutekeleza majukumu yao kufikia malengo ya taasisi na Taifa kama mafunzo hayatapewa kipaumbele. Kutoa mafunzo nijukumu la msingi la Serikali, hivyo kusomesha watumishi ni sawa na kuwekeza katika sekta ya barabara, afya na maji. Hivyo basi, umuhimu wa kuwaendeleza watumishi kila wakati haukwepeki. Unahitaji kutekelezwa ili kuwawezesha watumishi hao kwa kuwa ni nguvu na injini ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuzingatia mazingira yaliyopo.

Mheshimiwa Spika, Waraka Na. 5 wa mwaka 2011 unasisitiza watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza wapatiwe mafunzo elekezi ya awali ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu kuajiriwa; waajiri wote wahakikishe kwamba watumishi wapya wafanyiwe upekuzi kwanza na kupatiwa mafunzo elekezi yanayohusiana na majukumu yao; na tatu, waajiri wote wanapaswa kutenga fedha kwenye bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya mafunzo haya.

Mheshimiwa Spika, licha ya maelekezo ya waraka huo, katika Awamu ya Tano, waajiri wamekuwa wakitenga bajeti kidogo au kutengenya kabisa kwa ajili ya mafunzo, hivyo kutoa kipaumbele cha mwisho katika mipango na bajeti. Aidha, programu za mafunzo zimekuwa haziendani na mahitaji kwa maana kwamba mafunzo yatolewayo hayamwandai mtumishi kuwa mbobezi katika kazi yake au kupanda ngazi na kupata madaraka zaidi.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha zaidi kwamba hata pale mafunzo yanapotolewa, watumishi hushawishika kuacha kazi Serikalini kwa sababu ya mshahara kutolingana na ujuzi walioupata, mfumo usioruhusu mabadiliko yanayoendana na ujuzi mpya wa mtumishi na kukosekana kwa ushindani.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba programu ya mafunzo kwenye kila idara, ipewe kipaumbele katika bajeti.

Aidha, Serikali ipanue wigo wa mafunzo nje ya nchi kwani mazingira ya nje yanampa mtumishi uzoefu (*exposure*) kwa kutazama mambo kwa namna tofauti. Vilevile baada ya mafunzo, yawepo mabadiliko ya ngazi na majukumu yanayoendana na mafunzo mapya ya mtumishi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 2016, nilizungumzia kuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 5 ya mwaka 2002 kuhusu utumbuaji wa watumishi usiozingatia taratibu za kikanuni na kisheria. Ukiukwaji huo bado unaendelea licha ya kupingwa vikali na Tume ya Haki za Binadamu na wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, bado Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya wameendelea kukiuka sheria hiyo kwa kuwafukuza kazi watumishi kiholela na mbaya zaldi wanafanya hivyo hadharani, kwenye mikutano ya hadhara. Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi; narudia Kambi Rasmi ya Upinzani haipingi watumishi kuchukuliwa hatua za kinidhamu pale inapothibitika ni wakosaji, lakini hatua hizo zizingatie utaratibu wa sheria uliowekwa ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi ya kujieleza na kujitetea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kutokana utumbuaji holela, hofu imejengeka kwa watumishi, ari ya utendaji kazi imepungua, heshima ya utumishi wa umma imeshuka jambo ambalo limeshusha ufanisi katika utumishi wa umma. Watumishi wa umma hawana ubunifu tena, wala ujasiri wa kufanya maamuzi, kutokana na uwoga kwamba wanaweza kukosea halafu baadaye wakatumbuliwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaendelea kusisitiza kuzingatiwa kwa sheria, kanuni na taratibu katika kushughulikia nidhamu ya utumishi wa umma ili kujenga utumishi wa umma madhubuti, unaojiamini na unaozingatia haki na utawala bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni dhana inayoelewaka kwamba utumishi wa umma unatakiwa usiwe na mrengo wowote

wa kisiasa (*neutral and impartial*) na kwamba uwe tayari mara zote kutekeleza sera za Serikali ya chama chochote kitakachoingia madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lengo la dhana hiyo ni kuifanya sekta ya utumishi wa umma kuwa endelevu (*stable*) na kuepuka mabadiliko ya watendaji wakuu kila Serkali ya chama tofauti kinapoingia madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali hii ya Awamu ya Tano imekiuka dhana hiyo kwa kuingiza siasa katika utumishi wa umma. Katika Awamu hii ya Tano, tumeshuhudia nafasi za utendaji Serikalini zikitolewa kwa makada na wakereketwa wa Chama cha Mapinduzi ambaa baadhi hawana hata ufahamu wa uendeshaji Serikalini.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia uteuzi wa Afisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambaye alikuwa bado kazini akiteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kasulu na baadaye kuenguliwa nafasi yake na kurudishwa Jeshini. Tumeshuhudia pia Naibu Katibu Mkuu wa Tume ya Mipango akigombea Ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki huku akiwa bado mtumishi wa ngazi ya juu Serikalini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, idadi kubwa ya Wakurugenzi Watendaji 65 kati ya 195 walioteuliwa walikuwa wagombea wa Ubunge kwenye kura za maoni za CCM. Aidha, baadhi ya Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya na Makatibu Wakuu ni wakereketwa wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, matokeo ya maamuzi ni kuingiza siasa katika utumishi wa umma na kupoteza weledi (*professionalism*), ni kupanda mbegu mbaya ya ubaguzi wa kisiasa katika utumishi wa umma. Inakuwaje kwa mfano chama kingine kikichukua madaraka ya dola, hali ya watumishi wenye itikadi tofauti itakuwaje? Je, Naibu Katibu Mkuu wa Tume Mipango ambaye kura zake hazikutosha katika kugombea Ubunge wa Afrika Mashariki, amerudi kazini? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaiasa Serikali

kuacha kuteua au kuajiri watumishi kutokana na itikadi za kisiasa. (*Makof*)

Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali ijenge utumishi wa umma wenyewe weledi ambao uhai wake hautegemei chama kilichopo madarakani, bali utumishi wa umma endelevu unaotumikia wananchi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ilisitisha ajira mpya kwa maelezo kwamba iili kuwa ikifanya uhakiki wa watumishi. Hata hivyo, Serikali imeanza tena kutoa ajira mpya. Kambi Rasmi Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako Tukufu hili kama uhakiki umekamilika na ni kitu gani kilichogundulika katika uhakiki huo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na tatizo la ukosefu wa ajira kuendelea kukua katika nchi yetu na kutokana na matukio ya utumbuaji holelea na mfumo wa uajiri usiotabirika; vijana wengi wa nchi hii waliofuzu masomo yao wameingiwa na hofu na kukata tamaa kwa kuwa hawajui kesho yao itakuwaje.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri na kupendekeza kwamba Serikali iwe inatoa Mpango wake wa ajira katika sekta mbalimbali kwa kila mwaka wa fedha ili watu wajue ni ajira ngapi zitatoka katika mwaka husika wa fedha. Kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulielezaa Bunge hili kuwa imepanga kutoa ajira ngapi katika mwaka wa fedha 2017/2018? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, licha ya umuhimu wa kuwa na mpango wa ajira unaotabirika, ujira wa watumishi nalo ni jambo la kuzingatia. Ujira una faida za aina mbili; kwanza unamtegemeza mtumishi kwa maana ya kipato ambacho atakitungia kujikimu na kuendesha shughuli zake nyingine; lakini pili, ni chanzo cha mapato ya Serikali kuitia kodi ya mapato ya *Pay As You Earn*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali hiyo, maboresho ya ujira kwa watumishi ni jambo la msingi sana. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Tume ya Taifa ya Takwimu, zinaonesha kwamba ujira kwa mwezi kwa sekta zote za ajira, takriban asilimia 25.3 wanapokea kati ya shilingi 300,000 mpaka shilingi 500,000; asilimia 17.9 wanapokea kati ya shilingi 500,000 na shilingi 1,500,000. Hivi ndivyo viwango vya mishahara ambayo watumishi wengi wanapokea na hawa ndio walipa kodi wa uhakika wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya viwango hivi kwani haviendo na mpango wa maendeleo wa miaka mitano unaohitaji Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, maendeleo ni kwa watu na siyo kwa vitu; na uchumi ambao siyo shirkishi hauwezi kuwa ni uchumi endelevu. Naomba kunukuu kauli ya Mwalimu Nyerere kwamba; “*you cannot develop people, you must allow people to develop themselves.*” Hivyo ujira stahiki kwa kazi stahiki ndiyo nyenzo pekee ya kumletea Mtanzania maendeleo na siyo vinginevyo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitengewa kiasi cha shilingi billioni 30.3. Kati ya hizo shilingi billioni 22.7 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi billioni 7.5 kwa ajili ya kutegeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, Ofisi hii ilipokea jumla ya shilingi billioni 16.3 sawa na 53.8%; katи ya hizo, shilingi billioni 15.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 690 sawa na 9.1% tu kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kiasa cha fedha za maendeleo zilizotolewa mpaka Machi, 2017 haikidhi bajeti ya maendeleo katika Wizara. Kwa mwaka 2017/2018 Wizara inaombaa kuidhinishiwa shilingi billioni 32.5 ambalo niongezeko la shilingi

bilioni 2.2 ukilinganisha na maombi ya mwaka uliopita. Kati ya maombi hayo, shilingi bilioni 25.5 ni kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni saba ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha za maendelo zinazoombwaa kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni pungufu ya shilingi milioni 500.5 ukilinganisha na fedha za maendeleo za mwaka wa fedha 2016/2017. Tafsiri ya kutoteketeza bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 kwa asilimia 9na tafsiri ya kushusha kiwango cha fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kiashiria kwamba miradi ya maendeleo katika fungu hili siyo kipaumbele na kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza fungu hili lisitengewe kabisa fedha za maendeleo kwa kuwa inaonekana kwamba fedha hizo hazitolewi.

Mheshimiwa Spika, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni taasisi iliyo chini ya Ofisi ya Rais na inatekeleza majukumu mahususi kwa mujibu wa kifungu cha Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa mwaka 2007 ikiwa na jukumu kuu na la msingi la kuwezesha mchakato wa ajira katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya teknolojia yamegusa hata mchakato wa ajira duniani kote. Kuna mabadiliko ya nyenzo bora zinazotumika kuweza kupata watumishi wenyewe weledi na maadili. Hata hivyo bajeti ya Sekretarieti ya Ajira, haiakisi malengo ya mabadiliko hayo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Serkali kutenga bajeti ya kutosha kuwezesha Sekretariati ya Ajira ili wafanye kazi kitaalam, kwa sababu rasilimali watu ndiyo injini ya maendeleo. Bila kuajiri wataalam wananaofaa, lengo la kufikia uchumi wa kati litakuwa ndoto.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Maadili ya Viongozi ina jukumu kubwa la kusimamia maadili ya viongozi wa umma na kufanya uchunguzi wa awali wa malalamiko kuhusu ukiukwaji wa maadili na kufanya utafiti kuhusu hali ya uadilifu wa viongozi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu baadhi ya viongozi kukiuka maadili ya utumishi wa umma, kama kiongozi kudai kwa nguvu mali za watu kwa njia zisizo halali; kumiliki mali nydingi ukilinganisha na vyanzo vyake vya mapato; kuvamia ofisi za watu akiwa na askari ili kazi yake ipewe kipaumbele cha kwanza; kiongozi kufukuza na kuwadhalilisha watumishi wa umma hadharani bila ya kufuata utaratibu na kadhalika. Hizi zote ni changamoto ambazo zinatakiwa kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hatujawahi kusikia hatua ambazo zimechukuliwa na Tume hii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kwamba ili Tume hii iwe huru bila ya kuingiliwa na kiongozi yeyote, uteuzi wa Mtendaji Mkuu uthibitishwe na Bunge lako Tukufu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 taasisi hii ilipangiwa kupata shilingi bilioni 5.9 lakini hadi mwezi Machi, 2017 walipata kiasi cha shilingi bilioni 2.8 sawa na 49%; kati ya fedha hizo, matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 1.3 sawa na 52% ya matumizi ya kawaida. Taasisi hii kulingana na umuhimu wake wa kusimamia maadili ambapo ndiyo nguzo ya utawala bora kwa bajeti, hiyo bado ni kichekesho kutimiza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kupewa kiasi cha shilingi bilioni 5.9 na matumizi mengineyo wanaomba shilingi bilioni 2.6. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa umuhimu wa Taasisi hii iliyopo Kikatiba, kiasi hicho cha fedha ni kidogo katika kusimamia maadili ambayo ndiyo nguzo muhimu katika utawala bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika hitimisho, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuendelea kusisitiza suala la utawala bora katika nchi yetu. Kitendo cha Idara ya Usalama wa Taifa kutuhumiwa kwamba inaratibu na kuendesha vitendo vya utekaji na utesaji wa raia wasio na hatia ili kutimiza maslahi ya kisia ya baadhi ya viongozi, siyo jambo

lenye afya katika mustakabali wa usalama na amani ya nchi yetu iliyodumishwa kwa zaidi ya miaka 50. Aidha, kitendo cha Serikali kukanusha tuhuma hizo na kukataa kufanywa kwa uchunguzi juu ya jambo hilo, kunaacha maswali mengi yanayohitaji kupatiwa majibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, sisi ni viongozi ambao tuna jukumu la msingi la kujenga misingi ya utu, udugu na upendo kwa vizazi vijavyo ili Taifa liendelee kuwa salama na amani. Ushabiki wetu katika kuzuia jambo hili la utekaji nyara, mauaji ya viongozi wa Serikali za Mitaa, lisifanyiwe uchunguzi ni kubariki na kuhalalisha matukio hayo yaendelee kufanyika hapa nchini. Tarehe 14 Aprili tumeshuhudia si utekaji tena nyara au mauaji ya viongozi wa Serikali za Mitaa, bali limegusa sasa hata Jeshi letu la Polisi.

Mheshimiwa Spika, ni ombi langu binafsi na ombi la Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba katika hatua hii, Serikali itoe tamko kuhusiana na jambo hili ili kuondoa mashaka au mawazo ya watu ambao wanafikiri ukimya huu wa Serikali na kukataa huku kwa Serikali uchunguzi wa masuala haya usifanyike, yumkini Serikali ndiyo inayoratibu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ruth Mollel. Nakushukuru sana, kwa wasiomfahamu Mheshimiwa Ruth Mollel mara ya mwisho alikuwa Katibu Mkuu, Ofisiya Makamu wa Rais na mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati kwa hiyo kuna wakati alikuwa anaripoti kule kwangu ilikuwa shughuli, sasa siku hizi namkumbusha na wewe jel! (*Makofii/ Kicheko*)

Kwenye hotuba hii alitajwa mgombea mmoja wa Afrika Mashariki, napenda niseme tu kwamba katika uchaguzi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, wanaokatazwa na sheria ni Wabunge tu hawa mliopo ndani humu, lakini hakuna mahali panakataza mtumishi wa umma kugombea nafasi hiyo. Hiyo ni hivyo hivyo kwa Afrika Mashariki nzima.

Kwa hiyo, tusijetukamlamu mtu ye yeyote au kumvunja moyo mtu ye yeyote siku zijazo kama mtumishi au sio mtumishi akiomba nafasi hizo. Hata akikosa inakuwa haina athari. (*Makofii*)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – UTUMISHI NA UTAWALA  
BORA, MHESHIMIWA RUTH HIYOB MOLLEL (MB),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI RASMI YA  
UPINZANI BUNGENI (KRUB) KUHUSU BAJETI YA  
OFISI HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge,  
Toleo la Januari, 2016*

---

## **1. UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili lli kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais- Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii pia kutoa salamu za rambi rambi kwa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ofisi ya Bunge, na familia ya Macha kwa kuondokewa na Mbunge mwenzetu marehemu Dkt. Elly Macha. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

**Mheshimiwa Spika**, kabla sijatoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Rais – Utumishi na Utawala Bora, naomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kulaani kwa nguvu zote vitendo vinavyoendelea kutokea katika nchi yetu vya utekaji, utesaji na uuaji wa raia na polisi wasio na hatia hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika**, ni bahati mbaya sana kwamba, wakati matukio haya yanaendelea kutokea, Serikali nzima pamoja na vyombo vyake vya ulinzi na usalama, imekaa kimya na hajatoa tamko lolote juu ya jitihada zinazofanyika kukabiliana na matukio haya yanayoikumba nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshangazwa pia na kitie cha spika kiliviyotumika vibaya kuzuia wabunge ambaao ni wawakilishi wa wananchi na ambaao baadhi yao wamelalamika kuwa wametishiwa maisha, kujadili jambo hilo kwa kujificha nyuma ya kivili cha Kanununi za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imeshtushwa pia kuona Waziri anayehusika na Utawala Bora kukataa masuala yanayohusu utawala bora kujadiliwa Bungeni na kuongeza kwamba wanaolalamikia matukio ya utekaji na utesaji ni wachochazi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inalasa Serikali kuacha kuzuia Bunge kujadili suala hilo vinginevyo wananchi wanaweza kufikiri matukio hayo ya utekaji na utesaji yanayloratibiwa na vyombo vya dola na ndio maana serikali inaona ugumu wa kutoa kauli kuhusu jambo hilo. Mheshimiwa Spika, tukio la kuuwawa kwa polisi wanane tarehe 14/04/17 liisukume Serkali kutoa tamko kuhusu Ulinzi na Usalama wan chi yetu.

**Mheshimiwa Spika**, kuna usemi usemao kwamba “vyombo vya ulinzi na usalama vinapolinda Serikali basi vinakuwa adui wa wananchi” na hicho ndicho kinachotokea sasa katika nchi yetu. Mtazamo wa kuilinda Serikali usipobadilika basi usalama upo mashakani, kwani ni dhahiri kwamba vyombo hivyo vinatagema taarifa toka kwa wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri wahusika wajitafakari kwa amani ya nchi yetu.[**Maneno haya siyo sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

## 2. SERIKALI YA AWAMU YA TANO INAVYOKIUKA MISINGI YA NA UTAWALA BORA

**Mheshimiwa Sika**, dhana ya utawala bora imejengwa katika msingi wa Katiba ya nchi inayoheshimu mgawanyo wa madaraka katika mihimili mikuu ya dola ,demokrasia,

utawala wa sheria, haki za binadamu na uhuru wa kutoa maoni na kupata habari, uhuru wa kukusanyika na kuijunga na mashirika au vyama mbalimbali katika jamii n.k Aidha, utawala bora una sifa za uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu usawa na kuzingatia taratibu za kisheria na kikanuni katiaka utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Serikali.

## **2.1. Uwajibikaji wa Pamoja**

**Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoeleza hapo awali, dhana ya utawala bora ina sifa ya uwajibikaji wa pamoja. Tofauti na awamu zilizopita za utawala, Sifa hii muhimu ya utawala bora ya uwajibikaji wa pamoja (collective responsibility) imeanza kupotea katika Serikali hii ya awamu ya tano.

**Mheshimiwa Spika**, nasema hivi kwa sababu tumeshuhudla kwa nyakati tofauti kauli zinazokinzana za serikali hiyo hiyo moja. Kwa mfano, matukio ya hivi karibuni la mkuu wa nchi kutengua hadharani agizo la aliyekuwa waziri wake wa Katiba na sheria juu ya sharti la kuwa na cheti cha kuzaliwa ili mtu aweze kufunga ndoa, waziri wa afya kutofautiana na makamu wa rais juu ya upungufu wa dawa na vifaa tiba nchini, mkuu wa nchi kupinga taarifa za njaa alizopewa na baadhi ya wakuu wa wilaya na mikoa, waziri wa ardhi kupinga mchakato wa kumpatia ardhi mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na mengine yanayofanana na hayo ni ishara tosha kwamba kuna tatizo kubwa la mawasiliano na uwajibikaji wa pamoja katika Serikali hii. Aidha, ni dalili mbaya kwamba Serikali inaelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake, kutohana na kutokuwa na msimamo wa pamoja.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri na kupendekeza kwamba Serikali irudi katika misingi ya uwajibikaji wa pamoja ambao ni sifa muhimu ya utawala bora. Serekali izungumze lugha moja. Waziri mmoja anapotoa tamko, tamko hilo liwe ni kwa niaba ya Serikali nzima kwani kwa kutofanya hivyo Serikali itawachanganya wananchi. Aidha, Mkuu wa nchi awaache mawaziri wake wafanye kazi kwa kujiamini ili wawe na tija katika majukumu yao.

Kuwaingilia kila wakati au kuwapinga hadharani kunawavunja moyo na kunawafanya wafanye kazi kwa woga wakihofia kutumbuliwa au kuumbuliwa.

### **Usawa wa Jinsia na Ushirikishwaji katika vyombo vyamuzi**

**Mheshimiwa Spika**, usawa wa jinsia na ushirikishwaji katika vyombo vyamuzi ni miongoni mwa nguzo muhimu za utawala bora. Kumekuwa na tatizo duniani la ushirikishwaji hasa wa wanawake katika vyombo vyamuzi. Kutokana na hali hiyo kumekuwa na vuguvugu katika mataifa mbalimbali duniani ya kuhakikisha kuwa wanaweke wanawakilishwa vyya kutosha katika vyombo vyamuzi ili kukidhi matakwa ya utawala bora.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa bara la Afrika, vuguvugu la kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vyamuzi lilipelekea nchi wananchama wa Jumuiya ya SADC kuazimia kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vyamuzi angalau kufikia asilimia 50. Ibara ya 12 ya mkataba wa SADC inasema kwamba: *“Parties shall endeavour that, 2015, at least fifty percent of decision-making positions in Public and Private sector are held by women including the use of affirmative action measures as provided for in article 5”*

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya SADC na iliridhia mkataba huo. Kulikuwa na jitihada za kuongeza nafasi za wanawake katika vyombo vyamuzi hapa nchini katika Serikali ya awamu iliyopita lakini takwimu zinaonyesha kwamba nafasi za wanawake katika awamu hii ya tano zimezungua.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa taarifa ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) ni kwamba, hadi kufikia Julai, 2016 uteuzi wa Baraza la Mawaziri ulionyesha kushuka kwa idadi ya wanawake ukilinganisha na kipindi cha Serikali ya awamu ya nne. Wakati serikali ya awamu ya nne iliteua mawaziri wanawake 10 sawa na asilimia 33.3 ya Baraza lote, Serikali ya awamu ya tano iliteua mawaziri wanawake wanne tu kat

ya mawaziri 19 sawa na asilimia 21.1 na hivyo kufanya uteuzi wa wanawake mawaziri kushuka kwa asilimia 12.2.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya TGNP inaonyesha pia kwamba, kati ya makatibu wakuu 29 walioteuliwa, 26 walikuwa ni wanaume sawa na asilimia 89.7 huku wanawake wakipungua kutoka watano sawa na asilimia 21.7 ya mwaka 2014 hadi kufikia watatu sawa na asilimia 10.3 kwa sasa, na hivyo kufanya uteuzi wa wanawake katika nafasi hizo kupungua kwa asilimia 10.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa wakuu wa mikoa, idadi ya wanawake imeshuka zaidi. Kati ya wakuu wa mikoa 26 ya Tanzania Bara, 21 ni wanaume sawa na asilimia 80 na wanawake ni watano tu sawa na asilimia mbili. Hali kadhalika idadi ya wakuu wa wilaya imezidi kuporomoka ikillinganishwa na awamu iliyopita. Hali hii ya kushuka kwa uteuzi wa wanawake inaonekana pia kwa nafasi za makatibu tawala wa mikoa na wilaya na wakurugenzi wa halmashauri.

**Mheshimiwa Spika**, wakati Tanzania ni kati ya mataifa duniani yaliyordhia na kusaini mikataba mbalimbali ya kimataifa na kikanda inayoweka misingi ya usawa kwa binadamu ikiwamo ushiriki katika ngazi zote za maamuzi, lakini haitekelezi mikataba hiyo. Mikataba hiyo ni pamoja na Tamko la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu (UDHR: 1948), Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW: 1979), Mpango kazi wa Beijing (1995), Mkataba wa Ziada wa Maputo na Mkataba wa Nyongeza wa Jinsia na Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaikumbusha Serikali kwamba ni sera ya dunia ya kuhakikisha kwamba kuna ushirikishwaji (inclusiveness) katika ngazi za maamuzi kwa sababu makundi ya wanawak, walemavu nk yana mahitaji tofauti, hivyo uwakilishi wao ni muhimu sana. Aidha, Serikali itambue pia kwamba kundi la wanawake ndio kundi la uhakika la wapiga kura hivyo,

### **3.0. MAFUNZO KWA WATUMISHI WA UMMA**

**Mheshimiwa Spika**, Watumishi ni Rasilimali ya msingi katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu na malengo ya Serikali katika ngazi ya Taasisi na Taifa kwa ujumla. Nguvu na mafanikio ya Taasisi yoyote na Taifa lolote inategemea aina ya watumishi waliopo kwenye Taasisi au Taifa husika. Kwa msingi huo hawana budi kuendelezwa ili waweze kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania 2010/11-2014 (MKUKUTA - II) uliopangwa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, unasisitiza suala la kujenga uwezo, weledi upangaji na matumizi mazuri ya Rasilimaliwatu kuwa ni moja ya njia muhimu ya kuliwezesha Taifa kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo 2025.

**Mheshimiwa Spika**, Kimsingi utumishi wa umma hauwezi kuwa na watumishi bora wenye upeo wa kutekeleza majukumu yao kufikia malengo ya taasisi na taifa kama mafunzo hayatapewa kipaumbele

**Mheshimiwa Spika**, Kutoa mafunzo ni jukumu la msingi la serikali, hivyo kusomesha watumishi ni sawa na uwekezaji katika sekta ya barabara, afya na maji. Hivyo basi, Umuhimu wa kuwaendeleza watumishi kila wakati haukwepeki. Unahitaji kutekelezwa ili kuwawezesha watumishi hao kuwa nguvu na injini ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuzingatia mazingira yалиyopo. Waraka Na. 5 wa mwaka 2011 unasisitiza kwamba:

- i. Watumishi wanaoajiriwa kwa mara ya kwanza wapatiwe mafunzo elekezi ya awali ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu kuajiriwa.
- ii. Waajiri wote wahakikishe kwamba watumishi wapya wafanyiwe upekuzi kwanza na kupatiwa mafunzo elekezi yanayohusiana na majukumu yao.

- iii. Waajiri wote wanapaswa kutenga fedha kwenye bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya mafunzo haya.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya maelekezo ya waraka huo, katka Awamu hii tano, waajiri wamekuwa wakitenga bajeti kidogo au kutotenga kabisa kwa ajili ya mafunzo, hivyo kutoa kipaumbele cha mwisho katika mipango na bajeti. Aidha, Programu za mafunzo zimekuwa haziendani na mahitaji kwa maana kwamba mafunzo yatolewayo hayamwandai mtumishi kuwa mbobezi katika kazi yake au kupanda ngazi na kupata madaraka zaidi. I

**Mheshimiwa Spika**, inasikitisha zaidi kwamba, hata pale mafunzo yanapotolewa, watumishi hushawishika kuacha kazi Serkalini kwa sababu ya mshahara kutolingana na ujizi walioupata, mfumo usioruhusu mabadiliko yanayoendana na ujizi mpya wa mtumishi na kukosekana kwa ushindani.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba program ya mafunzo kwenye kila idara ipewe kipaumbele katika bajeti. Aidha, Serikali ipanue wigo wa mafunzo nje ya nchi kwani mazingira ya nje yanampa mtumishi *exposure* uzoefu wa kutazama mambo kwa namna tofauti. Vilevile, baada ya mafunzo, yawepo mabadiliko ya ngazi na majukumu yanayoendana na mafunzo mapya ya mtumishi

#### 4. UTUMBUAJI WA WATUMISHI USIOZINGATIA SHERIA.

**Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16, nilizungumzia kuhusu ukiukwaji wa sheria ya Utumishi wa Umma na 5 ya mwaka 2002 kuhusu utumbuaji wa watumishi usiozingatia taratibu za kikanuni na kisheria. Ukiukwaji huo bado unaendelea licha ya kipingwa vikali na Tume ya Haki za Binadamu na wananchi kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika**, bado Mawaziri, wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya wameendelea kukiuka sheria hiyo kwa kuwafukuza kazi watumishi kiholela na mbaya zaidi wanafanya hivyo hadharani kwenye mikutano ya hadhara.

Kambi rasmi ya Upinzani haipingi watumishi kuchukuliwa hatua za kinidhamu pale inapothibitika ni wakosaji lakini, hatua hizo zizingatie utaratibu wa sheria uliowekwa ikiwa ni pamoja na kuwapa nafasi ya kujieleza na kujitetea.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana utumbuaji holela, hofu imejengeka kwa watumishi, ari ya utendaji kazi imepungua, heshima ya utumishi wa umma imeshuka jambo ambalo limeshusha ufanisi katika utumishi wa umma. Watumishi wa umma hawana ubunifu tena, wala ujasiri wa kufanya maamuzi, kutokana na woga kwamba wanaweza kukosea halafu baadaye wakatumbuliwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza kuzingatiwa kwa sheria, kanuni na taratibu katika kushughulikia nidhamu ya utumishi wa umma ili kujenga Utumishi wa Umma madhubuti, unaojiamini na unaozingatia haki na utawala wa sheria

## 5. USHIRIKI WA WATUMISHI WA UMMA KATIKA SIASA

**Mheshimiwa Spika**, ni dhana inayoeleweka kwamba utumishi wa umma unatakiwa kuwa '*neutral and impartial*' (yaani usiwe na mrengo wowote wa kisiasa) na kwamba uwe tayari mara zote kutekeleza sera za Serikali ya chama chochote kitakachoingia.

**Mheshimiwa Spika**, lengo la dhana hiyo, ni kuifanya sekta ya utumishi wa umma kuwa endelevu (stable) na kuepuwa mabadiliko ya watendaji wakuu kila Serkali ya chama tofauti kinapoingia madarakani. **Mheshimiwa Spika**, Serikali hii ya awamu ya tano imekiuka dhana hiyo kwa kuingiza siasa katika utumishi wa umma. Katika awamu hii ya tano, tumeshuhudia nafasi za utendaji Serikalini zikitolewa kwa Makada na wakereketwa wa CCM ambao baadhi hawana hata ufahamu wa uendeshaji Serkalini(Government Adminisration). Tumeshuhudia uteuzi wa Afisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania ambaye alikuwa bado kazini akiteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kasulu na baadaye kuenguliwa nafasi yake na kurudishwa Jeshini. Tumeshuhudia

pia Naibu Katibu Mkuu wa Tume ya Mipango akigombea ubunge wa Bunge la Afrika Mashariki huku akiwa bado mtumishi wa ngazi ya juu Serkalini.

**Mheshimiwa Spika**, Idadi kubwa ya Wakurugenzi Watendaji 65 katи ya 195 walioteuliwa walikuwa wagombea wa ubunge kwenye kura za maoni za CCM. Aidha, baadhi ya Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya na Makatibu wakuu ni wakereketwa wa Chama cha Mapinduzi.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya maamuzi ni kuingiza siasa katika utumishi wa umma na kupoteza weledi "Professionalism" na ni kupanda mbegu mbaya ya ubaguzi wa kisiasa katika utumishi wa umma. Inakuwaje kwa mfano, chama kingine kikichukua madaraka ya dola? Hali ya watumishi wenye itikadi tofauti itakuwaje? Je Naibu Katibu Mkuu wa Tume Mipango ambaye kura zake hazikutosha katika kugombea Ubunge wa Afrika Mashariki amerudi kazini? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaiasa Serikali kuacha mara moja kuteua au kuajiri watumishi kutohana na itikadi za kisiasa. Aidha, Kambi Rasmi ya upinzani inaishauri Serkali ijenge, utumishi wa umma wenye weledi ambaouhai wake hautegemei Chama kilichopo madarakani, bali Utumishi wa Umma endelevu unaotumikia wananchi.

## **6. UHAKIKI WA WATUMISHI, AJIRA MPYA NA UJIRA WA WATUMISHI**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilisitisha ajira mpya kwa maelezo kwamba ilikuwa ikifanya uhakiki wa watumishi. Hata hivyo, Serikali imeanza tena kutoa ajira mpya. Kambi Rasmi Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili kama uhakiki umekamilika na ni kitu gani kilichogundulika katika uhakiki huo.

**Mheshimiwa Spika**, kutohana na tatizo la ukosefu wa ajira kuendelea kukua katika nchi yetu, na kutohana na matukio ya utumbuaji holelea na mfumo wa uajiri usiotabirika, vijana wengi wa nchi hii waliofuzu masomo yao wameingiwa na hofu na kukata tama kwa kuwa hawajui kesho yao itakuwaje.

Kutokana na hali hiyo. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri na kupendekeza kwamba Serikali iwe inatoa Mpango wake wa ajira katika sekta mbalimbali kwa kila mwaka wa fedha ili watu wajue ni ajira ngapi zitatoka katika mwaka husika wa fedha. Kwa muktadha huo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulielezaa Bunge hili kuwa imepanga kutoa ajira ngapi katika mwaka wa fedha 2017/18?

**Mheshimiwa Spika**, licha ya umuhimu wa kuwa na mpango wa ajira unaotabirika, ujira wa watumishi nalo ni jambo la kuzingatia. Ujira una faida za aina mbili; kwanza unamtegemeza mtumishi kwa maana ya kipatoa ambacho atakitungia kujikimu, na kuendesha shughuli zake nyingine, lakini pili, ni chanzo cha mapato ya Serikali kupitia kodi ya mapato kwa watumishi (PAYE).

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia hali hiyo, maboresho ya ujira kwa watumishi ni jambo la msingi sana. Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Tume ya Taifa ya Takwimu zinaonesha kwamba ujira kwa mwezi kwa sekta zote za ajira, takriban asilimia 25.3 wanapokea kati ya shilingi 300,001/- na 500,000/- Asilimia 17.9 wanapokea kati ya shilingi 500,001/- na 1,500,000/. Hivi ndivyo viwango vya mishahara ambayo watumishi wengi wanapokea na hawa ndio walipakodi wa uhakika wa nchi yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuangalia upya viwango hivi kwani haviendani na mpango wa maendeleo wa miaka mitano unaohitaji Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati.

**Mheshimiwa Spika**, maendeleo ni kwa watu na sio kwa vitu, na uchumi ambao sio shirikishi hauwezi kuwa ni uchumi endelevu. Naomba kunukuu kauli ya Mwalimu Nyerere kwamba *"You cannot develop people, you must allow people to develop themselves"*, hivyo ujira stahiki kwa kazi stahiki ndiyo nyenzo pekee ya kumletea Mtanzania maendeleo na si vinginevyo.

**7. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS -  
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA  
BORA**

**7.1. Menejimenti ya Utumishi wa Umma ( Fungu  
32)**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Menejimenti ya Utumishi wa umma ilitengewa kiasi cha **shilingi bilioni 30.341**, kati ya hizo shilingi bilioni 22.79 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7.55 kwa ajili ya kutegeleza miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Machi, Ofisi hii ilipokea jumla ya shilingi bilioni 16.338 sawa na 53.8% kati ya hizo shilingi bilioni 15.65 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 690 sawa na asilimia 9.14 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kiasa cha fedha za maendeleo zilizotolewa hadi Machi, 2017 haikidhi bajeti ya maendeleo katika Wizara . Kwa mwaka 2017/18 Wizara inaomba kuidhinishiwa shilingi bilioni 32.578 ambalo niongezeko la shilingi bilioni 2.237 ukilinganisha na maombi ya mwaka uliopita. Kati ya maombi hayo shilingi bilioni 25.578 ni kwa matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 7 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, fedha za maendelo zinazoombwa kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni pungufu ya shilingi milioni 500.5 ukilinganisha na fedha za maendeleo za mwaka wa fedha 2016/17. Tafsiri ya kutotekeleza bajeti ya mwaka wa fedha 2016/17 asilimia 90, na tafsiri ya kushusha kiwango cha fedha za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2017/18 ni kiashiria kwamba miradi ya maendeleo katika fungu hili sio kipaumbele na kwa maana hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza fungu hili isitengewe kabiasa fedha za maendeleo kwa kuwa inaoneka kwamba fedha hizo hazina kazi.

## 7.2. Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67)

**Mheshimiwa Spika**, Sekretarieti ya ajira katika utumishi wa umma, ni taasisi iliyo chini ya Ofisi ya Rais na inatekeleza majukumu mahususi kwa mujibu wa kifungu cha 29(4) na (6) cha sheria ya Utumishi wa Umma Na.8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 18 ya mwaka 2007, ikiwa na jukumu kuu na la msingi la kuwezesha mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika**, Mabadiliko ya teknologia, yamegusa hata mchakato wa ajira duniani kote, kuna mabadiliko ya nyenzo bora zinazotumika kuweza kupata watumishi wenyewe weledi na maadili, Hata hivyo bajeti ya Sekretariat ya ajira haikisi malengo ya mabadiliko hayo.

**Mheshimiwa Spika** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Serkali, kutenga bajeti ya kutosha kuwezesha Sekretariati ya Ajira ili wafanye kazi kitaalam. Rasilmali watu ndio engini ya Maendeleo bila kuajiri wataalam wananaofaa lengo la kufikia uchumi wa kati litakuwa ndoto.

## 7.3. Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (fungu 33)

**Mheshimiwa Spika**, taasisi hii ina jukumu muhimu la kusimamia maadili ya viongozi wa umma na kufanya uchunguzi wa awali wa malalamiko kuhusu ukiukwaji wa maadili, na kufanya utafiti kuhusu hali ya uadilifu wa viongozi wa umma.

**Mheshimiwa Spika**, kumekuwepo na malalamiko mengi kuhusu baadhi ya Viongozi kukiuka maadili ya Utumishi wa Umma km kiongozi kudai kwa nguvu mali za watu kwa njia zisizo halali, kumiliki mali nyingi kulinganisha na vyanzo vyake vya mapato, kuvamia ofisi za watu akiwa na askari ili kazi yake ipewe kipaumbele cha kwanza, kiongozi kufukuza na kuwadhalilisha watumishi wa umma hadharani bila ya kufuata utaratibu n.k. hizi zote ni changamoto ambazo

zinatakiwa kutatuliwa. Hata hivyo, hatujawahi kusikia hatua ambazo zimechukuliwa na Tume hii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaishauri Serkali kwamba ili Tume hii iwe huru bila ya kuingiliwa na kiongozi yeyote, Uteuzi wa mtendaji mkuu uthibitishwe na Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2016/17 Taasisi hii ilipangiwa kupata shilingi bilioni 5.914 lakini hadi mwezi March, 2017 fedha zilizopokelewa ni shilingi bilioni 2.885 sawa na 49% kati ya fedha hizo, matumizi mengineyo ni shilingi bilioni 1.317 sawa na 52% ya matumizi ya kawaida. Taasisi hii kulingana na umuhimu wake wa kusimamia maadili ambalo ndio nguzo ya Utawala bora kwa bajeti hiyo bado ni kichekesho kutimiza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka huu wa fedha 2017/18 Sekretarieti ya maadili ya viongozi wa umma inaomba kupewa kiasi cha shilingi bilioni 5.99 na matumizi mengineyo wanaomba shilingi bilioni 2.604. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa kwa umuhimu wa Taasisi hii iliyopo Kikatiba kiasi hicho cha fedha ni kidogo katika kusimamia maadili ambayo ndio nguzo muhimu katika utawala bora.

## 8. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, napenda kumalizia hotuba yangu kwa kuendelea kusisitiza suala la Utawala Bora katika nchi yetu. Kitendo cha Idara ya Usalama wa Taifa kutuhumiwa kwamba inaratibu na kuendesha vitendo vya utekaji na utesaji wa raia wasio na hatia ili kutimiza maslahi ya kisiasa ya baadhi ya viongozi wa Serikali, sio jambo lenye afya katika mustakabali wa usalama na amani ya nchi yetu iliyodumishwa kwa zaidi ya miaka 50. Aidha, kitendo cha Serikali kukanusha tuhuma hizo na kukataa kufanywa kwa uchunguzi juu ya jambo hilo kunaacha maswali mengi yanayohitaji kupatiwa majibu.

**Mheshimiwa Spika**, sisi ni viongozi ambao tuna jukumu la msingi la kujenga misingi ya utu, udugu na upendo kwa vizazi vijavyo ili taifa liendelee kuwa salama na amani. Ushabiki wetu katika kuzuia jambo hili la utekaji nyara, mauaji ya

viongozi wa serkali za mitaa, lisifanyiwe uchunguzi ni kubariki na kuhalalisha matukio hayo yaendelee kufanyika hapa nchini. Ijumaa tumeshuhudia si utekaji nyara au mauaji ya viongozi wa serkali za mitaa, bali limegusa sasa hata jeshi letu la polisi.

**Mheshimiwa Spika**, ni ombi langu binafsi na ombi la Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba, katika hatua hii, Serikali itoe tamko kuhusiana na jambo hili ili kuondoa mashaka au mawazo ya watu ambao wanafikiri ukimya huu wa Serikali, na kukataa huku kwa Serikali uchunguzi wa masuala haya usifanyike, yamkini Serikali ndiyo inayoratibu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Ruth Hiyob Mollel (Mb)

**WAZIRI KIVULI, NA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMMA NA UTAWALA BORA**

18 Aprili, 2017

**SPIKA:** Kama nilivyosema, katika wachangiaji wetu tunaanza na Mheshimiwa Bonnah Kaluwa, Dkt. Rashid Chuachua na Mheshimiwa Elias Kwandikwa. Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia katika Wizara hii nyeti. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka salama na kunipa nguvu za kuweza kuchangia siku hii ya leo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, napenda kutoa pongezi zangu kwa Mawaziri wote wawili ambao wameweza kutoa hotuba zao ambazo zimeonekana zina mashiko. Pia napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali yangu kwa miradi ambayo inaendelea kuzinduliwa katika Mkoa wa Dar es Salaam. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo, sasa naomba nianze mchango wangu kwa huduma za afya na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wizara hii ndiyo inayosimamia na kuratibu utoaji wa huduma za afya katika nchi yetu na ni Sera ya ya Wizara ya Afya kwamba kila Kata itakuwa na kituo cha afya. Pamoja na Jimbo la Segerea kuwa mjini na mpaka sasa lina watu 700,000 lakini Jimbo hili bado halina kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, miezi mitatu iliyopita tulifanya ziara na Naibu Waziri wa Afya na kugundua kwamba tuna zahanati ambazo zingeweza kupandishwa kutoka *level* ya zahanati kwenda kituo cha afya, lakini mpaka sasa hivi hazijapandishwa kuwa kituo cha afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kumalizia kusoma hotuba yake kwenye *ku-wind up* aweze kutuambia je, atatumia njia gani kutujengea kituo cha afya au atupandishie vituo vya afya ambavyo tunavyo viwili; kimoja kipo Tabata 'A' na kingine kipo Mnyamani ambacho ni *Plan International*? Hizi zahanati zote zina vigezo vya kuitwa vituo vya afya, lakini mpaka sasa hivi ni vitu vidogo vidogo tu ambavyo havijafanyika ili waweze kupandisha na kuwa vituo vya afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa namwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kumalizia kwenye hotuba yake aangalie ni jinsi gani kama wanaweza kutujengea kituo cha afya au waweze kutupandishia kituo cha afya au waweze kupandisha hivi ambavyo viro na vyenye upungufu mchache. Kwa hiyo, nilikua naomba hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nachopenda kuongelea ni kuhusu miundombinu ya elimu hususan Mkoa wa Dar es Salaam lakini katika Jimbo langu la Segerea. Mkoa wa Dar es Salaam, naomba kwa niaba ya wananchi wa Segerea, unakuta mtoto amefaulu anakaa Kata ya llala, lakini yule mtoto anapelekwa kwenda kusoma

Msongola. Msongola ni mbali; na hakuna mzazi ambaye anaweza kumlipia mtoto wake nauli kila siku ya kutoka llala kwenda Msongola. Kwanza mazingira yenyewe ni magumu na ukiangalia kwa watoto wetu wa kike wanakutana na changamoto nydingi sana wanapokuwa wanakwenda huko mashulen. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kutoka Kata ya llala kwenda Msongola kwanza ukifika Msongola kwenyewe hakuna tena basi ambalo linaenda huko kwenye hiyo shule.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mtoto inabidi atumie pipipiki. Pipipiki kutoka kituo ambacho anatoka kwenda kwenye shule ni shilingi 10,000. Ina maana ni shilingi 20,000 kwa siku. Hakuna mzazi ambaye anaweza kutoa shilingi 20,000 aweze kumlipia mtoto wake kila siku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu watoto wetu wa Dar es Salaam wanafeli kwa sababu hiyo na tuligundua taarifa ilipokuja kwamba Mkao wa Dar es Salaam umekuwa wa mwisho na Wilaya ya llala ndiyo imekuwa ya mwisho kielimu. Watoto wengine wameamua kupanga vyumba huko karibu na shule. Unakuta mtoto wa kike amepanga chumba, lakini kile chumba ana-share na mvulana. Kwa hiyo, unaweza ukajua kabisa kwamba hapa hakuna kitu chochote ambacho kinaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kuitia Wizara hii ambayo najua inashughulikia mambo ya elimu, watoto waweze kupangiwa sehemu waliyofaulu. Mtoto kama anakaa llala, amefaulu llala, apelikwe shule ya Kata ya llala. Kama anakaa Kipawa, basi apelekwe shule hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwa sababu siyo kwamba nafasi hazipo; nafasi zipo lakini sijui wanatumia utaratibu gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa nataka kuongelea...

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah, Maafisa Elimu wako ndio wanahusika na hilo, nakushauri tu. Endelea tu Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. BONNAH M. KALUWA:** Sawa.

Mheshimiwa Spika, lingine nililotaka kuongelea ni kuhusu fao la kujitoa. Linasema kwamba mtu anatakiwa afikishe miaka 55 ndiyo aweze kupewa yale mafao yake. Sasa hivi kuna watu wanaajiriwa kwa mkataba, anapewa kazi ya mkataba wa mwaka mmoja au miwili. Ina maana amepata mkataba wa kazi wa miaka miwili, halafu amalize hapo asubiri mpaka miaka 55! (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, licha ya hayo, kutokana na maisha magumu ya sasa hivi yanayoendelea, kwanza mtu unakuwa hauko *sure* kama utaishi kwa muda wa mlaka 55. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri aangalie tena upya kuhusu hili fao la kujitoa ili watu waweze kupewa mafao yao wanapomaliza kazi na kazi zenyewe kama nilivyosema ni kazi za mkataba. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nilichokuwa nataka kuongelea ni Mfuko wa Barabara. Pamoja na kwamba kuna miradi mingi inaendelea katika Mkoa wa Dar es Salaam lakini pia pamoja na Jimbo la Segerea, lakini tunajua kuna barabara zetu nyingi ambazo ndiyo barabara za mitaa ambapo Waziri wa TAMISEMI ndio anahuksika nazo. Katika Kata ya Kiwalani pamoja na Kata ya Minazi Mirefu kuna mradi mmoja wa DMDP. Huo mradi umekuwa ukipangiwa kila mwaka, sasa hivi mfululizo ni miaka mitano kwamba barabara za mitaani zitatengenezwa, lakini mpaka sasa hivi hatujajua. Tukiuliza Manispaa, bado wanasesma kwamba wanasubiri TAMISEMI ili waweze kuwalettea taarifa rasmi ni lini wataanza kutengeneza hizo barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri atakapomaliza, atueleze ili hawa wakazi ambao wanasubiri barabara zao kutengenezwa na kuna

wengine tayari wanasubiri kulipwa kwa sababu kuna nyumba ambazo inabidi zibomolewe, wapate muda *specific* ni lini barabara zinaanza kutengenezwa ili wajue na sisi tujue kwamba ni muda gani barabara hizo zitaanza kutengenezwa na mimi Mbunge maswali yapungue.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.  
(*Makofi*)

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia muda wa kuchangia eneo hili la TAMISEMI.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri wa TAMISEMI kwa kazi kubwa anayoifanya na wasaidizi wake, hongera sana Mheshimiwa Waziri. Kazi unayoifanya Watanzania wanalone na hotuba yako inaonesha kabisa mwelekeo wa bajeti yetu, lakini pia mwelekeo wa mambo ambayo yamefanywa katika bajeti iliyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia eneo la elimu. Ni kweli kabisa kuna tofauti kubwa kati ya elimu bila malipo na elimu bure. Hii tofauti ipo na Serikali imejitahidi kwa kiasi kikubwa kufafanua majukumu ya Serikali ni yapi, lakini pia majukumu ya jamii au wananchi ni yapi. Ni kweli kwamba tofauti kati ya elimu bila malipo na elimu bure inapaswa ifike kikamillifu kwa wananchi wetu kule chini.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu letu sisi kama wanasiasa kuwaeleza wananchi, lakini pia ni jukumu la Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa kawaida wanajua majukumu yao. Uelewa wa wananchi bado haujakaa sawasawa na kwa maana hiyo, ninaishauri Wizara ifikishe elimu hii kwa kutumia Idara ya Elimu kwa ngazi ya chini kabisa ili wananchi wajue majukumu yao ni yapi kama yalivyoafanuliwa na miongozo ya Serikali.

Kimsingi suala la elimu bila malipo lina changamoto zake na ndio maana tuko hapa kwa ajili ya kutatua changamoto hizo. Serikali ilipoamua kupeleka fedha katika

shule za msingi na sekondari imekwenda sambamba na kubana matumizi ambayo yanasaababisha baadhi ya maeneo kutotekelawa vizuri katika utoaji wa elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba niliongelee eneo moja tu la mitihani. Ni kweli kabisa ili mwanafunzi aweze kujifunza, anahitaji kichocheo cha kuwa na majaribio na mitihani ya mara kwa mara. Kwa maana hiyo basi, pamoja na kwamba tunakwenda vizuri katika kutoa elimu hii bila malipo, lakini tunaiomba Serikali iongeze fedha ambazo zitawasaidia walimu kutoa majaribio ya mara kwa mara ili tuweze kuungeza ufaulu wa wanafunzi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine muhimu ni eneo la miundombinu ya shule zetu. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri inaonesha wazi kwamba tunalo tatizo kubwa la miundombinu katika shule zetu, tuna matatizo ya vyoo, tuna matatizo ya majengo na matatizo ya nyumba za walimu. Nadhani sasa umefika wakati wa Serikali kutenga fedha ya kutosha na kuzisimamia vizuri Halmashauri zetu ili fedha nyingi itengwe katika maeneo haya kuondoa hizi changamoto ambazo tumekuwa tukizieleza kila siku.

Mheshimiwa Spika, suala la kuboresha miundombinu ya elimu liende sambamba na kuangalia shule zenyé mahitaji maalum hasa zile zinazopokea watoto wenye mahitaji maalum yaani watoto wenye ulemavu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Masasi kuna shule mbili; shule moja ilipata fedha katika mwaka wa fedha uliopita na kuboresha kwa kiwango kikubwa shule moja kwa ajili ya watoto wenye ulemavu, lakini shule ya msingi Lugongo hali ni mbaya na hakuna vifaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine muhimu tunapozungumzia elimu ni suala zima la idadi ya walimu katika shule zetu. Umefika wakati Serikali iseme, wanapofanya majumuisho Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI atuambie, ni lini hasa wanaajiri walimu wa shule za msingi na ni lini hasa wanaajiri walimu wa shule za sekondari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, hata tufanye vipi, kwa uelewa wangu na kwa uzoefu wangu wa eneo la elimu, ni afadhali mwanafunzi asomee kwenye mwembe lakini walimu awepo. Mwalimu ndiye ambaye ana msaada mkubwa wa kumpa maarifa mwanafunzi. Tuna changamoto kubwa na tumekuwa tukisema muda mrefu sana kwamba pamoja na kwamba tumetatua changamoto ya madawati, pamoja na kwamba tunaendelea kujenga majengo, lakini kama walimu wapo wa kutosha, hali haiweze kuwa nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuna shule nyingine zina walimu wanne, wanafunzi 600. Hali haiwezi kuwa sawasawa katika kujifunza kwa watoto. Katika Jimbo la Masasi tunapungukiwa na walimu takribani 219 wa shule za msingi, tunapungukiwa na walimu 60 wa masomo ya sayansi; wanatakiwa walimu 84, wapo walimu 24 tu. Hatuwezi kuongeza ufaulu wa watoto katika mazingira ya namna hiyo. Kwa hiyo, lazima Serikali ifike wakati iajiri walimu hawa.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo mambo haya yanatakiwa tuwianishe. Tunajenga mazingira mazuri ya kujifunzia watoto, lakini pia tunatengeneza mazingira ya maslahi kwa walimu wetu. Ni kweli kwamba Serikali inalipa madeni, hasa madeni yaliyo nje ya mshahara kwa walimu wetu. Pia ni kweli kwamba walimu bado wana malalamiko, tuendelee kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto zinazowakabili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016 Serikali iliwapandisha baadhi ya walimu madaraja. Katika Jimbo langu, walimu 397 wa Masasi walipandishwa wakapokea mshahara mmoja baadaye wakashushwa. Hawa ni walimu wa Jimbo moja tu, eneo moja tu, walimu wana malalamiko, wanakata tamaa. Ulishapewa mshahara, baadaye unashushwa. Tunaomba Serikali iangalie namna gani inaweza kuyaangalia mazingira haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, wapo walimu ambao walitakiwa kupanda madaraja kutoka mwaka 2014 mpaka leo hawajapandishwa madaraja. Mwaka 2010 Serikali iliondoa

*annual increment* kwa walimu na ilikuwa pengine ni tofauti na mazingira ya mikataba waliyosaini wakati wanaajiriwa, lakini mpaka leo walimu hawa hawajaambiwa kwa nini *annual increment* imeondoka, lakini hata kama wanaambiwa, bado wanabaki kuwa na malalamiko. Tuangalie mazingira ya walimu ili tuone namna gani walimu hawa wanaweza kuwa na motisha pia ya kufundisha. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo eneo la uratibu katika shule zetu. Ipo changamoto hasa maeneo yale ambayo yana changamoto ya usafiri. Waratibu wa Elimu wa Kata wanashindwa kufanya kazi yao ya uratibu vizuri kwa sababu wengi hawana usafiri. Tunasikia kuna baadhi ya maeneo, waratibu wana usafiri, lakini tungeomba sasa tuyaangalie na maeneo ya kusini hususan katika Jimbo langu la Masasi, waratibu wetu wapewe usafiri angalau wa pilkipiki ili waweze kuyafikia maeneo ya shule zao mara kwa mara. (Makof)

Mheshimiwa Spika, nizungumze kidogo katika eneo la afya. Kama kuna eneo lina changamoto kubwa sana ni eneo la afya. Tuna tatizo kubwa. Katika Jimbo langu, tuna tatizo linaloendana na upungufu mkubwa wa watumishi, hili ni tatizo kubwa sana!

Mheshimiwa Spika, tuna zahanati lakini hazina watumishi wa kutosha; tuna upungufu na tumeomba kupatiwa watumishi wa hospitali, takribani watumishi 56 wa huduma ya afya lakini hakuna hata mmoja aliyeajiriwa mpaka sasa. Huu ni wakati ambapo Serikali inatakiwa kusema ni lini inaajiri watumishi wa afya ili tuweze kupata rasilimali watu katika maeneo yetu ya huduma za afya?

Mheshimiwa Spika, katika eneo la afya hususan katika Jimbo langu bado kuna changamoto kubwa. Pamoja na kupungua kwa watumishi, lakini hatuna magari ya wagonjwa. Wilaya nzima kuna magari mawili tu ambayo moja ni bovu na moja ndiyo linalofanya kazi; siyo rahisi kuweza kuwapeleka wagonjwa wanaohitaji msaada wa haraka hospitali.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tungependa katika eneo la huduma za afya kuwe na upatikanaji wa dawa kwa wakati; hili pia limekuwa ni eneo lenye changamoto kubwa sana. Katika Hospitali yetu ya Mkomaindo mwaka 2014 ulifanyika ubadhirifu wa fedha za dawa.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kuuliza swalii, niliwahi kueleza masuala haya mara nyingi, lakini kila Waziri anapotoa majibu hapa, sijapata majibu ambayo yanaridhisha ni kwa nini hatua hazichukuliwi kwa watu ambao walihusika na ubadhirifu huu wa dawa mwaka 2014? tunaomba Serikali ichukue hatua katika eneo hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni ujenzi wa jengo la utawala. Jimbo langu la Masasi halina jengo la utawala lakini kwa bahati mbaya sana, fedha ambazo zilikuwa zime...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa dakika zako kumi zimekwisha.

**MHE. RASHID M. CHUACHUA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia kwenye hotuba ambazo ziko mbele yetu na niazee kwa kuunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dharti kwa Mheshimiwa Rais kwa nia yake thabiti ya kusaidia wanyonge, namshukuru Waziri Mkuu, sikupata nafasi ya kuchangia kwenye hotuba yake, lakini namshukuru sana kwa kutusikiliza, tunapokuwa na masuala anayashughulikia kwa haraka sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri, ndugu yangu Mheshimiwa George Simbachawene, Mheshimiwa Jafo na dada yangu Mheshimiwa Kairuki kwa hotuba nzuri. Nimepitia hotuba hizi na jedwali hili ambalo Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI ametuwasilishia hapa, yapo mambo ambayo kwa kweli inaonesha kabisa Wizara imejipanga vizuri, na mimi nimefarijika sana kuona kumbukumbu nzuri ambazo pia zitatusaidia katika kutekeleza majukumu yetu. Kwa hiyo, nashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianze kutoa mchango wangu kwa kuzungumza juu ya uratibu, hususan najikita kwenye hii Wizara ya TAMISEMI, kwamba Wizara hii inayo majukumu mengi lakini napenda tu nipate nafasi hii niweze kuomba sana katika kuratibu maeneo mbalimbali ambayo pia yanasisimamiwa na sekta nydingine kwa mfano kwenye kilimo waweze kuangalia vizuri ili watusaidie wananchi wetu. Sisi tunaotoka majimbo ambayo pia ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya kilimo, waweze kutusaidia. Kwa sababu najua wanasisimamia upande wa pembejeo, tumekuwa na shida kubwa, tunahitaji uratibu uwe wa mapema ili wananchi wetu wapate pembejeo mapema tuweze kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, yapo maeneo mengine ambayo yanahitaji kufanya utafiti. Tunaona kuna suala hili la kuwa na akiba ya chakula, imefika wakati sasa Wizara ijaribu kuangalia kama tunaweza kupata fursa pia ya kuhifadhi chakula, tuwe na maghala kwenye upande wa Serikali za Mitaa kwa maana ya Halmashauri zetu ili tuwe na akiba lakini pia tunaweza kufanya biashara kuititia zoezi hili la kuhifadhi chakula. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia napenda kushauri kuhusu usimamizi wa mikopo kwa wakulima wetu kwa sababu Wizara hii kwa idara ambazo zipo kwenye Halmashauri zetu, ikisimama vizuri tutaweza kuwasaidia wananchi. Kwa sababu utaweza kuona kwamba mikopo ambayo inakwenda kwa wakulima kwa mfano wa zao la tumbaku, utaona ile mikopo na mikataba inayotolewa na vyombo vyetu ambavyo

vinakopesha wananchi kumekuwa na biashara ndani yake ambayo inawaumiza sana wakulima.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mikataba ambayo inakuwa imetengenezwa kwa kufuata fedha za kigeni, kwamba wakati wa kukopa unapopewa pesa kwenye kubadilisha pesa kutoka dola kwenda shilingi, pale kuna gharama ambazo zinakuwepo na wakati wa malipo kadhalika kunakuwa kuna gharama ambazo mwisho wa safari wakulima wetu wanapata gharama kubwa kutokana na mikopo hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napenda nishauri kwenye kuratibu, tuimarishe maeneo ambayo kwa upande wa idara ambazo zinasimamia wakulima hawa hususan hawa wa tumbaku tuweze kuona kwamba mikataba yao pla inakuwa mizuri kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumze juu ya uongezaji wa makusanyo katika Halmashauri zetu. Kwa maana hiyo, naiomba Wizara hii ya TAMISEMI iweze kutusaidia pale ambapo kwa upande wetu sisi kama Halmashauri tunavyokuwa na mipango ya kuwekeza ili tuweze kupanua makusanyo katika maeneo yetu, kwa sababu hapa kuna tatizo kwamba tunavyotaka angalau tu-*cross border*, tuweze kufanya uwekezaji kwenye maeneo mengine. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI anajua kwamba sisi tuna dhamira kubwa ya kutokutegemea ushuru tu wa mazao, tunapenda pia twende tufanye uwekezaji ili Halmashauri zetu ziweze kuongeza mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba tu Wizara hii iweze kufanya *coordination* nzuri ili tutakapofika kwenye maeneo ambayo tunataka kupanua vyanzo, basi watu-*support* ili tuweze kuongeza makusanyo. Kuongezeka kwa makusanyo ina maana huduma kwa wananchi wetu itakuwa inaongezeka.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze juu ya udhibiti wa ndani (*internal controls*), lakini nataka nijikite kwenye maeneo mawili; kuimarisha hili eneo la Wakaguzi wa Ndani na upande mwininge nitazungumza juu ya Kamati za Ukaguzi ambazo hazijafanya vizuri, zimeleteleza kutokuwa na udhibiti mzuri katika makusanyo na katika matumizi. Kwa hiyo, nafikiria nizungumze maeneo haya mawili.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwamba katika maeneo yetu upande wa Wakaguzi wa Ndani bado tuna matatizo makubwa. Kwanza Wakaguzi hawa wa Ndani ni wachache sana, hawawezi kumudu kuwa na mawanda ya kutosha (*scope*) ili ule ushauri wao uweze kusaidia Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Spika, nafikiri Wizara hii itazame sana eneo hili, kwa sababu ukiangalia Wakaguzi wa Ndani, hawana hata ule mpango. Sisi tunao Wakaguzi wawilli; hawana hata ule mpango ambao utaonesha kwamba wamejipanga vizuri ili kuweza kupitia maeneo ya kutosha na kuweza kushauri katika Halmashauri ili tuweze kufanya vyema.

Mheshimiwa Spika, utakuta Wakaguzi hawana hata ule ujuzi wa kutosha kuweza kuangalia labda kuwa na uwezo kwenye mifumo hii, ujuzi wa TEHAMA uko mdogo, hawawezi ku-access information kwenye EPICA, Lawson, kwenye PLANREP, kwa hiyo, utaona kwamba hili ni tatizo. Hawa Wakaguzi wa Ndani waongezwe lakini pia waweze kuwa na weledi wa kutosha waweze kuzisaidia Halmashauri zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, utakuja kuona kwamba hata bajeti, nilipokuwa nikipitia bajeti ya kwenye Halmashauri yangu, niliwaliza Wakaguzi wa Ndani kama fedha zinatosha. Kwa hiyo, unaona kwamba hata pesa wanazopangiwa ni kidogo sana kuweza kumudu majukumu yao na pia wana shida ya vifaa, hawana kompyuta, hawana magari ya kutembelea maeneo mbalimbali, maeneo ya kwetu ambayo ni makubwa sana. Kwa hiyo, utaona kwamba ule mchango wao ni mdogo sana ambao kimsingi kama maeneo haya

tutayaboresha, watatuwezesha pia Maafisa Masuhuli kufanya kazi zao vizuri kwa sababu watapata ushauri na kwa mapema zaidi.

Mheshimiwa Spika, hili eneo la Kamati za Ukaguzi utaona Kamati ya Ukaguzi ni muhimu sana kuwepo katika Halmashauri yetu, lakini bado hatujaziwekea msimamo mkubwa kuweza kuhakikisha kwamba Kamati hizi zinafanya kazi na kusaidia mambo mengi sana.

Kwa hiyo, utaona eneo hili ni muhimu sana, TAMISEMI ilitazame ili waweze kusaidia. Hizi Kamati zitamwezesha Afisa Masuhuli kutimiza wajibu wake kwa sababu ataweba kumshauri vizuri majukumu yake ya kiuongozi, zitasaidia sana kama zitaimarishwa. Pia tutapata ufanisi katika hiki kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kwa sababu hii Kamati ya Ukaguzi inamsimamia kwa ukaribu sana huyu Mkaguzi wa Ndani. Kwa hiyo, nafikiri eneo hili pia tuweze kulitazama.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie juu ya maboma. Tunayo maboma mengi sana ambayo wananchi wametumia nguvu nydingi sana kujenga, katika hili TAMISEMI watusaidie sana kuyakamilisha haya maboma. Nilikuwa najaribu kuangalia kwenye haya majedwali, utaona kabisa kwamba kuna upungufu sana. Kwa mfano, nilikuwa najaribu kutazama nikaona upungufu wa madarasa katika shule za msingi na sekondari. Kuna upungufu mkubwa sana ukiangalia majedwali haya, lakini wananchi wamejitolea vya kutosha; yako maboma mengi sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ninazo nyumba 170 ikiwemo madarasa, zahanati, majengo ya utawala, nyumba za walimu, nyumba za wafanyakazi wa afya 170 ambazo zinasubiria kukamilishwa. Hii idadi ni kubwa sana, bila Serikali kutusaidia Halmashauri peke yake haiwezi. Pia yapo majengo 117 ambayo yako kwenye hatua mbalimbali; hatua ya msingi, hatua ya madirisha na hatua ya *lenter* Serikali naomba itusaidie sana ili tuweze kupunguza huu upungufu ambaou upo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana TAMISEMI watazame eneo hili kwani wananchi wameweka nguvu nyingi, watapata moyo sana kama Serikali itatusaidia kuweza kukamilisha masuala haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, nilipokuwa nikipitia hili jedwali, nimeona kuna shule zimesahaulika. Nashukuru kwamba tumepata walimu wa sayansi wachache, lakini ninaamini kwamba sisi katika Halmashauri ya Ushetu tunayo shule ya *high school* inaitwa *Dakama secondary school*, haikupangiwa walimu na ina upungufu; haina walimu wa sayansi. Walimu wa *physics*, tunaye mmoja ambaye ndio Mkuu wa Shule, anafundisha kuanzia *form one* mpaka *form six*.

**MBUNGE FULANI:** Loh!

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Hatuna mwalimu wa *biology*! Sasa naomba Wizara itazame ili tuweze kusaidia hawa watoto. Isipokuwa nimegundua kwamba ilisahaulika kwa sababu, ukiangalia hata katika majedwali kwenye mgao wa fedha za usimamizi wa mitihani, hatukupangiwa *high school*. Kwa hiyo, naamini kwamba shule hii ilisahaulika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba uitazame hii shule ili tuokoe hawa watoto waweze kupata huduma na tuweze kufanya vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kumwombwa Mheshimiwa Waziri TAMISEMI, kusaidiwa madaraja matatu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kwandikwa.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Hayo maombi mwandikie tu Mheshimiwa Waziri. Yapeleke kwa kumwandikia Mheshimiwa Waziri maombi yako hayo. Mheshimiwa Kasuku Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi hii. Naomba nianze na Utumishi na hasa nikiendeleza lile suala langu la asubuhi linalohusiana na ajira.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa kauli yake mwezi wa Sita mwaka 2016 kwamba inasitisha ajira huku ikifuatilia suala la watumishi hewa na kwamba zoezi hilo likiisha, ajira mpya zingetoka. Mpaka leo suala la ajira mpya halizungumzwi.

Mheshimiwa Spika, juzi wamezungumzwa wachache, walimu wa sayansi kama 4,000 na kidogo lakini kwenye orodha iliyotoka juzi, kuna walimu wawili wa masomo ya *book-keeping* na *commerce, history* na kiswahili na wao wameajiriwa kwenye hiyo orodha ya walimu wa sayansi. Siwaonei vivu, lakini nataka kujua tu kwamba na hii *history* na kiswahili siku hizi ni sayansi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Serikali ifike mahali ituambie, uhakiki wa wafanyakazi unaisha lini na ajira mpya zinatoka lini? Watu wasikae na matumaini tu bila kujua wanaajiriwa au hawaajiriwi katika Awamu ya Tano. Nilitaka nizungumzie hilo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba sekta ya elimu haina wafanyakazi/walimu wa kutosha. Afya haina wafanyakazi wa kutosha, kwa hiyo, Serikali itoe ajira na wale watoto walioko mitaani wanaendelea kuichukia tu Serikali bure bila sababu, wakati ajira zingeweza kutoka.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, wale hewa walioondolewa 18,000 kazi zao wanafanya nani leo? Hakuna *replacement*, pamebaki wazi au inakuaje? Hao wangeweza kuajiriwa wengine ingetusaidia kupunguza idadi ya ambao hawana ajira. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala la vyeti *fake*. Hili nalo limekuwa kizungumkuti katika nchi hii. Kuzungumzia vyeti *fake* nchi hii mpaka uwe na roho ngumu kwa sababu kuna cheti kimoja hapa sasa kimekuwa ni tatizo kabisa. Hiki cheti cha Bashite kina shida gani? Kina tatizo gani imekuwa sasa

kinachafua mpaka jina la watu wakubwa kabisa. Hata mtu akifungwa magoli manne bila kitu chochote, wanasema ni nne kwa Bashite; yaani tunaongeza misamiati isiyo na sababu. Hiki cheti cha Bashite kinalindwa kwa sababu zipi? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Utumishi utakapoanza kushughulikia vyeti kwa watu wasio na vyeti na kuchukua hatua, hiki cha Bashite sijui kitabaki wapi. Ingawa siyo mamlaka yako, lakini najua utashauri kwa utaratibu fulani ili na Bashite naye awajibike pamoja na wale walio na vyeti *fake* na ionekane, isije ikatokea *double standard* katika hili. Huyu achukuliwe hatua zake na huyu apate haki zake, tumalize suala la Bashite nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuzungumzia kidogo suala la utawala bora. Ukiona haki inapotea...

**SPIKA:** Mheshimiwa Bilago, hiyo Bashite ndiyo kitu gani? Mheshimiwa endelea kuchangia tu, endelea. (*Kicheko*)

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Ni cheti cha Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambacho siyo cha kwake, alisomea cheti cha mtu mwingine. Kwa hiyo, nilitaka nacho kiangaliwe na Waziri anayehusika.

Mheshimiwa Spika, suala la utawala bora; ukiona haki inapotea; haki inakwenda sambamba na amani. Hawa maaskari wetu waliofariki Mungu awaweke mahali pema Peponi; mkiangalia kwenye mitandao, kwa nini baadhi ya wananchi wamefurahia? Yaani binadamu wenzetu wanapoteza maisha, lakini baadhi ya watu wanafurahia kwenye mitandao? Ni kwa sababu kuna baadhi ya haki zinapotezwa na hao watu wanaokufa. Sasa wakifa, watu wanapumua kidogo. Kwa hiyo, tuangalie mahusiano, tulete mahusiano mazuri kati ya wananchi na vyombo vyaya dola vyote, Usalama wa Taifa, Polisi, Jeshi tuwe na mahusiano mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hapo awali tulikuwa na Polisi Shirikishi, watu walikuwa wanakwenda vizuri. Leo hii ukipita kwenye mitandao unaona watu wanakuwa, wengine wanashangilia. Siyo kitu kizuri, hata mimi sikipendi. Siyo kitu kizuri, lakini chanzo chake ni pale ambapo haki ya watu inapotezwa, watu wengine wanaona sasa likitokea la kutokea wapate mahali pa kupumua. Maandamano ya moyoni hayo, yanaendelea moyoni, watu wanaandamana. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumzie upande wa afya kidogo sana, kwamba Waziri wa TAMISEMI atusaidie namna bora ya kupunguza vifo nya akina mama wajawazito kule kwenye Halmashauri zetu. Sasa hivi takwimu zinafikia kama 550.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, tunapolizungumza kwenye Kamati yetu, tunaona kama lilihitaji Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI awepo na sijui kuna siku utatupa hiyo *offertumpate* Waziri wa TAMISEMI kwenye Kamati yetu, wawepo pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Afya. Tukizungumzia la afya na elimu wote wakiwepo pamoja, nadhani inaweza ikawa na mantiki nzuri kwenye Kamati yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nilitaka nizungumzie suala la Wakala wa Barabara Vijijini, nimeliona. Suala hili linaweza kutufikisha mahali pazuri kama litasimamiwa vizuri, kwa sababu kuna baadhi ya barabara zinashindikana kutengenezwa kule kwenye Halmashauri zetu na hasa zile zinazotokana na Madiwani wa Upinzani. Kwa mfano, Jimboni kwangu, ninazo barabara za kufungua Jimbo na nchi jirani ya Burundi; Rumashi - Burundi, Malenga - Burundi, Kiga - Burundi, Kimiha - Burundi, Katanga – Burundi; zile ambazo zina Madiwani wa CHADEMA hazitengenezeki kwamba zitaendelea kuwapa umaarufu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wakala huyu hawezи kuwa na tabia kama hiyo, nadhani atakuwa na tabia nzuri kuliko hii. Kwa hiyo, ni vyema hili jambo likaenda vizuri

tukapata huyu Wakala wa Barabara Vijijini, anaweza akatusaidia kuliweka vizuri ili wananchi wapate barabara bila kujali itikadi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni ushuru wa mazao. Mheshimiwa Rais aliwahi kutoa maelekezo ya ushuru utozwe namna gani katika hotuba yake, akihitubia wananchi kwenye Mkutano wa Hadhara, likaanza kutekelezeka, lakini bado lina mkanganyiko. Ni ujazo gani unatakiwa kutozwa ushuru katika mazao haya ya nafaka na kadhalika? Maana debe moja halitozwi ushuru. Kule kwangu Kakonko, ukienda baadhi ya vijiji wanatoza ushuru debe moja, baadhi ya vijiji hawatozi debe moja. Kwa hiyo, kunakuwa na mkanganyiko.

Mheshimiwa Spika, hebu tupate *uniformity* nchi nzima; mazao yatatozwa ushuru wa ujazo wa kiasi fulani ili kuondoa huu mkanganyiko katika nchi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni elimu. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, tuepuke madeni ya walimu yasiyo na sababu. Mkurugenzi anaamua anahamisha walimu 50, 60 hana hata senti tano, anawaambia nendeni tu mtalipwa. Watalipwa na nani? Kama huna hela ya kuwalipa watu, usiwahamishe. Kuna walimu 85,000 mwaka jana walipanda madaraja; tena madaraja ya kufungua vidato (*E to F; F to G; G to H; H to I*). Wale watu *wage bill* yao ya mwezi ni shilingi bilioni 21; inaendelea ku-*pile up* tangu mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, ni vyema Serikali ingelipa hili deni likasimama kwanza wakabaki wanadai hizi nyininge. Yaani likasimama kwa sababu kila mwezi kuna shilingi bilioni 21 na ndio inakwenda kufika kwenye shilingi trilioni 1.06 wanayodai Walimu nchi hii.

Mheshimiwa Spika, sasa na Walimu wenyewe wamesema wanadai, imeanza kufanyika uhakiki; uhakiki huu ni kama una dalili za *delaying tactics*, yaani unafanya uhakiki polepole ili usifikie wakati wa kulipa, lakini mwisho wa siku deni lile lipo na walimu wanaendelea kuhangaika nchi hii, wanafanya maandamano moyoni, wanafanya mgomo wa

kutofundisha moyoni. Hawa watu kama hawajatekelezewa mambo yao, hawawezi kufanya kazi yao vizuri. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, mimi ni mwalimu, nimefundisha darasani, nafahamu namna ya kugoma polepole. Kwa hiyo, tuwatekelezee mambo yao. Mwalimu huyo huyo, kimshahara hicho kidogo, halafu hata madai yao, zaidi ya Walimu asilimia 70 wote wana madai.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Taarifa.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Sasa kama walimu asilimia 70 wana madai...

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** ...tusitarajie miujiza kwenye elimu.

**SPIKA:** Taarifa iko wapi? Ruksa mwenye taarifa. Ahsante Mheshimiwa, endelea. Mheshimiwa Kasuku Bilago upokee taarifa.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa mujibu wa kanuni ya 68(8). Kaka yangu Mheshimiwa Mwalimu Bilago, kazungumzia kwamba Kata ambazo zina Madiwani wa CHADEMA, miradi haipelekwi. Ni kitendo ambacho kinanisikitisha kwa sababu Madiwani ni Wajumbe kwenye Baraza la Halmashauri, Madiwani ni Wajumbe kwenye Kamati mbalimbali katika Halmashauri, Madiwani wanaibua miradi kwenye Kata zao ndiyo wanazileta kwenye Halmashauri kwa ajili ya kuingia kwenye bajeti na vilevile kwa mujibu wa kanuni, asilimia 60 ya mapato ya ndani inatakiwa iingie katika bajeti kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nampa taarifa Mheshimiwa Bilago kwamba kauli yake siyo sahihi, mfano mzuri tu, Jimbo langu la Nsimbo Mkoa wa Katavi nina Diwani wa CHADEMA

na mwaka 2016 alipewa shilingi milioni 132 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na kukarabati shule ya msingi Teka 'A'. Vilevile kwenye Mfuko wa Jimbo tumempa shilingi milioni 2.5 kwa ajili ya shule nyingine kwenye kijiji. Kwa hiyo, nampa taarifa kwamba Serikali haibagui kwa mujibu wa kanuni na taratibu za nchi.

**SPIKA:** Mwalimu Bilago, taarifa hiyo unaipokea?

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, naomba ulinde muda wangu kwa mtua ambaye alikuwa hana nafasi ya kuchangia, akatafuta pa kudandia. Hiyo taarifa siipokei kwa sababu nina uhakika na ushahidi wa kutosha. Barabara nilizozitaja ambazo baadhi zimeshindikana, ziko kwenye mpango zikaondolewa kwa sababu Diwani ni wa CHADEMA. Asilinganishe Halmashauri yangu na ya kwake. Abaki kwake, mimi aniachie Halmashauri yangu.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo...

**SPIKA:** Unajua mambo mengine huwa hatupendi tu kuingilia na kusema kila wakati, kidogo tu mwalimu. Ukae kidogo tu dakika moja, nakutunzia muda wako. Hivi hiyo barabara ambayo inapita kwenye Kata moja, yaani haipiti hata Kata nyingine, yaani hiyo barabara iko kwenye Kata ya huyu wa CHADEMA vijiji vitatu, yaani iko hapa tu! Hiyo barabara inafananaje? (*Kicheko/Makofii*)

La pili, kwa sababu hii Serikali imeanza juzi tu, ina mwaka mmoja na nusu tu, hata miaka miwili haijafika. Ina maana kwenye Wilaya yako hamna Kata za Madiwani wa CCM ambao kwa mwaka huu mmoja na nusu wao hawajaguswa na hiyo miradi ya maendeleo na wenyewe barabara zao hazijachongwa au ikishakuwa upande huu, basi tayari!

Endelea tu mwalimu, yaani ni mambo tu watu wanawaza. (*Kicheko*)

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, naomba ulinde na huo muda wako uliomega kidogo.

**SPIKA:** Umelindwa, umelindwa. Endelea mwalimu, tusikucheleweshe.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ni ukweli usiopingika kwamba mimi ni mtu mzima, nina zaidi ya nusu karne. Kata hizo ninazozizungumza barabara zake, inaanzia ndani ya Kata inaenda mpakani mwa Burundi; haiwezi kupita kwenye Kata nyingine. Lazima ianzie ndani ya Kata kwenda mpakani. Sijazungumza barabara za ndani, niko makini na hilo. Kwa hiyo, nilikuwa nalizungumza hili kwamba huyu Wakala wa Barabara Vijijini anaweza akatufikisha mahali pazuri kama kweli utaratibu utakwenda kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa bado naendelea na hoja ya walimu nikitaka kuzungumzia juu ya motisha kwa walimu. Tuliwahi kutoa wazo wakati niko Chama cha Walimu na walimu wa nchi hii niwaambie wana matumaini makubwa sana na Serikali hii.

Kwanza, wakijua Rais ni mwalimu, Waziri Mkuu ni mwalimu, tena kiongozi aliyekuwa wa Chama cha Walimu kama mimi, huenda hata mimi tutakaposhika Serikali nitakuwa Waziri Mkuu, kwa sababu ndio Makatibu wa Chama cha Walimu wameanza kuwa Mawaziri Wakuu. (*Kicheko/Makofi*)

Kwa hiyo, walimu wana matumaini makubwa sana juu ya hili, tunaomba Serikali iwasikilize. Najua na sekta nyingine, sawa wana madai lakini tuangalie hii *population* kubwa ambayo inagusa karibu kila kijiji, kuna mwalimu anayekuwa na madai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, motisha ambayo tulikuwa tunazungumzia ilikuwa ni *teaching allowance*. *Teaching allowance* mpaka leo haizungumzwi kabisa. Naomba Waziri anayehusika anaposimama atueleze, *teaching allowance*

lengo lake ilikuwa; muda wanaofanya kazi walimu ni tofauti na sekta nyingine. Walimu walioko shule za bweni (*boarding*) wanatakiwa kuangalia watoto usiku mpaka asubuhi. Mtoto akiugua, mwalimu anampeleka hospitali. Muda wa kusahihisha, mwalimu hawezi kusahihisha shulenii akamaliza kazi, lazima kazi ile aende nayo mpaka nyumbani, itamfuata mpaka nyumbani.

Kwa hiyo, ndiyo maana tukasema *teaching allowance* iwepo ku-offset hizi gharama za *overtime* na kadhalika. Nayo ilifanywa vizuri tu wakati ule wa Tume ya Makweta, ikaja ikatuletea taarifa nzuri kama hiyo na Walimu wakawa wanapata *teaching allowance*. Wale tuliofundisha zamanii kama mimi, nilikuwa napata 55 percent ya mshahara wangu, kwa sababu mimi ni mwalimu wa sayansi.

Kwa hiyo, Serikali ikifanya hilo, ita-motivate walimu, itawafanya waipende kazi yao na wafundishe watoto wa nchi hii ili tuweze kupata wataalam wazuri katika nchi hii.

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuzungumzia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ni kengele ya pili, yaliyobaki unaweza ukayaandika mwalimu.

**MBUNGE FULANI:** Muda wake!

**SPIKA:** Muda wake tumeulinda kabisa. Ahsante sana, tunakushukuru.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Tunakushukuru sana. Atafuata Mheshimiwa Stansalaus Mabula.

Mheshimiwa Mwalimu Bilago, kama Mbunge, una nafasi pale kwenye Wilaya, kama Diwani wako fulani hapati

nafasi, unaingilia kama Mbunge. Sasa ukilalamika hivyo, maana yake na wewe una matatizo, huwajibiki ipasavyo. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mabula, Mbunge wa Nyamagana. (*Makofi*)

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Kwa kuokoa muda nianze tu kwa kutoa pole kwa Mstahiki Meya wa Jiji la Mwanza, Mkurugenzi pamoja na Madiwani, lakini kwa wananchi wa Kata ya Mandu kwa kuondokewa na Diwani wao mpendwa Mheshimiwa Wambura, naamini Mungu ataendelea kuwatunza vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru na mimi kwa kupata fursa ya kuchangia Wizara hili ya TAMISEMI. Pamoja na mambo mengi ilionayo, lakini ningejielekeza kwenye mambo machache. La kwaza, namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri wa Wizara hili ya TAMISEMI kwa namna ya kipekee ambavyo wamekuwa wakijishughulisha katika kuhakikisha wanatatua changamoto tulizonazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo moja kubwa ambalo naanza nalo ni juu ya usafi wa mazingira. Nami nimeshangaa kidogo, kwenye kitabu cha taarifa, Mheshimiwa Waziri kama usipojitetengenezea mazingira ya sisi kukusemea na mwenyewe huwezi kujisemea, Serikali hili kwa mwaka huu wa fedha tulionao kwenye Majiji manne na Manispaa tatu, imetumia fedha nydingi sana katika kuhakikisha inaboresha taratibu za upatikanaji na uzoaji wa taka na kuboresha miji na majiji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeangalia taarifa hili imezungumza mistari michache sana, inataja tu kununua vifaa. Vifaa vilivyoko Mwanza peke yake ni vya zaidi ya thamani ya shilingi bilioni nne. Kuna *truck* zaidi ya 12, kuna *excavator*, *duzor*, *compactor* na kadha wa kadha na sasa

tunajenga dampo la kisasa kuhakikisha usafi wa Mji. Haya yote nilitegemea niyaone na haya yamefanyika Arusha, Tanga, Mbeya, Dodoma, Mtwara pamoja na Kigoma. Sasa usipojisifia wewe Mheshimiwa Waziri, sisi tutakusifia mpaka lini?

Mheshimiwa Spika, naomba nijielekeze kwenye suala la wafanyabiashara ambayo inaitwa sekta isiyo rasmi ya wafanyabiashara ndogo ndogo (Machinga). (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Hapo sasa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika, wafanyabiashara ndogo ndogo kwa sasa ingewezekana wakatambuliwa kama Sekta Rasmi, kwa sababu wako zaidi ya 30,000 nchini kote. Mara kadhaa tumekuwa tunawachukulia kama watu ambao hatuoni umuhimu na thamani yao na ndiyo maana mara kadhaa wamekuwa wakifukuzwa na mgambo, wamekuwa wakipigwa mabomu, lakini mwisho wa siku wanaharibiwa malizao, kunyang'anywa na kuteketezwa. Siyo wao tu, hapa namwongelea Mmachinga wa kawaida, mama lishe, baba lishe na kadhaa wa kadhaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa sote tunafahamu kwa sasa suala zima la Halmashauri zetu katika kukusanya kodi, limekwenda chini sana na mfano mzuri, ukichukua tu takwimu za Mkoa wa Mwanza na Halmashauri zake zote kwa ujumla, mwaka 2016/2017 tulitazamia kukusanya shilingi bilioni 34, mpaka leo tunazungumza, taarifa inasema tumekusanya shilingi bilioni 16. Tunakusudia bajeti ya mwaka 2017/2018 tukusanye shilingi bilioni 35, ongezeko la milioni 600 peke yake.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema nini? Machinga hawa wa leo ambao tunawaona sio watu muhimu kwenye shughuli zetu, tunaweza tukawafanya wakawa sehemu kubwa sana ya kipato kwenye Halmashauri ambazo Machinga hawa wamekaa mjini sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukichukulia Mwanza peke yake, nimeangalia Dar es Salaam, Mbeya, Arusha na maeneo mengine ikiwemo na Dodoma. Kwa Mwanza peke yake, chukulia tunao Machinga 5,000. Machinga biashara yao inajulikana ni kwa siku, tu-*assume* Machinga mmoja kwa siku popote alipopanga alipie shilingi 1,000 peke yake ya kile kieneo kidogo ambacho amekitenga.

Mheshimiwa Spika, kwa Machinga 5,000 tutakusanya shilingi milioni tano, mara 26 kwa mwezi ukiondoa Jumapili, unatengeneza zaidi ya shilingi milioni 130; kwa mwaka mzima Halmashauri ya Jiji la Mwanza inaweza kuingiza zaidi ya shilingi 1,200,000,000. Fedha hizi hatutakaa tutegemee fedha za Serikali kuwasaidia wafanyabiashara ndogo ndogo, lakini kuwasaidia kuweka miundombinu ambayo kesho tutawapeleka wakakae katika miundombinu iliyo bora na sahilhi (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, lakini kupitia mfumo huu, tukikubali haya maeneo tuliyowapa sasa kwa muda wakakaa kwa miaka mitatu mpaka miaka mitano; tunaweza kutumia fedha zao wenyewe kujenga miundombinu rafiki na wao wakawa tayari kwenda kufanya biashara kwenye maeneo yale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hili linasambaa maeneo yote ya nchi ambayo mara nydingi ni maeneo ya Miji. Tunaweza kufanya hivi na tukawasaidia wafanyabiashara hawa. Kwanza watakuwa na uhakika na maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya kufanya biashara. Wakiwa na uhakika, wamekuwa na uhakika na shughuli yao na kesho yao kwa sababu tunataka tuwasaidie. Hili linajidhihirisha! Ukiangalia fedha za vijana na wanawake, kati ya shilingi 56,800,000,000; tumepeleka shilingi bilioni 27.5 peke yake, sawa na asilimia zisizozidi 27.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa kufanya hivi pia tutakuwa tumemsaidia sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mavunde pale anayehangaika na kutatua kero za vijana kila siku. Kwa sababu siyo kweli kwamba ipo siku Halmashauri

zitafikia asilimia mia kupeleka fedha za wanawake na vijana kwa sababu mahitaji ni mengi kuliko kawaida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nimeongea sana hapa kwa sababu ni changamoto kubwa sana na sisi tunawaogopa kwa sababu hawa ndiyo watu ambao tunaamini wakitengenezwa vizuri, kwa haya tunayoyasema, Dar es Salaam kule llala peke yake, pale Kariakoo wanasesma wana Machinga zaidi ya 5,000. Ukiwafanyia utaratibu huu tunaouzungumza na wao watapata kipato, lakini na Manispaa nyingine pia pamoja na Majiji wanaweza kuwa na hatua kubwa sana ambayo itawapelekea kupiga hatua kubwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nigosie kidogo juu ya suala la ufya. Uboreshaji wa sekta ya afya, kwenye ripoti inaeleza wazi kwamba imejikita na inaelekeza katika kujenga vituo vya afya zaidi ya 244 lakini kujenga hospitali zetu za rufaa. Sasa ni lazima tukubali, tunapojenga Hospitali za Rufaa ni lazima pia tuwe tayari kuimarisha.

Mheshimiwa Spika, mwaka uliopita tulisema tutajenga zahanati na kituo cha afya kwenye kila Kata. Sasa mpaka leo tunatazamia kujenga Vituo vya Afya 244. Tunavijenga kwenye Kata zipi? Waziri atakapokuja tunaomba pia tujue ni Majiji gani na Halmashauri zipi, Kata zipi zitakazofaidika na hospitali hizi 244. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, pia Hospitali za Wilaya; tunazo Hospitali za Rufaa za Kanda na Mikoa. Leo kama hatuna Hospitali za Wilaya kwenye Wilaya zetu, ni vigumu sana kutoa huduma zilizo bora kule kwenye hospitali zetu za rufaa.

Mheshimiwa Spika, ukienda pale Wilaya ya Illemela, ni Wilaya mpya, haina Hospitali ya Wilaya, wanategemea Hospitali ya Jeshi. Tunafahamu Jeshi namna na wao walivyo na shughuli zao nyingi, tuna wajibu wa kuhakikisha Wilaya ya Illemela inapata Hospitali ya Wilaya ambayo kimsingi imeshaanza kujengwa kwenye eneo la Busweru. Siyo hivyo tu, wamejikakamua kwa namna wanavyoweza, wameanza

na jengo la wagonjwa kutoka nje, lakini uwezo wa kukamilisha kwa gharama ya shilingi bilioni tatu haiwezekani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunaomba fedha hizi zinazokwenda kujenga Hospitali za Rufaa, tuelekeze pia kwenye Hospitali za Wilaya ili tupunguze mzigo hata kwenye hizi hospitali za rufaa tunazozijenga kuanzia huku wilayani. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo, leo kwenye Jimbo la Nyamagana kupitia Mfuko wa Jimbo na wadau mbalimbali tunayo maboma manne kwa ajili ya vituo vyta afya; Kata ya Buhongwa, Kata ya Lwang'ima, Kata ya Kishiri na Kata ya Igoma, tunataka kukamilisha, tunayamaliza vipi? Uwezo wa Halmashauri zetu kukusanya mapato kwa nguvu unaelekea kuwa siyo mzuri sana. Ni lazima tuhakikishe tunajikita kwenye kuboresha hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, tunazungumza sasa hivi, tunaelekeea kwenye kukusanya kodi kwa wafanyabiashara ndogo ndogo waanze kulipa *service levy*, wenyewe leseni za kuanzia shilingi 40,000. Mfanyabiashara mwenye saluni yenye kiti kimoja au viti viwili anayelipa leseni ya shilingi 40,000; baada ya miezi mitatu anatakiwa alipe *service levy*. Ni wafanyabiashara wa namna gani tunaowakusudia?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa. Ni kengele ya pili.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba niunge hoja mkono na ninashauri hayo yafanyiwe kazi. Ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hamad Salim Maalim, upande wa CUF, una dakika kumi.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adhimu ya kuchangia katika hotuba ya bajeti ya TAMISEMI na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah Wataallah* kwa kunijalia uzima nikasimama hapa leo kwa ajili ya kuchangia hotuba hii. Baada ya shukurani hizo, pia naomba nikipongeze chama changu kwa kukamilisha ziara ya Wilaya zote za Unguja na Pemba kwa kuimarisha chama, ziara hiyo iliyofanywa na Katibu Mkuu wa Chama Maalim Seif Sharif Hamad. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba niende moja kwa moja katika suala zima la utawala bora. Hapa naomba nigosie kipengele kizima cha uhuru wa kuabudu.

Mheshimwa Spika, naelewa kwamba suala la uhuru wa kuabudu ni suala la kikatiba, lakini pia katika suala zima la utawala bora ni suala ambalo limejadiliwa kwamba suala la ibada ni suala ambalo linadumisha amani ndani ya nchi. Ni suala ambalo haliangalii itikadi za vyama, ni suala ambalo linawakutanisha watu wa vyama vyote.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba katika suala hili la ibada ndani ya Jimbo langu lilizua mtafaruku mkubwa sana kwamba katika kufanya ibada upande wa chama kimoja walilazimisha kwamba lazima atajwe Mheshimiwa Rais kwenye hotuba ya Ijumaa, suala ambalo lilizua mtafaruku mkubwa sana, ikabidi kwamba Mkuu wa Wilaya aingilie kat, achukue Jeshi la Polisi livamie kijiji kile, masuala ambayo ni kinyume na taratibu na sheria na nchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, suala la ibada tunajua kwamba ni suala ambalo ni huru, jamii inatakiwa iabudu yenye we kwa kufuata dini yao ambavyo inawaelekeza. Sasa Mkuu wa Wilaya aliamrisha Jeshi la Polisi livamie kwenye msikiti ule na baada ya kuvamia ule msikiti kwa kweli ikawa ni tafrani kubwa sana ndani ya Jimbo lile.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba Jeshi la Polisi tunaomba lifuate masuala mazima ya utawala bora, lisiingilie masuala ambayo yako nje na mamlaka yao. Suala la ibada ni suala la uhuru wa kila mtu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Jeshi la Polisi kuvamia, lilikamata watu wawili. Naomba niseme kwamba kuna mzee wa miaka 65 alikuwa anahuzunisha, lakini pia kuna kijana wa miaka 35. Huyu kijana kwa sababu wazee wake walikuwa ni CCM, Mkuu wa Wilaya alikwenda akamtoa ndani.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba Jeshi la Polisi lisivae magwanda ya kijani, litumie sheria, yule mzee maskini jamaa zake walifika kumwombea dhamana, lakini kwa sababu *RPC* alikataa katakata, siku iliyofuata alipelekwa mahakmani na akawekwa ndani kwa muda wa wilki mbili. Yule kijana alitolewa baada ya dhamana ya Mkuu wa Wilaya. Hivi kweli Mkuu wa Wilaya anatoa dhamana kwa mshitakiwa aliyefika polisi au polisi ndiyo wanaotoa dhamana? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara husika ya Utawala Bora, Mheshimiwa Waziri alisema hapa kwamba anatoa mafunzo kwa viongozi wa polisi. Wawaelimishe kwamba watende kazi zao bila kuangalia itikadi za vyama. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba niende kipengele kingine. Suala hili la utawala bora nilisema kwamba linaingia katika taasisi mbalimbali. Tuliona hapa kwamba suala la vyama vya siasa kuingiliwa na Msajili wa Vyama ni kukiuka suala zima la utawala bora. Tulieleza kwa kina hapa kwamba Profesa Lipumba alijiuzulu kwa hiari yake na baada ya kujijuzulu, Msajili wa Vyama akaingilia katika kumrejesha kwenye chama.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme jamani au naomba niulize Wizara ya Utawala Bora, Katiba ya Chama; kuna Katiba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kuna Katiba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, naomba mtueleze ni

Katiba ipi kati ya hizi tatu inayota uhuru wa mtu ye yote ambaye ni kiongozi kujiuzulu halafu akarudi katika nafasi yake? Mtueleze kama kuna kifungu ambacho kinaeleza, basi mtuambie kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu namba fulani kinamruhusu mtu kujiuzulu halafu akarudi katika nafasi yake au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaruhusu mtu kujiuzulu halafu akarudi katika nafasi yake?

Mheshimiwa Spika, iweje leo Msajili wa Vyama aingilie maamuzi ya chama yaliyofanywa kihalali? Yeye anasema kwamba kikao kilikuwa ni halali, kilifikia *quorum* lakini maamuzi yalikuwa ni batili. Hii ni sawa na kumchanganya nguruwe na kuku ukawapika mahali pamoja halafu ukasema kwamba kuku ni halali, nguruwe ni haramu. Hiyo naona itakuwa haileti tija jamani. Tuangalie suala zima la utawala bora. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli suala la utawala bora ni suala lenye uwanja mpana sana na ni suala ambalo linastahili kuangaliwa kwa macho yote kwa kweli. Wenzangu walizungumzia hapa kwamba hata ajira zinatolewa kwa kuangalia itikadi za vyama.

Mheshimiwa Spika, hivi kweli mnalipeleka wapi Taifa hili kama kweli mpaka leo hata ajira inaangalia mtu kwa chama jamani? Hivi tutalipeleka wapi Taifa leo? Ina maana kwamba watendaji ambao ni wa vyama vyaa upinzani hata kama ana sifa kiasi gani, asiajiriwe ndani ya nchi hii kwa sababu yeye ni mpinzani? Nafikiri tutakuwa hatulitendei haki Taifa letu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad!

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Naam!

**SPIKA:** Sikukatizi, lakini kuna wakati napata taabu kidogo kukufuatilia. Sijui unaongelea wapi, yaani sielewi. Maana nawaangalia Mawaziri hawa sasa nashindwa kuelewa. Huyo Mkuu wa Wilaya yuko chini ya hawa Mawaziri? Yuko wapi huyo? Hao walioajiriwa kwa dini wanajiriwa kwa

nafasi ipi? Yaani kuna nini na wapi? Tufafanulie tukuelewe tuweze kufuatilia.

Endelea Mheshimiwa Hamad.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Wanaoajiriwa kwa dini; kwa sababu inayohusika na Utumishi na Utawala Bora ni Wizara ya Utumishi na Utawala Bora. Ndiyo niliyosema kwamba naongelea suala zima la Wizara ya Utumishi na Utawala Bora. Nilipoanza utangulizi wangu nilisema hivyo.

**SPIKA:** Yaani hao walioajiriwa kidini ni akina nani na kwenye *post zipi*? Ili hata Waziri aweze kuandika kitu. Naona amekaa tu!

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, hata walimu. Hili suala liko Bara na hata Visiwani.

**SPIKA:** Wewe sasa unataka kuleta mambo ambayo kidogo ni hatari katika nchi.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, siyo hatari. Nakupenda ushahidi...

**SPIKA:** Sasa kaa chini. Hilo sitakupa nafasi tena kama ndiyo hivyo.

Waheshimiwa Wabunge, sisi wenyewe tunaweza tukapanda chuki za kidini, chuki za nini, sisi ni viongozi. Hivi kweli walimu wameajiriwa kidini kweli.

Mheshimiwa Hamad nikupeleke kwenye chombo mahali uende ukapeleke huo ushahidi wako wa kidini watu wameajiriwa kweli! Maana mnataka watu wakifika hapa kila dakika mbili, maadili, inawezekana kweli! Kabla mtu hujazungumza, pima sana kitu chako, usikrupuke tu! (*Makofii*)

Mimi kama Spika, siko hapa kuruhusu hayo. Ndiyo maana mnahisi ooh, tunazuiliwa kusema. Huzuiliwi, lakini

kidogo mambo mengine ni ya hatari. Ni *border line*; ni kama unaweka kiberiti kwenye petroli kwa jambo ambalo sote hatuna uhakika. Kama una uhakika, endelea, wala sikukatazi, lakini kumbuka mwisho, nitataka sasa ushahidi.

**MBUNGE FULANI:** Afute kauli.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, samahani. Sikusema wanaajiriwa kidini, nilisema wanaajiriwa kufuatana na itikadi za vyama na hili nilisema hata kule kwetu Zanzibar linafanyika, kwa sababu binafsi nina mwanangu alifanya usaili wa benki, lakini wakawa wanafuatiliwa majumbani kwao. Wanaulizwa hasa, wewe baba yako ni nani, mama yako ni nani, yuko chama gani? Kwa kweli unafikia mahali...

**SPIKA:** Suala la mwanao kama Mbunge lazima u-declare *interest*, yaani huwezi kuongelea mambo ya mwanao na familia. Yaani...

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, sasa si ulitaka ushahidi.

**SPIKA:** Ongelea mambo ya wananchi zaidi.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, ulitaka ushahidi. Sasa nilikuwa nakupa hata ule ushahidi kwamba haya yameanza hapa mpaka Visiwani yameendelea. Ahsante, namalizia suala hilo la ajira.

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye suala zima la TASAF. TASAF kwa kiasi fulani wameonesha mwelekeo mzuri kwenye suala zima la kunusuru kaya masikini, lakini pia katika ajira za muda. Kwa kweli katika kaya maskini, wamesaidia pakubwa sana, isipokuwa niseme kwamba kwa upande wetu kule Zanzibar kuna suala zima la usimamizi wa hizi kaya maskini. Usimamizi wa kaya maskini umelengwa zaidi kwa upande wa Masheha. Tunakuta kwamba baadhi ya Masheha wanazitumia vibaya nafasi zao kwamba

wanaingiza watu ambao hawastahili kwa sababu ni jamaa zao. Kwa hiyo, *TASAF* walifuatilie suala hili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad, tulia kidogo nipokee utaratibu.

### **KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunapata shida hapa na ndiyo maana umetuona, kwa sababu tunashindwa tuandikaje. Yanazungumzwa ni masuala ya Utawala Bora wa Zanzibar. Sasa suala la utawala bora, siyo suala la Muungano na kule kuna Wizara ya Utawala Bora na ina Waziri wake. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wanapochangia, wangejitahidi sana kujikita kama ni masuala ya utawala bora, basi yazungumzwe kwa huku Bara. Unapo-*generalize* ukazungumza na mifano ya Zanzibar, inatupa taabu sana namna tutakavyoweza ku-*respond*. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Bahati nzuri na muda wenyewe umeisha. Nakukubalia kabisa Mheshimiwa Waziri, kwa hili ulilolisema na ni vizuri wengi tukafahamu na ndiyo maana nikasema mbona hatuelewi unachozungumzia. Maana hata ajira za ubaguzi hizo wa kidini kwa mfano kule Zanzibar, Zanzibar karibu watu wote kule ni waislamu; unaweza ukasema hivyo katika hesabu za kisayansi. Sasa kama watu wote ni waislamu wanabaguliwa kidini, wanabaguliwaje kwenye ajira tena huko huko Zanzibar? Yaani unajiliza maswali, unatuacha njiani. Wewe unaweza ukawa unaelewa vizuri zaidi, lakini walio wengi hapa hawaelewi kidogo picha ya mambo hayo. (*Makofi*)

Wakati mwingine tunapokaa kwenye kikombe cha chai, muwe mnatuelimisha kidogo na sisi tuweze kuelewa, maana tunapata taabu kidogo kuhusiana na mambo hayo. Pia hata hizo ajira kama ni za kule, sasa sisi tutafanyaje? Tuzungumze ajira hizi za walimu ulizosema. Pamoja na zote, lakini tuna taratibu tofauti tofauti. Kwa hiyo, twende vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, mnapokuwa mmeomba kuchangia, ni vizuri kujipanga hasa. *Level yetu ya debate* inashuka sana tu, unapoomba kuchangia uwe umejipanga kwamba leo nataka kusema; kama huna cha kusema, basi unakaa kimya.

Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, kama umejipanga.

**MHE. HAMAD SALIM MAALIM:** Mheshimiwa Spika, muda wangu umeukata, kwa sababu nilikuwa nazungumzia suala la *TASAF*, *TASAF* ni ya Tanzania nzima.

**SPIKA:** Tayari, sijaukata, muda wako umeisha.

Mheshimiwa Rwamlaza. Kama hayupo naendelea na wengine.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ngoja nibadili uelekeo kidogo basi.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia katika bajeti ya TAMISEMI na mimi napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia na mimi nakuombea angalau hukuwa na hasira leo, mambo yameenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, nina machache sana kuhusu bajeti ya Wizara hii. Kwanza nianze na fedha za Mfuko za Wanawake na Mfuko wa Vijana zile asilimia kumi ambazo zinapaswa kukatwa katika mapato ya Halmashauri (*own source*) ili ziweze kusaidia wanawake na vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu katika Kamati zetu ambapo TAMISEMI tumekuwa tukisisitiza sana kwamba Halmashauri hizi ziweze kutenga fedha hizi ili 5% na 10% iweze kuwasaidia wanawake na vijana katika kuboresha maisha yao, kufanya biashara na hivyo kujajiri na kuwaondoa mitaani ili waweze kuwa na shughuli za kufanya.

Mheshimiwa Spika, baada kuweka msisitizo huo, Halmashauri nyingi sasa zinaanza kutenga fedha hizo. Binafsi nimekuja na mawazo yangu haya nikiiitaka TAMISEMI na kuuliza swali. Fedha hizi ambazo zinatolewa kwa makundi mbalimbali ya wanawake na vijana huwa zinarudishwa au tunatoa zaka? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ziko fedha nyingi ambazo zinatolewa kwa vikundi katika nchi hii, lakini mifuko hili lko wapi? Zinarejeshwa wapi? Katika akaunti ipi? Je, kama hatutoi sadaka au kama hatuzitoi kama ruzuku, kama *TASAF* ni kwa nini hazina *return* yake?

Mheshimiwa Spika, ukienda katika Halmashauri utawaambia toa fedha na hata *CAG* hata siku moja hajawahi kuonyeshwa namna fedha hizi zinavyorejeshwa. Fedha zinapelekwa kwa makundi, basi zinaishia pale. Kila mwaka Halmashauri itasisitiza, tunaziweke msimamo kwamba mchange fedha hizo mpeleke kwa makundi, lakini hatuangalii hizi fedha zinarejeshwa vipi. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, binafsi nilikuwa nawaza kwamba kama mabenki yanaweza kukopesha fedha kwa watu na baadaye mwisho wa mwaka wanatuonyesha kwamba sasa benki hii tulikopesha shilingi bilioni tano, lakini tumezalisha hivi, tumekuwa na mfuko endelevu. Ni kwa nini ndani ya Halmashauri yetu hakuna kitu kama hicho?

Mheshimiwa Spika, nimegundua kwamba fedha hizi zinapotea kiholela, hakuna anayeziona na hata kwenye Halmashauri hatukuambiwa kwamba ziko kwenye akaunti ya *deposit*, wapi? Kwa hiyo, naomba Wizara itazame ni jinsi gani huu mfuko unaweza ukasimamiwa ukawa endelevu.

Mimi siupingi, naupenda sana, lakini fedha za walipa kodi ndani ya Halmashauri zinapotea bila ninyi kujua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hebu jaribu kufanya *research* kidogo muone kama hizi fedha huwa zinarejeshwa au zinapotea jinsi zinavyopelekwa? Maana yake Halmashauri zina-*respond* sasa hizi, zinapeleka shilingi milioni 200, shilingi milioni 300, shilingi milioni 400, *that is the end of the story*, zinaenda wapi? Hakuna mahali ambapo zinarejeshwa, hakuna *return* yoyote, hakuna Bunge hata kuelezwu kwamba Halmashauri ya mahali fulani ilikopesha shilingi milioni 500, mwisho wa mwaka tumekuwa na shilingi milioni tano na tumeweza kuendeleza mfuko huu na kama tungefanya hivi, tumekuwa tumeacha hii biashara. Hii biashara ya kuwaambia Halmashauri itenge kila mwaka, kuwasisitiza, kungekuwa na mfuko wao ambao umekuwa endelevu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho nimegundua, hii mifuko haina sheria. Hii mifuko inaendeshwa kiholela ndani ya Halmashauri. Kwa vile hakuna sheria, hakuna kanuni na hakuna kamati. Hizo kamati zinaundwa hata Madiwani wa Viti Maalum hawapo. Kwa hiyo, unaweza kuona ni kwamba pamoja na kusisitiza kwamba fedha hizi zipelekwe, lakini hazina uangalizi hata kidogo. Kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali na TAMISEMI kwamba sasa twende mbali, tutunge sheria, tuwe na kanuni, lakini mifuko hiyo iwe endelevu, ionyeshe faida, izae tupate mfuko maalum ndani ya Halmashauri ambapo fedha zake zinakwenda zina-*rotate* zinakopeshwa kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali hii inaamua tuzitoe kama zaka, tuwatangazie watu wote ziwe sadaka tujue kwamba Halmashauri inatoa sadaka kwa watu na hazirudishwi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nije kwenye kodi ya majengo. Amesema vizuri Msemaji wa Kambi ya Upinzani, amejaribu kutoa ushauri. Ninachotaka kukwambia ni kwamba kweli Kamati ya Bajeti imetuambia kwamba hizi fedha zitakuwa

zinarejeshwa kwenye Halmashauri kutokana na jinsi walivyoweka makadirio. Binafsi nikajiuliza, je, kuna sheria inayo-guide kwamba Halmashauri inaweza kupata kiwango fulani? Maana yake mimi nilikuwa kwenye RCC tarehe 2 Machi katika Mkoa wangu wa Kagera, wakatupa taarifa kwamba fedha za kodi ya ardhi hazijarejeshwa mpaka Disemba mwaka 2016, mkoa ulikuwa haujapata hata senti tano.

Mheshimiwa Spika, pale kuna sheria ambayo inasema kwamba asilimia 30 itarudi katika Halmashauri na hata Mfuko wa Barabara una sheria yake; ni kwa nini kwa upande wa majengo hakuna sheria ambayo ina-guide kiasi ambacho kitarudishwa ndani ya Halmashauri? Tunaacha tu holela. Ni kwamba Serikali inaweza ikaamua. Nilikuwa naongea na Mbunge wa Tunduma hapa, ameniambia karibu shilingi milioni 78 za ardhi hazijarudishwa katika Halmashauri yake. Kwa mtindo huo na kwa style hiloni kwamba hata hizi fedha za majengo hazitarudishwa, kwa sababu hakuna sheria, hakuna kitu chochote kinacho-guide Halmashauri ikajua kwamba itapata kiwango hiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naishauri Serikali ifikirie namna ya kuweka sheria ambazo zitawezesha Halmashauri wajue angalau katika kodi itakayokusanywa ndani ya Halmashauri yetu tunastahili kupata asilimia au asilimia 50. Kutoka hapo hata Wabunge wanaweza kuwa *mandate* ya kusaidia kudai ili Halmashauri zao ziweze kupata fedha.

**SPIKA:** Wale wasiofahamu namna ya Mbunge kuchangia, mnaona anavyoteremka huyu Mbunge! Huo ndiyo uchangiaji huo! Endelea Mheshimiwa. (*Kicheko/Makof*)

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ngoja niendelee. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, leo limetoka swali hapa linalohusu miradi ya maji la Mheshimiwa Kaboyoka, tukapewa majibu; majibu haya wakati mwingine ya kimzaha mzaha hii Serikali ya CCM inatoa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilianzia katika Kamati ya TAMISEMI, leo niko kwenye Kamati ya LAAC kwa hiyo, napata *chance* ya kukagua miradi. Tena nashukuru wewe huendi huko, kwa sababu ungekuwa unaenda, ungekuja huo upara umeota nywele. Hakuna miradi ya maji. (*Kicheko*)

**SPIKA:** Ukimsifia mgema? (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, tena nakusihii usijaribu kwenda kule. Nakwambia karibu asilimia 43 ya miradi ya maji haifanyi kazi katika nchi hii. Ukienda kule utakuta mambo ya ajabu. Hakuna umwagiliaji, hakuna mabwawa, mabilioni ya pesa yamelipwa yaani unabaki kushangaa. Mimi nataka Serikali iwe inatujibu swalii kwa nini? Msituambie michakato. Ni kwa nini Serikali ya Chama cha Mapinduzi illhindwa kusimamia miradi hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuna mkanganyiko kati ya Wizara ya Maji, kuna mkanganyiko katika Halmashauri; ukienda wale wanakwambia aah, sisi wapembuzi yakinifu walitoka kwenye Wizara ya Ardhi. Wamekuja pale wamefanya Wizara ya Maji, wamekuja wamefanya upembuzi yakinifu wanaondoka, wameacha Wakurugenzi hawajui cha kufanya hata fedha wakati mwagine... Halafu na ninyi mna tabia ya kuingilia ingilia mambo ya watu, msini-*distract* mimi. (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Taarifa nini?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Kama nimekosea nikataja ardhi, ni makosa ya ...

**SPIKA:** Taarifa, Mheshimiwa Conchesta uipokee tu. Iko wapi taarifa ile? Ooh, sawa sawa Mheshimiwa Naibu Waziri.

## NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO

**YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi nitoe taarifa kwa kanuni ya 68(8). Napenda kumpa taarifa msemaji ambaye anasema vizuri kama ulivyozungumza, lakini nilitaka kumpa taarifa tu juu ya madai ya asilimia 30 kwa sababu ameiongelea; marejesho yanayotokana na ile michango ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, nadhani mwaka 2016 hapa wakati tunapitisha bajeti, kwenye *Finance Bill* pia ilionyeshwa hiyo. Tulizungumzia habari ya *retention* kwamba hakuna hakuna tena pesa hiyo asilimia 30 anayoidai kwamba ipo kwamba wanadai Wizara. Isipokuwa sasa hivi pesa zinazokuja ni zile ambazo zimebekwa kwa ajili ya kuhudumia Halmashauri zote bila kujali kwamba ni asilimia 30 au siyo asilimia 30 lakini kutegemeana na utaratibu ambao kwa mwaka huu zilikuwa zimetengwa shillingi billioni 10 na baadhi ya Halmashauri zimepata. Kwa hiyo, hakuna deni la asilimia 30 Wizarani. (*Makofii*)

**SPIKA:** Ilikuwa ni taarifa tu, inamsaidia Mbunge wa Tunduma pia. Mheshimiwa Rwamlaza endelea.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, halafu hii tabia ya Mawaziri kujibu kabla ya majumuisho kwa kweli inatupa shida. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, nilichosema, nilikuwa kwenye *RCC* yangu Mkoa wa Kagera tarehe 2 Machi taarifa ile ninayo. Mimi naenda kwenye vikao mwenzako, nilikuta wanadai tangu Disemba Mkoa wangu wa Kagera hakuna chapa; sasa kama umepeleka jana, hewala. Kwa hiyo, ninachojua ni kwamba hizo fedhahaziendi na siyo kwangu tu. Sehemu zote mkifuatilia mtakuta hizi fedhahaziendi; na siyo ajabu hata kwako. Kama umepeleka, basi ni ubinafsi huo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, nilikuwa naongelea kuhusu mambo ya miradi ya maji, akanipeleka huko, mnani-*distract memory* kitu ambacho sipendi kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama miradi ya maji haitekelezeki, Waziri atuambie ni kwa nini Serikali inashindwa kusimamia? Wasituletee mambo ya michakato hapa. Watuambie ni kwa nini, miradi hiyo imekwama?

Mheshimiwa Spika, maji ni kero katika nchi hii. Ninyi hamjaona, nendeni katika majimbo yenu labda mahali pengine hamuendi. Kuna mahali nimewahi kwenda kusimamia kampeni sitawasema, watu hawaoshi vyungu, yaani kile chungu kinapika maharage, kinapika na kahawa ya kunywa. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni namna gani nchi hii ilivyo katika matatizo makubwa ya maji. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachowaomba hakikisheni nchi hii iweke *priority* katika kazi hii na msimamie mabilioni ya pesa, mabilioni; na mabilioni hayo ni pesa za watu, ni mikopo, watakwenda kulipa Watanzania.

Kwa hiyo, kama mnaona kuna miradi hewa, unakwenda Mkurugenzi anakutembeza hata mradi haujulikani mahali ulipo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, hayo ndiyo mambo ambayo nilisema nichangie machache...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili ya Mheshimiwa Conchesta.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, ya pili eeh, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana. Umetuchangamsha kidogo. (*Makof/Kicheko*)

Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, dakika kumi, utakuwa mchangiaji wa mwisho.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia afya njema na kupata fursa ya kuchangia bajeti hii ya Wizara. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuchangia bajeti ya Wizara naomba kwa dhati ya moyo wangu niishukuru Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa kufanikisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, barabara inayotoka Dar es Salaam mpaka Tunduru - Namtumbo mpaka Songea. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nilihisi sitaitendea haki nafsi yangu kama zitazungumza jambo hill. Kwa dhati ya moyo wangu napenda sana niishukuru sana Serikali hii, kwa kipindi cha nyuma tumekuwa tukipata shida sana, wananchi walikuwa wakisafiri kwa muda mrefu, lakini kwa sasa inaleta faraja. Kwa kufanya hivyo, inachangia hata vyombo vya usafiri kuwepo na ushindani, tumekuwa na magari mazuri na wananchi wananeemeka na wanaahidi kuendelea kukiunga mkono Chama cha Mapinduzi katika siku zijazo. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la Wabunge wa Viti wa Maalum kutokushiriki katika Kamati za Fedha. Toka nimeingia kwenye Bunge hilli nimekuwa nikisikiliza Wabunge wenzangu wakieleza masikitiko yao. Kwa bahati nzuri, mimi nimekuwa Diwani katika vipindi vinne na nimemaliza nikiwa Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri, nialewa vizuri sana Halmashauri. Nilikuwa Diwani wa Viti Maalum lakini nilikuwa Mjumbe katika kikao cha Kamati ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, nimesema nilizungumze hili kwa sababu tumekuwa tukizungumza masuala mengi yanahuusu akina mama, masuala ya mikopo, maji na mambo mengine. Ili sisi Wabunge wa Viti Maalum tupate fursa nzuri ya kuchangia masuala haya, ni lazima tuwe Wajumbe wa Kamati ya Fedha, nasema Kamati ya Fedha kwa sababu nafahamu ndio kamati mama katika Halmashauri. Masuala yote tunayozungumza ni lazima yaanzie kule. Tunapokuja kwenye

vikao vya Baraza la Madiwani ni kama Bunge, kunakuwa na dakika za kuchangia. Kwenye Kamati ya Fedha kama sijaelewa jambo lolote linalohusu mama mwenzangu ambapo mimi namuwakilisha, ninayo fursa ya kuomba kuchangia mpaka pale ninapoelewa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri anayehusika kwenye hii Wizara, na mimi naanza kupata shida kwenye hii Wizara sijui kwa sababu Waziri ni mwanaume na Naibu Waziri ni mwanaume. Mimi naamini wangkuwa akina mama wenzetu, tungkuwa tunawauliza wenzetu nyie mna nini na sisi? Sasa naomba niliache leo kwa Wizara inayohusika ili itusaidie na katika kutenda haki. Na mimi naamini hata tukiwa kwenye vikao vya Bunge, sisi Wabunge wote ni kitu kimoja. Tumekuwa tukishiriki Kamati mbalimbali, tatizo ni nini kwenye Halmashauri? Naomba kupitia jambo hili, Mheshimiwa Waziri anayehusika atupe majibu kwa sababu tumekuwa tukisema sana.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwa majibu ambayo yamekuwa yakitolewa, hata kama angekesha kuyaeleza nisingeelewa, kwa sababu tunavyozungumza, Madiwani wa Viti Maalum wanaingia kwenye Kamati ya Fedha, iweje Mbunge wa Viti Maalum unamzuia asiingie kwenye Kamati ya Fedha? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nikija kwenye ukurasa wa 11...

**SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani, nilitaka kukwambia tu, Waziri kabla yake, alikuwa mwanamke. Endelea kuchangia tu. (*Kicheko*)

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, lakini tunazungumzia sasa. Sasa alikuwa mwanamke, mimi sikuwa Mbunge. Nazungumzia sasa ambapo nimemkuta Mheshimiwa Simbachawene. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie ukurasa wa 11. Kwenye ukurasa wa 11 wamezungumzia suala la usuluhishi wa migogoro. Wewe na hata Waheshimiwa Wabunge

wenzangu watakuwa mashahidi kwamba kumekuwa na tatizo la migogoro ya wananchi katika maeneo yetu kati ya kijiji na kijiji, kati ya Wilaya na Wilaya; kati ya Mkoa na Mkoa; na kati ya wafugaji na wakulima. Hili jambo tumelisema sana kupita vikao vya Bunge na tuliambiwa kwamba imeundwa kamati ambayo itakuwa inashughulikia. Kamati zile tunatumaini zitafika kwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kutueleza, atuambie katika kusuluuhisha na katika kuunda hizi Kamati ambazo zitahusisha Wizara tano, atuambie wamefikia wapi, ili tupate majibu. Kama hawajafikia ni vizuri sasa hatua zichukuliwe kwa sababu hali ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji sio nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, naomba nzungumzie tena suala la afya. Kwenye suala la afya kwenye ahadi yetu ya Chama cha Mapinduzi tuliahidi kujenga zahanati kila kijiji, lakini tuliahidi kujenga kituo cha afya kwenye kila Kata. Nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri anapokuja atuambie mpaka sasa tumefikia wapi? Pamoja na kwamba hii ahadi ni kwa kipindi cha miaka mitano, lakini lazima tuoneshe hatua, tumefikia wapi? Nilikuwa naomba anapokuja atueleze sasa tumepata vijiji vingapi ambavyo vina zahanati na tumepata kata ngapi ambazo zina vituo vya afya.

Mheshimiwa Spika, katika kutenda haki, tumeunda Mabaraza ya Kata na kwenye Vijiji vyetu, lakini mabaraza yale ambayo kwa namna moja au nydingine yamekuwa yakishughulikia migogoro ya wananchi, wale Makarani hawaajaajiriwa na wameeleza.

Kwa hiyo, naomba tupate ufanuzi, katika kutenda haki. Ili haya masuala ya rushwa tunayoyazungumza yasiwepo, ni lazima yule mtu awe ameajiriwa; kama hatujaajiri, tunawezajaze kufanya kazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo naweza kulizungumza ni suala la kukaimu watendaji kwenye vijiji vyetu na Kata. Tumesema sana kupitia kwenye vikao vyetu

kwamba tunalo tatizo la kukaimu nafasi hizi, tunaomba sasa na wakati umefika wale kwenye vijiji vyetu tuwaajiri watendaji; unapomwajiri mtu anakuwa na mamlaka kamili. Kama hiyo haitoshi, hata Wakuu wa Idara, maeneo mengine Wakuu wa Idara hawajathibitishwa. Nilikuwa naomba kwamba kwa maana ya hao Wakuu wa Idara ambao wamekidhi vigezo, basi tuwathibitishe ili wafanye kazi wakiwa wanajijua kwamba wao ni Wakuu wa Idara kamili. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, nije katika suala la *TASAF*, Mheshimiwa Waziri, amekuwa akilizungumza vizuri sana na amegusa kwamba katika kipindi kilichopita amezungumzia kwamba umefanyika uhakiki wa kuangalia watu ambao walikuwa wanapata zile fedha ambao hawastahili. Wameguswa watu wengine ambao wanastahili kupata pesa, ni vizuri Mheshimiwa Waziri anayehusika arudi aangalie upya, kwa sababu pesa zile zimelenga kusaida kaya masikini, ni vizuri arudi aangalie upya kuona kweli hizi takwimu tunazozipata ni takwimu sahihi? (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo naomba nilizungumze ni suala la kuongeza mamlaka za utawala. Miongoni mwa Wilaya kongwe katika nchi hii ni pamoja na Wilaya ya Tunduru. Wilaya ile ilianzishwa mwaka 1905 na ina kilometra za mraba zisizopungua 18,000 yaani ukiichukua Wilaya tu ya Tunduru, ni sawa na Mkoa wa Mtwara. Imefika mahali wananchi wale wa Tunduru wanahisi kwamba siyo sehemu ya Tanzania kwa sababu eneo la utawala lile ni kubwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, naomba kwenye Wizara hiyo wakati unapofika, ni vizuri sasa wakaangalia kuona katika kugawa maeneo ya utawala na sisi kwenye Wilaya ile watufikirie katika ule Mkoa wetu wa Ruvuma. Wilaya ile ni kubwa. Katika kuhakikisha huduma za wananchi zinakuwa karibu, ni vizuri sasa tuone uwezekano wa kugawa hizo Wilaya, lakini ikiwemo na Wilaya ya Tunduru. Kama Mheshimiwa Rais itampendeza na ninafurahi kwamba Wizara hii sasa iko chini ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa mchango wangu. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ni makofi ya nini? Ya kugawa Wilaya ya Tunduru? (*Kicheko*)

Atajibu mwenyewe Waziri wakati ukifika, japo Halmashauri nyingine Viti Maalum wako ishirini, sasa wote mtaingia kwenye Kamati ya Fedha!

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru tumefika pazuri na kesho tutaendelea na uchangiaji, ataanza Mheshimiwa Juliana Shonza na Mheshimiwa George Lubeleje, atafuatia na orodha nyingine itaendelea kesho kutokana na mapendekezo tutakayoyapata kutoka kwa viongozi wetu ambao wanahuksika na jambo hili kama ilivyo kawaida.

Nawashukuru sana kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana, lakini Makatibu nawapa kazi, hebu niangazilieni kule Upinzani anayeandika hizi hotuba ni nani hasa? Hotuba za kumshutumu Spika, huyu ni nani? Kwa sababu kuna baadhi ya watu wako huko wameajiriwa kwa muda na wanalipwa na Spika halafu wanaandika tena kumshutumu Spika, halafu ni waajiriwa wangu. Yaani waajiriwa wenu lakini ninawalipa mimi. Sasa wasije wakajisahau wakafikiri kuingia kwenye geti hapo unaweza ukaingia tu na ukawa unaandika vitu vyaa jabu tena kuhusu viongozi wa mahali hapo hapo, wanaokulipa hao hao. Kwa kweli tunakuwa *so lenient* kiasi ambacho inafika mahali lazima uanzze kuangalia vizuri, *what is wrong some where?* Tutapata tu majibu. (*Makofi*)

Lile la mchana lilinipa taabu sana jinsi ya kuliongelea, nimepitia kwenye mkeka nikaangalia, hali siyo nzuri kwa wengi wetu na karibu nusu, hali ni mbaya sana. Kwa hiyo, nimezungumza na *staff* na *nime-consult* tukaona kwamba kwa kuwa jambo hili ni kujaribu, kwenye mahesabu ya kihasibu wanasesma wanajaribu kununua *future* kwenye mambo haya ya *shares*, lakini kwa *ku-peg ile gratuity* yetu peke yake na siyo kwa mkopo mwngine wowote wa kawaida, siyo jambo baya.

Kwa hiyo, tumekubaliana kwamba kesho wale wenye nia hiyo mtaenda kule uhasibu, halafu baada ya kutoka kule ndiyo mtaenda katika benki zetu zilizo hapa karibu, hizi mbili mnazifahamu ili kuzuia mtu kwenda kwenye benki hii na kwenye benki hii *at the same time*, halafu wala asielekee kwenye kinachozungumzwa. (*Kicheko*)

Kwa hiyo, hatuwalazimishi, hatutakufuutilia kwamba umeenda wapi, hilo *is your money*, lakini utaenda pale halafu wataweka utaratibu mzuri, tutaenda kule, kuna mahali tumeweka kwamba itakuwa ni siri ili kwa kweli wale wenye nia ya kuingia kwenye jambo hilo tusije tukalaumiana kwamba Spika hakuwezesha, *after all is our money* na kadhalika. Nadhani tumeelewana (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo.

**SPIKA:** Basi baada ya kufikia hapo Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.43 Usiku Bunge lillahirishwa hadi siku ya Jumatano,  
Tarehe 19 Aprili, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*